Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 9 Agosti, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika, (Mhe.Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVIVU:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda kumwuliza Waziri Mkuu kwa kipindi cha kuanzia miaka ya mwisho ya tisini mpaka kufikia hivi sasa, Serikali imefungua mianya mingi sana ya uwekezaji hapa nchini na hii inapelekea wageni

wengi sana kuingia kuja kuwekeza lakini lipo tatizo kwamba wageni hawa sasa wamekuwa hawaji kuwekeza kwa maana ya uwekezaji kwa sababu uwekezaji wao haukidhi viwango ambavyo vimewekwa na Serikali.

Je, Serikali inatoa tamko gani katika hili?

**WAZIRI MKUU**: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mangungu swali lake zuri kama ifuatavyo. Ni kweli kwamba Sera tuliyonayo sasa ni ile ambayo inaruhusu uwekezaji kutoka kwenye sekta binafasi kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini, lakini nadhani jambo la msingi hapa ni kwamba wako wawekezaji wazuri ambao wanafanya kazi nzuri, lakini inawezekana vile vile wako wawekezaji ambao kazi zao si nzuri sana.

Kwa hiyo, mimi nadhani tulichokubaliana Serikalini huku ni kwamba zoezi ambalo linaendelea sasa ni kupitia mikataba ya maeneo yote ambayo tumeingia na hawa wawekezaji kwenye sekta mbalimbali ili wale watakaobainika dhahiri kwamba wameshindwa kutekeleza makubaliano yetu basi tuweze kuvunja ile mikataba ili tutoe fursa kwa watu wengine. Kwa hiyo, nadhani jitihada hizi pengine zitatusaidia kuweza kuimarisha uwekezaji ambao una tija zaidi. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini ningependa kuuliza swali la nyongeza kwamba aina ya uwekezaji ambao tunaukataa ni ule

ambao sasa wageni wanaingia mpaka Vijijini hali ya kuwa fursa hazikufunguliwa kufika huko.

Sasa kwa nini Serikali isitoe tamko sasa wawekezaji wote waishie katika ngazi za Miji ili kutoa fursa kwa wazawa kuweza kushiriki katika uchumi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, anachokisema ndiyo hasa Sera ya nchi kwamba hakuna mwekezaji ambaye anaruhusiwa kwenda moja kwa moja na kuingia katika uwekezaji katika maeneo ya Vijijini kama hakuna ridhaa ambayo iko katika ngazi ya Taifa na ndiyo maana utaona kwenye masuala ya ardhi hawezi mtu kwenda pale moja kwa moja labda kama imepita kwenye mikondo ambayo tumejiridhisha kwamba mradi unaokwenda kufanyika utakuwa na masilahi na manufaa kwa Watanzania na hasa Wanavijiji wenyewe.

Lakini bado inawezekana katika baadhi ya maeneo pengine kuna kupuuzwa kwa hiyo, tutajaribu kulisisitiza hili kupitia Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ili kuhakikisha kwamba hakuna uwekezaji wa namna hiyo.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata hii nafasi ya dhahabu kumwuliza Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tanzania tunajitahidi sana katika kulinda amani duniani na barani Afrika na kutokana na hilo, nchi yetu inapeleka askari katika ulinzi wa amani sehemu mbalimbali duniani ikiwemo Dafur na pengine hivi karibuni hata *Gongo DRC* tutapeleka.

Katika kikao cha sitini na tano cha Umoja wa Mataifa kilichofanyika tarehe 1 Julai, 2011, jumla ya dola bilioni 85 za Kimarekani ziliidhinishwa ili kulipa zile nchi zote ambazo askari wake wanatumika katika ulinzi sehemu mbalimbali duniani. Kwa nini Tanzania wanatubagua hatupati fungu hilo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli uko utaratibu wa Kimataifa ambao unasaidia katika kuwezesha nchi ambazo wanakwenda kuingia katika kulinda amani kwenye maeneo ambao unawezesha sasa askari wetu kwenda kufanya kazi kule kwa malipo kwa kiwango ambacho tumekubaliana na nilitaka nitumie nafasi hii kuweza kumshukuru sana Dada yangu Asha Migiro kwa sababu alipokuwa New York ametusaidia sana kwenye eneo hili na mimi mwenyewe ndiyo nilikuwa msemaji mkubwa sana kwenye eneo hili kuhakikisha kwamba na sisi tunanufaika kwa sababu kikubwa ni mafunzo ambayo mnatakiwa muwe nayo yanayowawezesha muweze kupata hizo fursa.

Kwa hiyo, kupitia Mheshimiwa Migiro, tumeweza sasa kufanya mawasiliano mazuri sana na IGP na tunao mpango mzuri sana utakaotuwezesha kutumia fursa hiyo vizuri na hata hivi sasa tumekwishaanza karibu kila inapotokea na sisi tunawapeleka vijana wetu ili na wao wawe ni sehemu na hii inasaidia, inawakomaza, inawapa uwezo zaidi wa kuweza kuhimili mikikimikiki inapotokea kwamba inahitajika.

Kwa hiyo, ni jambo zuri na mimi nakushukuru sana kwa jambo hili kwa sababu unatukumbusha kitu kizuri, tutaendelea na sisi kuliimarisha na bahati nzuri hata Serikali ya Marekani nayo imekubali kusaidia kwenye mafunzo yatakayo tuwezesha kutumia nafasi hiyo vizuri zaidi. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika huo mgao kama Tanzania tunapata. Je, *propotion* tunayo wapatia askari wetu walioko Darfur na sehemu nyingine unalingana na wenzao walioko kule katika kukidhi maisha ya huko?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa inategemea kwa kweli makubaliano tunayoingia kati ya sisi upande wetu wa Serikali na kule tunakokwenda kuhudumia kutokana na mchango ambao unatokana na nchi zinazounga mkono jambo hili. Sasa ni eneo ambalo siwezi nikalijibu moja kwa moja kwa sababu sina uelewa mpana juu ya nini kinatokea katika mgao huo.

Lakini pengine rai yako ni nzuri kwamba pengine tuliangalie na sisi huku tuone kama je tukifanya vile ni kwa kiwango gani hicho tunachopata kinawiana au kinatusaidia kuweza kukidhi kwa sehemu kubwa *you know* matatizo yetu ya hapa ndani.

**MHE.MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ilikuwa na nia njema sana kwa kuleta Sheria ya Manunuzi ili taratibu ziwe zinafuatwa punde Serikali na taasisi za mashirika ya Umma zinapofanya manunuzi.

Lakini uchunguzi nilioufanya, Sheria hii ya Manunuzi imekuwa chanzo cha kupandisha bei za bidhaa na shughuli zinazonunuliwa na Serikali. Lakini pia Sheria hii ya Maunuzi imekuwa chanzo cha kupata miradi ambayo iko chini ya kiwango kwa sababu ya pande mbili yaani mwenye kampuni pamoja na wataalamu wasio waaminifu kujihusisha kwa biashara isiyo halali?

Lakini pia Sheria hii imekuwa ikisababisha bei kupanda kwa ajili ya mchakato wake mrefu na tumeona hivi karibuni, ushahidi uliopo ni kwamba hata kwenye Wizara ya Nishati na Madini tulishuhudia manunuzi ya mafuta yaliyofanyika kwa *direct sourcing* yakawa yameokoa takribani bilioni 6 kwa mwezi ambazo ni bilioni 72 kwa mwaka na nimeshuhudia hata kwenye ngazi ya Halmashauri ukiangalia makanisa au misikiti iliyojengwa kwa *direct sourcing* yana gharama nafuu na uhimara kuliko majengo yaliyojengwa kwa zabuni.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kwenda kwenye Sera ya *Direct Sourcing* kama nambari moja, halafu zabuni iwe inafuatia ili kupunguza gharama na kubana matumizi?(*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, analolieleza Mheshimiwa Mchemba ni kweli ni eneo moja bado lina utata, lina ugumu sana, lakini kubwa ni uaminifu wa wale ambao tumepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria hiyo.

Ukisema *direct sourcing* pengine ndiyo suluhu, inawezekana ikawa ikawa suluhu siku moja, lakini vile vile inaweza ikawa kitanzi siku ya pili kwa sababu inategemea nani yuko pale na ni mwaminifu kiasi gani.

Yote unayoyaona kwenye Sheria hii, ni kwa sababu mara nyingi watendaji sio waaminifu. Wana-*lick* ile *information* kwa wahusika, wanakubaliana apandishe gharama kiasi ili mradi tu na yeye mle ndani apate chochote.

Kwa hiyo, matokeo yake ndiyo hiyo inayofanya gharama zinakuwa kubwa sana.

Sasa ina changamoto zake, lakini nakubaliana na wewe kwamba kimsingi Serikali imeshaona tatizo lililopo, tumekubaliana kwamba tujaribu kuipitia tena ile Sheria vizuri, tuone kama kuna maeneo au namna nzuri ya kuweza kuziba mianya ambayo sasa inasababisha uvujaji mkubwa wa fedha za Umma. Lakini bado narejea kusema changamoto ninayoiona mimi kubwa katika Sheria hii ni watendaji kutokuwa waaminifu.

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo limeonekana kwenye Sheria na kwenye Uaminifu, Serikali je itakuwa tayari kuorodhesha upya makosa ya uhujumu uchumi na haya yote yanayojitokeza kwenye ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali yote yawe kwenye uhujumu uchumi na kila mwaka tunapofanya kumbukumbu ya mashujaa wa Taifa hili iwe ni siku ya kuwaachia vibaka wadogo wadogo walioiba heleni, simu na kuwapeleka ndani wote walioko kwenye ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali *(CAG)*? (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Sheria ile inayozungumza suala la wahujumu uchumi ipo na hata hawa baadhi yao ambao wanaingia katika makosa yanayotokana na Sheria za Manunuzi kutegemea na aina ya kosa lilivyo wanaweza vile vile wakawa ni wahujumu uchumi.

Pengine jambo la kusisitiza hapa ni kuona tu kwamba ni kwa kiasi gani tunao uwezo wa kuweza kubaini yale yanayoendeshwa kisirisiri kati ya sisi tunaopewa dhamana hiyo na wale ambao tumewapa kazi hiyo kuweza kuitekeleza. Tukifaulu, bado hata kwa Sheria hii tunaweza, lakini bado ni wazo zuri kwamba pengine tungelilitazama kama njia pengine ya kuongeza wigo wa watu ambao wanaweza kuwa wanahusika na eneo hili.

**MHE. RAJABU MBAROUK MOHANED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali yetu imetunga Sera na pamoja na kupitisha Sheria ambazo zimepitishwa na Bunge letu hili, hususani Sheria ambazo au Sera ambazo zinazungumzia suala zima la usafiri, usafirishaji, majanga, maafa pamoja na uokoaji.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko kubwa la maafa, majanga pamoja na ajali na wananchi wetu wengi kuweza kupoteza mali zao pamoja na maisha yao.

Hivi, Mheshimiwa Waziri Mkuu ukiwa kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni, Serikali yetu imejikwaa sehemu gani? Au Sera hizi hazitekelezeki?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Rajabu Mbarouk Mohamed, swali lake kama ifuatavyo. Ni kweli tunayo Sera na tunazo Sheria mbalimbali ambazo zinasimamia eneo hili na viko vyombo ambavyo vimepewa dhamana ya kuhakikisha vinasimamia eneo hili kwa ujumla wake pande zote mbili.

Kwa upande wa Zanzibar na upande wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Kinachojitokeza ni kwamba usimamizi kwenye eneo hili katika baadhi ya maeneo hauwi wa makini sana. Kwa mfano, chukua hata hizi meli tunazoagiza, taratibu ziko wazi, zinaeleza meli ukiinunua ni lazima iwe na umri gani wa ambao imekwishafanya hiyo kazi.

Inapozidi ni dhahiri umekiuka utaratibu na ndiyo maana katika zoezi hili kwa maafa yaliyotokea hivi karibuni, utaona Viongozi wote Rais wa Zanzibar, Rais wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania wote wamekuja na kauli moja kwamba vyombo hivi vya pande zote mbili ni lazima vishirikiane katika kuhakikisha kwamba viwango vinazingatiwa wakati wa ununuzi wa vyombo hivi.

Vinginevyo, maafa yanaweza kuendelea kutokea bila sababu za msingi. Lakini kwa sababu hiyo hiyo, utaona upande wa Serikali ya Zanzibar kwa makusudi wakaamua hata ile meli pacha ambayo ilinunuliwa pamoja na hii ambayo imeleta janga juzi na yenyewe isifanye kazi pamoja na kwamba kulikuwa na maelezo kwamba iko katika hali nzuri.

Kwa hiyo, kwa kweli kwa upande huo, lazima tukubali kwamba inawezekana kulikuwa na upungufu wa namna fulani kwa upande wa vyombo hivi, lakini imani yangu ni kwamba baada ya maelekezo yaliyotoka juzi na kama kutakuwepo ushirikiano wa karibu baina pande hizi mbili, hakuna chombo kitakachoweza kufanya kazi kama kweli hakikutimiza masharti yanayotakiwa. *(Makofi)*

**MHE. RAJABU MBAROUK MOHANED:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jibu lako zuri. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa vile umekiri kwamba usimamizi hauko makini.

Je, meli inapoondoka katika Bandari ya Dar es Salaam, mhusika mkuu ambaye anatoa *Certificate* ya kuondoka meli ile anakuwa ni SUMATRA, utachukua hatua gani kwa watendaji wale wa SUMATRA ambao waliiruhusu meli ile kuondoka siku ile?

**SPIKA:** Sasa hapo unaingia viwandani. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba ujibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, *of course* ukiniuliza kwa sasa na mimi nitaonekana vilevile nimechelewa kwa sababu jambo limeshatokea. Kwa hiyo, kama ni hatua zilitakiwa kuwa zimeshachukuliwa tayari. Pengine tukubaliane kwamba yaliyopita sindwele kwa maana hiyo Sisi tutaliangalia hili kwa makini sana na tutaona kama kulikuwa na uzembe wa namna yoyote basi tutajaribu kuchukua hatua kulingana na maelezo tutakayokuwa tumepata.

Lakini ni dhahiri uchunguzi ambao Serikali ya Zanzibar imeamua kufanya kwa vyovyote vile lazima utabaini maana lazima uje uanzie huku waone upungufu uliotokea ni upi na uende mpaka ukamalizie upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, nadhani katika uchunguzi tutabaini ukweli wa jambo ulivyokuwa na mimi nina hakika wote waliohusika wataadhibiwa kulingana na maelezo tutakayokuwa tumeyapata.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilivyo leo inakataza mtu ambaye ni Afisa Mwandamizi katika Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuwa Mbunge au

inamnyang'anya sifa mtu ambaye ameteuliwa kuwa Afisa Mwandamizi kwenye utumishi wa Serikali kuendelea kuwa Mbunge. Na kwa kuwa, kuna Wakuu wa Wilaya na Mikoa ambao wamechaguliwa kuwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa wakiwa Wabunge na kwa hiyo, wananyang'anywa sifa za kuendelea kuwa Wabunge.

Je, kwa nini Serikali inaendelea kuwaruhusu Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuendelea kuja Bungeni wakati ni Maafisa Waandamizi wa Serikali?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sina hakika sana na analolisema Mheshimiwa Tundu Lissu kama ndiyo *position* ilivyo, lakini kama ndivyo ilivyo bahati nzuri Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo, amelisikia na atalifanyia kazi.

Lakini ninachokijua mimi ni kwamba utaratibu ule ulikuwa unamzungumzia mtumishi wa Serikali kwa maana ya *Public Servant* tunayemjua ndani ya Utumishi wa Serikali, bahati mbaya au nzuri Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa ni viongozi ambao wana kofia ya Siasa vilevile, si moja kwa moja watendaji kama tulivyokuwa tunaitazama wakati tunapitisha yale maamuzi. Kwa hiyo, ndiyo maana unaona kwa muda wote limekuwa ni eneo ambalo halina chokochoko sana lakini inaonekana kwako wewe kama vile hapana, pengine tunakiuka Katiba na mimi nasema ni vema acha tulifanyie kazi kitaalamu zaidi ili tuone kama kuna mahali tumekosea. Lakini kwa utaratibu tuliokuwa nao tuliamini ni sawasawa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa umeridhika? Siyo lazima uulize kama huna la kuuliza lakini endelea tu kama una swali la nyongeza.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, wala siyo swali la nyongeza ila naomba nimweleze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tafsiri ya Afisa Mwandamizi wa Serikali ilikuja mwaka 1965 na Katiba ya kwanza ya chama kimoja, yaani kwamba mtumishi wa Serikali siyo Mkuu wa Wilaya au Mkoa kwa sababu wakati ule walikuwa wanaruhusiwa kuingia Bungeni. Baada ya mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 1992 hiyo tafsiri iliondolewa. Kwa hiyo, watu wamerudi kuwa Maafisa Waandamizi wa Serikali hawatakiwi kuwa Bungeni na ninaomba kwa sababu umesema Serikali yako itaifanyia kazi naomba wataalamu wa Sheria wa Serikali walifanyie kazi na wajiridhishe kwamba hawa watu hawastahili kuwa humu ndani.

**SPIKA:** Haya!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na wewe ndiyo maana nimesema sina hakika, na wewe umetumia neno Maafisa Waandamizi wa Serikali. Wewe kwa tafsiri yako unawachukulia wale nao ni Maafisa Waandamizi wa Serikali na mimi nasema sidhani kama hiyo ni tafsiri ambayo tunaitumia. Ndiyo maana nimesema katika hili tusiipeleke mbali, kingunge mwenzako mwenye kujua madudu haya vizuri yupo. Kwa hiyo, nadhani atalitazama na ikibidi tutakuja kutoa kauli ya Serikali na litawekwa vizuri.

Lakini bado naamini Waziri Mkuu hajakosea sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Mariam Msabaha. Naomba muulize kwa kifupi ili kusudi wote mfikiwe.

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna sheria ya mtoto tuliipitisha katika Bunge hili Tukufu na sheria hii imeridhiwa mpaka Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwa na watoto wengi sana katika miji ambayo inakua kwa mfano, Dodoma, Mwanza, Arusha na Jiji la Dar es Salaam na watoto hawa wamekuwa wakizurura ovyo na kulala mabarazani na wengine kufikia hata kubakwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna Wakuu wa Wilaya yaani Ma-*DC* na Wakuu wa Mikoa wanafanya nini wanashindwa kudhibiti hali hii? Naomba swali langu lijibiwe.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri dada yangu Msabaha ameacha vilevile kwamba na wengine ni wapiga kura wetu sisi Wabunge ili uone ukubwa wa tatizo lilivyo. Ni tatizo la kijamii na linatugusa sisi wote yaani viongozi kwa ujumla wake na jamii kwa upande mwingine. Kwa hiyo, wakati nakubaliana na wewe kwamba lipo tatizo na ndiyo maana tunafanya jitihada nyingi sana kujaribu kuona

ni namna gani tuwasaidie hawa watoto. Tumejaribu kuanzisha vituo, tumejaribu kuwakusanya ili tuje kuwasaidia na kuna *NGO's* zimejitahidi sana kufanya kazi nzuri sana. Lakini eneo hili ni gumu, hata katika jitihada hizo tunazozifanya bado baadhi ya watoto wanatoroka wanakwenda tena barabarani na purukushani tu kila kukicha. Lakini hatujakata tamaa bado tutaendelea kulisimamia kwa sababu ni kazi yetu wote yaani Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, viongozi kwa ujumla wake na vilevile jamii ni lazima ijue kwamba eneo hili ni letu sisi wote vinginevyo vita ile hatuwezi kufaulu sana. Ndiyo! Hata kwenye *level* za kaya, kwenye vijiji vyetu na kwenye miji yetu ni lazima tulikubali kwamba tatizo ni letu wote.

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Waziri ahsante kwa mazuri. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, kundi hili limekuwa mpaka linafika kwenye milango ya Bunge la Jamhuri ya Muungano na linaleta picha mbaya kwa wageni wetu ambao wanatembelea Bunge ambao wanatoka nchi za nje.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, utadhibiti vipi kundi hili ambalo sasa hivi limeshaanza kuingia kwenye milango ya Bunge kuja kuomba misaada mbalimbali ya kimaisha?

**SPIKA:** Siyo ndani ya Bunge lakini, Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu tafadhali! (*Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri tatizo siyo kuja kwenye lango la Bunge lakini tatizo ni kwamba wapo watoto mitaani ambao ni changamoto

ya nchi ya Tanzania ambayo ni lazima tuitazame kwa upana wake.

Ombaomba unaowasema wapo tu, Dar es Salaam wapo, ukija Dodoma ukizunguka mitaani wapo, lakini hoja ni kwamba tunafanya nini kwa pamoja kama Watanzania namna ya kusaidia watoto hawa? Kama nilivyosema, jitihada zipo na mimi nataka nizishukuru sana *NGOs* na Mashirika ya madhehebu mbalimbali ya dini kwani wamejaribu sana eneo hili na mimi ndiyo maana nimekwambia kwamba si rahisi maana huwezi kukaa na Polisi ukaanza kukamata watoto wadogo, hapana! Ndiyo maana tunafanya kila jitihada kuwa na nyumba za watoto na kuona tufanye nini lakini bado tutaendelea kulifanyia kazi kwa sababu si jambo ambalo nitasimama siku moja tu na likaisha.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sensa ni jambo la muhimu sana katika nchi yoyote kwa maendeleo lakini zaidi kwa mgawanyo wa raslimali na ni wazi kwamba katika zoezi zima la sensa mambo muhimu yanahitajika ikiwemo umri, jinsia na mengineyo ili kuweza kutoa mahitaji halisi kwa jamii inayohusika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, utakubaliana nami kwamba siku za hivi karibuni kumekuwa na malumbano makali sana kwa baadhi ya waumini wa dini moja wakidai kwamba kipengele cha dini kiwekwe katika suala zima la sensa. Naomba kujua ni kwa nini Serikali imeondoa kipengele hicho?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa namna alivyouliza swali inakuwa ni kama vile na yeye anadhani kwamba ni busara kuendelea na swali lile kwenye hojaji, na mimi nasema kwamba tumekuwa na sensa kadhaa kuanzia miaka ya nyuma ambayo hili swali kusema kweli halijawahili kujitokeza ukiachilia mbali kwenye sensa za miaka ya nyuma zaidi lakini miaka ya 67 na baadaye miaka ya hivi karibuni halikuwa ni eneo ambalo tunalitazama kwa mtazamo huo. Lakini sababu yake ni rahisi tu kwamba hatupangi maendeleo yetu sisi kwa kuzingatia vigezo vya dini, hapana! Sisi ni Watanzania na ni Watanzania ambao ni wamoja tunajaribu kupanga kwa kuzingatia mambo fulanifulani ambayo tunadhani ni ya msingi yaani jinsia ina msingi wake kwa sababu ni lazima tujue uwiano uliopo kati ya makundi haya. Tunajaribu kutazama vilevile kama kuna walemavu humo ndani kwa sababu ni vizuri tukajua namna ya kuwasaidia hawa walemavu. Lakini ukishaanza kuingiza dini Kiserikali sisi tuliona kuwa halina tija wala sababu kwa sababu si kitu cha msingi katika hojaji zetu kwa maana ya kupanga Mipango ya Maendeleo.

Hofu tuliyokuwa nayo na mimi ni mmojawapo ni kwamba jambo hili baadaye linaweza likazua migogoro ambayo si ya lazima sana, mnapoanza kujilinganisha nani mwingi, nani wachache na nani wengi , hiyo haina tija sana. Ndiyo maana Serikali ikasema, jamani tusiende huko kwani si jambo la maendeleo bali ni jambo ambalo linaweza likatuingiza katika migogoro. Kwa hiyo, tuzingatie mambo ya msingi tu katika ile hojaji. Sababu kubwa ni hiyo tu!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante na ninashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Walimu wamekuwa ndiyo mara nyingi wasimamizi wa sensa zetu na kwa kipindi hiki baada ya mgomo wa Walimu tumeambiwa kwamba Walimu hawatashiriki katika zoezi hilo na wote tunajua kwamba Walimu katika sensa wamekuwa ni waaminifu sana na vilevile wamekukwa wakipata kipato hicho kama posho za kuwasaidia.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, unasema nini kuhusu hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kilichotokea ni nini? Tulisema katika sensa hii tutoe fursa kwa makundi mbalimbali na Walimu ni moja kati ya makundi hayo, wafanyakazi wengine katika maeneo yetu ya vijijini kama wapo wenye sifa tuwachukue.

Lakini tukasema tuna vijana wengi wamemaliza *Form Six,* wengine ni *Graduates* na wengine ni *Form Four*, wapo huko ambao nao wangeweza kutumia fursa hiyo kwa ajili ya kujisaidia katika hizo wiki mbili au tatu tutakazokuwa tunafanya hiyo kazi. Kwa hiyo, ndiyo maana lile tangazo ni pana na tunajua kabisa kwamba wapo baadhi ya Walimu watakuwepo, watakuwepo pia baadhi ya vijana ambao walikuwa nje na wengine katika utumishi mbalimbali lakini halikuwa eneo kwamba hili sasa ni la Walimu peke yao, hapana! Hatukuwa na mtazamo huo hata kidogo, tulilipanua sana na ndiyo maana tunashukuru kwamba inawezekana watakuwepo watatu au wanne

au watano ambao wamekosa lakini vijana wengine watakuwa wamepata nafasi ya kuingia pale. Kwa hiyo, haina uhusiano wowote na mimi naomba niseme kwamba hatuna matatizo na Walimu, hatuna matatizo nao kama ni waaminifu ni waamini tu lakini kwa hili msingi haukuwa kwamba wao lazima wote, hapana! Hatukuwa na mtazamo wa namna hiyo. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali yetu ilianzisha *general purpose grant* kwa ajili ya kusaidia akina Mama wenye biashara ndogondogo wasitozwe ushuru kwenye masoko yote nchini na juzi Waziri wako wa *TAMISEMI* ametoa maelekezo Mjini Kigoma kwamba watu wote sokoni yaani wanaouza Dagaa, Nyanya, Ndizi moja, Vitunguu na kadhalika wasitozwe ushuru. Lakini Halmashauri na Manispaa ya Kigoma Mjini in *particular* nadhani na Halmashauri nyingi nchini wamekataa kutekeleza agizo hili la Serikali. Nataka kujua sasa hii *general purpose grant* tunaendelea kuipeleka huko kwa sababu gani?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, hii fedha ya zuruku ambayo Serikali inaitoa kufidia pengo la kodi mbalimbali na ushuru lengo lake kubwa ni hilohilo ambalo analolitaja Mheshimiwa Serukamba. Tuliondoa baadhi ya ushuru ambao tuliona ni kero haukuwa na tija sana ndiyo maana tukasema badala yake ngoja tusaidie kurejesha hizo fedha na bado tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri alipokuwa Kigoma ni kweli alitoa kauli na ni kauli sahihi kabisa kabisa na nimeshawaelekeza watu wa *TAMISEMI*

kwamba inawezekana hamjapeleka maagizo kwa maandishi. Kwa hiyo, nimewaambia wapeleke kwa maandishi kwa sababu ushuru mwingine mdogomdogo huu wa sokoni mtu anauza Nyanya na Mchicha tulikaa tukalizungumza sana na ndiyo maana tukasema kwamba vitu vingine vidogovidogo hivi mnapoteza nguvu zenu nyingi bure badala ya kwenda kuziingiza kwenye maeneo ya maana zaidi, acheni na badala yake tufanye hili. Lakini kama unavyosema kama Kigoma wanaona ile *general purpose grant* haina thamani sisi tuta *withdraw* ili tuwaruhusu waendelee na hiyo kama wanadhani watafaulu katika tija hiyo ambayo unaitarajia. Lakini mimi nasema tusirudi nyuma bali Halmashauri zijue kwamba ruzuku ni kusaidia kuondoa maamuzi kwenye sekta ya *TAMISEMI* kwa yale maeneo ambayo ni kero na bughudha tu na badala yake unachokipata ni kidogo sana. Ndiyo maana tukasema hiyo na mimi bado nasisitiza tuitekeleze.

Mheshimiwa Serukamba, kwa hiyo, nataka nirudie kwa msisizo mkubwa kabisa kwamba tutapeleka maagizo kwa maandishi halafu tutaona nani ambaye anatukatalia baada ya maandishi hayo kwa sababu hayana sababu hata kidogo. (*Makofi*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nikushukuru kwa maelekezo yako, lakini wana Kigoma nao ni Watanzania ambao wangependa wafaidike na ruzuku za Serikali yetu ambazo zinawasaidia kuondoa kero. Lakini Meya wa Manispaa amefunga masoko yote kwa kusema lazima watozwe. Naomba sasa Serikali iseme hapa sasa

kwamba mwenye dhamana ya ku-*deal* na kuwasaidia wananchi ni nani? Ni Meya ama ni Serikali yetu hasa ya Chama cha Mapinduzi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sina hakika nimjibu vipi Ndugu yangu Peter Serukamba, kwa sababu unajua upande mmoja na yeye ni sehemu ya Baraza la Madiwani hilohilo la Kigoma na hiyo kidogo inakuwa inaniletea taabu kidogo. Lakini nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Peter Serukamba kwamba hebu tuachie hilo jambo la Kigoma tulitazame vizuri na sisi tutalirekebisha vizuri na litakwenda vizuri tu. Huyo Meya na kadhalika kubwa tu ni kwamba acha tuone kilichotokea ni kitu gani na tutatoa maelekezo ambayo yatakidhi mahitaji ya Watanzania walio wengi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru kwa majibu, tunaelewa kwamba ndiyo umeshuka kwenye ndege na kuja moja kwa moja Bungeni. Lakini na maswali ya Wabunge pia hayakuwa mabaya sana, ingawa siku hizi maswali ya nyongeza yanatengeneza swali lingine kabisa, hayawi ya nyongeza bali mnatengeneza mengine kabisa yaani yanakuwa mawili kwa mtu mmoja, tusifanye hivyo. Tunaendelea!

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 345

### Hati Chafu Wilaya ya Kishapu

**MHE. SELEMANI SAID JAFO (K.n.y. MHE. MASOUD SULEIMAN NCHAMBI)** aliuliza:-

Wilaya ya Kishapu imepata Hati Chafu kutokana na ubadhilifu wa fedha unaofanywa na watendaji wake. Kwa nini Serikali haikuwafukuza kazi na kuwafikisha Mahakamani watumishi waliohusika na ubadhilifu huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Suleiman Nchambi Mbunge wea Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mwaka wa fedha 2009/2010 Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ilipata Hati Chafu, kutokana na uzembe wa baadhi ya watendaji katika kusimamia matumizi ya fedha za umma. Kwa mujibu wa Sheria namba 8 ya Utumishi wa Umma kifungu cha 5(1) (a)(iii) ikisomwa pamoja na kanuni ya 35(2)(b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003 Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ndiye mwenye mamlaka ya nidhamu ya Wakurugenzi wote wa Halmashauri isipokuwa wale wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais. Kwa kutumia kanuni F.14 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 zilizotungwa chini ya kifungu cha 35(5) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ameamua

kumvua madaraka aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Madiwani katika kikao chake cha kujadili taarifa ya ukaguzi maalum uliofanywa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kwa mwaka wa fedha 2007/2008-2010/2011 kilichofanyika tarehe 19-20/032012 kilisimamisha kazi jumla ya Watendaji kumi na tatu (13).

Aidha, uchunguzi wa baadhi ya watumishi unaendelea kupitia vyombo mbalimbali vya kisheria vikiwemo Polisi, (*DCI*) na TAKUKURU ili kubaini waliohusika na ubadhilifu wa fedha za umma waweze kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamojana kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, baada ya Polisi kufikia hatua ya juu ya uchunguzi na kujiridhisha na vielelezo, watuhumiwa wanne (4) kati ya kumi na tatu (13 na mtumishi mmoja (1) wa Benki ya Tawi la *NMB* Manonga Mkoa wa Shinyanga Wamefikishwa Mahakamani mwanzoni mwa mwezi Mei, 2012 kujibu mashitaka ya kuhusika na ubadhilifu wa fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, watuhumiwa bado wanaendelea kuchunguzwa kubainikama wamehusika na ubadhilifu huu, ili wachukuliwe hatua za kisheria mara moja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya

nyongeza. Kwa kuwa, mara nyingi sana Halmashauri inapopata Hati Chafu inajikuta ndiyo inahukumiwa kwa kukosa fedha na watumishi wale waliokula fedha wamekuwa wanabaki bila kutoa *compensation* kwa halmashauri husika.

(i) Je, Serikali sasa haioni kwamba pindi Halmashauri inapopata Hati Chafu waliohusika ikiwezekana mali zao zifilisiwe ili mradi shughuli za maendeleo wilayani humo ziweze kuendelea?(*Makofi*)

(ii) Kwa kuwa tatizo kubwa sana katika Halmashauri ni kukosekana udhibiti na hii ni kwa sababu Waheshimiwa Wabunge na Wenyeviti wa halmashauri hawana *access* ya kujua *transaction* ya kila mwezi inapoyokuja kwenye halmashauri yao.

Je, Serikali sasa haioni kuna kila sababu ya kuanzisha *Financial Communication Protocol* ambayo kila mwezi Mheshimiwa Mbunge na Mwenyekiti wa Halmashauri watapata *transaction* za kila mwezi ili waweze kufanya *control on monthly basis*? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Seleman Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, anachozungumza Mheshimiwa Mbunge hapa ni kweli tumekuwa tunafanya. Fedha hizi

ambazo zinazuiwa kama umepata Hati Chafu ni fedha za *Local Government Capital Development Grant*.

Wabunge wengi wamezungumzia jambo hilo analozungumzia Mheshimiwa Mbunge kwamba, inakuwaje sasa unatoa adhabu kwa halmashauri badala ya kutoa adhabu ile kwa watumishi wale kwa maana ya Mkurugenzi, Mkuu wa Idara na wale wengine waliohusika na jambo hili.

Wakati ule tulipofikiri jambo hili na kuamua kwamba tufanye hivyo nia na shabaha ya mpango ule ilikuwa ni kupandisha hasira ya Baraza la Madiwani ili wadhibiti. Kwa kufanya hivyo tulishuka kutoka Halmashauri 78 zilizokuwa zimepata Hati Chafu mpaka Halmashauri nne (4).

Baadaye kama mlimsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi amekuwa anazungumzia tunaenda ku-consider kwamba badala ya kuchukua *local government capital development grant* yote walau tuwapelekee asilimia 25. Bado haya ni mawazo kama tunavyofikiri, lakini nimetoa takwimu hizi ili kuonesha kwamba ule mwarobaini tulioutumia kuzuia kupeleka hizi fedha umesababisha sasa Hati Chafu zimepungua na ndiyo tukafikia katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini tunalichukua ili tukalifanyie kazi na tuone kwamba tunafanyaje. Kinachotakiwa hapa ni kuona tu kwamba wote tunasimamia kwa pamoja.

Sasa kuna hii *protocol* anayozungumza hapa. Wabunge wote ni wajumbe wa Baraza la Madiwani. Kwa hiyo kila baada ya miezi mitatu taarifa zote zinatoka mpaka zile za Mkaguzi wa ndani zinatoka mle ndani na wao wanazipata hizi taarifa hapa.

Sasa kwamba wanashindwa ku-*access* hii nimeshindwa kumwelewa Mheshimiwa Jafo atanielimisha vizuri, tutakaa tuzungumze. Lakini ninavyojua kwa utaratibu ulioko katika Halmashauri Mbunge anatakiwa apate taarifa zote anazozihitaji kama Mbunge ili uwakilishi wake uweze kuwa madhubuti.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba tu nimwulize Naibu Waziri kwamba matatizo makubwa yako TAMISEMI ni kwa sababu Wakurugenzi wanasababisha Halmashauri kupata Hati Chafu lakini wanaopelekwa mahakamani ni wale watendaji wadogo wadogo. Mkurugenzi anaachwa palepale, analindwa na anaendeleza tabia yake ileile ya kukumbatia ufisadi ndani ya Halmashauri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika,kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI kwa kweli hatukumbatii Wakurugenzi. Kutokana na Hati Chafu mbalimbali zilizojitokeza wapo Wakurugenzi ambao

tumewavua madaraka na wengine tumewapeleka katika vyombo vya sheria na wengine wako mahakamani. Kila tunapojiridhisha kwa kweli tunachukua hatua.

Tunachotaka tu kusema ni kwamba, sisi TAMISEMI hatuna TAKUKURU wala hatuna polisi. Kwa hiyo, tunavitegemea sana hivyo vyombo vitusaidie kwa sababu tunapokuwa na tuhuma mbalimbali tunawapeleka kwenye vyombo vya sheria.

Sisi pia hatuna mahakama kwa hiyo lazima tuwapeleke mahakamani kwani mahakama ndiyo inaweza kuwafunga au kuwaachia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Chilolo swali la mwisho.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba zipo sababu zingine ambazo hazihusiani na Halmashauri. Kwa mfano; Halmashauri kupewa Hati Chafu kutokana na wakuu wa idara kuwa makaimu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuipitia sheria hii upya ili kuondoa vigezo vyote ambavyo havihusiani na Halmashauri katika utoaji wa Hati Chafu kwani haviwatendei haki wananchi wanaokosa hiyo ruzuku?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo.

Kuwa na makaimu si kigezo cha kufanya halmashauri ipate Hati Chafu, isipokuwa kuna baadhi ya idara zikikaimiwa zinaweza kuisababishia halmashauri ikashushwa baadhi ya vigezo katika upimaji, lakini siyo kwenye Hati Chafu. Unaweza ukawa na Hati Safi isipokuwa ukiwa na Kaimu Mweka Hazina inaweza ikakusababishia kupata matatizo ya kukosa fedha zile zinazotakiwa kwa kiasi kikubwa za *Capital Development Grant* ambazo zinatolewa na Serikali.

Lakini hata hivyo suala hilo sasa tunalifanyia kazi kuhakikisha kwamba halmashauri zote zinakuwa na wakuu wa idara na wakurugenzi ambao siyo makaimu.

Na. 346

**Kufufua Kiwanda cha General Tyre Arusha**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitoa ahadi ya kufufua kiwanda cha *General Tyre Arusha* bila kutekeleza ahadi hiyo japo kiwanda hicho ni muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa.

Je, Serikali inaweza kueleza kuwa ni lini kiwanda hicho kitafunguliwa na kuanza kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu**:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ahadi ya kufufua kiwanda cha *General Tyre* ambacho ni muhimu sana kwa uchumi wa taifa imechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya kuchelewa kutekeleza ahadi hiyo ni kutokana na Serikali kukosa fedha kwa ajili ya kukiendesha kiwanda hiki na mbia mwenza (Kampuni ya *Continental AG)* kutoonesha nia ya kuendelea kuwekeza katika kiwanda hiki kwa madai kwamba hakikuwa muhimu kwake (*non core business*).

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kiwanda hiki kwa taifa Serikali imeamua kuachana na mbia huyo na kulipa Shirika la Maendeleo ya Taifa *(NDC)* jukumu la kusimamia ufufuaji na kukiendeleza kiwanda cha General Tyre. Mpaka sasa tayari NDC imeishafanya mazungumzo ya awali na wawekezaji kutoka Malyasia, Afrika Kusini na China ambao wameonesha nia ya kuwekeza katika kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia *NDC* imejipanga vizuri na itahakikisha kuwa kiwanda cha *General Tyre* kinaanza kufanya kazi katika mwaka huu wa fedha wa 2012/2013. Hivi sasa *NDC* inafanya uhakiki wa mahitaji ya ukarabati wa kiwanda na fedha kwa ajili ya kazi hiyo imeishapatikana na kazi inatarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia sasa.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali imeachana na mbia wa mwanzo ambaye ni *Continental AG* na sasa imewapa shirika la maendeleo ya Taifa *(NDC).*

(i) Je, ni athari gani za kimkataba ambazo zinaweza kutokea iwapo mbia wa mwanzo *(Continental AG)*akiamua kwenda mahakamani?

(ii) Je, Serikali imejipanga vipi kuwawezesha vijana kushika nyadhifa za uongozi mara tu baada ya kufunguliwa kwa kiwanda hiki?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali hili ambalo kwa kweli linaonesha lina tija kwa sababu

baada ya kuachana na mbia mwenza uwezekano wa kwenda mahakamani ni mkubwa sana.

Lakini naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba Serikali imelifahamu hili na inafanya hivi kwa umakini mkubwa sana na kuweza kukirudisha kiwanda hiki cha *General Tyre.*

Tunafahamu kwamba anaweza akaenda mahakamani lakini Serikali imejipanga vizuri na itazingatia sheria ambazo zipo kuweza kufanya kazi hii ya kuirudisha *General Tyre* na kufanya kazi ambayo inakusudiwa ya kuzalisha matairi hapa nchini.

Ukiangalia sana hatuna wasiwasi kwa sababu hisa za Serikali ni asilimia 74 na za huyu mbia mwenza ni asilimia 26. Kwa hiyo, msemaji mkuu katika hili ni Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la kuhusu kwamba endapo *General Tyre* itaanza kufanya kazi basi vijana waweze kushika nyadhifa katika kuendesha kiwanda hili. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli lakini tufahamu kwamba *NDC* itakapopata mwekezaji katika kiwanda hiki atatumia njia zilezile za kutangaza nafasi za kazi.

Niwashauri wale vijana na wengine ambao wataona wana sifa zmbazo zitakidhi kushika nyadhifa hizo basi waombe nafasi hizo. Si vijana tu ambao wana kisomo, bali hii itatoa fursa ya ajira kwa wengine wengi wa ngazi ya katikati na chini kabisa kuweza kupata nafasi ya kufanya kazi katika kiwanda chetu hiki.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kuna baadhi ya wabia wanajitoa, na kwa kuzingatia umuhimu wa *Public Private Partnership (PPP)* Serikali inachukua jukumu gani la kuhamasisha wawekezaji ili waingie ubia na Serikali badala ya ku-*pick* tu mwekezaji yoyote? Vilevile Serikali inatumia vigezo gani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba sasa hivi tumewapa shirika la maendeleo ya taifa *(NDC)* jukumu la kuweza kufufua kiwanda hiki na wenyewe ndiyo shirika hodhi ambalo linafanya hii kazi.

Nimesema kwamba mazungumzo ya awali kupitia wawekezaji mbalimbali wakiwemo wale wa China, *South Africa, Malaysia* hata na wengine ambao wanaona wana uwezo sasa hivi kwa kushirikiana na *NDC* kwa lengo la kutaka kufufua kiwanda hiki wote wanakaribishwa kwa utaratibu ule ule wa *PPP. (Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, atauliza swali hilo.

Na. 347

**Kupunguza Msongamano wa wafungwa nchini**

**MHE. MASOUD A. ABDALLAH** aliuliza:-

Kumekuwa na msongamano katika Magereza nchini karibu mara mbili ya idadi ya Wafungwa na Mahabusu kulingana na uwezo wa Magereza; na Mheshimiwa Rais amesema ili kukabiliana na tatizo hilo ni vyema kuwepo na Sheria ya adhabu mbadala ya makosa anayopatikana nayo mtu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada katika kupunguza msongamano wa Mahabusu na Wafungwa Magerezani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwezo wa magereza yetu ni kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,552 ambapo kwa sasa yanahifadhi wafungwa na mahabusu 38,000 kwa siku sawa na ongezeko la asilimia 28.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo sheria ya adhabu mbadala jitihada nyingine zinazochukuliwa na Serikali katika kupunguza msongamano huo ni pamoja na:-

- Kuharakisha upelelezi wa mashauri kwa kutenganisha upelelezi na uendeshaji wa mashtaka mahakamani.

- Kuongeza ajira ya watendaji kwa upande wa mahakama, upelelezi na waendesha mashtaka mahakamani.

- Kuanzishwa kwa jukwaa la haki jinai (*National Criminal Justice Forum*) chini ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kusimamia mfumo wa uendeshaji wa mashtaka na kuhakikishia kuwa kunakuwepo ushirikiano na vyombo vingine katika kushughulikia mashauri.

- Kuhimiza kufanyika kwa vikao vya kusukuma mashauri mahakamani (*Case Flow Management Committees*).

- Kukarabati na kupanua Magereza chakavu na ya zamani ili yaweze kuhifadhi wafungwa wengi zaidi,

- Kuendelea kuboresha usafirishaji wa mahabusu kutoka gerezani kwenda mahakamani katika mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya Wilaya za mkoa wa Pwani ili kesi zao zimalizike mapema. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD A. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Ni miezi sita (6) sasa tangu Mheshimiwa Rais apendekeze kuwepo kwa adhabu mbadala ili kupunguza msongamano wa wafungwa.

Pia ni dhahiri kwamba tunatumia bilioni 25 hadi 32 kwa huduma ya chakula na mahabusu na wafungwa hasa wengi wao wakiwa ni wale ambao wameiba mbuzi wanne (4) wakafungwa miaka mitano, ng'ombe watatu wakapewa kifungo cha miaka mitano(5);

Je, kwa kuwa tangu Mheshimiwa Rais apendekeze jambo hili imechukua muda. Serikali iko tayari sasa kuleta Muswada wa sheria ili kupunguza msongamano wa wafungwa sambamba na kuokoa fedha za umma?

(ii) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imebainika katika baadhi ya Magereza kuna mchanganyiko wa makusudi baina ya mahabusu watu wazima na watoto jambo ambalo mahabusu watoto wamekuwa wakilalamika kila siku kwamba wanafanyiwa vitendo viovu, vya kinyama kinyume na haki za binadamu.

Serikali hii ina kigugumizi gani tangu pale ambapo Waheshimiwa Wabunge tulipaza sauti zetu kwamba ni vyema mahabusu watu wazima watofautishwe na mahabusu watoto angalau kuondoa tatizo hili?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika,naomba nijibu swali lake la kwanza la umuhimu wa kuleta sheria Bungeni ili Bunge lipitishe haraka na kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Salim kwamba kwa sasa hatuna upungufu wa sheria, tunachohitaji ni kuzitendea kazi tu zilizopo. Kwa hiyo, tukihisi upungufu huo tutaleta mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kuhusu kuchanganya watu wazima na watoto. Si sera ya Serikali na wala si utaratibu wa kisheria.

Kwa hiyo, maeneo yote ambayo unatokea mchanganyiko huo haitokei kwa makusudi, ni jambo ambalo linafanyiwa kazi kwa karibu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalifanyia kazi kwa karibu sana kuhakikisha kwamba yale maeneo machache ambayo kuna tatizo hilo linatatuliwa.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kuwa msongamano mkubwa wa Magerezani unasababishwa na wafungwa wa muda mfupi na waliokosa dhamana kwa makosa madogo madogo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuagiza vyombo vinavyohusika hasa Mahakama kutoa dhamana kwa makosa hayo na kuwapa wafungwa wa muda mfupi adhabu za nje?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mustapha Akunaay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kwanza katika utaratibu wa sheria Serikali haina utaratibu wala kifungu cha sheria kinachoipa nafasi ya kuiagiza Mahakama.

Lakini lipo jukwaa la haki jinai ambapo vyombo vya sheria vinafanya kazi pamoja. Kwa kutumia vyombo hivi tutaendelea kufuatilia jambo alilolisema Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Na. 348

**Ahadi ya Umeme wa REA Mkoani Lindi**

**MHE. SAIDI M. MTANDA** aliuliza:-

Serikali kupitia Mamlaka ya Usambazaji Umeme Vijijini *(REA)* iliahidi kupeleka Umeme Mkoa wa Lindi katika kipindi cha Mwaka 2011/2012:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitengwa katika kukamilisha usambazaji wa umeme Mkoa wa Lindi?

(b) Je, ni lini maeneo ya vijiji vya Rutamba, Milola, Kitangale, Kitomanga, Mipingo na Kilolambwani yatapatiwa umeme?

(c) Je, ni fedha kiasi gani zitatumika kusambaza umeme katika vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa katika kukamilisha usambazaji wa umeme katika Mkoa wa Lindi ni jumla ya shilingi bilioni 3.3 kwa kipindi cha mwaka 2011/12, fedha hizi zinahusisha miradi ya umeme iliyoko maeneo ya Wilaya ya Ruangwa Vijijini, Kiwanja cha Ndege cha Lindi, Kijiji cha Dodoma

kilichopo Wilaya ya Ruangwa na eneo la Ugogoni B na Mianzini Voda Wilayani Nachingwea.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* kwenye Mpango Kabambe wa awamu ya pili (REA) itasambaza umeme katika vijiji vifuatavyo yaani vijiji vya Rutamba, Milola, Kilangala, Kitomanga, Mpingo na Kilolambwani, Kijiweni, na Nangalu. Miradi hii itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

(c) Mheshimiwa Spika, gharama za kutekeleza mradi katika vijiji hivyo ni shilingi bilioni 5.0 fedha hizo zitatolewa na Wakala wa Nishati Vijijini *(REA).*

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba maeneo ya kijiji cha Dodoma kule Ruangwa bado umeme haijaingia kama ambavyo majibu yake yanaonyesha hapa na *DC* wa Ruangwa ninaye hapa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nimwulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza je, maeneo kama kijiji cha Moka na Kikomolela ambayo yana idadi kubwa ya watu yatapitiwa na umeme kwa sababu mtandao huo wa umeme utaelekea Nangaru kupitia maeneo hayo ambayo hayamo kwenye program.

Je, sasa vijiji hivyo vitapatiwa umeme kwa sababu umeme hauwezi kufika kule Nangaru wakati vijiji hivi vinavyopita katikati havijapatiwa umeme.

Lakini swali la pili, kumekuwa na ucheleweshwaji mkubwa sana wa ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao wanatoa maeneo yao kupisha utandazaji wa hizi nguzo na miundombinu mbalimbali ya umeme katika mkoa wa Lindi. Tukichukua mfano wa Kijiji cha Manzese kilichopo Kilwa. Nauliza swali.

Je, Serikali sasa inawahakikishia wananchi wa vijiji hivi nilivyouliza katika swali langu la msingi kwamba watalipwa fidia yao kabla ya utekelezaji wa mradi huo wa umeme kuanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kusema mara zote hapa kwamba kwa stahili ya sasa kama umeme unaelekea katika uelekeo fulani haiwezekani na wala haina mantiki kama tutaruka maeneo ambayo tutajua yamechangamka na maeneo ambayo ya kiuzalishaji.

Kwa hivyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mtanda kwamba haiwezekani tukaruka na tutafanya marekebisho hayo haraka iwezekanavyo kwa miradi ambayo bado inaendelea.

Kwa hili la pili, kwamba kuna ucheleweshaji wa fidia. Niseme tu kwa vijiji vya Manzese, Kilwa na kwamba fidia italipwa lini. Nimesema mara nyingi hapa kwa miradi hiyo mingine mikubwa ambayo ina programu kubwa kubwa hiyo sawa tukizungumza fidia inaeleweka.

Lakini kwa miradi hii ya *REA* ambayo ni fedha kidogo ya Serikali ambayo inatengwa kwa ajili ya kuwapelekea wananchi umeme pamoja na haki ya msingi ya watu kufidiwa mali zao kama tu pale ambapo pengine ni nyumba inahusika au ni shamba lenye mazao ya kudumu, pengine inaweza ikawa na maana.

Lakini kwa kweli niseme kwa fedha kidogo iliyonayo Serikali sio rahisi sana na pengine nichukue nafasi hii kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge wale wenye nia ya dhati kwa miradi ambayo tumeisema na kwamba wananchi wao watawaeleweshwa na wakachangia au wakaionea huruma ili iweze kutekelezwa na Serikali miradi yao ya umeme na wanahitaji umeme watoe ushirikiano huo na sisi tuko tayari kupeleka miradi hiyo kuliko huko sehemu nyingine ambako wanahitaji fidia na sisi Serikali tukiwa hatuna fedha.

Lakini niseme tu kwamba suala la kulipa fidia ni suala tunalitambua, lakini kwa kweli kwa fedha tulizonazo sio rahisi sana tukaweza kwenda kwa kasi ya fidia pamoja na kutekeleza miradi yenyewe. *(Makofi)*

Na. 349

**Kuwanyang'anya Wananchi Rasilimali Zao Kwa Nguvu Bila Fidia**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU** aliuliza**:-**

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni unakataza Serikali za Nchi wanachama ikiwamo Tanzania kunyang'anya wananchi wao rasilimali zao bila kuwalipa fidia ya haki na timilifu.

Lakini pia Serikali za Nchi Wanachama zinatakiwa kuwapa wananchi wao ulinzi wa kisheria wa rasilimali na makazi dhidi ya vitendo vya kuwahamisha kwa nguvu kutoka kwenye maeneo yao kwa vitisho vingi na bila kuwalipa fidia kama ilivyotokea kwa wananchi wa eneo la Taru katika Kata ya Mang'onyi – Singida Mashariki na kuharibiwa kwa makazi, mali na vitendea kazi vyao ili eneo hilo litumiwe na Mwekezaji wa nje katika Sekta ya Madini:-

(a) Je, ni lini Serikali ya Tanzania itaanza kuheshimu na kutekeleza Sheria na Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Bindamu inayoridhiwa na Bunge?

(b) Je, Serikali inazo takwimu za wananchi walioondolewa kwa nguvu kwenye maeneo yao kwa ajili ya Wawekezaji wa Madini na athari za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni kwa waathirika kama wale wa Bulyanhulu na Lusu, Nzega mwaka 1996, Nyamongo –

Tarime Mwaka 2001 na Mang'onyi Singida Mwaka 2011?

(c) Je, ni wananchi waathirika wangapi wa matukio hayo wameshalipwa fidia timilifu na ya haki kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika Juu ya Haki za Binadamu na za Wananchi, 1981?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania imekuwa ikiheshimu na kutekeleza Sheria na Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Bindamu iliyoridhiwa na Bunge.

Serikali muda wote imekuwa makini katika kuhakikisha kuwa sheria zilizopo zinazingatiwa ikiwa ni pamoja na wakati wa kuhamisha wananchi wanaopisha shughuli za uchimbaji wa madini.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 95 cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010, lakini pia kifungu hicho hicho cha Sheria ya Mwaka 1998 kinamtaka mmiliki wa leseni yoyote ya madini kuheshimu eneo lolote linalomilikiwa na mtu au mamlaka yoyote. Ili eneo liweze kutumika kwa ajili ya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini ni lazima mmiliki wa eneo hilo atoe ridhaa kwa maandishi kwa mwenye leseni ya madini. Iwapo mmiliki wa eneo atatakiwa kupisha shughuli za

uchimbaji madini ni lazima uthamini wa mali katika eneo hilo ufanyike na fidia stahiki ilipwe kwa mhusika.

Aidha, mmiliki wa leseni ya madini anawajibika kutafuta eneo mbadala ambalo anayepisha ujenzi wa mgodi atahamia. Utaratibu huu umekuwa ukifanyika na utaendelea kufanyika kwa kuwa ni matakwa ya kisheria.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa makini katika kuhakikisha kuwa mwananchi yeyote mwenye kumiliki ardhi na mali zingine anafidiwa ipasavyo ili kupisha ujenzi wa migodi. Kwa wale ambao kwa mujibu wa sheria hawastahili kupata fidia kama ilivyo katika miradi mingine hutakiwa kuheshimu sheria na kuondoka katika eneo husika. Katika mazingira kama haya Serikali haiwezi kuweka takwimu kwa kuwa hawakai katika utaratibu wa kisheria wa kupata fidia.

(c) Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa kuheshimu sheria jumla ya familia 1,105 wameshalipwa fidia katika maeneo mbalimbali ya nchi ambayo migodi mikubwa na ya kati imeanzishwa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kama Serikali imekuwa makini katika kuhakikisha wananchi wanaostahili wanalipwa fidia. Je, kwa nini wananchi wa Kata ya Mang'onyi katika jimbo la Singida Mashariki hawajalipwa fidia mpaka sasa hivi wakati Tume ya Mkuu wa Mkoa wa Singida ilishaagiza

walipwe fidia tangu mwaka 2006 walipoondolewa kwenye maeneo yao ili kupisha mgodi wa *Shanta Mining.*

Suala la pili, kama katika migodi yote ambako wananchi wameondolewa ni watu 1,105 tu ambao wamelipwa fidia wakati kuna zaidi ya watu 500,000 wameondolewa katika maeneo hayo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kuna tatizo katika mfumo mzima wa fidia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwamba Kata ya Mang'onyi Tume ilishaagiza na iliagizwa kupitia Mkuu wa Mkoa kwamba walipwe. Tutafanya mawasiliano tuweze kuona hilo kwa nini halikutekelezwa.

Lakini la pili, migodi kwa mujibu wa takwimu zake anasema watu zaidi ya 500,000, lakini sisi tumewalipa watu 1,105. Takwimu alizozisema hapa sidhani kama ni *authentic.* Kwa hiyo, mpaka nizifanyie kazi tuweze kulinganisha tuone uwiano huu wa watu 1,105 unalinganishwaje na hiyo 500,000.

Baada ya kufanya hivyo ninaweza nikawa kwenye nafasi nzuri ya kuweza kujadiliana na Mheshimiwa Lissu, tuone wapi pametokea nini.

**SPIKA:** Wakati ukiwa umekwisha, umeisha tu. Kwa hiyo maswali yamekwisha na muda umeisha na naomba niwatambulishe wageni.

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni walioko ukumbini bado nina wale wageni wetu wa Tume kutoka Malawi bado wapo. Tutakuwa nao tena nawatambua wagen i wetu, wapo 10. *If they could stand where they are all of them The Parliament Service Commissioners of Malawi, if you can raise wherever you are please. Thank you.*

Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi yuko Katibu Mkuu Dkt. Charles Nyamrunda. Ahsante sana. Tunaye Naibu Katibu Mkuu Dkt. Yohana Budeba. Naomba asimame. Wako Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi, Mameneja wa Taasisi zilizoko chini ya Wizara hii naomba wote wasimame walipo. Ahsanteni sana. (*Makofi)*

Sasa nina wageni pia wa Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi Dkt. David Mathayo David, ambayo ni familia yake ikiongozwa na mke wake mpendwa anaitwa Mrs. Pamela David Mathayo na wote wasimame, ahsante sana. (*Makofi)*

Wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo ni wanachuo 100 kutoka Chuo cha Ualimu ambacho kinatiwa *Capital* cha Dodoma wenyewe wako *Basement.* Naona walikuwa wengi mno labda watapata nafasi mchana. Kuna wanafunzi 80 pamoja na walimu wao kutoka *Tetra School* - Arusha. Hawa wako wapi? Ahaa !! ahsante sana tena wadogo wadogo tu. Haya tumefurahi kuwaoneni ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 91 kutoka *University Computer Centre (UCC)* - Dodoma kituo cha Kompyuta. Wako wapi na wenyewe hawa *Computer Specialists.* Ahsante sana ninyi ni wenyeji wetu wakati wowote mahali pako wazi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna viongozi wa Elimu ya Juu TAHILISO ambao ni wageni wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii ikiongozwa na Ndugu Paul Makonda. Naomba hawa wageni wa TAHILISO wasimamie walipo au wamekosa nafasi kwa sasa. Ahsante watapata nafasi baadaye.

Ninao, eeh !!! hapa kuna orodha kubwa. Ninao wageni wa Waheshimiwa Wabunge nao ni makundi makubwa makubwa. Kuna wageni watatu, Waheshimiwa Wabunge wageni wenu wawe na sababu sio kuwataja majina tu maana inaleta shida hapa. Kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Namelock Sokoine naomba wasimame hapo walipo ambao ni Bwana Jafo Kaikanyi na Esther Labali Maleto. Ahsante sana, leo ni siku ya mifugo kwa hiyo hawa wamekuja rasmi mnajua tena. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa January Makamba, ambao ni uongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wasimame walipo. Tutakutana na nyinyi saa 5.00 asubuhi Ofisini kwangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, ambao ni Wachungaji 60 kutoka Wilaya ya Iramba wakiongozwa na Askofu Msaidizi Mstaafu Mchungaji Yohana Mujungu. Wako wapi hawa wote 60. Ahsante sana, karibuni sana Wachungaji.(*Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa John Shibuda, wakiongozwa na Peace Kaionza kutoka *AMREF.* Wako wapi wageni wa kutoka AMREF. Ahsante sana tunashukuru sana. *Makofi)*

Tuna wageni wanane wa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, ambao ni wafugaji wakiongozwa na Dkt. Mosses Ole-Nesele. Wako wapi. Ahsanteni sana leo ndio Wizara yenu kwa kweli. *(Makofi)*

Tuna wageni 10 wa Mheshimiwa Juma Njwayo ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango - Dodoma. Hawa wanafunzi 10 wako wapi. Ahsante sana tunaomba mkazane na kusoma. (*Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile na Mheshimiwa Abas Mtemvu ambao ni viongozi wa wasanii kutoka Temeke wakiongozwa na Fred Dile. Wenyewe hawa wasanii wako wapi? Wako wapi wale wasanii wa kutoka Temeke. Nafikiri watapata nafasi baadaye. *(Makofi)*

Halafu nina Dkt. Yusuph Lawi, Muadhiri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Yeye ni mgeni ameletwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu,

TAMISEMI Mheshimiwa Mwanri. *Doctor* yuko wapi ahsante sana karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ndio wageni tulionao. Sasa matangazo ya kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Mheshimiwa James Lembeli anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 5.00 asubuhi watakuwa na kikao katika chumba namba 225. Ni saa 5.00 kwa sababu kesho wanajiandaa kwa ajili ya Wizara inayofuata kwa hiyo nimewapa ruhusa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Andrew Chenge anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 5.00 pia wakutane katika chumba Na. 231. Hawa pia wanamalizia *Finance Bill*. Kwa hiyo *Finance Bill* kama kuna watu wanafikiri wanataka kushiriki pia mnaweza kwenda kule. Halafu nina tangazo kutoka kwa Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Cheyo anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake saa 7.15 mchana watakuwa na kikao chumba Na. 133.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii Mheshimiwa Margaret Sitta anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 watakuwa na kikao katika ukumbi wa Pius Msekwa B, kwa hiyo naomba sana tufanye hivyo.

Waheshimiwa baada ya hapo ninao wageni, kwa hiyo nitamwomba Mwenyekiti Mheshimiwa Jenista Mhagama aweze kuendelea na shughuli kwa siku ya leo.

*(Hapa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama Alikalia Kiti)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea naomba sasa nimwite Katibu tuendelee na hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa 2012/2013 Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

**MWENYEKITI:** Ahsante Katibu, Waheshimiwa Wabunge sasa tunaingia kwenye hoja ambayo iko katika ratibu yetu ya leo ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ili aweze kutusomea sasa hotuba ya Makadirio ya Bajeti yake.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, iliyochambua bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kupitisha taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka

2011/2012 na mwelekeo wa kazi za Wizara kwa mwaka 2012/2013.

Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza nchi yetu kwa busara na hekima ambayo imeendelea kuleta amani, utulivu na maendeleo.

Aidha, nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwa na imani nami kuongoza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kukupongeza wewe mwenyewe binafsi, kumpongeza Spika wa Bunge Mheshimiwa Anne S. Makinda Mbunge wa Njombe Kusina, Naibu Spika Mheshimiwa Job Ndugai Mbunge wa Kongwa, pamoja na Wenyeviti wa Bunge la

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, Mbunge wa Dole na Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala, kwa kusimamia vema shughuli za Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara mbalimbali. Aidha, naomba kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya walioteuliwa na Rais ambao ni Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vilevile, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliongia Bunge hili kupitia chaguzi ndogo ambao ni Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Jimbo la Igunga; Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Jimbo la Arumeru Mashariki na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Viti Maalum. Naahidi kushirikiana nao katika kutekeleza majukumu ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu; Hayati Mheshimiwa Mussa Hamis Silima aliyekuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Jeremia Solomon Sumari, aliyekuwa Mbunge wa Arumeru

Mashariki. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salaam za rambirambi kwa familia za marehemu, ndugu na wananchi waliokuwa wanawakilishwa na wabunge hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwakumbuka wananchi wenzetu waliopoteza maisha yao kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ajali za Meli za *Spice Islander* iliyotokea Nungwi *Bay* Zanzibar tarehe 10 Septemba, 2011 na *Mv Skagit* iliyotokea eneo la Chumbe Zanzibar tarehe 18 Julai, 2012, mafuriko na maafa mengine yaliyotokea hapa nchini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi, Amina. Vilevile, naomba kuwapa pole wananchi wenzetu waliopoteza makazi na mali zao kutokana na maafa mbalimbali.

Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kwa ushauri, maoni na ushirikiano wao mkubwa waliotupatia katika utekelezaji wa majukumu yetu ikiwa ni pamoja na maandalizi ya bajeti hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itazingatia ushauri, mapendekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu hii leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi kwa hotuba yake nzuri yenye kutoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi za Serikali kwa mwaka 2012/2013.

Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Uhusiano na Uratibu Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira, Mbunge wa Bunda kwa hotuba yake kuhusu hali ya uchumi wa nchi yetu na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, kwa hotuba yake kuhusu bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Mawaziri wote waliotangulia kwa hotuba zao ambazo zimeainisha maeneo mbalimbali tunayoshirikiana katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Vilevile, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao kuhusu masuala ya maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi kupitia hotuba zilizotangulia.

Napenda pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Same Magharibi kwa kuniamini na kuendelea kunipa ushirikiano katika kusimamia na kutekeleza majukumu

yangu na ninaahidi kushirikiana nao katika kuendeleza Jimbo letu. Vilevile, napenda kuishukuru familia yangu Mke wangu Pamela, Watoto wangu Cleopatra, Kelly, David Junior kwa kuendelea kunipa nguvu na kunitia moyo ninapoendelea kutekeleza majukumu ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Sekta za Mifugo na Uvuvi; sekta za mifugo na uvuvi zimeendelea kuwa muhimu katika kuwapatia wananchi ajira, kipato na lishe bora, hivyo kuchangia katika kumwondolea mwananchi umaskini. Aidha, sekta ya uvuvi ina fursa katika utalii rafiki wa mazingira *(eco-tourism*). Mafanikio katika sekta hizi ni muhimu katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Umaskini nchini (MKUKUTA II).

Mkakati huu unazingatia Dira ya Taifa 2025 na Malengo ya Kimataifa ya Kuondoa Umaskini *(Millenium Development Goals - MDGs).*

Katika mwaka 2011, sekta ya mifugo ilikua kwa asilimia 3.9 ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2010 na kuchangia asilimia 3.7 katika pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2010. Kupungua kwa mchango wa sekta ya mifugo kunatokana na kukua kwa sekta nyingine za kiuchumi nchini. Kulingana na takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2011, idadi ya mifugo nchini inafikia ng'ombe milioni 22.8, mbuzi milioni 15.6 na kondoo milioni 7.0. Pia,

wapo kuku wa asili milioni 35.5, kuku wa kisasa milioni 24.5 na nguruwe milioni 2.01.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulaji wa mazao ya mifugo kulingana na viwango vya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*, 2011) ni kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka. Kwa upande wa nchi yetu viwango vya ulaji wa mazao hayo kwa sasa ni wastani wa kilo 12 za nyama, lita 45 za maziwa na mayai 75 kwa mtu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina maeneo mengi ya uvuvi ikiwa ni pamoja na eneo la maji baridi linalojumuisha maziwa ya Ziwa Victoria (kilometa za mraba 35,088), Ziwa Tanganyika (kilometa za mraba 13,489), na Ziwa Nyasa (kilometa za mraba 5,700). Pia kuna maziwa ya kati na madogo 29, mabwawa 19,443, mito na maeneo oevu ambayo ni muhimu kwa uvuvi na ufugaji wa samaki.

Aidha, eneo la maji chumvi hujumuisha Ukanda wa Pwani wenye urefu wa kilometa 1,424 na upana wa maili za kwenye maji *(nautical miles*) 200. Eneo hilo la Bahari limegawanyika katika maji ya kitaifa *(Territorial Sea*) lenye kilometa za mraba zipatazo 64,000 na eneo la Ukanda wa Uchumi wa Bahari *(Exclusive Economic* Zone - EEZ) lenye kilometa za mraba zipatazo 223,000,

eneo hilo linaweza kutumika kwa uvuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utafiti uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), kiasi cha samaki kilichopo katika maziwa makuu ni wastani wa tani 1,490,338 (Ziwa Victoria tani 1,027,338, Ziwa Tanganyika tani 295,000 na Ziwa Nyasa tani 168,000).

Pia, utafiti uliofanywa na Tume ya Umoja wa Mataifa ya Uchumi kwa Afrika (*United Nations Economic Commission for Africa - UNECA),* katika ukanda wa pwani kuhusu ufugaji viumbe kwenye maji ulionesha kuwa, kuna maeneo sehemu za Tanga, Bagamoyo na Mtwara ambayo kwa pamoja yana ukubwa wa hekta 3,000 na yanaweza kuzalisha tani 11,000 za kambamiti kwa mwaka.

Aidha, katika mwaka 2011, sekta ya uvuvi ilichangia asilimia 1.6 katika pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 1.4 mwaka 2010 na kukua kwa asilimia 1.2 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2010. Kiwango kidogo cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa ushindani wa mauzo ya samaki na mazao yake nje ya nchi; kupungua kwa kasi ya uvuvi, hususan katika maji baridi uliotokana na kudhibiti uvuaji holela na uharibifu wa mazingira katika mazalia ya samaki; vitendo vya uvuvi haramu; na matumizi ya zana duni za uvuvi.

Aidha, kutokana na taarifa ya *FAO* ya mwaka 2011, ulaji wa mazao ya uvuvi nchini kwa mtu kwa mwaka ni kilo 8.0 ikilinganishwa na kilo 16.7 zinazopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta za mifugo na uvuvi katika mwaka 2011/2012 zimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuongeza uwekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi ili kuongeza uzalishaji, tija na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi;

(ii) Upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa ufugaji na uvuvi;

(iii) Kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi;

(iv) Kuainisha, kupima, kumilikisha na kuendeleza maeneo ya ufugaji endelevu ili kudhibiti kuhamahama, kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, kupunguza uharibifu wa mazingira na kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo;

(v) Kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mifugo, hususan ya mlipuko;

(vi) Upatikanaji wa elimu na teknolojia pamoja na matumizi ya teknolojia sahihi kwa ufugaji na uvuvi endelevu;

(vii) Upatikanaji wa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi;

(viii) Upatikanaji wa pembejeo na zana za gharama nafuu kwa ajili ya ufugaji na uvuvi;

(ix) Kuwa na wataalam wa kutosha kukidhi mahitaji ya sekta za mifugo na uvuvi; na

(x) Kuwa na rasilimali fedha ya kutosha kukidhi mahitaji ya sekta za mifugo na uvuvi.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, Wizara imeandaa na kuanza kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo *(Livestock Sector Development Programme)* na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi *(Fisheries Sector Development Programme)* ambazo zimeainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2011/2012 na Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka 2012/2013; Ukusanyaji wa Mapato; katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 22,475,299,785.

Kati ya hizo, shilingi 9,435,738,377 (42%) ni kutoka sekta ya mifugo na shilingi 13,039,561,408 (58%) ni kutoka sekta ya uvuvi. Hadi tarehe 30 Juni, 2012 jumla ya shilingi 17,025,384,378.72 zilikusanywa ikiwa ni asilimia 75.8 ya lengo la makusanyo. Katika mwaka

2012/2013, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 18,657,050,000.00. Kati ya hizo, shilingi 8,499,861,000.00 zitatoka kwenye Sekta ya Mifugo na shilingi 10,157,189,000.00 zitatoka kwenye Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Fedha; katika mwaka 2011/2012 Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 59,461,601,606.66. Kati ya hizo, shilingi 38,607,918,606.66 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 20,853,683,000.00 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi 20,862,841,587.66 ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (*OC*) na shilingi 17,745,077,019.00 ni kwa ajili ya mishahara (*PE*) ya Wizara. Vilevile, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo, shilingi 4,358,694,000.00 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi 16,494,989,000.00 fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012, jumla ya shilingi 43,209,871,764.82 zimetolewa (sawa na asilimia 72.7). Kati ya hizo, shilingi 32,426,557,620.82 (sawa na asilimia 84) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo shilingi 32,358,057,620.82 (sawa na asilimia 99.8) zilitumika na shilingi 10,783,314,144.00 (sawa na asilimia 51.7) zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi 10,627,779,729.36 zilitumika (sawa na asilimia 98.6).

Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi 17,745,077,019.00 zilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi 14,681,480,601.82 kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC). Kati ya fedha za maendeleo, fedha za ndani ni

shilingi 2,481,953,000.00 na shilingi 8,301,361,144.00 ni za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubunifu na Utekelezaji wa Sera na Sheria za Sekta, katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kusambaza na kutoa elimu kwa wadau kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006. Jumla ya nakala 2,500 za Sera ya Taifa ya Mifugo na nakala 1,500 za Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati (1997) zimesambazwa kwa wadau mbalimbali.

Aidha, Wizara imechapisha nakala 250 za Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo wa mwaka 2011 na kusambazwa kwa wadau. Pia, elimu kwa wadau imeendelea kutolewa kupitia matukio mbalimbali ya kitaifa pamoja na mikutano mbalimbali ya kitaaluma na ya wadau yakiwemo Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru, Sikukuu ya Nanenane na Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kusambaza na kutoa elimu kwa wadau kuhusu sera za sekta ya mifugo na uvuvi. Aidha, itakamilisha kutafsiri Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo (2011) katika lugha ya Kiswahili ambapo nakala 5,000 zitasambazwa kwa wadau kwa ajili ya utekelezaji. Vilevile, itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati (1997) na kuandaa Mkakati wa kutekeleza Sera hiyo na kuisambaza kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta, imeendelea kuandaa na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya sheria za sekta za mifugo na uvuvi. Katika mwaka 2011/2012, Sheria ya

kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania *(Tanzania Livestock Research Institute Act)* imepitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2012.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa mapendekezo ya kutunga na kurekebisha Sheria zifuatazo:-

(i) Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu *(The Marine Parks and Reserves Act )* Na. 29 ya mwaka 1994;

(ii) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(The Tanzania Fisheries Research Institute Act) Na. 6* ya mwaka 1980; na

(iii) Sheria ya Uzalishaji wa Mbari Bora ya Wanyama *(Animal Breeding Act).* Vilevile, katika mwaka 2011/2012, Wizara imeandaa kanuni mbalimbali za kutekeleza sheria za mifugo ambazo ni:-

(i) Kanuni nne (4) chini ya Sheria ya Veterinari Na. 16 ya mwaka 2003 na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali GN Na. 357, 358, 359 na 360; na

(ii) Kanuni chini ya Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010 na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali GN Na. 362. Pia, Wizara imefanya tafsiri ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 katika lugha ya Kiswahili na rasimu kuwasilishwa kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa hatua zaidi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau itakamilisha sheria zilizoainishwa hapo juu na kuandaa

kanuni mbalimbali za kutekeleza sheria za sekta za mifugo na uvuvi.

Aidha, itaandaa tafsiri ya Kiswahili ya Sheria Na. 13 ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendelezaji wa Sekta ya Mifugo; Mifugo na Mazao yake. Zao la Maziwa:

Tasnia ya maziwa imeendelea kukua katika maeneo ya uzalishaji, ukusanyaji, usindikaji na masoko ya maziwa. Uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita bilioni 1.74 mwaka 2010/2011 hadi lita bilioni 1.85 mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 6. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa idadi ya ng'ombe wa maziwa pamoja na kuboreshwa kwa mfumo wa ukusanyaji wa maziwa. Kutokana na ongezeko hili, unywaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita 44 kwa mtu kwa mwaka 2010/2011 hadi lita 45 kwa mtu kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuboresha mashamba ya kuzalisha mifugo ili kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo ya asili.

Katika mwaka 2011/2012, jumla ya mitamba 789 ilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji, sawa na ongezeko la asilimia 9.8 ikilinganishwa na mitamba 712 iliyozalishwa mwaka 2010/2011 Katika kuimarisha uzalishaji wa mitamba bora, Wizara imenununua ng'ombe wazazi 65 kwa ajili ya mashamba ya

Ngerengere (30) na Sao Hill (35), na madume bora 21 ya ng'ombe wa mbegu kwa ajili ya mashamba ya Kitulo (*Friesian*, 12), Nangaramo (*Friesian*, 5) na Sao Hill (*Ayrshire*, 2 na Boran 2). Pia, imenunua vifaa vya uhimilishaji na kukarabati miundombinu ya mashamba ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo ya maji, barabara na njia za kuzuia moto. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mifugo bora ikiwa ni pamoja na kununua mifugo wazazi na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (*NAIC*-Arusha) na vituo vitano (5) vya kanda vya Dodoma, Kibaha, Lindi, Mbeya na Mwanza ili kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya dozi 172,000 za mbegu bora zimezalishwa ikilinganishwa na dozi 150,000 zilizozalishwa mwaka 2010/2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.8.

Pia, jumla ya ng'ombe 81,300 walihimilishwa ikilinganishwa na ng'ombe 76,800 waliohimilishwa mwaka 2010/2011. Vilevile, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kuzalisha lita 39,150 za kimiminika cha naitrojeni (*Liquid Nitrogen*); kuanzisha vituo vidogo viwili vya uhimilishaji vya Tabora na Tanga; kufundisha wataalam 105 wa uhimilishaji kutoka maeneo mbalimbali nchini na kununua madume bora 10 kutoka Kenya kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora.

Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuboresha vituo vyake vya uhimilishaji kwa kuimarisha miundombinu na kuviongezea vitendea kazi; kuzalisha dozi 185,000 za mbegu bora za uhimilishaji; kufundisha wataalam 120 wa uhimilishaji kutoka kwenye maeneo mbalimbali nchini na kujenga vituo vya uhimilishaji vya Mpanda na Sao Hill (Mufindi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la Nyama. Wizara imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa nyama katika maeneo mbalimbali nchini. Katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa nyama umeongezeka kwa asilimia 5.7 kutoka tani 503,496 mwaka 2010/2011 hadi tani 533,711 mwaka 2011/2012. Kati ya hizi, nyama ya ng'ombe ni tani 289,835, mbuzi na kondoo tani 111,106, nguruwe tani 47,246 na kuku tani 84,524. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo kutokana na ongezeko la idadi ya walaji na kupanuka kwa wigo wa soko la nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara imehamasisha wafugaji na wafanyabiashara kunenepesha mifugo, ambapo jumla ya ng'ombe 132,246 walinenepeshwa katika mikoa mbalimbali ikilinganishwa na ng'ombe 98,700 mwaka 2010/2011. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na UNIDO imeandaa Programu ya Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Nyama Nyekundu (Red Meat *Value Chain Development Programme)* inayotekelezwa katika mikoa ya Morogoro, Iringa na Mbeya kwa ufadhili wa *UNIDO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuhamasisha wafugaji na wafanyabiashara ya mifugo kunenepesha mifugo. Aidha, Mpango wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Nyama Nyekundu utawezesha ujenzi wa machinjio bora mbili (2) za mfano zenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 80 hadi 100 kwa siku katika Jiji la Mbeya na Manispaa ya Iringa na kusimika vifaa vya kuchinjia, kupoza na kusindika nyama.

Pia, karo bora mbili (2) za mfano zenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 5 hadi 10 kwa siku zitajengwa katika Halmashauri za Wilaya za Iringa na Mbeya. Vilevile, mafunzo ya kiufundi na kibiashara yatatolewa kwa wanenepeshaji wa mifugo, wachinjaji na wauzaji wa nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, jumla ya vifaranga milioni 41.9 vya kuku wa nyama na mayai vilizalishwa nchini ikilinganishwa na vifaranga milioni 38.4 mwaka 2010/2011. Pia, vifaranga 330,000 vya kuku wazazi wa mayai na mayai milioni 8.2 ya kutotolesha vifaranga yaliingizwa nchini ikilinganishwa na vifaranga 251,503 na mayai milioni 6.03 mwaka 2010/2011. Vilevile, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka bilioni 3.34 mwaka 2010/2011 hadi mayai bilioni 3.5 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kuhamasisha ufugaji wa kuku wa asili, Wizara kwa kushirikiana na wadau zikiwemo asasi za Building *Resources Across Communities (BRAC)* na *Rural*

*Livelihood Development Company (RLDC)* imeendelea kuhamasisha ufugaji bora wa kuku wa asili kwa kuboresha mazingira ya ufugaji, ulishaji, utunzaji wa vifaranga na udhibiti wa magonjwa.

Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha Chama cha Wadau wa Tasnia ya Kuku *(Tanzania Poultry Breeders Association)* kwa kuwajengea uwezo katika nyanja za ujasiriamali, usimamizi na uendeshaji wa vikundi.

Katika mwaka wa 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuhamasisha ufugaji wa kuku wa asili kibiashara kwa kuhamasisha teknolojia rahisi ya kutotolesha, kulea vifaranga, kudhibiti magonjwa na kuimarisha mfumo wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa nyama ya nguruwe umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kuongezeka kwa ulaji. Katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa nyama ya nguruwe umeongezeka kutoka tani 43,647 mwaka 2010/2011 hadi tani 47,246 sawa na ongezeko la asilimia 8.2. Ili kuboresha kosaafu za nguruwe, Wizara imeendelea kuimarisha shamba la Kuzalisha Mifugo la Ngerengere kwa kulipatia madume yenye kosaafu bora.

Aidha, tafiti za kuanzisha teknolojia sahihi za kuongeza uzalishaji wa nguruwe zinaendelea katika vituo vya utafiti. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuimarisha shamba la Kuzalisha Mifugo la Ngerengere kwa kulipatia madume yenye kosaafu bora kwa lengo la kuzalisha na kusambaza nguruwe

bora kwa wafugaji. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ufugaji wa nguruwe bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendelezaji wa Zao la Nyama katika Kampuni ya Ranchi za Taifa *(National Ranching Company - NARCO); Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)* imeendelea kuzalisha, kunenepesha na kuuza mifugo kwa ajili ya nyama. Kampuni ina ranchi 10 za mfano za Kikulula, Kagoma, na Missenyi (Kagera), Kongwa (Dodoma), Mzeri (Tanga), Ruvu (Pwani), Mkata (Morogoro), Kalambo (Rukwa) na West Kilimanjaro (Kilimanjaro). Ranchi hizo kwa pamoja zina jumla ya hekta 230,384 zenye uwezo wa kuweka ng'ombe kati ya 80,000 na 90,000. Kwa sasa, Kampuni ina jumla ya ng'ombe 26,236, kondoo 1,580, mbuzi 685, farasi 43 na punda 50. Aidha, Kampuni inatoa ushauri kuhusu ufugaji bora kwa wafugaji wanaozunguka ranchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, *NARCO* imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuzalisha na kukuza ndama 6,286 kutokana na ng'ombe wazazi 9,347 sawa na asilimia 67 ya malengo ya uzalishaji;

(ii) Kuuza ng'ombe 9,147 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.5 wakiwemo walionunuliwa chini ya Programu ya Unenepeshaji 1,327, walionunuliwa na *NARCO* na kunenepeshwa 407 na waliozaliwa na kukuzwa katika ranchi za *NARCO* 7,413;

(iii) Kununua ng'ombe 5,530 kutoka kwa wafugaji wanaozunguka maeneo ya ranchi kwa ajili ya programu ya unenepeshaji;

(iv) Kuendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa katika Ranchi ya Ruvu ambao umefikia asilimia 50;

(v) Kutoa hati miliki ndogo *(sub-lease)* 19 na kufikia idadi ya hati miliki ndogo 75 kati ya 104 zinazotakiwa kutolewa;

(vi) Kusimamia na kutoa ushauri wa ufugaji bora kwa wawekezaji wazalendo 213 ambao wamemilikishwa vitalu ndani ya Ranchi za Taifa, ambapo ranchi hizo zimewekeza ng'ombe 54,300, mbuzi 4,400 na kondoo 1,800; na

(vii) Kuendelea na majadiliano na wawekezaji watatu (3) walioonyesha nia ya kuwekeza katika Ranchi ya West Kilimanjaro baada ya mgogoro wa ardhi kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, *NARCO* itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuzalisha na kukuza ndama 6,714 kutokana na ng'ombe wazazi 8,997 walioko kwenye ranchi za *NARCO;*

(ii) Kuendelea na ujenzi wa machinjio katika Ranchi ya Ruvu ambao ulisimama kwa muda kutokana na kuchelewa kukamilika kwa michoro, na hivyo kuilazimu

Kampuni kuvunja mkataba. Kampuni imetangaza upya zabuni ya kutafuta Mshauri Mwelekezi wa kusimamia ujenzi na hatimaye kupata Mkandarasi mpya ambapo Benki ya Rasilimali (TIB) imekubali kugharimia mradi huo;

(iii) Kuuza ng'ombe 15,056 watakaokuwa na thamani ya takriban shilingi bilioni 7.5 wakiwemo 6,600 watakaonunuliwa chini ya programu ya unenepeshaji, 2,550 watakaonunuliwa na fedha ya *NARCO* kutoka kwa wafugaji wanaozunguka maeneo ya ranchi na 5,906 watakaozaliwa na kukuzwa katika Ranchi za *NARCO;*

(iv) Kusimamia na kushauri kuhusu ufugaji bora katika ranchi ndogo zilizomilikishwa kwa wawekezaji watanzania;

(v) Kuzalisha ng'ombe bora wa nyama kwa kutumia teknolojia zilizokubalika kwa kushirikiana na SUA chini ya ufadhili wa *COSTECH;* na

(vi) Kuendelea kutafuta wawekezaji ili waingie ubia na *NARCO* katika masuala ya mifugo katika ranchi nyingine saba (7) zilizobaki.

Utatuzi wa Migogoro katika Vitalu vya Ranchi za *NARCO* Mkoani Kagera; Wizara imeendelea kuhimiza sekta binafsi kuwekeza katika ufugaji wa kisasa na kibiashara. Katika kutekeleza azma hii, Serikali iliamua kugawa baadhi ya maeneo ya ranchi za *NARCO* kwa wawekezaji binafsi. Katika mkoa wa Kagera, wawekezaji binafsi 41 walipatiwa vitalu katika ranchi za Missenyi, Kagoma, Kikulula na Mabale.

Aidha, jumla ya vitalu 14 viligawiwa kwa vijiji vikiwemo vitalu (9) kutoka ranchi ya Missenyi, Kagoma (1), Kikulula (2) na Kitengule (2). Pamoja na nia nzuri ya Serikali, kumekuwa na migogoro mingi katika vitalu vya wawekezaji binafsi kutokana na kuvamiwa na wananchi na wavamizi kutoka nchi jirani hususan katika ranchi za *NARCO* mkoani Kagera.

Kutokana na hali hiyo, Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Kagera iliunda Kamati iliyoshirikisha watalaam wa Wizara, *NARCO* na Ofisi ya Mkoa wa Kagera; na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera kwa ajili ya kubaini vyanzo vya migogoro katika ranchi na kutoa mapendekezo mbalimbali yatakayowezesha kupunguza matatizo haya.

Mapendekezo hayo ni pamoja na kuhakiki uraia wa wawekezaji na wanavijiji wanaozunguka maeneo ya ranchi na kuondoa baadhi ya vitalu kutoka kwa wawekezaji kwa ajili ya matumizi ya Taasisi za Umma na wananchi wanaoishi maeneo hayo kwa ajili ya ufugaji wa kisasa na wa kibiashara. Kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati, Serikali katika ranchi ya Missenyi imedhamiria kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuvirudisha Serikalini vitalu Na. 287/1, Na. 287/3 na Na. 287/7 ambavyo vimekuwa na migogoro ya muda mrefu kutokana na kuvamiwa na wafugaji na mifugo yao kutoka nchi jirani. Vitalu hivyo vitatolewa kwa Taasisi za Umma. Wawekezaji waliokuwepo katika vitalu hivyo watagawiwa maeneo mbadala yanayomilikiwa na *NARCO;*

(ii) Kubadilishiwa kitalu Na. 287/3 kinachomilikiwa na kikundi cha kinamama ambao wamekuwa wakiathirika na migogoro ya uvamizi wa mara kwa mara na kugawiwa sehemu ya kitalu Na. 287/6;

(iii) Kumwagiza mwekezaji mwenye kitalu Na. 287/6 kuanza uwekezaji kwa kuwa hali ya usalama itakuwa imeimarika; na

(iv) Suala la kitalu Na. 287/11 liko mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ranchi ya Kagoma kutokana na kuwa na huduma za kijamii zikiwemo shule na hospitali, Wizara imedhamiria kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kugawa vitalu Na. 291/3 na Na. 291/9 kwa ajili ya matumizi ya kijiji cha Rutolo na wawekezaji katika vitalu hivyo watapewa maeneo mbadala katika ranchi hiyo;

(ii) Kuwahamisha wananchi waliovamia kitalu Na. 291/1 na kwenda katika vitalu Na. 291/3 na Na. 291/9; na

(iii) Kufanya tathmini katika vitalu Na. 291/6, 291/7, 291/8, 291/10, 291/11, 291/12, 291/13 na 291/14 ili kubaini idadi ya kaya zilizovamia vitalu vya wawekezaji. Baada ya tathmini hiyo kukamilika wanavijiji na wawekezaji hao watapangwa upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Serikali kuwa hatua hizi zitawezesha kuwepo kwa amani, utulivu na matumizi endelevu ya rasilimali katika maeneo hayo. Naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa maeneo hayo ambao walishiriki kubaini vyanzo vya migogoro hiyo na kutoa mapendekezo ambayo Serikali itayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya mifugo na mazao yake. Biashara ya mifugo na mazao yake imeendelea kuongezeka ndani na nje ya nchi kutokana na kuimarishwa kwa huduma za mifugo na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama katika miji na masoko maalum. Katika mwaka 2011/2012, idadi ya mifugo iliyouzwa minadani imeongezeka kutoka ng'ombe 925,097, mbuzi 704,987 na kondoo 168,313 yenye thamani ya shilingi bilioni 423.9 mwaka 2010/2011 hadi kufikia ng'ombe 1,015,067, mbuzi 771,967 na kondoo 179,289 wenye thamani ya shilingi bilioni 775.4. Aidha, mifugo iliyouzwa nchi za nje (Comoro, Zambia na Kongo) iliongezeka kutoka ng'ombe 1,041 na mbuzi 657 wenye thamani ya shilingi milioni 965.4 mwaka 2010/2011 hadi ng'ombe 3,362 na mbuzi/kondoo 4,060 wenye thamani ya shilingi bilioni 3.81 mwaka 2011/2012. Vilevile, tani 31.6 za nyama ya ng'ombe, 647 za mbuzi na 151.8 za kondoo ziliuzwa nje ya nchi zikiwa na thamani ya shilingi bilioni 19.3 ikilinganishwa na tani 20.3 za nyama ya ng'ombe, 286 za mbuzi na 97 za kondoo zenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, ukusanyaji wa ngozi uliongezeka kwa asilimia 25.5

ambapo jumla ya vipande vya ngozi za ng'ombe milioni 2.8, mbuzi milioni 3.4 na kondoo 650,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 33 vilikusanywa ikilinganishwa na vipande milioni 2.5 vya ngozi za ng'ombe, milioni 2.4 vya mbuzi na 200,000 vya kondoo vyenye thamani ya shilingi bilioni 16.1 mwaka 2010/2011. Aidha, jumla ya vipande vya ngozi ghafi za ng'ombe milioni 2.0, mbuzi milioni 2.9 na kondoo 578,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 17.5 viliuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhamasishaji wa kusindika ngozi humu nchini kumekuwa na mwitikio mkubwa kutoka kwa wafanyabiashara kuongeza usindikaji. Katika mwaka 2011/2012, ngozi zilizosindikwa zimeongezeka kwa asilimia 49.8 kutoka vipande 782,447 vya ng'ombe, milioni 1.5 vya mbuzi na 61,200 vya kondoo vyenye thamani ya shilingi bilioni 10.6 hadi vipande milioni 1.0 vya ng'ombe, milioni 3.0 vya mbuzi na 600,000 vya kondoo vyenye thamani ya shilingi bilioni 62.3 vilisindikwa na kuuzwa nje ya nchi kwa thamani ya shilingi bilioni 77.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kusimamia na kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Halmashauri 65 na Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania. Kazi zilizotekelezwa ni:-

(i) Kutoa mafunzo kwa wagani 1,300 kuhusu mnyororo wa thamani wa zao la ngozi;

(ii) Kutoa mafunzo kwa wadau 10,399, wakiwemo wachinjaji/wachunaji 5,879, wawambaji na wachambuzi wa madaraja 715, wasindikaji 65, wafanyabiashara 874 na wafugaji 2,866;

(iii) Kuwezesha uendeshaji wa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ngozi ili iweze kutekeleza majukumu yake;

(iv) Kuendelea na mchakato wa kuanzisha Chama cha Wazalishaji wa Ngozi nchini ambacho kitasimamia maslahi ya wazalishaji wa ngozi wakiwemo wafugaji, wachinjaji na wakusanyaji wa ngozi katika halmashauri zote nchini;

(v) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ngozi na kanuni zake; na

(vi) Kusimamia ulipaji wa ushuru wa ngozi ghafi zinazouzwa nje ya nchi kwa lengo la kuwezesha ngozi zote ghafi kusindikwa nchini. Kamati maalum imeanzishwa ili kuchambua nyaraka za wafanyabiashara wa ngozi kwa lengo la kudhibiti mianya ya ukwepaji wa kulipa ushuru kabla ya kuuza ngozi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutekeleza mkakati huu na kusimamia ulipaji wa ushuru wa ngozi ghafi zinazouzwa nje ya nchi kwa lengo la kuwezesha ngozi zote ghafi kusindikwa nchini, kujenga vituo maalum sita

(6) vya kutolea mafunzo ya uendelezaji wa zao la ngozi, kutoa mafunzo kwa wadau kuhusu uzalishaji, uhifadhi na usindikaji wa ngozi unaozingatia hifadhi ya mazingira na kukamilisha mchakato wa kuanzisha Chama cha Wazalishaji wa Ngozi nchini ambacho kitasimamia maslahi ya wazalishaji wa ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa minada ya upili na matumizi ya mizani. Wizara imeendelea kuhamasisha biashara ya mifugo kwa kusisitiza matumizi ya mizani kwenye minada, kuikarabati minada ya upili na kujenga minada mipya. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukamilisha usimikaji wa mizani kwenye minada ya Igunga, Pugu, Mhunze (Kishapu) na Meserani (Monduli);

(ii) Kununua mizani minne (4) ya kupimia uzito wa mifugo katika minada ya Nyamatala (Misungwi), Weruweru (Hai), Kizota (Manispaa ya Dodoma) na Ipuli (Tabora);

(iii) Kusambaza Waraka wa Matumizi ya Mizani kwenye Minada;

(iv) Kusambaza Mwongozo wa Masoko ya Mifugo wa Matumizi Bora na Utunzaji wa Miundombinu ya Minada;

(v) Kuendeleza ujenzi wa mnada wa Nyamatala (Misungwi) na kukarabati mnada wa Pugu kwa kuweka mfumo wa maji;

(vi) Kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za masoko ya mifugo kutoka minada 53 iliyounganishwa na mtandao wa *LINKS*; na

(vii) Kuhamasisha ukusanyaji wa maduhuli katika minada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendeleza ujenzi wa mnada wa Kirumi na kuanza maandalizi ya ujenzi wa minada ya Muyama (Buhigwe - Kigoma) na Longido. Aidha, Wizara itakarabati minada ya upili mitano (5) ya Pugu, Meserani, Igunga, Kizota na Mhunze. Pia, Wizara itanunua mizani minne (4) ya kupimia mifugo minadani ambayo itasimikwa katika minada ya Sekenke (Iramba), Lumecha (Songea) na minada ya mbuzi ya Kizota (Dodoma) na Pugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya kusindika mazao ya mifugo. Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ili kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika ujenzi na ukarabati wa machinjio za kisasa na viwanda vya kusindika maziwa na ngozi. Mazingira hayo ni pamoja na kuondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vya kusindika na kukusanyia maziwa, vyombo vya kubebea maziwa, vifungashio na ushuru wa kuingiza magari ya kupoza na kusafirisha maziwa na nyama. Hatua hii imewezesha kuanzishwa kwa viwanda vipya vya maziwa vya Kilimanjaro *Creameries* (Siha) na *Ayalabe Cooperative Society* (Karatu). Aidha, kiwanda cha *Tanga Fresh* kimeongeza ukusanyaji wa maziwa kutoka lita 30,000 hadi 40,000

kwa siku ambapo lita 10,000 ni kutoka kwenye maeneo mapya ya Chalinze (Bagamoyo), Kimamba na Dumila (Kilosa). Vilevile, kupitia miradi ya *DADPs* vituo 18 vya kukusanyia maziwa vimejengwa katika Mikoa ya Arusha (4), Mara (3), Tanga (3), Iringa (2), Manyara (2), Kilimanjaro (1), Morogoro (1), Rukwa (1), na Mwanza (1). Kutokana na hatua hizo, usindikaji wa maziwa umeongezeka na kufikia lita 130,400 kwa siku sawa na asilimia 15.7 ikilinganishwa na mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza na kuongeza usindikaji wa maziwa. Aidha, Wizara itaandaa Mpango wa Uwekezaji kwenye Tasnia ya Maziwa *(Tanzania Dairy Investment Plan*) kupitia Mradi wa Maziwa wa Afrika ya Mashariki Awamu ya Pili *(East Africa Dairy Development – EADD II)* unaofadhiliwa na *Bill and Melinda Gates Foundation (BMGF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa nyama, uwekezaji katika ujenzi wa machinjio ya Manyara Ranchi (Monduli) na Orpul (Simanjiro) umefanyika. Ukarabati wa Kiwanda cha Kusindika Nyama cha Shinyanga kilichobinafsishwa kwa Kampuni ya *Triple S* unaendelea baada ya kupata mkopo kutoka Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*). Ukarabati uliofanyika ni pamoja na kujenga uzio kuzunguka machinjio, mfumo wa maji, umeme, sakafu na kuta. Ubinafsishaji wa kiwanda cha nyama Mbeya unaendelea na zabuni imetangazwa mwezi Juni na Julai, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha viwanda vya ngozi vya ndani vinapata ngozi za kutosha, katika mwaka 2012/2013, Serikali imepandisha ushuru wa ngozi ghafi zinazouzwa nje ya nchi kutoka asilimia 40 au shilingi 400 kwa kilo hadi asilimia 90 au shilingi 900 kwa kilo kutegemea ipi ni kubwa. Hatua hii imelenga kuviwezesha viwanda vya ngozi hapa nchini kukabiliana na ushindani wa wafanyabiashara wa ngozi ghafi na hivyo kuongeza usindikaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa malisho na mbegu. Wizara imeendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mbegu bora za malisho kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kuboresha maeneo yanayoendelea kutengwa kwa ajili ya ufugaji. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya tani 45 za mbegu aina mbalimbali na marobota 403,604 ya hei yalizalishwa katika mashamba 11 ya Serikali. Aidha, sekta binafsi ilizalisha jumla ya tani 50 za mbegu za malisho na marobota 500,000 ya hei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba haya kwa kuyapatia vitendea kazi muhimu ili yaweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Pia, itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu za malisho na hei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia mradi wa Matumizi Endelevu ya Nyanda za Malisho *(Sustainable Rangeland Management Project - SRMP)* uliotekelezwa katika Wilaya za Kiteto, Bahi, Chamwino na Kondoa, ilitoa mafunzo kwa wafugaji 1,270 juu ya uandaaji wa

Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, usimamizi wa ardhi ya ufugaji na haki za makundi mbalimbali ya raia katika kutumia ardhi. Asasi zinazotekeleza mradi huu ni pamoja na *DONET*- (Kondoa), BAENET (Bahi), KINNAPA (Kiteto) na MMC (Chamwino). Aidha, mafunzo ya aina hiyo yalitolewa kwa wataalam 22 wa Nyanda za Malisho kutoka Halmashauri 20 za Mikoa ya Shinyanga, Mara, Mwanza na Kagera. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itahimiza Halmashauri kujumuisha kazi zilizokuwa chini ya mradi katika mipango yao na kuzitekeleza. Pia, itatoa elimu ya matumizi bora ya ardhi kwa Halmashauri 10 katika Mikoa ya Katavi, Rukwa, Morogoro, Tabora na Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa rasilimali za ardhi, maji na malisho ya mifugo. Migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini imeendelea kujitokeza katika maeneo mbalimbali. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika; na Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilishiriki katika utatuzi wa migogoro katika Halmashauri za Igunga, Meatu, Kilosa, Kilombero, Mvomero na Rufiji (Ikwiriri). Halmashauri husika katika maeneo hayo, zimeagizwa kutenga maeneo na kuweka miundombinu kwa ajili ya ufugaji. Aidha, ili kuhakikisha kuwa migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi haijitokezi mara kwa mara, Serikali imeendelea kutoa elimu ya matumizi bora na usimamizi wa ardhi, ufugaji unaozingatia uwiano kati ya idadi ya mifugo na malisho, uundaji na matumizi ya mabaraza ya ardhi na kamati za usuluhishi.

Vilevile, Wizara imetoa mwongozo wa taratibu za kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Vijiji 624 imekamilika na vijiji 430 vimehakikiwa na kufanya jumla ya maeneo yaliyopimwa na kuhakikiwa kufikia hekta milioni 1.26 za ardhi kati ya hekta milioni 2.3 zilizotengwa kwa ajili ya ufugaji katika Wilaya 66 za Mikoa 19 ya Tanzania Bara. Pia, wataalam 15 kutoka Halmashauri 10 za Bunda, Tarime, Magu, Kwimba, Misungwi, Meatu, Kishapu, Kahama, Geita na Chato wamepewa mafunzo kuhusu uzalishaji, uhifadhi, uwiano wa mifugo na eneo la malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na uhaba wa maji ya mifugo, mwaka 2011/2012, Wizara imeandaa na kusambaza miongozo ya ujenzi na usimamizi wa miundombinu ya maji kwa mifugo kwenye Halmashauri zote nchini. Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imeendelea kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza upatikanaji wa maji kwa matumizi ya mifugo kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) katika Halmashauri mbalimbali nchini. Kupitia *DADPs*, ujenzi wa malambo mapya 53; ukarabati wa malambo 45 na uchimbaji visima virefu 18 unaendelea. Pia, Wizara imekamilisha mfumo wa digitali na kijiografia *(GIS)* wa kuonesha maeneo ya vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo na kuufanyia majaribio katika Wilaya ya Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imeainisha Wilaya zenye mahitaji ya haraka ya kujenga

mabwawa, malambo na visima virefu kwa ajili ya mifugo ili kupunguza uhamishaji wa mifugo na migogoro inayojitokeza. Wilaya hizo ni zile zenye mifugo mingi na zile ambako mifugo inahamia ambazo ni pamoja na Biharamulo, Chunya, Handeni, Kilindi, Kilosa, Kilombero, Korogwe, Rufiji, Mvomero, Lindi, Ulanga, Maswa, Meatu, Mbarali, Monduli, Ngorongoro, Longido, Same, Kiteto, Kondoa, Bagamoyo, Simanjiro, Siha, Mwanga, Nachingwea, Kisarawe na Kilwa. Wizara inahimiza Halmashauri za Wilaya husika kutekeleza jukumu lao la kubuni, kuandaa mipango na kuhakikisha kwamba maeneo ya malisho yanatengwa na miundombinu ya maji kwa mifugo inajengwa ili kudhibiti uhamaji wa mifugo na kuondoa migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Serikali za Mitaa, itaendelea na kazi ya upimaji na utengaji wa maeneo ya malisho na ujenzi wa miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa kifuta machozi kwa wafugaji. Kutokana na ukame uliotokea mwaka 2008/2009 na kusababisha vifo vingi vya mifugo, hususan katika Mikoa ya Kaskazini mwa nchi, Serikali iliahidi kutoa kifuta machozi kwa kaya zilizopoteza mifugo yote katika Wilaya za Longido (2,852), Monduli (1,484) na Ngorongoro (1,791).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alizindua mpango wa ugawaji wa mifugo ya kifuta

machozi/mbegu tarehe 19 Februari, 2012, Longido kwa kutoa ng'ombe 500 na mbuzi 30 wenye thamani ya shilingi milioni 213. Utekelezaji wa zoezi hili uliendelea ambapo kwa kuanzia Wilaya ya Monduli ilipewa shilingi milioni 205.63 na Wilaya ya Ngorongoro shilingi milioni 218.01 na ununuzi wa ng'ombe 500 kwa kila Wilaya unaendelea. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kutekeleza mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekamilisha zoezi la uzinduzi wa mpango huu katika Wilaya ya Monduli tarehe 02 Agosti, 2012 na Wilaya ya Ngorongoro tarehe 03 Agosti, 2012, kwa kutoa ng'ombe 500 kwa kila Wilaya. Mpango wa ugawaji wa mifugo unaendelea na utagharimu jumla ya shilingi 12,109.900,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usindikaji wa vyakula vya mifugo. Wizara imeendelea kuratibu uzalishaji wa vyakula vya mifugo na kusimamia ubora wake kwa kushirikiana na Shirika la Viwango la Taifa *(TBS).* Aidha, imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza zaidi katika usindikaji wa vyakula vya mifugo nchini. Uzalishaji wa vyakula vya mifugo umeongezeka kutoka tani 852,000 mwaka 2010/2011 hadi tani 900,000 mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia sita (6%).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Wizara imeendelea kutambua viwanda vilivyopo, uwezo wake na mahali vilipo kwa lengo la kurahisisha utoaji ushauri na ukaguzi. Kwa sasa, vipo jumla ya viwanda 80 vyenye uwezo wa kusindika tani milioni 1.4 za vyakula vya mifugo kwa mwaka. Viwanda hivyo vipo katika Mikoa ya Dar es

Salaam (34), Kilimanjaro (6), Mbeya (5), Mwanza (10), Shinyanga (3), Singida (1), Dodoma (1), Lindi (1), Morogoro (3), Arusha (7) na Pwani (9).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itatoa mafunzo kwa wakaguzi 45 wa vyakula vya mifugo kutoka Halmashauri za Jiji, Manispaa na Miji yenye viwanda vinavyosindika vyakula vya mifugo. Vilevile, itafanya ukaguzi wa ubora wa vyakula vya mifugo katika viwanda, maduka, maghala na watumiaji katika Halmashauri 30 ili kuona kama vinakidhi viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa magonjwa ya mifugo. Kuainisha maeneo huru ya magonjwa ya mifugo. Serikali imeanza kutekeleza Mpango wa Kuainisha Maeneo Huru ya Magonjwa ya Mifugo *(Disease Free Zones)* ya Mlipuko ambayo ni kikwazo katika biashara ya mifugo na mazao ya mifugo kimataifa ili kuwezesha wafugaji kufuga kibiashara na kuwaongezea mapato. Katika mwaka 2011/2012, Serikali imeainisha Wilaya za Sumbawanga na Nkasi katika Mkoa wa Rukwa kuwa eneo litakalokuwa kwa ajili ya kunenepesha mifugo, kuchinja na kuuza nyama bora ndani na nje ya nchi. Ramani ya maeneo huru ya magonjwa katika Wilaya za Sumbawanga na Nkasi imekamilika na ramani kwa ajili ya Wilaya ya Mvomero inaandaliwa. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itafanya utafiti wa chanjo ya ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD) kuendana na matakwa ya uanzishaji wa eneo huru la magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ya mlipuko. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kudhibiti magonjwa ya mlipuko. Mradi wa *Vaccines for Control of Neglected Animal Diseases in Africa (VACNADA)* unaofadhiliwa na Jumuia ya Ulaya umewezesha ununuzi wa dozi milioni 3.5 za chanjo dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe. Chanjo hii imetumika kuchanja ng'ombe milioni 3.2 katika Mikoa ya Mara, Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Vilevile, kupitia mradi huu, jumla ya dozi milioni 3 za chanjo ya Sotoka ya Mbuzi na Kondoo zilinunuliwa ambapo mbuzi na kondoo milioni 1.3 wamechanjwa katika Wilaya 14 za Mikoa ya Arusha, Mtwara, Ruvuma, Morogoro na Mara. Uchanjaji bado unaendelea. Kazi nyingine zilizotekelezwa na Wizara kupitia mradi wa VACNADA ni:

(i) Kuimarisha vituo saba (7) vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo *(VICs)* kwa kununua vifaa vya uchunguzi wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo, vifaa vya kubebea chanjo *(vaccine carriers)* 176, majokofu 97 na pikipiki tatu (3). Vilevile, mitambo ya mfumo baridi *(Cold rooms)* ilifungwa katika Maabara Kuu ya Mifugo Temeke na Vituo vya Kanda vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo vya Mwanza na Iringa; na

(ii) Kuchangia shilingi 729,371,000.00 kwa ajili ya uchanjaji dhidi ya magonjwa ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo katika Wilaya 14 za mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi ilichanja mbuzi na kondoo milioni 2.7 katika Halmashauri 31 katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa kwa ajili ya kudhibiti sotoka ya mbuzi na kondoo kwa ufadhili wa FAO. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kutoa mafunzo ya kutambua ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo kwa wataalam tisa (9) kutoka Maabara Kuu ya Mifugo na *VICs* za Arusha, Iringa, Mtwara, Mwanza na Temeke;

(ii) Kujenga uwezo wa *VICs* za Iringa, Mtwara na Temeke kwa kuzipatia vifaa na vitendanishi *(reagents)* kwa ajili ya kutambua sotoka ya mbuzi na kondoo; na

(iii) Kununua vifaa vikiwemo *cool boxes* 120, *ear notchers* 80, *gumboots* 40, *overalls* 40, sindano za kuchanjia 13,800, forceps 80 na *ice packs* 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itachanja mbuzi na kondoo 850,000 katika maeneo hatarishi kwa msaada wa *FAO* ambayo ni ya mipakani kuanzia Mkoa wa Mtwara mpaka Rukwa na eneo la Igunga na Iramba ambalo kwa sasa limeonekana kuwa na ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii na Maliasili na Utalii iliendelea

kufuatilia mwenendo wa ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege. Hadi sasa nchi yetu bado haijapata maambukizi ya ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imeendelea kudhibiti Ugonjwa wa Mdondo nchini kwa kusambaza dozi milioni 14 za chanjo inayostahimili joto katika Halmashauri zote nchini kupitia vituo vya kanda vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo. Halmashauri zimehimizwa kuhamasisha matumizi ya chanjo hii ili kuongeza tija katika uzalishaji wa kuku wa asili. Pia, Mpango Mkakati wa Udhibiti wa Mdondo umefanyiwa mapitio kwa lengo la kuuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe *(African Swine Fever - ASF)* umeendelea kujitokeza na kuua jumla ya nguruwe 4,476 katika Wilaya za Makete (80), Sumbawanga (1,933), Njombe (803), Kilombero (715), Mufindi (250), Iringa (296), Kilosa (70) na Kilolo (329). Katika kukabiliana na ugonjwa huu hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuweka karantini, kudhibiti usafirishaji wa nguruwe na mazao yake, kuelimisha wananchi kuhusu ugonjwa huo na kusafisha mabanda na kuyapulizia dawa aina ya *v-rid.* Aidha, katika maeneo ambapo nguruwe huzurura wafugaji walitakiwa kujenga mabanda na kuwafungia nguruwe wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi kutoa elimu kwa wafugaji na kudhibiti usafirishaji holela wa wanyama na mazao

yake ili kudhibiti magonjwa ya mlipuko kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kusambaza Mpango Mkakati wa Tahadhari dhidi ya Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege;

(ii) Kurejea na kuboresha Mpango Mkakati wa Mawasiliano katika Tahadhari na udhibiti wa Mafua Makali ya Ndege;

(iii) Kuandaa Mpango Mkakati wa Kudhibiti Homa ya Nguruwe;

(iv) Kurejea na kuboresha Mpango Mkakati wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo;

(v) Kufuatilia mienendo ya magonjwa ya mlipuko nchini; na

(vi) Kukamilisha Mpango Mkakati wa Udhibiti wa Mdondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo *(FMD)* umeendelea kutekelezwa na Wizara kupitia Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko ya Mifugo *(SADC–TADs Project)* unaotekelezwa katika nchi za Tanzania, Angola, Malawi, Msumbiji na Zambia. Jumla ya sampuli 92 za nyati na 155 za ng'ombe zilichukuliwa kutoka Hifadhi za Taifa za Mikumi, Mkomazi na Ruaha na kupelekwa Botswana ili kubaini aina ya virusi vya ugonjwa wa *FMD*. Pia uchunguzi wa sampuli 373 za ng'ombe kutoka

kanda za Ziwa na Mashariki ulifanyika na kubaini virusi aina ya *FMDV O*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mradi huu umekamilisha taratibu za ununuzi wa vifaa vya maabara ya kisasa *Bio-Security Level 3 (BSL3)* Temeke. Vilevile, ili kuimarisha utoaji huduma, wataalam 11 wa mifugo wanahudhuria mafunzo ya uzamili na 9 wamepata mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi. Katika mwaka 2012/2013, mradi utaendelea kugharimia mafunzo ya wataalam ndani na nje ya nchi na ununuzi wa vifaa vya maabara na kuendeleza uchunguzi wa *FMD* kwenye nyati katika Hifadhi ya Selous na mapori ya akiba ya Moyowosi na Kigosi. Aidha, uchunguzi wa magonjwa ya mlipuko utaendelea kwenye ng'ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe katika maeneo mbalimbali nchini ili kubaini aina ya virusi na chanjo itakayosaidia kudhibiti ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa yanayoenezwa na kupe ni tatizo kubwa kwa afya na uzalishaji mifugo. Hasara zinazosababishwa na kupe na magonjwa wayaenezayo ni pamoja na vifo, kuharibu ubora wa zao la ngozi na kupungua kwa mapato ya mfugaji na taifa. Katika mwaka 2011/2012, Serikali kupitia *DADPs* ilikarabati majosho 51 na kujenga majosho mapya 57 ili kudhibiti tatizo hili na hivyo kuongeza idadi ya majosho yanayofanya kazi kutoka 1,756 hadi 1,864. Pia, ruzuku ya asilimia 40 kwa dawa za kuogesha mifugo iliendelea kutolewa ambapo lita 62,500 za dawa ya kuogesha mifugo zilinunuliwa kwa

gharama ya shilingi bilioni 1.0 na kuzisambaza katika Mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali iliendelea kuhamasisha na kuratibu matumizi ya chanjo ya ugonjwa wa Ndigana kali ambapo kupitia sekta binafsi ng'ombe 162,637 walichanjwa dhidi ya ugonjwa huo katika Mikoa 12 ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Mtwara, Pwani, Tabora na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine katika kudhibiti kupe na magonjwa wayaenezayo kwa kuhamasisha uibuaji wa miradi ya ukarabati na ujenzi wa majosho mapya na kuiombea fedha za utekelezaji kutoka kwa wadau mbalimbali. Pia, Wizara kwa kushirikiana na taasisi ya *GALVmed* itaratibu uchanjaji dhidi ya ugonjwa wa Ndigana Kali ambapo dozi 55,000 za chanjo zitatumika kwa kuanzia katika Mikoa ya Morogoro, Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbung'o na Nagana. Ugonjwa wa Nagana unaoenezwa na mbung'o unaendelea kudhibitiwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Katika mwaka 2011/2012 jumla ya ng'ombe 389 kati ya ng'ombe 36,432 walioko katika maeneo hatarishi katika Mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mtwara, Rukwa na Tanga walitolewa taarifa ya kuugua Nagana ambapo kati yao ng'ombe 21 walikufa. Kazi zilizotekelezwa katika kukabiliana na mbung'o na Nagana ni pamoja na:-

(i) Kuchunguza na kutathmini mtawanyiko wa mbung'o na kuchora ramani mpya ya mtawanyiko wa mbung'o katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Morogoro na Pwani. Tathmini ya awali inaonesha kupungua kwa eneo lenye mbung'o na mbung'o wengi wapo kwenye Mbuga na Hifadhi za Wanyamapori;

(ii) Kununua vitendea kazi kwa ajili ya ukusanyaji wa takwimu na uandaaji wa ramani za mtawanyiko wa mbung'o;

(iii) Kuhamasisha wafugaji 239 kutumia mbinu shirikishi na endelevu ikiwa ni pamoja na matumizi ya mitego na vyambo vya kudhibiti mbung'o katika Wilaya za Babati, Mbulu, Monduli na Ngorongoro;

(iv) Kuandaa Mpango Mkakati wa Kutokomeza Mbung'o na Ndorobo utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2012/2013 – 2016/2017) katika maeneo yaliyoathiriwa na Nagana na Malale katika Mikoa ya Kigoma, Tabora, Rukwa, Katavi na Kagera;

(v) Kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kukusanya takwimu na kuandaa ramani ya maeneo hatarishi ya Malale na kuanisha uwezo wa vituo vya afya katika udhibiti wa ugonjwa huo kupitia Mpango wa *"Network for Mapping African Trypanosomosis – Tanzania" ( NetMATT);* na

(vi) Kudhibiti mbung'o katika maeneo ya mwingiliano kati ya makazi na hifadhi za wanyamapori katika Wilaya za Urambo na Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea na utekelezaji wa mkakati wa kudhibiti mbung'o na ndorobo kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kujengea uwezo Halmashauri kuhamasisha jamii kuanzisha miradi kuhusu matumizi ya mbinu shirikishi na endelevu za kudhibiti mbung'o na ndorobo katika Halmashauri za Kilombero, Kondoa, Manyoni, Mbulu, Nanyumbu na Ulanga;

(ii) Kuwezesha Halmashauri kusambaza kemikali na vifaa vya kudhibiti mbung'o na ndorobo vikiwemo viuatilifu, mitego 180 na vyambo vya kuua mbung'o 3,200 katika Halmashauri za Bagamoyo, Handeni, Kaliua, Kisarawe, Kondoa, Mpanda na Nkasi; na

(iii) Kwa kushirikiana na Shirika la Rasilimali za Wanyama la Umoja wa Afrika *(African Union - InterAfrica Bureau for Animal Resources- AU-IBAR)* kuandaa Mpango wa pamoja wa kutokomeza maambukizi ya Nagana na Malale kati ya Tanzania na Kenya kwa kudhibiti mbung'o katika maeneo ya Hifadhi za Serengeti (Tanzania) na Masai-Mara (Kenya).

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu. Wizara imeendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo yanayoambukiza

binadamu yakiwemo Kichaa cha Mbwa, Homa ya Bonde la Ufa, Kutupa Mimba na Kifua Kikuu cha Ng'ombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kichaa cha Mbwa. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilitekeleza Mradi wa Kutokomeza Kichaa cha Mbwa nchini kwa ufadhili wa Taasisi ya Bill & Melinda Gates Foundation chini ya Uratibu wa Shirika la Afya Duniani kwa kununua na kusambaza dozi 375,000 za chanjo ya kichaa cha mbwa katika Halmashauri 79, ambapo jumla ya mbwa 122,677 na paka 6,941 walichanjwa, na uchanjaji unaendelea katika Halmashauri mbalimbali. Pia, Wizara ilifanikisha maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa kwa kutoa elimu shuleni na uhamasishaji wa jamii juu ustawi wa wanyama. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kudhibiti Kichaa cha Mbwa kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kununua na kusambaza dozi 180,000 za chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa katika maeneo ya Mradi;

(ii) Kununua na kusambaza dozi 100,000 za chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa katika maeneo nje ya mradi; na

(iii) Kuandaa na kuratibu maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Homa ya Bonde la Ufa. Mwaka 2011/2012, Wizara imenunua na kusambaza

dozi 566,666 za chanjo ya Homa ya Bonde la Ufa *(Rift Valley Fever)* kwenye Halmashauri 22 zilizopo kwenye ukanda wa Bonde la Ufa na ziko katika hatari ya kupata maambukizi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa kwa kununua dozi milioni 1.0 na kuzisambaza katika Halmashauri 29 zilizoathiriwa mwaka 2007 ili kuimarisha kinga ya mifugo iliyozaliwa baada ya hapo. Pia, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ugonjwa huo na kuwashauri hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ugonjwa wa Kutupa Mimba na Kifua Kikuu. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilifanya upimaji wa kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa Kutupa Mimba (*Brucellosis*) kwa ng'ombe 7,166 na mbuzi 1,845 kwa kipimo cha ELISA katika mashamba ya mifugo ambapo ng'ombe 81 waligundulika kuwa na maambukizi na kuchinjwa chini ya uangalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na watoa huduma binafsi itaendelea kupima kiwango cha maambukizi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba kwa mbuzi 2,500 na kondoo 2,500 na Kifua Kikuu kwa ng'ombe 5,000 katika mashamba ya taasisi za umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa mifugo na mazao yake. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya ng'ombe milioni 1.5, mbuzi 542,556, kondoo 220,794, kuku milioni 3.8 na nguruwe 128,610 walikaguliwa kabla na baada ya kuchinjwa. Aidha, jumla ya vifaranga vya

kuku wazazi 330,000 na mayai ya kutotolesha vifaranga 8,193,000 yalikaguliwa na kuingizwa nchini. Pia, mayai 76,530 na vifaranga 520,000 vilivyoingizwa nchini kinyume cha sheria vilikamatwa na kuteketezwa na wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuimarisha vituo 18 vya mipakani vya ukaguzi wa mifugo na mazao yake kwa kuvipatia vitendea kazi pamoja na mafunzo kwa wataalam 100 kuhusu ukaguzi wa mifugo na mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi na utafiti wa magonjwa ya mifugo. Serikali imeanzisha Wakala wa Maabara ya Mifugo *Tanzania (Tanzania Veterinary Laboratory Agency – TVLA)* na kutangazwa katika Gazeti la Serikali GN. Na. 74 la tarehe 12 Machi, 2012. Lengo la kuanzisha Wakala huu ni kuimarisha uchunguzi wa magonjwa ya mifugo na kutoa huduma za kimaabara. *TVLA* inaundwa na Maabara Kuu ya Mifugo Temeke *(CVL),* Taasisi ya Utafiti wa Mbung'o na Ndorobo *(TTRI)* Tanga, Kituo cha Utafiti wa Mbung'o na Ndorobo *(TTRC)* Kigoma na Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo *(VICs)* vya Arusha, Iringa, Mpwapwa, Mtwara, Mwanza, Tabora na Temeke. Majukumu ya *TVLA* ni pamoja na kufanya uchunguzi, utambuzi na utafiti wa magonjwa mbalimbali ya mifugo; utafiti wa wadudu na magonjwa wayaenezayo, kutengeneza na kufanya majaribio ya dawa na chanjo mpya za kuzuia magonjwa ya mifugo; kuchunguza ubora wa bidhaa zitokanazo na mifugo, nguvu za dawa za majosho na ubora wa vyakula vya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Maabara Kuu ya Mifugo Temeke imezalisha na kusambaza dozi milioni 11.9 za chanjo ya mdondo (I-2), 242,850 za Chambavu, 173,000 za Kimeta na dozi 19,000 za S19. Aidha, imechunguza sampuli 393 za vyakula vya mifugo ili kubaini ubora wa vyakula hivi na kufanya utafiti wa vimelea vinavyosababisha *Contagious Caprine Pleuro Pneumonia (CCPP)* kwa sampuli 556 katika Wilaya za Karatu, Longido, Babati, Kiteto, Igunga na Nzega. Utafiti umeonesha kutoweka kwa ugonjwa huu katika Wilaya hizi. Utafiti unaendelea kufanyika kuhusu ubora wa chanjo ya *CCPP* kwenye Wilaya za Handeni, Kilosa na Muheza. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:

(i) Kuzalisha, kutathmini na kuendeleza aina nne (4) za chanjo ya Homa ya Bonde la Ufa, Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, Ndui ya Kuku na *biologicals*;

(ii) Kufanya chunguzi tatu (3) kubaini uwepo wa viuatilivu/madawa ya kuogeshea mifugo *(Paranex, Cypermethrine na Stelladone)* kwenye nyama na maziwa na tatu (3) kuhusu uchafuzi wa vimelea wa bakteria na kuvu katika vyakula vya binadamu vitokanavyo na mifugo. Uchunguzi unaendelea kubaini viuatilifu na vimelea chafuzi kwenye sampuli zilizokusanywa;

(iii) Kufanya uchunguzi wa sampuli 348 za vyakula vya mifugo kutoka Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambapo sampuli 16 sawa na asilimia 4.6 zilibainika

kuwa na vimelea vya uchafuzi (*contaminants*) ambavyo vizingeweza kuwa na madhara kwa mifugo;

(iv) Kuendelea kufanya uchunguzi wa sampuli 657 za damu, 893 za maziwa na 349 za dawa za kuogesha mifugo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Chakula na Dawa;

(v) Kuchunguza jumla ya sampuli 2,093 (Simanjiro 610, Kondoa 355, Mtwara Vijini 300, Pangani 213, Longido 340 na Ngorongoro 275) kwa ajili ya utafiti wa CBPP. Matokeo ya ng'ombe 47 kati ya ng'ombe 213 wa shamba la Mivumoni Wilaya ya Pangani, walikuwa na ugonjwa wa Homa ya Mapafu;

(vi) Kufanya utafiti wa ustahimilivu wa chanjo ya mdondo (I-2) na kuweka muda wa matumizi. Utafiti wa kutumia chanjo hii kwa kufuata ratiba ya kuchanja mara tatu kwa mwaka umeonesha kudhibitiwa kwa ugonjwa wa mdondo kwenye vijiji 140 vya Wilaya za Singida Vijijini na Ikungi. Pia, utafiti katika Mikoa ya Mtwara, Iringa, Mbeya, Mwanza na Shinyanga iliyotumia chanjo hii umeonesha kupungua kwa vifo vya kuku kutoka asilimia 90 hadi asilimia nne (4%);

(vii) Kufanya utafiti wa *FMD* na ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo *(PPR)* kuhusu uwezo wa kinga ya chanjo ya magonjwa haya ambapo sampuli 2,500 kutoka Mikoa ya Mtwara, Morogoro, Iringa na Mara zilichukuliwa na kufanyiwa uchunguzi na utafiti unaendelea;

(viii) Kuendelea na utafiti wa kuchanganya chanjo ya Kimeta na Chambavu;

(ix) Kupitia mradi wa *EAAPP*, utafiti wa magonjwa ya Ndigana Kali, Kutupa Mimba na Kifua Kikuu kwa ngo'mbe wa maziwa umefanyika katika Vijiji vya Mbeya mjini na Amani Muheza ili kubaini kuwepo au kutokuwepo kwa magonjwa hayo. Jumla ya ng'ombe 404 kutoka vijiji vya Mbeya Mjini (202) na Amani Muheza (202) walifanyiwa uchunguzi. Matokeo ya awali yameonesha kutokuwepo kwa ugonjwa wa Ndigana Kali na Kifua Kikuu kwenye ng'ombe wa maziwa waliofanyiwa uchunguzi katika maeneo ya mradi. Uchunguzi wa ugonjwa wa kutupa mimba unaendelea katika maabara ya *CVL*;

(x) Kufanya utafiti wa aina ya kupe na dawa zinazofaa kuwadhibiti katika Wilaya za Rufiji na Mvomero ambapo kwa sasa utafiti umeonesha kuwepo kwa aina 6 za kupe;

(xi) Kutathmini, kuhakiki na kukubali matumizi ya njia za *c-ELISA,* Biolojia ya vinasaba *(molecular biology), Gamma Interferon* na *LAMP test* za uchunguzi wa kimaabara wa magonjwa ya mifugo;

(xii) Kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kudhibiti Mbung'o na Nagana. Utafiti wa aina ya mbung'o waenezao ndorobo na dawa zinazofaa kuwadhibiti unaendelea katika Wilaya za Kilosa, Rufiji na Serengeti; na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire. Utafiti huu umeonesha viuatilifu kupunguza mbung'o na ndorobo kwa kiwango kikubwa;

(xiii) Kuboresha maabara kwa kuzipatia vifaa (darubini, majokofu, *incenerator, diagnostic kits* na *glasswares*), vitenganishi na kemikali;

(xiv) Kukamilisha ujenzi wa majengo matatu (3) ya Kituo cha Kuzalisha Chanjo Kibaha, Maabara ya Kuzalisha Mabuu ya Mbung'o *(insectaries)* TTRI Tanga na kuendelea kukarabati Kituo cha Magonjwa ya Kuambukiza na bio-teknolojia *(Centre for Infectious Diseases and Biotechnology - CIDB) Temeke;*

*(*xv) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam 12 ndani na nje ya nchi (*CVL*- 6, Zanzibar - 2, Burundi - 2, Sudan - 2) kuhusu matumizi ya *molecular biology diagnostic techniques;*

(xvi) Kuwezesha mafunzo kwa wataalam 14 ngazi ya Uzamili na watano (5) ngazi ya Uzamivu;

(xvii)Kuanzisha na kutekeleza mfumo wa usimamizi wa utendaji bora wa maabara ya *CVL* ili kupata ithibati ya kimataifa *(International Accreditation – ISO 17025);* na

(xviii) Kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 30 kutoka vyuo vya *SUA* (17), *UDSM* (4), Chuo cha Ardhi (3) na Chuo cha Utumishi wa Umma (6).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania itazalisha na kusambaza katika Halmashauri chanjo dozi milioni 100 za Mdondo, 500,000 za Kimeta, 400,000

za Chambavu, 250,000 za Kutupa Mimba, 200,000 za Homa ya Bonde la Ufa na 100,000 za Homa ya Mapafu ya Ng'ombe. Pia, Wakala itafanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kufanya uchunguzi wa ubora wa vyakula vya mifugo, kuhakiki na kutathmini njia za kuchunguza kemikali za *sumu (toxicological analytical assays)* kwenye mifugo na mazao yake na kufanya uchunguzi wa ubora wa dawa za kuogeshea mifugo;

(ii) Kufanya uchunguzi na utafiti wa magonjwa mbalimbali ya mifugo na kufanya majaribio ya chanjo za kudhibiti magonjwa ya mlipuko;

(iii) Kuandaa na kuweka katika matumizi teknolojia 2 za *Sterile Insect Technique (SIT)* na Mitego kwa ajili ya kudhibiti mbung'o na magonjwa yaenezayo na mbung'o;

(iv) Kuimarisha vituo vya wakala kwa kukarabati na kuvipatia vitendea kazi na kuendelea na taratibu za kuipatia maabara ya Temeke ithibati ya kimataifa;

(v) Kuanzisha kitengo cha *cell culture* kwa ajili ya matumizi ya utafiti na uzalishaji wa chanjo; na

(vi) Kutengeneza chanjo za ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa *(RVF)* na Homa ya Mapafu ya Ng'ombe *(CBPP)* na kuzifanyia majaribio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo. Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo unaotekelezwa na Halmashauri. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

(i) Kuratibu na kujenga uwezo wa wataalam wa mifugo 53 kutoka Halmashauri 40 za Mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kagera, Mbeya, Pwani, Mara, Ruvuma, Rukwa na Shinyanga;

(ii) Kusajili wafugaji 100,000 na kutambua ng'ombe wa asili 502,572 katika Halmashauri za Musoma (177,312), Bunda (139,953), Tarime (111,419), Missenyi (61,823), Kishapu (9,418), Kwimba (2,131) na Bukombe (445);

(iii) Kununua na kusambaza madaftari ya usajili 232, vyuma vya chapa 1,176, hereni 20,000, tufe za kumezwa tumboni (electronic rumen boluses) 3,000;

(iv) Kuendelea na utaratibu wa kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo kwa ufadhili wa *FAO*;

(v) Kutoa mafunzo kwa wataalam wa mifugo 100 kutoka Halmashauri kuhusu Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Sura 184 na Kanuni zake; na

(vi) Kuandaa na kusambaza kwa wadau nakala 2,000 za vipeperushi kuhusu Mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wataalam wa mifugo 100 kuhusu Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Sura 184 na Kanuni zake;

(ii) Kukamilisha uanzishwaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo;

(iii) Kuratibu utekelezaji wa mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo; na

(iv) Kununua hereni 45,000 na tufe za tumboni 5,000 kwa ajili ya kutambua ng'ombe wa maziwa 50,000 na kusajili wafugaji 1,000 kupitia mradi wa *EAAPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sensa na Takwimu za Mifugo. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuboresha upatikanaji wa takwimu za mifugo kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na wadau wengine. Aidha, Wizara kupitia Mradi wa Benki ya Dunia wa Kuboresha Takwimu za Mifugo *(Livestock Data Innovation Project in Africa)* imeshiriki katika mafunzo ya kujenga uwezo kwa Maafisa Takwimu 30 wa Mifugo kuhusu kuchambua na kuainisha vikwazo katika upatikanaji wa takwimu za sekta ya mifugo. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itashiriki katika Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika tarehe 26 Agosti, 2012 nchini. Katika sensa hiyo, masuala kuhusu idadi ya wafugaji pamoja na mifugo muhimu ambayo ni ng'ombe, mbuzi na kondoo yamejumuishwa katika dodoso la sensa. Kutokana na sensa hii, Serikali

inatarajia kupata takwimu muhimu zitakazowezesha kuandaa na kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo ya sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa sekta ya uvuvi. Uvunaji wa samaki na uuzaji wa mazao ya uvuvi. Uvuvi umeendelea kuwa chanzo muhimu cha ajira kwa baadhi ya wananchi. Idadi ya wavuvi imeongezeka kufikia 177,527 katika mwaka 2011/2012 ikilinganishwa na wavuvi 176,632 mwaka 2010/2011. Aidha, idadi ya vyombo vya uvuvi imeongezeka kutoka 54,997 mwaka 2010/2011 hadi kufikia 55,299 mwaka 2011/2012. Jumla ya tani 341,065.98 za mazao ya uvuvi zilivunwa mwaka 2011/2012 ikilinganishwa na tani 347,156.9 zilizovunwa mwaka 2010/2011. Upungufu huu unatokana na kupungua kwa rasilimali ya uvuvi ambako kumesababishwa na uvuvi haramu, uchafuzi na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Pamoja na upungufu huu, thamani ya mazao ya uvuvi imepanda kutoka shilingi bilioni 747.5 mwaka 2010/2011 hadi shilingi trilioni 1.2 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia uuzaji wa samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi kwa kuzingatia sheria na viwango vya kitaifa na kimataifa. Katika mwaka 2011/2012, tani 37,996.4 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 61,215 vyote vikiwa na thamani ya shilingi bilioni 233.7 waliuzwa nje ya nchi na kuiingizia Serikali mapato ya shilingi bilioni 6.2 ikilinganishwa na tani 39,771.8 za mazao ya uvuvi na samaki wa mapambo 40,552 wenye thamani ya shilingi bilioni 263.1 waliouzwa nje ya nchi mwaka 2010/2011 na kuipatia Serikali

mapato ya shilingi bilioni 5.9. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kuratibu na kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi. Aidha, itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika maeneo mbalimbali yakiwemo uvuvi, ujenzi wa viwanda (zana za uvuvi, kuchakata mazao ya uvuvi, vifungashio), uongezaji wa thamani kwenye mazao ya uvuvi na ujenzi wa boti bora za uvuvi. Pia, kwa kushirikiana na wadau itaunganisha wazalishaji na masoko ya kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya mazao ya uvuvi. Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vya kuchakata na kuhifadhi mazao ya uvuvi. Kutokana na uhamasishaji huu, hadi sasa kuna jumla ya viwanda 34 vya kuchakata mazao ya uvuvi nchini kati ya hivyo, viwanda 31 vinafanya kazi. Kati ya viwanda hivyo, 9 viko Ukanda wa Ziwa Victoria, 21 Pwani na kimoja (1) Ziwa Tanganyika. Pia, kuna maghala 84 ya kuhifadhi mazao ya uvuvi. Viwanda hivi vimeendelea kukidhi viwango vya ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kulingana na mahitaji ya soko la ndani na nje likiwemo soko la Kimataifa la Jumuiya ya Ulaya lenye Sheria na Viwango vya hali ya juu vya ubora na usalama. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vya kuchakata na kuhifadhi mazao ya uvuvi na matumizi ya teknolojia na miundombinu sahihi ya uandaaji, uhifadhi, uchakataji, usambazaji na uuzaji wa samaki na mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi na ufuatiliaji wa masoko ya samaki. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilifanya ukaguzi wa masoko ya samaki ya Kirumba, Magogoni Feri, Musoma, Kigoma na Bukoba. Pia, jumla ya mialo 40 ya kupokelea samaki ilikaguliwa katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi. Matokeo ya ukaguzi huu yameonesha kuwa hali ya usafi na huduma katika masoko na mialo hairidhishi kwa afya ya walaji na mazingira. Naendelea kuzihimiza Halmashauri ambazo ni wamiliki wa masoko na mialo hiyo kusimamia kikamilifu miundombinu hiyo kwa ajili ya kulinda afya za walaji, kulinda mazingira, kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi na kuongeza thamani yake. Masoko na mialo hii ikisimamiwa ipasavyo ni chanzo muhimu cha mapato kwa Halmashauri. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kufanya ukaguzi wa miundombinu hiyo ili kuiboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya samaki aina ya sangara katika Ukanda wa Ziwa Victoria. Tarehe 25 Juni 2012, nilitoa Kauli ya Serikali mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu kushuka kwa bei ya samaki aina ya sangara katika ukanda wa Ziwa Victoria kutoka wastani wa shilingi 4,500 hadi 3,000 kwa kilo bei ya viwandani. Baadhi ya sababu za kushuka kwa bei ni kushuka kwa sarafu ya Euro, kutetereka kiuchumi na kibiashara kwa baadhi ya nchi zikiwemo Hispania, Italia, Ugiriki na Ureno ambazo ni soko kubwa la minofu ya sangara kutoka nchi za Afrika Mashariki, kuwepo kwa aina nyingine za samaki wenye bei ya chini aina ya Basa au Pangasius kutoka Mashariki ya Mbali, Tilapia

wanaofugwa China, Cod kutoka Ulaya na Barramundi anayefanana na sangara kutoka Australia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kushuka kwa bei ya sangara, Wizara kwa kushirikiana na wavuvi na wenye viwanda imefuatilia mwenendo wa bei ya sangara katika nchi za Kenya na Uganda na kubaini kuwa bei katika nchi hizo hazitofautiani sana na bei zinazotolewa hapa nchini. Kwa mfano, wastani wa bei ya sangara katika mwalo wa Dunga Beach – Kisumu nchini Kenya ni shilingi 150 (shilingi za Tanzania 2,850) kwa kilo na katika mwalo wa Masese Beach – Jinja nchini Uganda ni shilingi 5,000 (shilingi za Tanzania 3,571) kwa kilo wakati bei ya sangara katika mwalo wa Sota (Rorya) ni shilingi 2,800 na mwalo wa Igombe (Mwanza) ni shilingi 2,700. Aidha, taarifa kutoka balozi zetu zilizoko nchi zenye masoko ya sangara zimeonesha kuwa bei imeshuka katika masoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imewashauri wavuvi kuanzisha vyama vya ushirika vyenye nguvu ili viweze kuuza samaki moja kwa moja kwenye viwanda na masoko badala ya kupitia kwa mawakala ili kuweza kuhakiki samaki wanaouza na bei yake; kuwepo na mkataba mmoja wa kisheria baina ya wenye viwanda, mawakala na wavuvi. Pia, Serikali imeendelea kuhamasisha ulaji wa sangara humu nchini ili Watanzania wale wanachozalisha na hivyo kupanua wigo wa soko la ndani la mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwawezesha wavuvi wadogo. Kwa kuwa zaidi ya asilimia 90 ya uzalishaji wa mazao ya uvuvi hutokana na wavuvi wadogo, katika

mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea kuwawezesha wavuvi kwa kuweka mazingira bora ya uwekezaji na miundombinu ili kuwa na uvuvi endelevu na wenye tija kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kukarabati na kujenga mialo ya kupokelea samaki katika ukanda wa Ziwa Victoria 25, ukanda wa pwani mitatu (3) na kufanya maandalizi ya ujenzi wa mialo minne (4) katika ukanda wa Ziwa Tanganyika;

(ii) Kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha boti cha Mbamba Bay – Ruvuma ili wavuvi wa Ziwa Nyasa waweze kupata vyombo bora vya uvuvi;

(iii) Kuendelea kuhimiza wavuvi kununua zana na vyombo bora baada ya Serikali kuondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye nyavu, injini za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu na vifungashio;

(iv) Kuendelea kuratibu na kusimamia miradi midogo ya jamii za pwani iliyoibuliwa na wananchi kupitia mradi wa *MACEMP* ikiwemo miradi ya uvuvi 240, unenepeshaji kaa 11, ufugaji nyuki 59, ufugaji ng'ombe 10, ufugaji kuku 64, ufugaji wa mbuzi 8, ufugaji wa samaki 23, uchakataji wa samaki 24, uzalishaji wa chumvi 9 na ukulima wa mwani 15;

(v) Kuratibu na kuhamasisha wananchi katika Wilaya za Kilwa, Mafia na Rufiji kuanzisha Benki za Wananchi ambapo jumla ya shilingi milioni 41 zimechangwa katika Wilaya ya Mafia. Aidha, ukarabati wa majengo kwa ajili ya benki za Kilwa na Mafia unaendelea;

(vi) Kushirikiana na Umoja wa Wavuvi Wadogo wa Dar es Salaam (UWAWADA) kuhamasisha wavuvi 600 kutoka Wilaya za Kinondoni (300), Ilala (150) na Temeke (150) ili kuanzisha na kuimarisha Vyama vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* kwa ajili ya kuongeza mtaji na kupata mikopo katika benki ya Rasilimali *(TIB)* kupitia dirisha la Kilimo;

(vii) Kuhamasisha wavuvi wadogo kununua boti za uvuvi za *fibre glass* 128 kutoka katika Kampuni za *Songoro Marine Transport - Mwanza* (15), Sam and *Anzai Boat Builders – Dar es Salaam* (70) na *Seahorse East African – Dar es Salaam* (43) ili kupunguza athari za uharibifu wa mazingira;

(viii) Kuanza upembuzi yakinifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa bandari za uvuvi katika maeneo ya Kigamboni, Kilwa, Mbegani, Mtwara na Tanga kwa ajili ya kuhudumia wavuvi wadogo na meli za uvuvi za bahari kuu; na

(ix) Kutoa mafunzo kwa wadau 1,935 kutoka Halmashauri 16 za mwambao wa pwani kuhusu mwenendo na mahitaji ya soko la Kimataifa la mazao ya uvuvi na kutoa elimu kwa wadau 120 kuhusu Sheria na Kanuni za Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, kupitia Programu na Miradi mbalimbali ya maendeleo, Serikali itaendelea kuwawezesha wavuvi kwa kuweka miundombinu, kuwapatia mafunzo, kuhamasisha wadau kuendelea kuwekeza katika uvuvi

wa Bahari Kuu, kuhamasisha wavuvi kutumia boti za *fibre glass* ili kupunguza ukataji wa miti na kuhifadhi mazingira na kuanzisha vyama vya ushirika na *SACCOS* vya wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthibiti wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilitoa mafunzo kuhusu teknolojia ya kukausha samaki kwa moshi kwa kutumia jiko sanifu *Chokor* au *Ghana oven* linalotumia kuni chache, kukausha dagaa kwenye vichanja, matumizi ya barafu, uhifadhi, ufungashaji na usafirishaji wa samaki wabichi. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wadau wa uvuvi 923 kutoka Halmashauri za Majiji ya Mwanza (45) na Tanga (90); Manispaa ya Ilala (44), Kigoma – Ujiji (24); na Wilaya za Pangani (40), Muheza (120), Mafia (80), Mtwara Vijijini (52), Lindi Vijijini (78), Mkuranga (50), Bagamoyo (40), Nkasi (130), Sumbawanga (50) na Mpanda (80). Pia, mafundi sanifu sita (6) wa maabara za uvuvi walipata mafunzo ya ufundi sanifu wa maabara na watalaam wawili (2) kuhusu *uncertainity measurement and method validation.* Aidha, kupitia ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya wakaguzi 10 walipata mafunzo ya *online certification of fisheries products export.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *WWF* imeandaa Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi wa Pweza *(Octopus Fishery Management Plan)* wa kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali ya pweza ili kuwezesha upatikanaji wa hati ya kiikolojia *(Ecolabelling Certificate)* kupitia *Marine Stewardship Council* kukidhi mahitaji ya soko la Kimataifa. Aidha,

wadau 127 walipewa elimu kuhusu umuhimu wa Mpango huu. Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na:-

(i) Kufanya kaguzi 64 za kina na 584 za kawaida kwenye viwanda vinavyochakata na maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi. Matokeo ya kaguzi hizo yanaonesha kukidhi viwango vya ubora na hivyo viwanda kuruhusiwa kuendelea na uzalishaji;

(ii) Kufanya kaguzi 2,438 za ubora wa samaki na mazao yake kabla ya kusafirishwa nje ya nchi na kwenye mialo 25 kwa lengo la kuhakiki usafi na miundombinu ya mialo hiyo; na

(iii) Kutoa mafunzo kwa watumishi 17 yakiwemo mafunzo ya muda mrefu (3) na muda mfupi (14).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kusimamia ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuchunguza sampuli 800 za mazao ya uvuvi, maji, udongo ili kubaini vimelea vya magonjwa, viuatilifu, madini tembo na kemikali mbalimbali;

(ii) Kufanya kaguzi 3,500 za ubora wa samaki na mazao yake kabla ya kusafirishwa nje ya nchi;

(iii) Kufanya kaguzi 100 kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, mialo na maghala ya kuhifadhia mazao ya uvuvi;

(iv) Kuandaa mafunzo kwa wakaguzi 40 wa mazao ya uvuvi, mafundi sanifu - maabara 20 na wadau 500

kuhusu uthibiti wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi;

(v)Kuimarisha na kuwezesha Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi-Nyegezi na Maabara ya Uchunguzi wa Sumu (Biotoxin) kwenye Mazao ya Uvuvi, Dar es salaam; na

(vi) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia na miundombinu sahihi ya uandaaji, uchakataji, usambazaji na uuzaji wa samaki na mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Nguvu za Atomiki *(International Atomic Energy Agency)* imeendelea kuimarisha Maabara ya Uchunguzi wa Sumu ya Mwani unaoelea kwenye Maji *(Harmful Algal Blooms-HABs*) - Temeke kwa kutoa mafunzo kwa watalaam 10 juu ya kutambua aina za mwani unaotoa sumu. Aidha, Maabara imepatiwa vitendea kazi mbalimbali. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuimarisha na kuijengea uwezo Maabara ya Uchunguzi wa Sumu ya Mwani unaoelea kwenye Maji – Temeke kwa kuipatia vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi -Nyegezi. Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi-Nyegezi, imeendelea na majukumu yake ya kukusanya sampuli na kufanya uchunguzi wa sampuli za samaki na mazao ya uvuvi, maji na udongo ili kubaini kuwepo kwa masalia ya viuatilifu, kemikali,

vimelea, sumu, madini tembo na madawa ya viwandani. Katika mwaka 2011/2012, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Kuchunguza sampuli 1,374 ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ambapo kati ya hizo, 1,144 ni kwa ajili ya vimelea haribifu na 230 ni kwa ajili ya mabaki ya sumu, madawa na madini tembo. Uchunguzi huo ulifanyika katika Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi Nyegezi (Mwanza), Chemiphar (Uganda) na Shirika la Viwango la Afrika Kusini (*SABS*). Sampuli zote zilizochunguzwa zilionekana kukidhi viwango vya usalama vya kitaifa na kimataifa;

(ii) Kukamilisha taratibu za kupata ithibati kwa upande wa Kemikali kwa ajili ya uchunguzi wa viuatilifu na mabaki ya sumu; na

(iii) Kuimarisha maabara kwa kuipatia vifaa, kukarabati jengo la maabara na kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi watatu (3) na ya muda mfupi kwa watumishi wanne (4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuimarisha maabara kwa kuipatia vitendea kazi na mafunzo kwa watumishi. Aidha, itaendelea kukamilisha taratibu za kuomba ithibati kwa upande wa kemikali kwa ajili ya uchunguzi wa viuatilifu na mabaki ya sumu. Pia, maabara itawezeshwa kufanya uchunguzi wa sampuli za mazao ya uvuvi, maji na udongo ili kuhakiki vimelea, viuatilifu na madini tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuzaji wa viumbe kwenye maji. Wizara imeendelea kuimarisha ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa samaki na mazao yake. Katika mwaka 2011/2012, Wizara iliimarisha vituo saba (7) vya ufugaji wa samaki vya Karanga (Moshi), Musoma, Bukoba, Kingolwira, Luhira (Songea), Mwamapuli (Igunga) na Mtama (Lindi) ili kuongeza uwezo wa kuzalisha na kusambaza vifaranga vya samaki. Katika kipindi hiki vifaranga 2,686,400 vya perege vimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mara, Morogoro, Mtwara, Pwani, Ruvuma na Tanga na vifaranga 800,500 vya kambale vilipandikizwa kwenye bwawa la Mindu (Morogoro). Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kujenga mabwawa ya mfano ya Bukoba 2 na Nyamirembe (Chato) 4;

(ii) Kukarabati mabwawa 10 katika vituo vya Kingolwira (4), Luhira (3), Musoma (2) na Karanga (1);

(iii) Kukarabati nyumba na kununua vifaa vya uzalishaji wa vifaranga katika Kituo cha Nyamirembe;

(iv) Kufanya tathmini katika Kijiji cha Nyengedi ili kuongeza eneo la ufugaji samaki kwa ajili ya Kituo cha Mtama;

(v) Kutengeneza vizimba *(hapas)* 22 katika vituo vya Kingolwira (6) na Luhira (16) vyenye uwezo wa kuchukua vifaranga vya samaki 200 kila kimoja;

(vi) Kujenga nyumba ya kutunza joto *(green house)* yenye ukubwa wa mita za mraba 275 kwenye mabwawa ya kuzalishia vifaranga katika Kituo cha Luhira;

(vii) Kuanza majaribio ya kuzalisha vifaranga vya kiume *(monosex - all male)* katika kituo cha Kingolwira; na

(viii) Kuhamasisha wafugaji wa kaa 15 kuhusu teknolojia ya kutengeneza vizimba vya kunenepesha kaa katika kijiji cha Mkwaja (Pangani) ambapo vizimba 114 vimetengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuimarisha kituo cha kuzalisha mbegu za viumbe vya maji bahari cha Mbegani kwa kujenga tenki mbili (2) za kukuzia vifaranga vya samaki, kukarabati ofisi na kununua vitendea kazi vikiwemo kompyuta na samani. Aidha, maeneo ya kuanzisha vituo vya kutotolea vifaranga vya samaki yamepatikana katika vijiji vya Machui (Tanga) ekari 1.5 na Chihiko (Mtwara) ekari 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara imehamasisha wafugaji 30 kufuga samaki aina ya *Tilapia mossambicus* katika vijiji vya Mbuo na Tangazo (Mtwara Vijijini) ambapo vifaranga wa mbegu 110 vimepandikizwa. Aidha, wananchi 25

kutoka vijiji vya Msimbati na Mkubiru (Mtwara Vijijini) wamehamasishwa kuhusu ufugaji wa chaza ambapo Msimbati wametengeneza mifuko 112 ya kukuzia chaza wa lulu. Uzalishaji wa lulu umeongezeka kutoka vipande 607 mwaka 2010/2011 hadi vipande 925 mwaka 2011/2012. Pia, ufugaji wa kambamiti katika mabwawa ya kampuni ya Tanpesca (Mafia) umeendelea ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 231.5 mwaka 2010/2011 hadi tani 290 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha kilimo cha mwani ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 651 zenye thamani ya shilingi millioni 260.6 mwaka 2010/2011 hadi tani 660.75 zenye thamani ya shilingi milioni 264.5 mwaka 2011/2012. Ongezeko hili limetokana na matumizi ya teknolojia ya chelezo inayowezesha kupatikana kwa mbegu kwa mwaka mzima. Aidha, katika mwaka 2011/2012, Wizara imewezesha maafisa sita (6) kuhudhuria mafunzo ya shahada za uzamili katika fani ya ukuzaji viumbe kwenye maji katika vyuo vikuu mbalimbali ndani (3) na nje ya nchi (3). Katika mwaka 2012/2013, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuimarisha vituo 10 vya uzalishaji wa vifaranga vya maji baridi vya Kingolwira (Morogoro), Luhira (Songea), Mtama (Lindi) Nyamirembe (Chato), Mwamapuli (Igunga), Kigoma, Karanga (Moshi), Mwanza, Bukoba na Musoma ili kuzalisha na kusambaza vifaranga milioni 5 vya samaki aina ya perege na kambale;

(ii) Kujenga na kuendeleza vituo vitatu (3) vya kuzalisha mbegu za samaki wa maji bahari katika Mikoa ya Mtwara (Chihiko), Tanga (Machui), na Pwani (Mbegani);

(iii) Kuhamasisha na kuimarisha teknolojia ya ukulima wa mwani na kuongeza thamani ya zao hilo katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani; na

(iv) Kwa kushirikiana na taasisi za utafiti kuendeleza utafiti wa ukuzaji wa chaza na samaki aina ya *Tilapia mossambicus* kwenye maingilio ya mito na bahari *(brackish water)* katika Mikoa ya Tanga na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwezesha wafugaji wa viumbe kwenye maji. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imewezesha wafugaji wa viumbe kwenye maji kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa wafugaji 1,565 kuhusu ukuzaji viumbe kwenye maji katika Halmashauri za Temeke, Kinondoni, Ilala, Chamwino, Njombe, Musoma, Kilolo, Manispaa ya Morogoro, Morogoro Vijijini, Mtwara Vijijini, Mtwara-Mikindani, Bagamoyo, Lindi, Songea, Mbinga na Jiji la Tanga;

(ii) Kuhamasisha uanzishaji wa vikundi viwili (2) vya umoja wa wafugaji wa samaki vyenye jumla ya wanachama 105 katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Vikundi hivyo ni Kikundi cha Ufugaji wa Samaki cha Mwambao Tuungane Group (MWATUGRO) kilichopo katika kijiji cha Sudi (Lindi

Vijijini) na Umoja wa Wafugaji wa Samaki Mkoa wa Mtwara (UWASA); na

(iii) Kuhamasisha wakulima wa mwani 3,000 kuunda vikundi vya kuzalisha na kusindika mwani ambapo vikundi vya Umoja wa Wakulima wa Mwani - Vijiji vya Naumbu na Mkungu (Mtwara) na Umoja wa Wakulima wa Mwani Tanzania vimeanzishwa. Vikundi hivi vimeanza kuongeza thamani ya zao la mwani kwa kutengeneza sabuni. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi, imeendelea kutafuta na kutoa taarifa za masoko ya zao la mwani kwa wakulima wa zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuwawezesha wafugaji wa viumbe kwenye maji kwa kuwapatia vifaranga bora vya samaki, kuimarisha na kuhamasisha uanzishaji wa vikundi vya wafugaji wa viumbe kwenye maji na kutoa elimu ya ufugaji bora na kilimo cha mwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa takwimu za uvuvi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kusimamia na kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za uvuvi kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kutengeneza *Database* kwa ajili ya kuchambua na kuhifadhi takwimu za uvuvi *(Catch Assessment Survey Database)* na kutoa mafunzo ya kuitumia kwa watalaam 18, wawili (2) kutoka kila Halmashauri ya Jiji la Tanga; Manispaa za Lindi, Mtwara Mikindani,

Ilala; na Wilaya za Muheza, Pangani, Mkinga, Lindi Vijijini na Mtwara Vijijini;

(ii) Kutoa mafunzo ya ukusanyaji takwimu kwa wanachama 49 wa BMUs katika Halmashauri za Manispaa za Kinondoni (21) na Temeke (28); na Maafisa Uvuvi wa Manispaa za Kinondoni tatu (3) na Temeke tatu ( 3);

(iii) Kutoa mafunzo kuhusu ukusanyaji wa takwimu za wavuvi wadogo katika ukanda wa Ziwa Tanganyika kwa maafisa 33 kutoka Halmashauri za Kigoma Vijijini (8), Mpanda Vijijini sita (6), Nkasi (10) na Sumbawanga vitano (5); na Manispaa ya Kigoma Ujiji vinne (4); na

(iv) Kuendelea kuratibu ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itafanya sensa ya uvuvi (*Fisheries Frame Survey)* katika maeneo ya ukanda wa bahari na maziwa, kukusanya takwimu za uvuvi kwa kutumia mfumo wa *Catch Assessment Survey (CAS)* na kutengeneza Mfumo wa ukusanyaji na uchambuzi wa Takwimu za uvuvi za kibiashara *(web based database).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa mifugo na uvuvi. Uwezeshaji na uratibu wa tafiti. Kuanzia mwaka 2011/2012, Serikali imeanza kutenga fedha za utafiti kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* ambapo taasisi za utafiti wa mifugo na

uvuvi zimepatiwa jumla ya shilingi bilioni 3.2. Kati ya fedha hizo, taasisi za Mifugo na Uvuvi zilipata shilingi bilioni 2.6 na milioni 600 sawia. Aidha, Taasisi za utafiti wa mifugo na uvuvi zimepatiwa jumla ya shilingi milioni 730.6 kutoka *Association of Strengthening Agriculture Research in Eastern and Central Africa (ASARECA)* ambapo TAFIRI imepatiwa shilingi milioni 380.0 na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo shilingi milioni 350.6. Pia, Taasisi za Utafiti wa Mifugo zimepatiwa shilingi milioni 327.9 kutoka *East African Agricultural Productivity Project (EAAPP).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuratibu na kutathmini huduma za utafiti na maendeleo ya ufugaji na uvuvi kulingana na programu zake. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali na watafiti wa ndani na nje ya nchi zikiwemo SUA, COSTECH, TCU, EAC, ASARECA, B&MGF, CCAFS, CGIAR na IAEA katika kutayarisha mikakati na mipango ya utafiti, kuratibu tafiti katika maeneo muhimu ya ufugaji endelevu na wa tija, mabadiliko ya tabia nchi, uhakika wa chakula na tiba za magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya miradi 13 ya utafiti kupitia mfuko wa *Zonal Agricultural Research and Development Fund (ZARDEF)* imekamilika na matokeo yamepelekwa kwa wafugaji, na miradi mingine 38 inaendelea. Pia, Wizara iliendelea kugharamia mafunzo ya watafiti saba (7) wa mifugo (wawili katika ngazi ya uzamivu na watano uzamili). Aidha, watafiti 24 (16 mifugo na nane uvuvi) wanaendelea na masomo katika ngazi za Uzamili na

uzamivu kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuratibu, kufuatilia na kutathmini huduma za utafiti na maendeleo ya mifugo na uvuvi kulingana na programu zilizotayarishwa pamoja na kuwezesha taasisi za utafiti wa mifugo na uvuvi kuendelea na utafiti;

(ii) Kuimarisha mfumo wa utunzaji kumbukumbu za utafiti wa mifugo na Uvuvi nchini na kushirikiana na Taasisi za kitaifa na kimataifa kuratibu utafiti shirikishi wa mifugo;

(iii) Kuwezesha kanda saba (7) za kilimo na ufugaji kuibua miradi ya utafiti itakayogharamiwa na mfuko wa ZARDEF kwa kushirikisha wafugaji kulingana na vipaumbele vya kanda kupitia programu ya ASDP; na

(iv) Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalam (*technical backstoping)* kwa watafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania. Wizara kwa kushirikiana na wadau iliandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania *(The Tanzania Livestock Research Institute Act - TALIRI)* ambayo ilipitishwa na Bunge tarehe 12 Aprili, 2012 na Mheshimiwa Rais kuipitisha kuwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania Na. 4 ya mwaka 2012. Sheria hii itasimamia na kuendeleza shughuli za utafiti wa mifugo nchini. Aidha, itaimarisha ushirikiano na asasi za utafiti ndani na nje ya nchi na uwajibikaji wa watafiti

katika kubuni na kupata rasilimali zaidi kwa ajili ya utafiti, ikiwa ni pamoja na kusambaza matokeo ya utafiti kwa walengwa. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itakamilisha taratibu za kuendesha *TALIRI*. Katika mwaka 2011/2012, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa kupitia vituo vyake saba (7) vya Mpwapwa, Tanga, Uyole, West Kilimanjaro, Kongwa, Mabuki na Naliendele iliendelea na utafiti wa mifugo kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mifugo nchini. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutathmini na kusambaza mifugo bora vijijini. Taasisi na vituo vyake ina jumla ya ng'ombe (1,753), mbuzi (1,320), kondoo (341) na kuku (858) kwa ajili ya utafiti. Aidha, ili kuongezea idadi hiyo, jumla ya ng'ombe wa asili 20 aina ya Singida White na Iringa red walinunuliwa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini ya ubora wa kosaafu kwa lengo la kuwaboresha na kuwasambaza kwa wafugaji. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa ndama aina ya Singida White walizaliwa wakiwa na wastani wa uzito wa kilo 18.8 kwa madume na kilo 18.2 kwa majike. Pia, ng'ombe 57 aina ya Kifipa wameendelea kutathminiwa katika shamba la mifugo la Sao Hill. Wastani wa uzito wa ndama ulikuwa ni kilo 16.7 katika mtawanyiko wa kilo 15 – 20. Vilevile, jumla ya ng'ombe 49 aina ya Ankole walifanyiwa tathmini katika kituo cha Mabuki na wastani wa uzito wa kuzaliwa kwa ndama ni kilo 27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, iliendelea na tathmini ya mbuzi ambapo jumla ya mbuzi 100 aina za Buha, Red Maasai, Pare White na Red Sonjo walinunuliwa kwa ajili ya

tathmini katika vituo vya Mpwapwa na West Kimanjaro. Aidha, jumla ya kondoo 34 aina za Red Maasai, Dorper na Black Head Persian (BHP) walinunuliwa kwa ajili ya tathmini katika kituo cha West Kilimanjaro. Pia, kuku wa asili aina 13 za Kuchi, Sasamala, Kawaida, Mtewa, Kishingo, Bukini, Kisunzu, Kuza, Sukuma, Msumbiji, Katewa, Mandendenga na Njachama wameendelea kutathminiwa katika vituo vya Mpwapwa na Uyole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilisambaza madume bora ya ng'ombe 103 aina ya Mpwapwa kwa wafugaji kwenye Wilaya za Mpwapwa (14), Chamwino (30), Kisarawe (30), Kongwa (19), Manyoni (6), Mbeya vijijini (2) na Jiji la Dar es Salaam (2) kwa lengo la kuboresha ng'ombe wa asili. Aidha, jumla ya ng'ombe 58 aina ya Friesian kutoka vituo vya utafiti vya Tanga (41) na Uyole (17) walisambazwa kwenda Mikoa ya Iringa, Mbeya na Tanga. Pia, madume 6 aina ya Ankole kutoka kituo cha utafiti cha Mabuki yalisambazwa kwa wafugaji wa kijiji cha Mabuki. Mifugo hii inayosambazwa ni kwa ajili ya utafiti katika mazingira ya wafugaji kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina utaratibu wa kufanya tathmini ya mifugo inayosambazwa kwa wafugaji baada ya miaka 5. Tathmini iliyofanyika kwa madume ya ng'ombe aina ya Mpwapwa 192 yaliyosambazwa katika kipindi cha mwaka 2006 hadi 2010 kwa wafugaji katika Wilaya za Mpwapwa, Bahi, Manyoni na Iramba, imebaini kuwa jumla ya ndama chotara 7,500 wamezaliwa kutokana na madume hayo katika Wilaya za Mpwapwa (2,125), Iramba

(2,600), Manyoni (1,250) na Bahi (1,425). Madume chotara yenye umri wa miaka minne (4) yaliweza kununuliwa kwa bei ya wastani wa shilingi 1,200,000 ikilinganishwa na shilingi 300,000 kwa ng'ombe wa asili wa umri huo. Aidha, katika mwaka 2011/2012, wafugaji kupitia Halmashauri waliuziwa jumla ya mbuzi 133 aina ya Malya kama ifuatavyo; Kisarawe (60), Chamwino (60), Manispaa ya Dodoma (1), Kongwa (10) na Handeni (2). Pia, jumla ya nguruwe bora 60 aina ya Landrace, walisambazwa kwa wafugaji katika Wilaya za Mbeya Mjini (26), Kyela (14), Mbarali (5), Mbozi (5), Rungwe (6) na Mbeya Vijijini (9).

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa malisho ya mifugo. Katika mwaka 2011/2012, utafiti wa malisho na utunzaji wa benki ya vinasaba uliendelea ambapo jumla ya vinasaba 152 vilifanyiwa tathmini katika Taasisi ya Utafiti ya Mifugo ya Mpwapwa (80) na Kituo cha Utafiti Uyole (72). Aidha, jumla ya miche 11,640 ya aina za Leucaena diversifolia (7,198), Leucaena pallida (426) na Calliandra (4,016) ilizalishwa na kusambazwa katika Wilaya za Mkoa wa Rukwa. Pia, kilo 999 za mbegu za Rhodes grass na kilo 540 za Desmodium zilizalishwa na kusambazwa kwenye vikundi vya wafugaji wa Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha Vituo Vya Utafiti. Katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kuimarisha vituo vya utafiti kwa kuvipatia vitendea kazi muhimu na kukarabati miundombinu ya majengo, maji, josho, umeme na maboma ya mifugo. Aidha, ujenzi wa *rest house* Mpwapwa, nyumba 6 za watumishi na maabara ya sayansi ya nyama (Mabuki), maabara ya

lishe ya mifugo (Tanga) na jengo la ofisi (Naliendele) uliendelea. Vilevile, ukarabati wa maabara ya *Embryo Transfer* (Mpwapwa) na ujenzi wa maabara ya teknolojia ya maziwa (Uyole) unaendelea. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kununua ng'ombe aina ya Iringa Red (20) na Maasai (20); na kusambaza madume ya ng'ombe aina ya Mpwapwa (120) na mbuzi aina ya Malya (120) kwa lengo la kutathmini na kuboresha kosaafu ya mifugo wa asili;

(ii) Kuzalisha na kusambaza kwa wadau kilo 1,500 za mbegu za nyasi na kilo 500 za mikunde kwa lengo la kuendeleza utafiti wa malisho katika ngazi ya mfugaji;

(iii) Kufanya tathmini ya teknolojia za uzalishaji na tija zilizopelekwa kwa wafugaji;

(iv) Kuboresha miundombinu ya utafiti kwa kuendelea na ujenzi wa maabara ya sayansi ya nyama (Mabuki), *Embryo Transfer* (Mpwapwa), maabara ya teknolojia ya maziwa (Uyole), maabara za lishe ya mifugo (Mpwapwa, Tanga na *West Kilimanjaro*), ujenzi na ukarabati wa nyumba za watumishi na ofisi; na

(v) Kutekeleza miradi ya utafiti wa mifugo ya kuboresha uzalishaji wa ng'ombe wa nyama na maziwa; nguruwe na masoko; kuku wa asili na malisho kwa ufadhili wa *ASARECA, COSTECH* na *EAAPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa uvuvi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)* imeendelea na tafiti mbalimbali ili kubaini wingi, mtawanyiko, aina za rasilimali zinazopatikana katika maji ya asili na ukuzaji wa viumbe kwenye maji. Kazi zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya tafiti katika ufugaji wa samaki na utafiti wa uhifadhi wa samaki kwa kutumia nishati ya jua;

(ii) Kufanya tafiti katika maziwa ya Itamba, Ilamba, Masoko, Kyungululu, Itende, Ikapu, Ndwati katika Wilaya ya Rungwe na Kingili katika Wilaya za Kyela na Rungwe. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa maziwa haya yana bioanuwai kubwa hivyo yanaweza kutumika kwa elimu ya viumbe na tafiti za kisayansi. Pia, maziwa ya Itamba, Masoko na Kyungululu yanafaa kwa utalii rafiki wa mazingira *(eco-tourism);*

(iii) Kubaini maeneo ya bahari yenye samaki wengi kupitia mradi wa *African Monitoring of Environment for Sustainable Development-AMESD*; na

(iv) Kukarabati meli ya RV Kiboko inayotumika kwa utafiti katika Bahari ya Hindi na kukipatia kituo cha Sota boti na injini kwa ajili ya utafiti na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea na utafiti wa samaki na mazingira katika maziwa makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa), maziwa madogo, mito na Bahari ya Hindi;

(ii) Kusambaza kwa wavuvi matokeo ya utafiti wa wingi wa samaki ili kuongeza ufanisi kwa wavuvi;

(iii) Kufanya utafiti wa ufugaji samaki ili kuwawezesha wananchi kupata elimu ya uzalishaji wa vifaranga vya samaki, vyakula bora vya samaki, kutambua maeneo stahiki ya ufugaji samaki na teknolojia ya ufugaji wa viumbe kwenye maji;

(iv) Kuendelea kuimarisha miundombinu na mazingira ya utafiti katika vituo vya Dar es Salaam, Sota, Kigoma na Kyela; na

(v) Kununua vitendea kazi kwa ajili ya vituo vya Kyela, Mwanza, Sota na Makao makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya mifugo na uvuvi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imeanzisha Wakala wa Mafunzo ya *Mifugo (Livestock Training Agency-LITA)* na Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (*Fisheries Education and Training Agency- FETA)* kwa lengo la kuboresha mafunzo ya mifugo na uvuvi ambazo zimeanzishwa rasmi kwa matangazo katika Gazeti la Serikali kwa GN. No. 355 na 356 ya 1 Septemba, 2011. LITA inajumuisha vyuo vya mafunzo ya mifugo vya Morogoro, Tengeru, Mpwapwa, Buhuri, Madaba na Temeke; na FETA inajumuisha vyuo vya mafunzo ya uvuvi vya Mbegani na Nyegezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, jumla ya wanafunzi 1,630 (Stashahada 977 na Astashahada 653) walidahiliwa katika vyuo vya mafunzo ya mifugo. Kati ya hao, 768 wamemaliza mafunzo mwezi Juni, 2012 wakiwemo 432 wa Stashahada na 336 wa Astashahada. Aidha, vyuo vya mafunzo ya uvuvi vilidahili jumla ya wanafunzi 675 (Stashahada 133 na Astashahada 542). Kati ya hao, 302 wamemaliza mafunzo yao mwezi Juni, 2012 wakiwemo 216 wa Stashahada na 86 wa Astashahada. Vilevile, mafunzo ya muda mfupi ya ufundi stadi yalitolewa kwa wanafunzi 47 katika vyuo vya uvuvi. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya maafisa ugani 465 waliohitimu katika vyuo hivyo wameajiriwa na Halmashauri 105.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau wakiwemo *Heifer international Tanzania, World Vision*, Taasisi za Dini, MVIWATA na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji 350 na wavuvi 68. Mafunzo haya yalihusu ufugaji bora wa kuku, ng'ombe na mbuzi wa maziwa, ufugaji wa samaki, malisho ya mifugo, uboreshaji wa zao la ngozi, usindikaji wa maziwa, uchakataji wa samaki, uvuvi endelevu na afya ya mifugo. Ili kuimarisha uwezo wa vyuo, wakufunzi tisa (9) wanapata mafunzo katika ngazi ya Shahada ya Uzamili na mmoja Shahada ya Uzamivu. Aidha, Wizara imeendelea kukarabati majengo katika vyuo nane (8) vya mifugo na uvuvi na kuvipatia vitendea kazi pamoja na samani. Katika mwaka 2012/2013 Wizara itaendelea kujenga uwezo

wa wakala za mafunzo ya mifugo na uvuvi ili kuweza kudahili wanafunzi 1,700 wa mifugo na 800 wa uvuvi katika ngazi ya Stashahada, Astashahada pamoja na mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ugani. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ilisambaza nakala za vipeperushi 25,000, mabango 6,600 na vijitabu 1,500 kwa wadau kuhusu ufugaji bora kwa lengo la kuongeza wingi, tija na mapato kwa wafugaji. Aidha, vipindi 52 vya redio na 12 vya luninga kuhusu ufugaji na uvuvi bora viliandaliwa na kurushwa hewani. Pia, kwa kushirikiana na Halmashauri za Mikoa ya Mwanza, Tabora na Kagera, wafugaji 378 walipatiwa mafunzo juu ya ufugaji wa kibiashara kupitia vyuo vya Mafunzo ya Wafugaji - Mabuki na Kikulula. Vilevile, Wizara ilikarabati ofisi ya chuo cha wafugaji cha Kikulula (Karagwe) na kununua samani kwa chuo cha wafugaji Mabuki (Misungwi). Pia, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Rorya imeanzisha kituo cha mafunzo kwa wafugaji na wavuvi cha Gabimori ambapo vyumba viwili (2) vya madarasa na ofisi vimekamilika na jengo la mafunzo kwa vitendo linaendelea kujengwa. Vilevile, Wizara ilishiriki katika maadhimisho ya Kitaifa na Kimataifa ya Nanenane, Siku ya Chakula Duniani na Siku ya Mvuvi Duniani kwa lengo la kusambaza teknolojia na elimu ya ufugaji, uvuvi na usindikaji wa mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia mradi wa *EAAPP* iliwawezesha wafugaji wa mfano 18 kufanya ziara ya mafunzo katika Mikoa ya Kilimanjaro na

Arusha; na wengine 10 nchini Kenya. Aidha, teknolojia 14 kuhusu ufugaji wa ng'ombe wa maziwa zilizobuniwa na kuhakikiwa ziliainishwa katika Kanda za Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini na kusambazwa kwa wafugaji kwa matumizi. Pia, vipindi sita (6) vya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa vilivyohusisha wafugaji vilitayarishwa na kurushwa katika redio na televisheni. Katika kuwajengea uwezo maafisa ugani, Wizara imegharamia mafunzo ya shahada ya uzamili kwa wataalam wawili (2) na muda mfupi watatu (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutoa huduma ya ugani katika sekta ya uvuvi ambapo wavuvi 300 kutoka Mikoa ya Iringa, Dodoma, Morogoro, Mara, Mwanza na Tabora walipatiwa elimu ya kufanya shughuli mbadala za kiuchumi ili kupunguza nguvu ya uvuvi kutokana na kupungua kwa rasilimali za uvuvi kwenye maji ya asili. Aidha, elimu ya ufugaji wa samaki katika mabwawa ilitolewa kwa maafisa ugani 12, vikundi 12 vya wafugaji wa samaki vyenye wanachama 62 na wafugaji wa samaki 150 katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Mwanza, Mara, Morogoro na Tabora. Pia, nakala za vijitabu 280 na vipeperushi 400 kuhusu mbinu bora za ufugaji wa samaki na hifadhi ya mazao ya uvuvi vimechapishwa na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuandaa na kurusha hewani vipindi 52 vya redio na 12 vya luninga kuhusu ufugaji bora na uvuvi endelevu;

(ii) Kutoa mafunzo kwa wataalam 100 kutoka Halmashauri mbalimbali watakaotumika kufundisha wataalam wengine kuhusu dhana ya Shamba Darasa;

(iii) Kutayarisha na kushiriki kwenye maonesho *(demonstration)* ya uvuvi katika ngazi ya Halmashauri na kutoa mafunzo elekezi kuhusu ufugaji wa samaki kwa Halmashauri zilizo jirani na vituo vya uzalishaji wa vifaranga vya samaki;

(iv) Kuwawezesha maafisa ugani sita (6) wa mifugo na uvuvi kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu;

(v) Kukarabati na kuimarisha vituo vya mafunzo kwa wafugaji vya Mabuki (Misungwi), Gabimori (Rorya) na Kikulula (Karagwe) ili viweze kutoa mafunzo kwa wafugaji wengi zaidi;

(vi) Kushirikiana na wadau wengine kuandaa na kushiriki katika maadhimisho mbalimbali ya Kitaifa ikiwa ni pamoja na Nanenane, Wiki ya Maziwa, Siku ya Mvuvi Duniani, Siku ya Chakula Duniani na Siku ya Veterinari Duniani; na

(vii) Kushirikiana na nchi za Afrika Mashariki kutekeleza mradi wa *EAAPP* kwa kuainisha teknolojia za

uzalishaji wa maziwa, kuzijaribu na kuzipeleka kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa ubora wa mazao na huduma za mifugo. Bodi ya Nyama Tanzania. Bodi ya Nyama Tanzania iliyoundwa kwa Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006 imeendelea kuratibu tasnia ya nyama nchini. Katika mwaka 2011/2012, Bodi ya Nyama Tanzania imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuajiri watumishi wawili (2) wa Sekretarieti ya Bodi na taratibu za kuajiri watumishi wengine wawili (2) zinaendelea;

(ii) Kujenga uwezo wa wadau ili kuanzisha majukwaa ya wadau wa nyama katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Mwanza na Rukwa;

(iii) Kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuainisha jumla ya wadau 45,455 wa tasnia ya nyama katika Mikoa ya Arusha, Manyara, Iringa, Rukwa, Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam. Kati ya hao, wafugaji ni 43,129, wafanyabiashara wa mifugo na nyama 2,315 na wasindikaji 11;

(iv) Kuhamasisha na kuelimisha wadau 287 kutoka katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Iringa, Mbeya na Rukwa juu ya Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006 na kanuni zake;

(v) Kuhamasisha uundaji wa Chama cha Wafugaji Kitaifa ambapo rasimu ya Katiba ya Chama hicho imekwisha andaliwa na kupelekwa kwa vyama vya wafugaji katika ngazi za Wilaya ili kujadiliwa na kupata maoni ya wafugaji;

(vi) Kushirikiana na *TBS* na *TFDA* kuelimisha wadau juu ya uzalishaji nyama unaozingatia viwango vya ubora wa nyama kitaifa na kimataifa na kuweka utaratibu wa kuthibiti ubora wa nyama;

(vii) Kuhamasisha wadau wa tasnia ya nyama kushiriki katika maonesho ya nanenane, wiki ya Chakula Salama na Miaka 50 ya Uhuru ambapo wadau 4 *(NARCO, TANMEAT 2002 LTD, Msigani Poultry Breeding Farm* na mtotoleshaji wa vifaranga wa kuku wa asili) walishiriki; na

(viii) Kufanya vikao vinne (4) vya kisheria vya Bodi na Baraza la Mwaka la Wadau wa Nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Bodi ya nyama itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuajiri watumishi sita (6) wa Sekretariati ya Bodi ya Nyama Tanzania;

(ii) Kuendelea kuhamasisha wadau kuhusu sheria na kanuni za nyama na kusimamia utekelezaji wa sheria;

(iii) Kuendelea kushirikiana na TBS na TFDA kuelimisha wadau juu ya viwango vya ubora wa

nyama vilivyopo na kuweka utaratibu wa kudhibiti ubora wa nyama;

(iv) Kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kusajili wadau wa tasnia ya nyama na kuanzisha mtandao wa ushirikiano kiuzalishaji ili kuhakikisha uendelevu wa tasnia;

(v) Kushirikiana na Tanzania Private Sector Foundation kujenga uwezo wa kiushindani miongoni mwa wadau wa sekta binafsi ili kuongeza ufanisi katika tasnia;

(vi) Kushirikiana na vyama vya wadau kuhamasisha uanzishwaji, kujiunga na kuimarisha vyama vya wadau ili kushiriki kikamilifu katika kuiendeleza tasnia ya nyama;

(vii) Kuhamasisha wadau wa tasnia ya nyama kushiriki katika maonesho ya Nanenane kitaifa, Wiki ya Chakula Salama na maonesho mengine ya biashara; na

(viii) Kuandaa na kuendesha vikao vya Bodi na Baraza kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Maziwa Tanzania. Tasnia ya maziwa nchini imeendelea kuratibiwa na Bodi ya Maziwa Tanzania iliyoundwa kwa Sheria ya Maziwa, Sura 262. Katika mwaka 2011/2012, Bodi ya Maziwa imeendelea na uratibu wa Programu ya Unywaji wa Maziwa Shuleni ambayo inatekelezwa kwenye shule 99 na kunufaisha jumla ya wanafunzi

64,655. Kazi nyingine zilizotekelezwa na Bodi ni pamoja na:-

(i) Kuajiri watumishi wanne (4) kwa ajili ya kuimarisha Sekretariati ya Bodi;

(ii) Kusajili wadau wa maziwa 17 wakiwemo wazalishaji watano (5), wasindikaji watatu (3), muuzaji mmoja (1), mtoa huduma mmoja (1) na waagizaji saba (7) katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Mara, Ruvuma na Kagera kwa lengo la kuratibu shughuli zao;

(iii) Kuandaa maadhimisho ya Siku ya Unywaji wa Maziwa Shuleni Duniani yaliyofanyika Arusha mwezi Septemba 2011 na maadhimisho ya Wiki ya Uhamasishaji Unywaji Maziwa nchini yaliyofanyika katika Manispaa ya Moshi, mwezi Mei/Juni 2012;

(iv) Kuhamasisha na kuelimisha wadau 300 juu ya Sheria ya Maziwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Kilimanjaro, Tanga, Manyara, Mbeya, Mwanza na Arusha;

(v) Kuitisha vikao vitano (5) vya Bodi na Baraza la Wadau wa Maziwa kwa mujibu wa sheria; na

(vi) Kushiriki kwenye mkutano wa Baraza la Wasimamizi wa Sekta ya Maziwa wa Nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki *(East Africa Dairy Regulatory Authorities Council – EADRAC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Bodi ya Maziwa itaendelea kufanya kazi zake ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kutoa mafunzo kwa wakaguzi 200 wa maziwa na kutoa testing kits kwa Halmashauri 40;

(ii) Kuendelea kuratibu mpango wa maziwa shuleni katika Halmashauri za Hai, Moshi, Jiji la Tanga, Njombe Mjini, Njombe, Sengerema na Musoma na kuhamasisha uanzishwaji wa mpango wa maziwa shuleni katika shule tatu (3) za Mkoa wa Dar es Salaam;

(iii) Kuendelea kuratibu maadhimisho ya Siku ya Unywaji wa Maziwa Shuleni Duniani mwezi Septemba 2012 na Wiki ya Uhamasishaji Unywaji Maziwa Nchini yatakayofanyika Songea, mwezi Mei/Juni 2013;

(iv) Kuanzisha mfumo wa takwimu za masoko ya maziwa na kuandaa *Code of Milk Hygiene*;

(v) Kuitisha vikao vinne (4) vya Bodi na kimoja cha Baraza la Wadau wa Maziwa kwa mujibu wa Sheria;

(vi) Kutoa mafunzo kwa watumishi watano (5) ili kuwajengea uwezo;

(vii) Kushiriki mikutano miwili (2) ya kikanda na kimataifa; pamoja na kuratibu na kushiriki maonesho ya Sabasaba, Nanenane na Wiki ya Maziwa; na

(viii) Kuhamasisha na kuelimisha wadau 400 kuhusu Sheria ya Maziwa katika Mikoa ya Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Veterinari Tanzania. Wizara kupitia Baraza la Veterinari iliendelea kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na wataalam wa huduma za afya ya mifugo, katika sekta za umma na binafsi. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kusajili madaktari 33 na kuorodhesha na kuandikisha wataalam wasaidizi 121 na kusajili vituo 10 vya huduma za mifugo;

(ii) Kusambaza nakala 500 za kanuni kuhusu maadili ya wataalam wa huduma za mifugo kupitia Halmashauri na taasisi za mifugo, nakala 150 za michoro kwa ajili ya viwango vya vituo vya huduma za mifugo;miongozo mitatu (3) ya matumizi ya dawa na vifaa tiba; na miongozo miwili (2) juu ya viwango vya taaluma katika mitaala;

(iii) Kutoa mafunzo kuhusu maadili kwa wataalam wa mifugo 112 wa uhimilishaji, ukaguzi wa nyama, ufundi sanifu wa maabara ya veterinari, wahitimu 547 wa SUA na vyuo vya mafunzo ya mifugo;

(iv) Kuhakiki viwango vya kitaaluma katika chuo cha Visele (Mpwapwa);

(v)Kufanya ukaguzi wa vituo 111 na maadili ya watoa huduma katika Halmashauri za Mikoa ya Mbeya

(22) Shinyanga (2), Iringa (4), Dar es Salaam (24), Ruvuma (9), Singida (6) na Manyara (44);

(vi) Kujenga uwezo wa Halmashauri wa kukagua na kusimamia maadili ya taaluma ya veterinari, ambapo wakaguzi 41 wameteuliwa kutekeleza majukumu hayo;

(vii) Kuhamasisha watoa huduma 173 wa sekta ya umma na sekta binafsi kutoka Kanda za Ziwa, Magharibi, Kati, Kaskazini na Mashariki kuhusu ushirikiano *(PPP)* katika utoaji huduma bora za mifugo; na

(viii) Kufanya mikutano miwili (2) ya kisheria ya Baraza la Veterinari, vikao 12 vya Sekretariati, vitatu (3) vya Kamati za Baraza (Disciplinary, Pharmaceutical Advisory and Registration and Examination) ambapo wataalam watatu (3) walichukuliwa hatua kwa kukiuka maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Baraza litaendelea kusimamia ubora wa huduma za mifugo nchini na kuimarisha ukaguzi kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kusajili madaktari wa mifugo 35, kuandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi 300, kusajili vituo vya kutolea huduma 25 na kuratibu mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wataalam 200 wa huduma za mifugo;

(ii) Kuwezesha vikao vinne (4) vya Baraza na sita (6) vya Kamati na Sekretariati ya Baraza;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa maadili katika Halmashauri 27 na wataalam 350 wa maabara, wahimilishaji, afya ya mifugo na wakaguzi wa mazao ya mifugo kwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma, *TVA, TAVEPA* na *TSAP*;

(iv) Kushirikiana na wakaguzi wa Halmashauri, Mikoa na kanda kufanya ukaguzi wa vituo 200 vya huduma za mifugo yakiwemo mashamba makubwa;

(v) Kuhamasisha matumizi ya viwango vya taaluma katika mashamba makubwa 15 ya mifugo, vyuo 6, makampuni 27 yanayoshiriki katika kutoa huduma za mifugo na Halmashauri 27 ambazo hazina wataalam wa afya ya mifugo;

(vi) Kuhakiki matumizi ya mitaala ya veterinari katika vyuo vya mafunzo ya mifugo nchini kwa lengo kuvitambua na kusajili wahitimu;

(vii) Kujenga uwezo wa Baraza na Sekretarieti kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi; na

(viii) Kuhakiki ubora wa wahitimu wa taaluma ya veterinari kutoka vyuo vya mafunzo ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa mazao na pembejeo za mifugo. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

imefanya ukaguzi katika maduka 14 ya jumla na 51 ya reja reja yanayotoa huduma za uuzaji wa dawa, chanjo, vyakula vya mifugo na vifaa tiba vya mifugo. Jumla ya viwanda 29 vya kusindika vyakula vya mifugo katika Jiji la Dar es Salaam vilikaguliwa na wazalishaji walishauriwa kuzingatia mbinu bora za uzalishaji. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itatoa mafunzo kwa wakaguzi 14 wa pembejeo za mifugo na kukagua viwanda 42 vinavyosindika vyakula vya mifugo hasa vyakula vya kuku kwa ajili ya kusimamia ubora na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilihakiki sifa za Wakaguzi wa Nyama 663 kutoka Halmashauri ambapo 240 waliteuliwa na majina yao kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali GN. Na. 77. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itatoa mafunzo rejea kwa wakaguzi 140 wa nyama na ngozi katika Halmashauri pamoja na kuendelea na zoezi la ukaguzi wa machinjio na uhakiki wa wakaguzi wa nyama na ngozi. Mafunzo yanatarajiwa kuboresha machinjio katika Halmashauri ambayo kwa sehemu kubwa bado hayakidhi viwango. Natoa wito kwa Halmashauri kusimamia usafi wa machinjio katika maeneo yao ili kulinda afya za walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu imeendelea kusimamia rasilimali za bahari kwenye maeneo ya hifadhi. Katika mwaka 2011/2012, kitengo kwa kushirikiana na wadau kilifanya mapitio ya Mipango ya Jumla ya Menejimenti *(General*

*Management Plans)* ya Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia na Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma na Mpango Mkakati wa Taasisi ambao muda wake umekwisha. Aidha, kilifanya doria ya siku-kazi 386 kwenye maeneo ya Hifadhi na Maeneo Tengefu zilizowezesha kukamatwa kwa nyavu aina ya monofilamenti 27, kokoro 30, baruti 15 na watuhumiwa 12 walifunguliwa kesi; na kukamilisha ujenzi wa nyumba nne (4) za watumishi katika Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma kupitia ufadhili wa *UNDP*. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:

(i) Kuendelea kuvutia wawekezaji kwa kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo maeneo yote ya hifadhi na taratibu za uwekezaji unaozingatia utalii rafiki wa mazingira *(eco-tourism);*

(ii) Kushiriki katika maonesho mbalimbali kwa lengo la kujitangaza yakiwemo maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Miaka 50 ya Uhuru, *Karibu Travel and Tourism Fair* na *INDABA Trade Fair* - Afrika Kusini;

(iii) Kuandaa na kurusha hewani vipindi viwili (2) vya luninga, kuchapisha na kusambaza makala tatu (3) na vipeperushi nakala 12,000 kuhusu vivutio vya utalii na shughuli za uhifadhi;

(iv) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi watatu (3) na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi sita (6) katika fani mbalimbali zinazohusu uhifadhi wa bahari na Maeneo Tengefu; na

(v) Kununua boti yenye kioo chini *(glass bottomed boat)* ya Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma kwa ufadhili wa Kampuni ya *British Gas International* kwa lengo la kutoa elimu ya mazingira chini ya bahari kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Taasisi ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu itaendelea kulinda na kuhifadhi rasilimali za bahari katika maeneo yote ya hifadhi kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kufanya doria kwa siku kazi 450 kudhibiti uvuvi haramu kwenye maeneo ya hifadhi;

(ii) Kuajiri watumishi wapya 13 ili kuimarisha ulinzi wa rasilimali ya uvuvi katika Hifadhi mpya ya Silikanti Tanga;

(iii) Kuendelea kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo yote ya hifadhi na taratibu za uwekezaji zinazozingatia utalii rafiki wa mazingira *(eco-tourism*);

(iv) Kuimarisha na kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi kwa kuwapa vitendea kazi na mafunzo ya muda mfupi na mrefu;

(v) Kufanya ufuatiliaji wa rasilimali za bahari hususan samaki, kasa, mikoko na matumbawe ili kubaini viwango vilivyofikiwa vya uhifadhi wa rasilimali hizo;

(vi) Kuandaa Kanuni kutokana na Mipango ya Jumla ya Menejimenti ya Hifadhi za Hifadhi ya Bahari ya Silikanti – Tanga, Hifadhi ya Bahari Mafia na Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma;

(vii) Kuendelea kutangaza kisheria maeneo zaidi ya hifadhi ili kulinda rasilimali ambazo kwa sasa ziko hatarini kutoweka kutokana na uvunaji usio endelevu; na

(viii) Kufanya maandalizi ya kuanzisha maeneo ya hifadhi kwenye maji baridi baada ya kukamilika marekebisho ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya 1994 kwa lengo la kulinda na kuhifadhi rasilimali za uvuvi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing Authority – DSFA)*. Majukumu makuu ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu ni kusimamia na kuendeleza uvuvi katika Bahari Kuu. Katika mwaka 2011/2012 Mamlaka ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mamlaka ambalo limejengwa eneo la Fumba Zanzibar na kuzinduliwa rasmi na Rais Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume mwezi Januari, 2012;

(ii) Kutoa leseni za uvuvi katika Bahari Kuu ambapo leseni 39 zilitolewa kwa meli kutoka nchi za Hispania

na Ufaransa pekee na jumla ya Dola za Kimarekani 1,256,118 zilikusanywa ikilinganishwa na Dola 2,111,400 zilizokusanywa kutokana na leseni 72 kwa mwaka 2010/2011. Sababu kuu iliyochangia kutoa leseni chache ikilinganishwa na kipindi kilichopita ni pamoja na uharamia baharini;

(iii) Kwa kushirikiana na Jeshi la Wanamaji, Polisi na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) doria za saa 280 za anga na maji zilifanyika ili kudhibiti uvuvi haramu;

(iv) Kufuatilia utendaji wa meli saba za uvuvi zilizosajiliwa na Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Bahari Zanzibar *(Zanzibar Maritime Authority)* na kupewa leseni na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali ya Australia, Kamisheni ya Uvuvi wa Jodari katika Bahari ya Hindi *(Indian Ocean Tuna Commission - IOTC),* Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Bahari *(International Maritime Organisation – IMO)* na Jumuiya ya Ulaya inafuatilia taarifa za meli za FV Baiyangdian, FV Wutaishi Anhui 44 na FV Shaanxi Henan 33 zinazodaiwa kupeperusha bendera ya Tanzania na kuendesha uvuvi haramu katika Bahari ya Kusini karibu na Bara la Antarctic, lakini hazijapewa leseni na Mamlaka;

(v) Mamlaka imepokea na kuzamisha baharini vifaa viwili (2) vya kuvutia samaki *(Fish Agregating Devices - FADs)* na kufanya jumla ya vifaa kuwa sita (6). Tathmini ya uvuvi wa kibiashara kwa kutumia *FADs* kwa kushirikiana na *TAFIRI* inaendelea;

(vi) Mamlaka kwa kushirikiana na *Indian Ocean Tuna Commision (IOTC) na South West Indian Ocean Fisheries Project (SWIOFP)* inaendelea na tathmini ya wingi wa samaki katika Ukanda wa Uchumi; na

(vii) Kugharamia mafunzo kwa watumishi wanne (4) wa Mamlaka kuhusu usimamizi wa fedha, sheria na uvuvi endelevu wa samaki wanaohamahama katika Ukanda wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuimarisha Mamlaka ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, Mamlaka itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu Na. 1 ya mwaka 1998 na Marekebisho yake ya 2007 (Sheria Na. 4, ya 2007) kwa pande zote za Muungano;

(ii) Kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu Na. 1 ya mwaka 1998 na Marekebisho yake ya 2007 (Sheria Na. 4, ya 2007) ili kuendana na hali ya sasa;

(iii) Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uvuvi wa kibiashara katika Ukanda wa Uchumi;

(iv) Kushirikiana na nchi za Msumbiji, Comoro na Kenya kufanya doria ya pamoja;

(v) Kuongeza vifaa vya kuvutia samaki (*FADs*), kutoa mafunzo kwa wavuvi kuhusu matumizi ya vifaa hivyo na kununua boti ndogo ya doria;

(vi) Kushirikiana na *World Wide Fund for Nature (WWF),* kufanya tathmini ya mnyororo wa thamani ya samaki aina ya Jodari na jamii zake; na

(vii) Kugharamia mafunzo kwa watumishi wa Mamlaka na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa uvuvi haramu. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kusimamia udhibiti wa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi, uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwa kuendesha doria za nchi kavu, kwenye maji na angani. Katika Mwaka 2011/2012, siku-kazi 5,964 za doria zimefanyika na kuwezesha kukamatwa kwa zana na vyombo haramu zikiwemo makokoro 665,141, kamba za kokoro mita 1,769,668, nyavu za makila 1,109,884, nyavu za dagaa (chini ya mm 10) 2,694, nyavu aina ya “monofilament” 1,046, mabomu 129, vifaa vya kuzamia jozi 125, mikuki 92, vyandarua 199, kasia 507, mtando 154, katuli 578, tambi za kulipulia bomu 89, bunduki za kwenye maji 108, ndoano 334, miwani ya kuzamia 97, vimia 373, magari 81, pikipiki 15, mitumbwi 483, injini za boti 30 na baiskeli 69. Pia, jongoo bahari kilo 280, samaki wa mabomu kilo 867, dagaa wakavu kilo 34,475, samaki aina ya sato waliouawa kwa sumu kilo 460, makombe kilo 1,337, samaki wachanga kilo 91,866, samaki wabichi kilo 2,426, na samaki wakavu kilo 47,104 walikamatwa. Vilevile,

watuhumiwa 623 walikamatwa kwa kujihusisha na uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi ambapo kesi 94 zilifunguliwa mahakamani. Wizara imezielekeza Halmashauri kutunga Sheria Ndogo kwa kuzingatia Kifungu cha 18 cha Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 hususan kuimarisha ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi katika maeneo yao. Aidha, natoa wito kwa Halmashauri zote kusimamia Sheria ya Uvuvi ili kulinda rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia programu ya Smartfish imetoa mafunzo ya kudhibiti uvuvi haramu kwa wadau wa uvuvi 72 kutoka Mikoa ya Mwanza (31) na Mara (41). Aidha, wataalam wa uvuvi nane (8) na mwakilishi mmoja (1) wa BMUs walipata mafunzo katika nchi za Uganda (7) na Kenya (2) kuhusu uendeshaji wa doria za pamoja katika ukanda wa Ziwa Victoria. Vilevile, wataalam watano (5) kutoka vituo vya mipakani vya Tunduma, Kigoma, Kasanga, Kipili na Kasumulo walipata mafunzo ya ukaguzi wa mazao ya uvuvi mipakani nchini Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuimarisha vituo 20 vya doria vya Dar es Salaam, Mwanza, Musoma, Bukoba, Tanga, Mtwara, Mafia, Kilwa, Horohoro, Kipili, Kasanga, Sota, Sirari, Kasumulu, Rusumo, Kanyigo, Kabanga, Kigoma, Mbamba Bay na Tunduma kwa kuvifanyia ukarabati na kuvipatia vitendea kazi. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana kwenye Tabaka la Juu (Pelagic Fishery Management Plan) katika maji ya kitaifa ya Bahari ya

Hindi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na wadau wengine itafanya siku-kazi 5,500 za doria, kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kuzingatia sheria, kuimarisha vituo vya doria vilivyopo na kuhamasisha jamii za wavuvi kuhusu utunzaji wa rasilimali za uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008/2009, Serikali ilitoa taarifa katika Bunge lako tukufu kuhusu kukamatwa kwa Meli ya TAWARIQ 1 iliyokamatwa tarehe 08 Machi, 2009 ikivua kinyume cha sheria na kuchafua mazingira kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari wa Tanzania. Watuhumiwa 37 walifikishwa mahakamani na hukumu ilitolewa na Mahakama Kuu ya Tanzania tarehe 23 Februari, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ilishinda kesi hii na watuhumiwa wawili (2) walipatikana na hatia na kuhukumiwa. Mahakama iliamuru meli ya TAWARIQ 1 itaifishwe na kuwa mali ya Serikali ya Tanzania. Hata hivyo, washitakiwa wamekata rufaa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania dhidi ya uamuzi huo, hivyo meli hii imebaki kuwa kielelezo cha Mahakama hadi pale ambapo rufaa hiyo itakapoamuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeendelea kuimarisha BMUs 703 katika maeneo mbalimbali nchini kwa kuzipatia mafunzo, vitendea kazi na elimu ya kuziwezesha kuanzisha miradi midogo ya uzalishaji ili

ziwe endelevu. Pia, BMUs 16 zimeanzishwa, ukanda wa pwani (13) na ukanda wa Ziwa Tanganyika (3) na kusajili BMUs 46 katika ukanda za Ziwa Tanganyika (5), Pwani (31) na Bwawa la Mtera (10). Aidha, Wizara imewezesha uandaaji wa Mipango ya Usimamizi wa Raslimali za Uvuvi katika Halmashauri za Manispaa za Mtwara-Mikindani 3, Lindi 3, Temeke 3, Kigoma-Ujiji 2; na Halmashauri za Wilaya za Mkinga 3, Mtwara Vijijini 3, Lindi Vijijini 3, Mkuranga (3), Bagamoyo 3 na Kigoma Vijijini 5. Vilevile, Wizara imewezesha kuandaa Sheria Ndogo za BMUs katika vijiji 25 vya Halmashauri za Manispaa za Mtwara-Mikindani (3) na Kigoma-Ujiji (2); na Halmashauri za Wilaya za Mkinga (6), Mtwara Vijijini (3), Pangani (3), Mkuranga (3), na Kigoma Vijijini (5). Pia, imewezesha uandaaji wa Rasimu ya Mwongozo wa kuanzisha Mtandao wa BMUs *(BMUs Networking Guidelines)* na kuimarisha Maeneo ya Usimamizi wa Uvuvi wa Pamoja *(Collaborative Fisheries Management Areas)* katika Halmashauri ya Mafia 2, Rufiji 3 na Kilwa 1. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kushirikiana na Asasi isiyo ya Kiserikali ya *"Sea Sense,"* kuelimisha wadau 48 kutoka Halmashauri za Rufiji (22) na Kilwa (26) kuhusu umuhimu wa kulinda viumbe vilivyo katika hatari ya kutoweka kama vile Kasa, Nguva na Papa aina ya Potwe kwa lengo la kukuza uhifadhi na kupanua utalii rafiki wa mazingira;

(ii) Kufanya savei katika maeneo ya Halmashauri za Mkinga na Mtwara ili kubaini kuwepo kwa Kasa, Nguva na Papa aina ya Potwe na matokeo yameonesha Nguva hawaonekani kwa wingi katika maeneo hayo;

(iii) Kutoa mafunzo ya uvuvi endelevu unaozingatia ikolojia na mazingira kwa wadau wa uvuvi 204 kutoka Halmashauri za Manispaa za Mtwara-Mikindani (42), Kinondoni (12), Lindi (42); na Halmashauri za Wilaya za Mtwara Vijijini (42), Lindi Vijijini (42), Bagamoyo (12) na Mkuranga (12); na

(iv) Kutoa mafunzo kwa vijana 43 kutoka Manispaa ya Temeke kwa ufadhili wa Kanisa Katoliki-Mtoni Kijichi kuhusu usimamizi endelevu wa rasilimali ya uvuvi na uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na wadau wengine itafanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuendeleza na kuwezesha uimarishwaji wa ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi;

(ii) Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo na Vyama vya Ushirika wa Wavuvi katika jamii za wavuvi; na

(iii) Kuchangia Miradi na Programu shirikishi za *"Lake Victoria Fisheries Organization" (LVFO), "International Whalling Commission" (IWC), Indian Ocean Tuna Commission (IOTC), Marine Legacy Fund (MLF)* pamoja na Operesheni Maalum ya Kuokoa Samaki aina ya Sangara Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kutekeleza Mradi wa Usimamizi wa Ikolojia na Mazingira

*(Ecosystem Approach to Fisheries - EAF Nansen Project)* kwa ufadhili wa *FAO* ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Katika mwaka 2011/2012, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaa rasimu ya Mpango wa Usimamizi wa Samaki Wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji; kutoa mafunzo ya uvuvi endelevu unaozingatia ikolojia na mazingira kwa wadau wa uvuvi 204 wakiwemo Maafisa Uvuvi 14 na wavuvi 190; na kuwezesha safari ya mafunzo kwa wataalam watatu (3) katika nchi za Kenya na Ushelisheli kujifunza juu ya masuala mbalimbali ya uvuvi katika Bahari. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itakamilisha Mpango wa Usimamizi wa samaki wanaopatikana katika tabaka la juu la maji *(Pelagic Fish)* na kutoa mafunzo na uhamasishaji wa usimamizi wa uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira kwa wavuvi wadogo katika ukanda wa pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani *(Marine and Coastal Environment Management Project - MACEMP).* Katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Mradi wa *MACEMP* imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuwezesha maandalizi ya Mipango 24 ya utekelezaji wa vikundi vya BMUs katika Halmashauri za Manispaa za Mtwara-Mikindani, Temeke na Lindi; na Halmashauri za Wilaya za Mkinga, Mtwara, Lindi, Mkuranga na Bagamoyo;

(ii) Kufanya tathmini ya miradi midogo 189 ya kiuchumi katika Halmashauri zote 16 za mradi;

(iii) Kuwezesha maandalizi ya Sheria Ndogo za BMUs katika vijiji 18 vilivyoko katika Halmashauri za Manispaa ya Mtwara-Mikindani; na Halmashauri za Wilaya za Mkinga, Mtwara, Pangani na Mkuranga;

(iv) Kwa kushirikiana na Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, kukamilisha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi katika vijiji 28 katika Halmashauri za Wilaya za Mkinga, Pangani, Muheza, Rufiji, Mafia na Kilwa;

(v) Kwa kushirikiana na Muungano wa Vyama vya Akiba na Mikopo Tanzania *(SCCULT),* kuhamasisha na kuratibu uanzishaji wa Benki za Jamii katika Wilaya za Kilwa, Mafia na Rufiji;

(vi) Kuwezesha ukarabati wa maeneo matatu ya kihistoria ya *''Makutani Palace, Sultani Tombs* na *Makutani Defence wall"*, yaliyoko Kilwa Kisiwani kama njia ya kuyahifadhi ili yaweze kuvutia utalii;

(vii) Kufadhili mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi, kwa ajili ya watumishi 39 ili kuwajengea uwezo;

(viii) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Mvuvi House (Temeke), Ofisi ya Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Kigombe (Muheza), na mialo mitatu (3) ya kupokelea samaki na mazao ya uvuvi ya Masoko Pwani (Kilwa), Kilindoni (Mafia) na Nyamisati (Rufiji);

(ix) Kuwezesha TAFIRI kufanya tathmini ya mienendo ya kibaiolojia ya kambamiti, kaa, kambakoche na dagaa wanaovuliwa kibiashara na wavuvi wadogo;

(x) Kuendeleza mchakato wa kuanzisha Mfuko maalum wa Kuhifadhi rasilimali na Mazingira ya Bahari na Pwani *(The Marine Legacy Fund);* na

(xi) Kujenga mfumo wa kutunzia taarifa za *MACEMP (The MACEMP Information Management System).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Mradi wa *MACEMP* itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa ghala la mwani katika Kijiji cha Jibondo (Mafia);

(ii) Kukamilisha ufungaji wa majokofu katika mialo ya Masoko Pwani (Kilwa), Kilindoni (Mafia) na Nyamisati (Rufiji);

(iii) Kwa kushirikiana na wadau wengine kuchunguza mtandao wa vyanzo, usambazaji na masoko ya mabomu yanayotumiwa katika uvuvi haramu na madhara yake katika eneo la mradi;

(iv) Kutathmini matokeo ya Mradi na kuandaa filamu ya video ya matokeo hayo; na

(v) Kukamilisha ununuzi wa maboya ya kuweka mipaka ya maeneo ya Hifadhi za Bahari za Mafia, Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma na Maeneo Tengefu ya Dar es Salaam na Maziwe (Pangani).

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya mtambuka. Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu. Watumishi ni rasilimali muhimu yenye kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara. Kutokana na umuhimu wake inahitaji kusimamiwa vizuri, kujengewa uwezo wa kiutendaji na mazingira mazuri ya kazi ili kuongeza ufanisi. Katika mwaka 2011/2012, watumishi 171 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi. Kati ya hao 68 wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu na 103 walipata mafunzo ya muda mfupi. Watumishi 236 walipandishwa vyeo ambapo watano (5) waliteuliwa kuwa Wakurugenzi Wasaidizi. Vilevile, Wizara iliwapangia kazi Maafisa Ugani 205 waliohitimu mafunzo katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na vyuo vya Mifugo na Uvuvi katika Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi (watumishi 64), Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika (watumishi 28) na Ofisi za Katibu Tawala Mikoa 12 (watumishi 13). Aidha, Wizara iliajiri watumishi 118 wakiwemo 67 wa kada za Mifugo, 31 Uvuvi na 20 wa fani mbalimbali. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuratibu utekelezaji wa Mfumo Shirikishi wa Ulipaji wa Mishahara kwa watumishi wa umma *(LAWSON)*;

(ii) Kuongeza ufanisi wa kazi kwa kununua vitendea kazi;

(iii) Kuwezesha watumishi 55 kushiriki mashindano ya SHIMIWI ili kuboresha afya zao, kuimarisha maelewano na mahusiano miongoni mwa watumishi wa Serikali;

(iv) Kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Upimaji wa Utendaji Kazi wa Wazi *(OPRAS)* kwa watumishi; kusimamia utoaji wa stahili zao; na kufanya mapitio ya kazi *(Job List)* na Mkataba wa Huduma kwa Mteja;

(v) Kufanya vikao viwili (2) vya wafanyakazi kwa kushirikiana na Vyama vya Wafanyakazi na vikao viwili (2) vya Baraza la Wafanyakazi kwa lengo la kuimarisha uhusiano na utendaji kazi mzuri katika maeneo ya kazi; na

(vi) Kuwezesha sekta binafsi za ulinzi na usafi kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaajiri jumla ya wataalam 145 wakiwemo 70 wa sekta ya mifugo, 50 sekta ya uvuvi na 25 fani nyingine. Aidha, watumishi 234 wa kada mbalimbali watapandishwa vyeo kulingana na sifa zilizoelezwa kwenye Miundo ya Utumishi wa Umma. Pia, watumishi 50 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu na 100 ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kutoa mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya 145 wa Wizara na kununua vitendea kazi;

(ii) Kuandaa vikao viwili (2) vya Baraza la Wafanyakazi;

(iii) Kusimamia utekelezaji wa Mfumo Shirikishi wa Ulipaji wa Mishahara kwa watumishi *(LAWSON)*;

(iv) Kufanya mapitio ya Miundo ya Utumishi kwa kada zilizo chini ya Wizara;

(v) Kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Upimaji wa Utendaji kazi wa Wazi *(OPRAS)* kwa watumishi wa Wizara; na

(vi) Kuwezesha watumishi kushiriki katika michezo mbalimbali ikiwemo ya SHIMIWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora, jinsia na UKIMWI. Wizara iliendelea kuwahamasisha watumishi kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya Utumishi wa Umma pamoja na kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za kazi. Aidha, masuala ya jinsia na UKIMWI yameendelea kuzingatiwa. Katika mwaka 2011/2012 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Kuelimisha watumishi 290 katika vituo 35 vya Wizara katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Arusha, Tanga na Kilimanjaro kuhusu maadili, wajibu na haki zao;

(ii) Kutoa huduma ya lishe kwa watumishi 8 wanaoishi na VVU;

(iii) Kuendelea kuhamasisha watumishi kuhusu kupima afya zao kwa hiari na kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI; na

(iv) Kufanya tathmini ya masuala ya jinsia kubaini upungufu katika sekta za mifugo na uvuvi. Upungufu uliojitokeza umejumuishwa katika mipango na mikakati mbalimbali ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuelimisha watumishi wa Wizara kuhusu maadili, wajibu na haki zao;

(ii) Kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja;

(iii) Kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa;

(iv) Kutoa mafunzo ya jinsi ya kuferejisha masuala ya jinsia katika mipango mbalimbali ya Wizara; na

(v) Kutoa huduma ya lishe kwa watumishi wanaoishi na VVU na walioathirika na kuendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari na kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano na elimu kwa umma. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika matukio mbalimbali kuhusu maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi. Baadhi ya matukio hayo ni mafanikio ya sekta za mifugo na uvuvi katika maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara, Nanenane, Wiki ya Unywaji Maziwa, Siku ya Chakula Duniani na Siku ya Mvuvi Duniani. Kupitia

matukio hayo wafugaji, wavuvi na wadau wengine wameelimishwa kuhusu ufugaji na uvuvi endelevu. Aidha, Wizara imetayarisha na kusambaza nakala 1,000 za majarida, 1,000 za vipeperushi na 4,000 za kalenda zinazoelezea kazi na majukumu mbalimbali ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutayarisha na kusambaza taarifa za matukio mbalimbali kuhusu maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi kupitia vyombo vya habari. Vilevile, Wizara itaandaa na kurusha hewani vipindi 20 vya redio na luninga kuhusu Sera, Mikakati na Mipango ya kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi. Pia, Wizara itatayarisha na kusambaza nakala 1,000 za kalenda na 1,000 za vipeperushi juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya TEHAMA. Wizara imeendelea kuimarisha teknolojia na upashanaji habari kwa lengo la kuimarisha mifumo ya kompyuta na matumizi ya TEHAMA katika utendaji wa kazi za Serikali. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa Sera ya TEHAMA ya Wizara;

(ii) Kukarabati na kufanya matengenezo ya vifaa vya huduma ya mawasiliano katika Wizara;

(iii) Kuboresha tovuti ya Wizara na kuhakikisha ina taarifa zinazohusisha sekta za mifugo na uvuvi ikiwemo fursa za uwekezaji;

(iv) Kusimamia ufungaji mifumo ya mawasiliano kwenye majengo ya Wizara na kuboresha kasi ya mtandao; na

(v) Kujenga uwezo wa watumishi kutumia mifumo mbalimbali ya kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa Mpango Mkakati wa kutekeleza Sera ya Wizara ya TEHAMA;

(ii) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA na kuhamasisha matumizi yake;

(iii) Kuwezesha kufanya matengenezo ya vifaa na mifumo ya kompyuta;

(iv) Kununua vitendea kazi vya TEHAMA;

(v) Kuunganisha mawasiliano kati ya Wizara, Wizara nyingine na vituo vya nje kwa lengo la kutekeleza utaratibu wa serikali mtandao *(e-Gov);* na

(vi) Kuwajengea uwezo watumishi wawili (2) kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi. Athari za mabadiliko ya tabia nchi zimeendelea kujitokeza katika sekta za mifugo na uvuvi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara

imeendelea kutoa elimu juu ya utunzaji wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za mifugo na uvuvi. Kwa upande wa ufugaji, Wizara imehimiza uvunaji wa mifugo mara inapofikia umri au uzito wa soko; kutumia vyanzo mbadala vya nishati; kupanda, kuvuna na kuhifadhi malisho, kuhifadhi mabaki ya mazao na kupanda miti-malisho kwa matumizi ya kiangazi. Aidha, Wizara inaboresha mfumo wa utoaji tahadhari ili wafugaji wapate taarifa na maelekezo ya hatua za kuchukua dhidi ya athari za mabadiliko ya hali ya hewa/tabia nchi (Livestock Early Warning System). Jumla ya wataalam watano (5) wamepata mafunzo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kijiografia *(GIS).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uvuvi, Wizara imeendelea kuhabarisha wavuvi na wafugaji viumbe kwenye maji kuhusu mabadiliko ya tabia nchi wapate taarifa na maelekezo ya hatua za kuchukua dhidi ya athari za mabadiliko ya hali ya hewa/tabia nchi. Pia, kuhimiza wavuvi na wakuzaji viumbe kwenye maji kutunza vyanzo vya maji na kuhifadhi mazingira. Aidha, inahimiza matumizi ya nishati na teknolojia mbadala za uzalishaji viumbe kwenye maji kama vile ufugaji samaki kwa kutumia uzio; ulimaji wa mwani kwa kutumia chelezo kwenye kina kirefu cha maji. Vilevile, kutumia teknolojia ya kukausha samaki kwa nishati ya jua na jiko sanifu linalotumia kuni chache na matumizi ya mitumbwi ya *fibre glass materials* ili kupunguza ukataji wa miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri itaendelea

kuhamasisha matumizi ya biogesi kwa jamii za wafugaji ili kupunguza matumizi ya nishati ya kuni na mkaa ili kutunza mazingira. Pia, kuendelea kutekeleza mfumo wa utoaji wa tahadhari kuhusu mabadiliko ya tabia nchi kwa wafugaji na wavuvi. Aidha, itaendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kukausha samaki kwa nishati ya jua na jiko sanifu linalotumia kuni chache na matumizi ya mitumbwi ya fibre glass ili kupunguza ukataji wa miti inayotumika kutengeneza mitumbwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadhimisho na makongamano muhimu katika sekta za mifugo na uvuvi. Siku ya Wakulima na Wafugaji (Nanenane). Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta za Mifugo na Uvuvi ilishiriki katika maadhimisho ya sikukuu ya wakulima nchini - NaneNane. Maonesho hayo yalijumuisha mashindano ya ubora wa ng'ombe kutoka sekta binafsi na taasisi za Serikali, ambapo Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Mgeni Rasmi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeshiriki katika kuandaa maadhimisho ya NaneNane yenye kauli mbiu "KILIMO KWANZA-Zalisha Kisayansi na Kiteknolojia Kukidhi Mahitaji ya Ongezeko la Idadi ya Watu".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Siku ya Chakula Duniani. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, pamoja na *FAO*, ilishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika kitaifa Mkoani Lindi tarehe 16 Oktoba 2011. Kauli mbiu ya Siku ya Chakula Duniani Mwaka 2011 ilikuwa "Bei ya

Vyakula-Kutoka Kuyumba hadi Kutengemaa". Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kushiriki maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Siku ya Mvuvi Duniani. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara na wadau wa Sekta ya Uvuvi, iliandaa na kuadhimisha Siku ya Mvuvi Duniani iliyofanyika kitaifa mjini Musoma. Maadhimisho haya hufanyika duniani kote tarehe 21 Novemba kila mwaka kwa lengo la kuelimisha jamii umuhimu wa uvuvi endelevu, hifadhi ya mazingira, matumizi ya zana bora za uvuvi, ufugaji bora wa samaki na viumbe kwenye maji, uvunaji na usindikaji bora wa mazao ya uvuvi. Kauli mbiu ilikuwa "Ukuzaji viumbe kwenye maji endelevu kwa uhakika wa chakula". Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuadhimisha Siku ya Mvuvi Duniani itakayofanyika tarehe 21 Novemba 2012 mjini Lindi kwa kushirikisha wadau wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa. Wizara imeendelea kuratibu maadhimisho ya Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa kila mwaka. Katika mwaka 2011/2012, maadhimisho hayo yalifanyika Manispaa ya Moshi kuanzia tarehe 29 Mei, 2012 mpaka tarehe 1 Juni, 2012 sambamba na kongamano la kitaifa la maziwa. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa, "Kuza Uchumi na Lishe: Fanya Maziwa kuwa Moja Kati ya Mazao Makuu ya Wilaya". Katika mwaka 2012/2013, Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa itafanyika Songea mwezi Juni, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Siku ya Veterinari Duniani. Wizara ilishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Veterinari Duniani tarehe 28 Aprili 2012. Maadhimisho haya husimamiwa na Chama cha Madaktari wa Mifugo Duniani na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani na huambatana na kaulimbiu maalum. Mwaka 2011/2012 kaulimbiu ilikuwa "Usugu wa Vimelea vya Magonjwa Dhidi ya Dawa za Tiba". Lengo kuu la maadhimisho lilikuwa ni kuwaelimisha wadau huduma zinazotolewa na wataalamu wa fani hii katika kulinda afya ya binadamu na ustawi wa wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kongamano la Kisayansi la Vyama vya Wataalam wa Uzalishaji Mifugo na Madaktari wa Mifugo. Wizara hushiriki katika makongamano ya kila mwaka ya Wataalam wa Uzalishaji Mifugo na Madaktari wa Mifugo nchini. Katika mwaka 2011/2012, kongamano la Wataalam wa Uzalishaji Mifugo lilifanyika Arusha tarehe 25 – 27 Oktoba, 2011 na maudhui yake yalikuwa ni "Mchango wa Sekta za Mifugo na Uvuvi katika Kuboresha Maisha Endelevu ya Watu na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi". Aidha, kongamano la Madaktari wa Mifugo nchini lilifanyika mjini Arusha tarehe 6 – 8 Desemba, 2011 na maudhui yake yalikuwa ni "Miaka 250 ya Taaluma ya Veterinari Duniani: Mchango wake katika Kuboresha Afya ya Wanyama na Binadamu".

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadhimisho yote niliyoyaeleza hapo juu yametoa changamoto, msukumo na mchango mkubwa katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, kwa niaba ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka uliopita yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za kitaifa na kimataifa, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na wawakilishi wao Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuzitambua na kuzishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC*), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*, Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Serikali za Australia, Austria, Brazil, Canada, Jamhuri ya Czech, Hispania, Iceland, Ireland, Japan, Jamhuri ya Watu wa China, Israel, Korea Kusini, Marekani, Misri, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *FAO, IAEA, UNICEF, UNDP, UNIDO* na *WHO* na mifuko ya kimataifa ya *GEF* na *IFAD* kwa kuchangia katika maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kutambua na kuzishukuru taasisi za kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya

Afrika; Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japan (*JICA*), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (*KOICA*), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (*USAID*), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (*DfID*), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika *(AU/IBAR),* Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE),* Shirika la Maendeleo la Uswisi (*SDC*), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (*GTZ*), United Nations University (*UNU*), Shirika la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden *(SIDA)* kwa michango yao katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kuyashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za Bill and M*elinda Gates Foundation, Association for Agricultural Research in East and Central Africa (ASARECA), International Livestock Research Institute (ILRI), World Wide Fund for Nature (WWF), Indian Ocean Commission (IOC), South West Indian Ocean Fisheries Commission (SWIOFC), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Co-operation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFAM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Security Studies (ISS), International Land Coalition (ILC), British Gas International , Sea Sense, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC), International Whaling Commission (IWC), SmartFish, Marine Stewardship Council (MSC),* Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini

zinazojihusisha na uendelezaji wa sekta za mifugo na uvuvi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa wananchi wote hususan wafugaji, wavuvi na wadau wengine kwa michango yao ya mawazo katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini. Wizara inaomba waendelee na moyo huo ili kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. Wizara itaendelea kushirikiana nao kuleta mapinduzi katika sekta za mifugo na uvuvi kwa lengo la kuboresha hali ya maisha yao na uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro, Mbunge wa Jimbo la Kiteto na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa msaada wake wa karibu katika kusimamia kazi za Wizara. Aidha, napenda pia nitoe shukurani zangu kwa Katibu Mkuu Dkt. Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Yohana Budeba, Wakuu wa Idara na Vitengo, Taasisi na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa na kufanikisha maandalizi ya bajeti hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi 54,566,124,000.00 kama ifuatavyo:-

(i) Shilingi 40,726,641,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi 13,959,071,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE); na shilingi 26,767,570,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengine (OC); na

(ii) Shilingi 13,839,483,000.00 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi 4,000,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 9,839,483,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani: www.mifugo.go.tz

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii nimeambatanisha Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki! *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwani ametoa hoja na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, hapa nimeletewa tangazo kwamba jana timu zetu za Bunge zilikuwa

kwenye mapambano makali sana, sasa tangazo la matokeo ya mpambano huo lilikuwa halijasomwa na ninadhani lilichelewa kuletwa. Kwa hiyo, matokeo ya michezo ya kirafiki kati ya *Bunge Sports Club* na *Mwananchi Communication Limited* kutoka Dar es Salaam, mechi zilizochezwa jana tarehe 08/08/2012 kwenye uwanja wa Jamhuri ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mpira wa miguu, *Bunge Sport Club* walishinda kwa goli moja lakini walitoka sare na Mwananchi na wao walifunga goli moja, huo ni mpira wa miguu.

Lakini timu ya Netball ndiyo wamenishangaza sana, *Bunge Sports Club* kwa maana ya timu ya *Netball*, wali-*score* magoli 25 na timu ya Mwananchi wao waliambulia magoli sita. Kwa hiyo, naona timu ya Bunge ya *Netball* jana ilifanya kazi nzuri sana.

Lakini michezo yote miwili ilikuwa ni mizuri, ya kufurahisha na yenye hamasa kwa watazamaji. Kwa hiyo, Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Amos G. Makalla, anaomba wachezaji waendelee na mazoezi kwa sababu huenda Jumamosi kukawa na mechi kali zaidi. Kwa hiyo, wasiache kuendelea na mazoezi. Naomba nipongeze timu zote za Bunge kwa kufanya kazi nzuri na tuwapongeze wageni wetu na tuwashukuru kwa kuja kujenga urafiki pamoja na Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia uchambuzi wa bajeti hii ili aweze kutoa taarifa ya Kamati, namwona Dkt. Kamani kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai, afya na kuniwezesha kusimama hapa leo. Lakini pili niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Busega kwa ushirikiano wanaonipa na nipende kuwahakikishia kuwa nitafanya kila niwezalo ili ndoto ya Busega Jimbo iweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niishukuru familia hususani mke wangu mpenzi Magdalena Mlengeya na watoto wangu, kwa uvumilivu wanaonipatia ninapokuwa sipo nikitumikia majukumu yangu ya Kibunge. Napenda kuwaambia kuwa nawapenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kwa sababu ya muda, napenda kueleza kwamba taarifa hii ichukuliwe kwa ujumla wake katika *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi katika Ofisi Ndogo ya

Bunge Dar es Salaam tarehe 5 na 6 Juni, 2012. Katika kikao hicho, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi alitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012, changamoto za utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2011/2012, malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2011/2012, Kamati ilitoa maoni na ushauri wa kuzingatiwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imeyafanyia kazi kwa kiasi cha kuridhisha maoni na ushauri wa Kamati kulingana na fedha zilizopatikana. Baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na:-

(a) Ili kuongeza idadi ya wataalam wa ugani, Serikali imekuwa ikiongeza uwezo wa kudahili wanafunzi kutoka 1,006 mwaka 2007/2008 hadi 1,630 mwaka 2011/2012 katika Vyuo vya Mifugo na kutoka wanafunzi 228 mwaka 2007/2008 hadi 714 mwaka 2011/2012 katika Vyuo vya Uvuvi.

(b) Serikali imeendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya dhana ya Kilimo Kwanza kupitia maadhimisho na makongamano mbalimbali katika Sekta za Mifugo na Uvuvi; matukio haya muhimu ni pamoja na Siku ya Wakulima na Wafugaji (Nane Nane), wiki ya uhamasishaji unywaji wa maziwa, siku ya

chakula duniani, siku ya mvuvi duniani na siku ya veterinari duniani. Kamati inasisitiza elimu itolewe zaidi kwa kutumia njia ya vyombo vya habari kwa kuwa taarifa za makongamano haziwafikii wananchi walio wengi.

(c) Kwa kupitia maadhimisho ya Wiki ya Kunywa Maziwa na Programu ya Unywaji Maziwa Mashuleni, Serikali imeendelea kuwahamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kunywa maziwa kwa afya zao pamoja na kukuza biashara ya Sekta ya Ufugaji. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa maziwa ya kutosha yanapatikana kwa wingi kwa kuwa watu wakihamasika bila maziwa kuwapo ni kazi bure.

(d) Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake sahihi wa kuanza kujenga machinjio ya kisasa hapa nchini. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa ujenzi huo uwe na ubora kwa kiwango cha kuridhisha ili machinjio hayo yadumu kwa muda mrefu na kuepuka gharama za kukarabati mara kwa mara, lakini vile vile nyama yake iweze kuvutia masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara pia imekumbana na changamoto mbali mbali katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Bajeti ndogo na ambayo pia inapungua kila mwaka hivyo kutotoa fursa ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi kukua;

(b) Kuchelewa kutolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo;

(c) Kutopatikana kwa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafugaji na wavuvi;

(d) Kutopatikana kwa pembejeo na zana za gharama nafuu kwa ajili ya ufugaji na uvuvi;

(e) Uhaba wa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi;

(f) Elimu na teknolojia za kisasa kutokuwafikia wafugaji na wavuvi;

(g) Uwekezaji mdogo katika sekta za mifugo na uvuvi; na

(h) Kushamiri kwa uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao mengine ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha na malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi chini ya Fungu 99, inaomba jumla ya shilingi 54,566,123,500/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 40,726,641,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 13,839,482,500/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi 26,767,570,000/= ni kwa ajili ya matumuzi mengineyo (*OC*) na shilingi 13,959,071,000/= ni kwa ajili ya mishahara (*PE*) ya Wizara. Aidha, kati ya fedha za

maendeleo, shilingi 4,000,000,000/= ni fedha za ndani na shilingi 9,839,482,500/= ni fedha kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi hayo ya fedha yatawezesha Wizara kutekeleza kazi mbalimbali ilizojipangia. Baadhi ya kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Sekta ya Mifugo

(i) Kuendeleza na kuboresha miundombinu ya mifugo na uvuvi, malisho na nyanda za malisho;

(ii) Kuongeza upatikanaji na matumizi ya pembejeo na zana za mifugo na uvuvi;

(iii) Kuimarisha huduma za ugani na utafiti wa mifugo; na

(iv) Kufanya maandalizi ya sensa kamili ya mifugo na kuanzisha mfumo wa kutambua na kusajili mifugo kwa mfumo wa ufuatiliaji.

(b) Sekta ya Uvuvi

(i) Kudhibiti ongezeko la zana haramu za uvuvi na utoroshaji wa samaki na mazao ya uvuvi mipakani;

(ii) Kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya kukuza uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta ya mifugo na uvuvi;

(iii) Kukuza ufugaji wa samaki kwa wafugaji wadogowadogo katika mabwawa;

(iv) Kuongeza thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi; na

(v) Kuhakikisha masoko ya mazao ya sekta hii yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Baada ya kueleza kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla. Bajeti ya Wizara bado ni ndogo na kwa asilimia kubwa inategemea wahisani kutoka nje. Kamati inasikitishwa na kupungua kwa bajeti ya wizara hii kila mwaka. Mwaka 2010/2011, Wizara ilitengewa shilingi bilioni 58.8 tu ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 1.6, mwaka 2011/2012, Wizara ilitengewa shilingi bilioni 57.2 wakati mwaka 2012/2013, Wizara imetengewa shilingi bilioni 54.6 tu ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 2.6. Wizara hii ina majukumu mengi sana katika kutekeleza dhamira ya Serikali ya kuifanya sekta hii ichangie kikamilifu katika pato la Taifa. Ukizingatia kuwa Tanzania ni ya tatu kwa wingi wa mifugo katika Bara la Afrika, Kamati inaamini kuwa Tanzania ingeweza kunufaika zaidi na utajiri huo iwapo ingewekeza vya kutosha katika sekta ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kuwa Tanzania yenye ng'ombe milioni 19.2, mbuzi milioni 13.7, kondoo milioni 13.6, nguruwe milioni 1.9 na kuku

milioni 58, pamoja na maji mengi ya bahari na maziwa; inazidiwa na nchi kama Botwana na Kenya zenye mifugo michache lakini zenye mafanikio makubwa. Kamati inaishauri Serikali kuipa kipaumbele Wizara hii katika mgao wa bajeti ili iweze kukua na kuchangia kikamilifu katika kipato cha mfugaji na mvuvi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji. Migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji imekuwa sugu na kila siku migogoro mipya inaibuka. Hili ni bomu ambalo lisipoteguliwa mapema litalipuka na kusababisha maafa makubwa. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali ifanye utafiti wa kina ili kujua sababu za wafugaji kuhamahama ili kuwapelekea huduma zinazowafanya wahame;

(ii) Serikali itenge na kuweka bayana maeneo ya mifugo na ya kilimo ili kuepusha migogoro inayotokea mara kwa mara;

(iii) Maeneo yatakayotengwa kwa ajili ya mifugo yapatiwe huduma muhimu za majosho na maji kwa kuchimba mabwawa, visima, malambo na huduma nyingine muhimu;

(iv) Serikali kuanzisha maeneo yasiyo na maradhi (disease-*free zones*) kwa ajili ya uwekezaji wa mifugo unaolenga soko la Kimataifa;

(v) Serikali iandae Sheria ya kulinda ardhi ya mifugo; na

(vi) Serikali iendelee kutekeleza mapendekezo ya Kamati ndogo ya Kilimo, Mifugo na Maji kufuatia migogoro ya mipaka ya Ranchi za taifa Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo Kwanza. Kamati inaamini kwamba dhana ya Kilimo Kwanza imekuja kwa nia ya kuleta mapinduzi ya kijani na kukifanya kilimo chetu kuwa cha kisasa, chenye tija na cha kibiashara. Hata hivyo, wakati wa kupitia bajeti ya Wizara, Kamati imebaini kwamba dhana hii bado haijafahamika kwa wananchi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi za kuielimisha jamii juu ya dhana nzima ya Kilimo Kwanza katika ngazi ya Wilaya badala ya kutegemea maonesho na makongamano ambayo yanakuwapo katika vipindi maalum. Aidha, Serikali iendelee kuhamasisha sekta binafsi katika utekelezaji wa Kilimo Kwanza kwa kuhakikisha inawawekea vivutio muafaka kwa kuzingatia kwamba sekta binafsi inachangia kwa asilimia kubwa katika kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa wataalamu. Idadi ndogo ya wataalam ni tatizo kubwa katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Hii ni sababu kubwa ya mchango hafifu wa sekta hii katika pato la taifa. Kamati inaamini kwamba kuwepo kwa wataalam wa kutosha na wenye kuwezeshwa kwa kupatiwa vitendea kazi na

kuboreshewa maslahi na mazingira ya kazi, hakika sekta hizi muhimu zitakua kwa kasi inayotakiwa kwani watafikisha huduma inayostahili kwa wafugaji na wavuvi. Kamati inaishauri Serikali:-

(i) Iongeze idadi ya wahitimu kwa kuongeza udahili wa idadi ya wanachuo wa fani ya ugani katika vyuo vilivyopo; na

(ii) Iboreshe mazingira ya kazi na maslahi ili kuhakikisha wataalam inaowasomesha wanabaki nchini kulitumikia Taifa; hii itapunguza idadi kubwa ya wataalam wanaokimbilia nje ya nchi kutafuta maslahi bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Utafiti. Taasisi za Utafiti ni muhimu sana katika kuongeza tija katika uzalishaji na utoaji huduma ndani ya jamii. Kamati imebaini kuwa wataalam wengi walioko katika vituo vya utafiti nchini ni wenye umri mkubwa ambao ama ni wastaafu au wanakaribia kustaafu. Aidha, taasisi hizi zina miundombinu duni na vitendea kazi haba. Kamati inashauri Serikali:-

(i) Kuandaa wafanyakazi wataalam watakaochukua nafasi zao watakapostaafu kwa kuajiri wataalam wa rika mbalimbali ili ujuzi wao usipotee katika vituo hivyo;

(ii) Iendelee kuongeza bajeti inayotengwa kwa taasisi hizi kwani inayotengwa haitoshi; na

(iii) Ihakikishe matokeo ya utafiti yanawafikia walengwa ambao ni wavuvi na wafugaji kwa nia ya kuboresha sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa madaraka. Halmashauri ndizo mamlaka za utekelezaji wa miradi mingi ya ufugaji na uvuvi, lakini Wizara haijui undani wa utekelezaji huo. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mahusiano ya kikazi yaliyopo kati ya Wizara na TAMISEMI (Halmashauri) ili kuleta ufanisi zaidi wa kazi katika kutekeleza miradi hiyo. Aidha, idara ya mifugo na uvuvi kwa upande mmoja na Idara ya Kilimo kwa upande mwingine pamoja na wataalam wake walioko katika Halmashauri zitenganishwe ili moja isionekane kumezwa na nyingine kama utaratibu ulivyo sasa. Hii pia itasaidia kuimarisha uwajibikaji wa kila sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo. Kodi ya maziwa na bidhaa zake. Sekta ndogo ya maziwa hapa nchini hususan usindikaji, inashindwa kukua na hivyo kutokulipatia Taifa mapato. Hali hii inachangiwa na utitiri wa kodi ambazo zinasababisha gharama kubwa ya usindikaji na biashara ya maziwa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maziwa ghafi (*Fresh Milk, UHT na Cream*) yanayozalishwa hapa nchini yamesamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani, lakini yakisindikwa yanaingia gharama mbalimbali kama vile umeme, vipuri na maji ambavyo vinatozwa kodi ya Ongezeko la Thamani; hivyo maziwa yanakuwa ghali kwa walaji na wasindikaji wanashindwa kuhimili ushindani wa bidhaa za maziwa kutoka nchi za nje. Aidha, kuna urasimu mwingi ili kuruhusu uwekezaji wa

viwanda vya maziwa hapa nchini. Hivi sasa ili kiwanda cha kusindika maziwa kiweze kuanza kinatakiwa kipate vibali kumi na sita (16) kutoka taasisi na mamlaka mbalimbali za serikali, kitu kinachokwamisha na kudidimiza uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sekta ya maziwa iweze kuchangia ipasavyo katika pato la Taifa, Kamati inaishauri Serikali:

(i) Maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa yanayozalishwa nchini ziondolewe *VAT* na kuwa *zero rated*; na

(ii) Iziangalie upya kodi na vibali vya kuruhusu uwekezaji katika viwanda vya maziwa ili kupunguza usumbufu na muda unaotumika kwa ajili ya maandalizi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Maziwa. Bodi ya Maziwa ilianzishwa tangu mwaka 2004 kwa ajili ya kuratibu na kuinua sekta ndogo ya maziwa nchini. Hata hivyo, hadi leo hii Bodi ina watumishi kumi tu licha ya mahitaji makubwa ya wafanyakazi ili iweze kutekeleza malengo yaliyokudiwa. Kamati inaiona hali hii kama ukosefu wa utashi wa makusudi na ubunifu ili kuifanya sekta ndogo ya maziwa ikue hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kuona kuwa Tanzania bado inaendelea kuagiza maziwa nje ya nchi licha ya kundi kubwa la ng'ombe ililonalo. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Bodi ya Maziwa

kifedha na rasilimali watu ili iweze kubeba jukumu la kukuza sekta ndogo ya maziwa na kukidhi mahitaji ya nchi na hata kushindana na nchi jirani za Kenya, Uganda na Rwanda ambazo sasa zinaingiza maziwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ngozi. Ngozi ni zao ambalo likitumiwa vizuri linaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa. Ngozi za mifugo hazichangii ipasavyo katika Pato la Taifa ikilinganishwa na idadi ya mifugo tuliyonayo na hii inatokana na ngozi zetu kutokuwa na ubora unaotakiwa katika soko na nyingi zikisafirishwa nje ya nchi bila ya kusindikwa. Kamati inasisitiza yafuatayo:-

(i) Elimu zaidi itolewe kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa kutunza mifugo yao;

(ii) Ili kukuza soko la ngozi nchini, Serikali iwekeze katika viwanda hapa nchini kwa nia ya kuongeza thamani ya ngozi, kwa mfano kutengeneza viatu, mikoba na kadhalika. Bidhaa hizi zikitengenezwa hapa nchini zitapunguza bei yake na kukuza ajira. Vilevile zikiuzwa nje ya nchi zitasaidia kuitangaza ngozi ya Tanzania;

(iii) Serikali iongeze kasi ya kukifufua Chuo cha Teknolojia ya Ngozi kilichopo Mwanza pamoja na kuongeza udahili ili kupata wataalam wengi katika taaluma hii; na

(iv) Serikali idhibiti usafirishaji holela nje ya nchi wa ngozi ambazo hazijasindikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji. Kamati inasikitika kuwa sekta ya mifugo imekuwa haipewi umuhimu stahiki katika bajeti ya Serikali kiasi kwamba miradi mingi ya sekta hii haitekelezeki. Kutokana na hali hii, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Sekta hii iongezewe fedha ili kukidhi haja ya kuwapatia wafugaji na mifugo yao mahitaji muhimu kama vile majosho na maji kwa njia ya malambo, mabwawa, visima na maeneo ya malisho. Huduma hizi zikipatikana zitawafanya wafugaji kuacha tabia ya kuhamahama kutafuta maji na malisho lakini pia ubora wa mifugo utaongezeka;

(ii) Ranchi ambazo walipewa wawekezaji lakini wakashindwa kuziendeleza zigawiwe kwa wafugaji watakaoweza kuendeleza maeneo hayo kiufugaji;

(iii) Serikali iendelee kutoa elimu juu ya ufugaji wa kisasa wa kuwa na mifugo michache inayolingana na eneo la malisho na huduma nyingine muhimu. Aidha, wafugaji wapatiwe elimu ya kunenepesha mifugo ili kuongeza thamani ya mifugo yao kabla ya kuipeleka sokoni; hatua hii itamwongezea mfugaji kipato chake mwenyewe na pato la taifa kwa ujumla;

(iv) Elimu kuhusu umuhimu wa uvunaji wa mifugo itolewe ili kuongeza pato la mfugaji na pato la taifa;

(v) Taasisi za fedha hususani dirisha dogo la kilimo katika Benki ya Rasilimali zitoe elimu kwa wafugaji ili

waweze kupata mikopo kwa ajili ya kuboresha ufugaji; na

(vi) Mashamba ya mifugo ya Serikali yakiwemo yale ya *NARCO*, yawezeshwe kuzalisha mitamba na madume bora kwa wingi kwa ajili ya kuwauzia wafugaji ili kuboresha mbegu za mifugo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Ranchi za Taifa (*NARCO*). Kampuni ya Ranchi za Taifa ni kampuni pekee ya kibiashara katika Wizara hii. Kama ilivyokuwa kwa makampuni mengi nchini zikiwemo *TRL* na *ATCL*, kampuni hii iliwekwa kwenye ubinafsishaji kwa zaidi ya miaka kumi hadi Mheshimiwa Rais alipoamua kubadilisha uamuzi huo. Katika kipindi chote hicho kampuni haikuruhusiwa kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NARCO* sasa ina jumla ya mashamba 10 kati ya 16 iliyokuwa ikimiliki baada ya kuyabinafsisha kwa wawekezaji wadogo wadogo. Kutokana na uhitaji mkubwa wa nyama na mazao mengine ya mifugo nchini na kwenye soko la Kimataifa, *NARCO* inayo fursa kubwa ya kupanuka, kuchangia uendelezaji wa mifugo kwa wafugaji nchini, kuwekeza na kuvutia uwekezaji katika viwanda vya nyama na kuwa chachu ya kukua kwa sekta ya mifugo nchini. Hata hivyo, kwa muda mrefu sasa *NARCO* imekuwa ikiomba kupewa na Serikali angalau shilingi bilioni 10 tu iweze kufufua uwezo wake wa kupata dhamana ya kukopesheka na taasisi za fedha bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashangazwa kuwa pamoja na kuishauri Serikali kwa muda mrefu kuhusu kuisaidia *NARCO*, suala hili halijazingatiwa. Kamati bado inasisitiza Serikali kuipa uwezo *NARCO* ili itimize malengo yake kwa kuipa uwezo wa kifedha kama ilivyofanya kwa *TRL* na *ATCL*. Aidha, Kamati inaishauri Serikali iongeze kasi ya kufufua na kujenga viwanda vipya vya nyama nchini ili hatimaye kupunguza uingizaji wa nyama kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi. Tanzania imebarikiwa kwa kupakana na bahari na kujaliwa maziwa na mito mingi. Fursa hizi zikitumiwa vizuri zinaweza kutoa mchango mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, lishe, kipato na kuingizia nchini fedha za kigeni. Pamoja na umuhimu wake, bado Sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo Kamati iniashauri Serikali kubuni mikakati madhubuti ya kukabiliana nazo. Changamoto hizo ni pamoja na:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uvuvi Haramu. Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi inazochukua katika kupambana na uvuvi haramu katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Pamoja na juhudi hizo uvuvi haramu hasa ule wa kutumia baruti na nyavu za matundu madogo umeendelea kuwa tishio kwa samaki na viumbe hai waishio majini. Kamati inashauri:-

(i) Mamlaka husika kuendelea kusimamia sheria zilizopo na ikibidi katika maeneo ya vijijini sheria ndogo ndogo zisimamiwe ili kudhibiti uvuvi haramu;

(ii) Serikali iongeze vifaa vya doria katika bahari na maziwa;

(iii) Watengenezaji na wauzaji wa zana za uvuvi wafuatiliwe kwa karibu kwa vile baadhi yao wanahusika katika kusambaza zana haramu;

(iv) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wavuvi juu ya umuhimu wa kutumia zana bora za uvuvi; na

(v) Wavuvi wapatiwe mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kununua zana bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushuka kwa bei ya minofu ya sangara. Katika siku za karibuni, kumetokea mtafaruku mkubwa katika jamii ya wavuvi wa sangara katika Ziwa Victoria. Hali hii ilisababishwa na kushuka kwa bei ya minofu ya Sangara katika soko la Hispania, Ureno na Italia ambao ndio wanunuzi wakubwa. Hali hiyo ilitokana na kuanguka kwa uchumi katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushuka kwa bei ya minofu kumeleta hofu kwa wavuvi kutokana na mapato duni ya samaki na hivyo kushindwa kukidhi gharama za uzalishaji. Kamati ilishiriki katika vikao vya kujadili mustakabali wa suala hili kwa kuhusisha wadau mbalimbali wakiwemo wavuvi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri wake wa kufuatilia kwa karibu mfumo wa uvuvi kwa nchi za Uganda na Kenya ili kusaidia kupata bei nzuri kwa wavuvi wetu. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuwahamasisha wavuvi kuanzisha Vyama vya Ushirika ili kuwasaidia kupanga bei ya samaki na mazao yake na wenye viwanda,

lakini pia kuweza kujenga mfuko wa kukopeshana pembejeo za uvuvi kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji. Kamati inatambua kuwa ili sekta ya uvuvi ikue kwa kiwango cha kuridhisha na kuchangia kukua kwa uchumi ni lazima kuwepo na uwekezaji wa kutosha. Uwekezaji katika uvuvi bado hauridhishi ingawa sekta hii ina rasilimali za kutosha kuinua kipato cha wananchi na Taifa kwa ujumla. Kamati imebaini kuwa viwanda vya samaki nchini vinatozwa kodi nyingi ikilinganishwa na viwanda kama hivyo vilivyopo nchi za Kenya na Uganda. Hali hii inavifanya viwanda vya Tanzania visiweze kushindana kwa kasi ya uwekezaji na kutoa bei nzuri kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto za viwanja vya ndege nchini, usafirishaji wa minofu ya samaki kwa sasa inabidi kuanzia Nairobi, Kenya au Entebbe, Uganda na hivyo kuongeza gharama za uzalishaji kwa viwanda vya Tanzania. Kamati imebaini pia kuwa meli nyingi za Tanzania zimesimamisha uvuvi wa bahari kuu kutokana na gharama kubwa inayotokana na kodi ya mafuta *(Fuel Levy).* Hali hii inaifanya Tanzania isishindane vyema na nchi nyingine katika uvunaji wa rasilimaji za bahari na hivyo kuikosesha nchi yetu mapato na ajira. Hasara zaidi kwa nchi yetu ni pale inaposhindwa kuvuna samaki wahamao mfano, Tuna, kupitia bahari yetu na kuvunwa katika nchi jirani za Msumbiji na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali iboreshe mazingira yatakayowavutia wawekezaji wa kati na wakubwa watakaofanya uvuvi wa kibiashara *(Large Scale Fishing)* na kujenga viwanda vya kusindika samaki kwa kuangalia upya kodi inazotoza viwanda vya samaki ili viweze kwenda sambamba na nchi zingine za Afrika ya Mashariki. Aidha, kodi za mafuta kwa zana za uvuvi ziangaliwe ili kuvutia uwekezaji wa uvuvi katika bahari kuu. Pia Kamati inaishauri Serikali kuziangalia changamoto za viwanja vya ndege ili minofu ya samaki iweze kusafirishwa kutokea nchini kwani siyo tu itapunguza gharama za wenye viwanda bali pia itaongeza ajira na biashara kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Napenda kuwatambua wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Mwenyekiti na Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Abdusalaam S. Ameir, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Namelok E. M. Sokoine Mheshimiwa Dkt. Christine G. Ishengoma, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso,

Mheshimiwa Sylevester M. Kasulumbayi, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Seleman Said Bungara, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani na Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David (Mb) na Naibu Waziri, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro (Mb), kwa ushirikiano wao mzuri waliyoipa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu, Dkt. Charles Nyamrunda na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Yohana Budeba pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah na Katibu wa Kamati Ndugu Elieka Saanya kwa kuiwezesha Kamati kufanikisha shughuli zake na kuratibu taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho japo siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati

yetu, Mheshimiwa Pof. David Mwakyusa kwa kunipatia heshima ya kuwasilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Fungu 99 kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 jumla ya shilingi 54,566,123,500/=

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Kamani kwa kuwasilisha hoja hii kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati. Nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni tunaendelea na mtoa hoja mwingine anayefuata. Sasa nitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Maji, Mifugo na Uvuvi na yeye ni Mheshimiwa Sylvester Muhoja Kasulumbai. *(Makofi)*

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa leo kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 kanuni ndogo ya (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, natoa shukrani zangu za dhati kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi wa Jimbo la Maswa Mashariki kwa imani yao kwangu, makamanda wote (vijana, wazee na akina mama wa vyama vyote) kwa kuendelea kuniunga mkono katika kuhakikisha kuwa moto wa Maswa Mashariki unasambaa katika Majimbo yote ya Mkoa wa Simiyu. Ahadi yangu kwenu ni kuwatumikia kwa uwezo wangu wote kwa kadiri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa CHADEMA kikiwa chini ya Mtendaji wake mkuu (Katibu Mkuu Taifa), Dkt. Wilbroad Peter Slaa. Hakika kila Mtanzania anaona kazi anayoifanya ya kuhakikisha chama chetu kinakuwa juu na Watanzania wote wanatuunga mkono. Mungu ampe uhai, naamini ipo siku tutaifikia nchi ya ahadi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, kwa kuniamini na kuniteua tena na Naibu wangu Mheshimiwa Sabreena Sungura kuwa

Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii. Shukrani pia ziwafikie Wabunge wenzangu wote wa Kambi kwa ushirikiano wao kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niishukuru sana familia yangu yote inayoishi Maswa, naomba iendelee kunivumilia kwa kipindi chote nitakachokuwa natimiza majukumu yangu ya ndani na nje ya Bunge pamoja na yale ya kichama. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya samaki. Ilani ya CCM 2010-2015 kifungu cha 26 kinasema, na nanukuu:-

*"Uvuvi ni moja ya sekta za uchumi ambazo hazijapatiwa msukumo wa kutosha. Modenaizesheni katika uvuvi italenga katika kuwapatia maarifa wavuvi yatakayobadili na kuongeza uzalishaji wa samaki. Kuongeza ufanisi na tija na kubadili maisha ya wavuvi ni moja ya mapinduzi yanayolengwa katika Ilani ya 2010-2015. Katika kutekeleza hili Serikali itatilia mkazo uwezeshaji wa wavuvi, kuendeleza viwanda vya samaki, kusimamia uvunaji endelevu wa samaki katika bahari kuu".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi ni sekta muhimu katika nchi hii kutokana na mchango wake mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, lishe, kipato na kuingiza nchini fedha za kigeni. Pamoja na umuhimu wake bado sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo sekta inakabiliwa nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina ukubwa wa kilomita za mraba 942,600, ambapo 6.55% ya eneo hilo limefunikwa na maji (kilomita za mraba 615,000). Mavuno ya samaki nchini Tanzania yamefikia tani 350,000, kiasi ambacho ni kidogo kuliko uwezo unaoweza kuvuliwa ambao ni tani 750,000. Kiasi kikubwa cha samaki wanaovuliwa nchini hutumika kama chakula ukiacha samaki aina ya sangara, kamba na dagaa ambao huuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitano iliyopita, Idara ya Uvuvi imekuwa ikichangia kiasi cha 1.6% hadi 3.1% ya uchumi wa nchi. Kwa makisio yaliyopo, ulaji wa samaki kwa mwaka ni kilo nane (8) kila mtu, ambayo ni chini ya kiwango cha *FAO* cha kilo 11. Takwimu za uzalishaji wa samaki zinaonyesha kupungua kwa samaki wanaovuliwa kutoka tani 375,535 mwaka 2005 hadi 335,674 tani 2009. Mauzo ya samaki nje ya nchi nayo yalipungua kutoka tani 57,289 2005 hadi tani 41,148 mwaka 2009. Kwa ujumla, mauzo ya samaki nje ya nchi yamekuwa ni kati ya asilimia 15 na 12 ya samaki wote wanaovuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Hali ya Uchumi inaonyesha kuwa shughuli za sekta ya uvuvi zilikua kwa asilimia 1.5 mwaka 2011. Aidha, shughuli hizo zilichangia asilimia 1.4 ya pato la Taifa kwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi inatoa ajira kwa zaidi ya watu 177,527 na takriban watu milioni nne (4) wanaendesha maisha yao kwa kutegemea sekta hii ya uvuvi. Kwa wastani, kati ya 2004 hadi 2010 mauzo ya nje ya samaki na bidhaa za samaki yaliingizia nchi yetu wastani wa dola za kimarekani milioni 195.17. Hii ni kwa mujibu wa *Investment opportunities in the fisheries industry, December, 2011*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Uvuvi ambayo lengo lake kwenye MKUKUTA II ni kuifanya sekta ndogo ya Uvuvi kukua kutoka 2.7% hadi 5.3% mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ambazo sekta ya uvuvi zinachangia asilimia zaidi ya tano (5%) katika pato la taifa au kwenye mapato ya fedha za kigeni ni pamoja na Mauritania, Senegal, Madagascar, Namibia, Mali, Ghana, Seychelles na Msumbiji. Hii ni kwa mujibu wa *Fisheries and Aquaculture in Sub-Saharan Africa: Situation and Outlook, by Fisheries Department FO, Rome, Italy.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Uvuviu (*FSDP*). Bajeti ya Mpango wa Utekelezaji wa Miaka Mitano katika kutekeleza programu ya maendeleo ya sekta ya uvuvi ilikadiriwa kuwa ni shilingi 302,683,000,000. Mpango huo unaonyesha kuwa kama uwekezaji huo katika sekta ya uvuvi itafanyika ni wazi kuwa faida zifuatazo hadi mwaka wa fedha 2015/ 2016 zinatarajiwa:-

(i) Kukua kwa sekta ya uvuvi ingekuwa kutoka asilimia nne (4%) hadi asilimia saba (7%) kwa mwaka;

(ii) Mchango wa sekta ya uvuvi kwenye pato la taifa litaongezeka kutoka asilimia 1.2 kwa mwaka ya sasa hadi asilimia tano (5%) kwa mwaka;

(iii) Kuongezeka kwa mapato ya taifa yatokanayo na sekta ya uvuvi kutoka shilingi bilioni 6.58 hadi shilingi bilioni 12 kwa mwaka;

(iv) Kuongezeka kwa bidhaa za uvuvi kutoka kwa makadirio ya sasa ya tani 350,000 hadi tani 450,000. Hii ni kutokana na taarifa ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, toleo la Juni, 2012, ukurasa wa 68;

(v) Kuongeza mauzo ya samaki nje ya nchi kutoka tani 51,426 zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 174 hadi tani 62,850 zenye thamani za dola za kimarekani milioni 215;

(vi) Kuongeza ajira kwa wale wanaojihusisha moja kwa moja kutoka ajira 170,038 za sasa hadi ajira 200,000; na

(vii) Kuongezeka kwa ajira ambazo si za moja kwa moja katika sekta ya samaki kutoka ajira 4,000,000 za sasa hadi ajira 4,200,000; ikiwa ni ongezeko la ajira 200,000. Hii ni kwa mujibu wa *Fisheries Sector Development Programme, Ministry of Livestock and Fisheries Development, December, 2010*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayoikabili sekta ya uvuvi na teknolojia ya ufugaji wa samaki ni kuwa gharama za uwekezaji katika sekta hiyo ni kubwa, wadau kushindwa kupata mikopo, utaalamu wa kuendesha sekta hiyo bado ni mdogo kutokana na wadau wengi kuwa na taaluma ya asili wakati teknolojia inabadilika kila mara na mwisho ni kukosekana kwa rasilimali watu yenye ujuzi kuweza kushirikiana vyema na wadau wakuu katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Uchumi wa Taifa wa Miaka Mitano kuhusu sekta ya uvuvi unasema kuwa maendeleo na matumizi ya rasilimali za uvuvi pamoja na masoko imetengewa jumla ya shilingi milioni 75,000/- na kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, sekta ilitakiwa kutengewa jumla ya shilingi milioni 18,320. Katika fedha hizo kuna fedha za kudhibiti ubora wa bidhaa za samaki, miundombinu na matumizi ya teknolojia ya ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Mpango wa Miaka Mitano inabainishwa kuwa kuwezesha maendeleo ya ufugaji wa samaki, kwa miaka mitano hadi mwaka 2015/2016 zitumike jumla ya shilingi milioni 11,550/- kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 ilitakiwa zitengwe jumla ya shilingi milioni 2,450/- kwa ajili ya maendeleo ya rasilimali ya ufugaji samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa kwa uvuvi wa Baharini. Nchi yetu ina urefu wa ukanda wa uvuvi wa baharini unaokadiriwa kufikia 1,450 km na ukubwa wa

eneo la bahari kuu - Bahari ya Hindi ni takriban kilomita za mraba 223 000 zenye uwezo wa kuzalisha samaki tani 730, 000. Hii ni kwa mujibu wa *Fisheries and fishing potential in Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji na matumizi ya samaki kwa soko la ndani na la nje bado ni makubwa sana, kiasi kwamba bado samaki wanaovuliwa hawatoshelezi; bahari kuu tunayoimiliki bado ina samaki wengi ambao kutokana na uwezo wetu mdogo kiteknolojia hatujaweza kuvua samaki wengi waliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kwa uvuvi wa baharini. Wavuvi wengi katika mwambao wa bahari wanakumbana na matatizo mengi ambayo yanasababisha kupata hasara au kushindwa kuvua kwa kadri ya uwezo wao na sababu hizo ni zifuatazo:-

(i) Kutokuwa na sehemu maalum kwa ajili ya kufikishia samaki;

(ii) Kukosa vifaa maalum kwa ajili ya kuhifadhia samaki kabla ya mauzo;

(iii) Kutokuwepo kwa mazingira safi na salama katika ukaangaji na ukaushaji wa samaki;

(iv) Kutokuwepo na meli na vifaa pamoja na teknolojia inayoweza kuwezesha wavuvi wetu kuvua samaki kwenye bahari kuu; na

(v) Na mwisho ni kukosekana kwa viwanda vya samaki katika mwambao mzima wa bahari ya Hindi sehemu inayomilikiwa na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa jarida la *East African Business Week* la tarehe 16 Januari, 2010, Serikali kupitia Mamlaka ya Uvuvi katika bahari kuu ilitiliana mkataba na Serikali ya Japan kupitia ushirika wa Japan *Tuna Association*, ambapo Serikali ilitarajia kupata mapato ya dola milioni 200 kwa mwaka kutokana uvuvi wa tuna utakaokuwa unafanyika katika bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na makubaliano hayo yaliyotiwa saini baina ya Tanzania na Japan, ushirika wa wavuvi hao wa Japan ulitarajiwa kuleta meli za uvuvi 30 kwa ajili ya kufanya kazi katika bahari kuu katika mwaka wa kwanza tu wa kusainiwa mkataba huo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Serikali ni kiasi gani cha mapato kimepatikana tangu kusainiwa kwa mkataba huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Februari mwaka huu, habari zilichapishwa kuhusu "ushindi" wa Serikali katika kesi maarufu kama *'Kesi ya Samaki wa Magufuli'* iliyokuwa ikiwakabili wavuvi raia wa China wamiliki wa meli ya uvuvi ya *Tawariq 1* waliofanya uvuvi haramu katika pwani ya Bahari ya Hindi, kwenye maji yaliyo katika eneo la Tanzania. Mwezi huohuo wa Februari, gazeti la Nipashe likachapisha habari kutahadharisha kuwa meli hiyo inazama kutokana na kuwepo kwa hujuma kwa mali na vifaa vya meli hiyo

kunakofanywa na baadhi ya watu ambao ni maafisa wa bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wale wote ambao meli hiyo ilikuwa chini ya uangalizi wao na ni kwa nini meli hiyo sasa haifanyi kazi wakati meli ilikuwa ni nzima kabisa na ilikuwa inafanyakazi kwa ushahidi dhahiri kuwa ilikamatwa ikiwa kazini. Ikiwa meli hii ni mali ya Serikali baada ya kushinda kesi, hujuma iliyofanyiwa na hasara inayopatikana kwa kuzama au kuja kuikarabati, tutakuwa tumetia adabu au tumetiwa adabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi Upinzani inauliza, je, hasara ya meli hiyo ya uvuvi ikiwa ni mali ya Wachina, *ikizaa* kesi nyingine, tunao uhakika kweli wa kushinda tena kesi? Au ndiyo tutaingia kwenye deni la gharama kubwa zaidi? Serikali yenyewe kila leo inalia na ukata, bajeti za Wizara kila mwaka wa fedha ni kuhemea kwa wafadhili na mikopo ya riba za kupaa, itazikamua wapi fedha kwa ajili ya kulipia gharama za kesi nyingine Mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa samaki. Shughuli za ufugaji wa samaki unafanywa na wafugaji wadogo wadogo. Hata hivyo, ufugaji wa samaki lazima ishindane na shughuli zingine za vijijini kwa eneo la ardhi, maji, nguvu kazi na vyakula. Hali hii hupelekea umuhimu wa kutathmini gharama na faida ya ufugaji samaki na mchango wake kwa maisha ya wakazi wa vijijini kulingana na shughuli zao zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo, ufugaji wa samaki hukabiliwa na matatizo na changamoto zingine kama ukosefu wa sera thabiti ya ufugaji samaki; mabadiliko katika sera za uchumi; ukosefu wa teknolojia bora; upungufu wa vifaranga bora; miundombinu ya usafiri duni; utafiti usiokidhi mahitaji; ukosefu wa takwimu za uzalishaji; upungufu wa taarifa sahihi za utunzaji wa bwawa la samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na uwezo wa kufanya shughuli kwa mafanikio, ni muhimu kuwa na takwimu ya utendaji na shughuli husika. Vivyo hivyo, ili kuendesha shughuli za ufugaji samaki kibiashara, mfugaji analazimika kuchukua na kutunza takwimu kwa hatua zote au shughuli yoyote anayoifanya ikiwemo ya kutunza matumizi na mapato ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti. Kambi Rasmi ya Upinzani inaelewa kuwa vituo hivi vya utafiti vilikuwepo miaka yote na vinaendelea kutimiza majukumu yake ya msingi kulingana na matakwa ya uanzishwaji wake. Swali la kuuliza ni kwani majukumu ya Taasisi ya siwe ni sehemu ya majukumu ya Wizara? Au ni kwa nini taasisi zote za utafiti zisiwe chini ya Tume ya Sayansi na Teknolojia-*(COSTECH)?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweka kumbukumbu vizuri ni kwamba, Februari 17 mwaka 2009, Serikali kupitia Rais Jakaya Kikwete, ilitangaza azma ya kutenga asilimia moja ya pato la taifa kwa ajili ya maendeleo ya utafiti. Fedha hizo zilitakiwa ziende moja kwa moja kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia. Kwa nukuu hiyo, ni kwa nini Serikali inashindwa kuoanisha

dhana nzima ya Rais na kuiweka katika hali halisi ya kiutendaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa migogoro mingi iliyopo baina ya wananchi na Serikali inatokana na ardhi, naomba kufanya marejeo kwa vituo viwili vya tafiti za mifugo kama mfano wa jinsi vituo hivyo utafiti unavyohitaji ardhi na eneo la kutosha na tuone ni ardhi kiasi gani inayomilikiwa na kila kituo, pengine vituo hivyo vinahitaji ardhi zaidi ili kufanikisha tafiti zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo. Ilani ya uchaguzi ya CCM kwenye sekta hii ilisema na nanukuu kifungu cha 25:-

"*Ufugaji ni moja ya sekta zinazohitaji kusimamiwa ili iweze kuchangia ipasavyo katika uchumi wa kisasa. Katika kipindi cha Ilani 2010-2015 mkazo utaelekezwa katika matumizi ya maarifa katika sekta ya mifugo. Jukumu kuu la msingi katika ufugaji na litakuwa ni kuleta mabadiliko yatakayoiondoa sekta hii kutoa uduni wa ufugaji na kuwabadili wafugaji wetu kutoka wafugaji wahamaji. Mkazo utaelekezwa katika kutatua matatizo ya malisho na maji na kuwafikisha wafugaji katika ukulima mchanganyiko na ufugaji wa mabandani wenye tija kubwa, utakaotoa nyama na maziwa bora".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha muongo mmoja uliopita ukuaji wa sekta ya mifugo umekuwa chini ya kiwango cha asilimia 2.7 ambacho ni chini ya

lengo la MKUKUTA la ukuaji wa asilimia 2.9 kwa mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina rasilimali kubwa ya maliasili ikiwemo ardhi, malisho na idadi kubwa ya mifugo. Kati ya jumla ya hekta milioni 94 za rasilimali ya ardhi, hekta milioni 60 ni nyanda za malisho zinazofaa kwa ufugaji. Kwa sasa kuna ng'ombe milioni 21.3, mbuzi milioni 15.2 na kondoo milioni 6.4. Mifugo wengine ni pamoja na nguruwe milioni 1.9, kuku wa asili milioni 58 (Taarifa ya Hali ya Uchumi 2011). Sekta ya Mifugo ina nafasi kubwa katika kujenga uchumi imara wa taifa, kuongeza kipato kwa Watanzania wanaotegemea mifugo na kutoa fursa za ajira sanjari na kuhifadhi rasilimali za taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mifugo umegawanyika katika mifumo mikuu miwili ambayo ni ufugaji huria na ufugaji shadidi. Mfumo wa ufugaji shadidi japo sio mkubwa nchini, unatiliwa mkazo zaidi katika kuendeleza ufugaji na uwekezaji kwani unachangia zaidi kwenye uchumi wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, mfumo wa ufugaji huria ambao hufanywa na wakulima-wachungaji na wachungaji -wahamaji, ni mfumo unaotegemea upatikanaji wa malisho na maji kwa msimu na matokeo yake husababisha wafugaji kuhamahama. Mfumo huu unakabiliwa na matatizo ya utunzaji duni wa mifugo, matumizi duni ya teknolojia za kisasa, kuhodhi mifugo wengi zaidi ya uwezo wa ardhi na ukosefu wa mazingira mazuri ya masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matatizo yanayoukabili mfumo huu, bado umeendelea kwa miongo mingi kuwa tegemeo kwa jamii ya wafugaji wahamaji. Ili kuendeleza na kufikia malengo yake, sekta ya mifugo inahitaji sera ya mifugo iliyo pana itakayotoa mwongozo kwa wadau wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba makubwa ya mifugo yana uwezo wa kuongeza viwango vya uzalishaji na uuzaji wa mifugo na mazao yake nje ya nchi, ajira na kuboresha maisha ya wafanyakazi wake. Mkakati umetumika wa kugawa mashamba makubwa ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (KARATA) na yale yaliyokuwa chini ya Kampuni ya Ng'ombe wa Maziwa *(DAFCO)* kuwa mashamba yenye ukubwa wa kati kwa ajili ya ufugaji wa kibiashara unaolenga kutekeleza dhana hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu umeongeza upeo wa umilikaji mashamba na pia kuwawezesha Watanzania kuingia katika ufugaji wa kibiashara. Maeneo ya Ranchi za KARATA yaliyobaki yataendelea kutumika kama ranchi za mfano na maeneo yasiyo na magonjwa ya mifugo kwa ajili ya soko la nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kuirudisha mifugo yote sambamba na wahamiaji haramu wa mifugo toka nchi za Rwanda na Uganda iliyoingizwa Mkoa wa Kagera isivyo halali ifikapo Mei Mosi, 2012. Lakini kwa masikitiko makubwa hadi sasa hivi hakuna zoezi lolote lililokwishafanyika.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwaeleza wananchi wa Mkoa wa Kagera walioathirika na wanaoendelea kuathirika na uvamizi huo. Swali wanalojiuliza wananchi wa Mkoa wa Kagera ni hili, waendelee kuitegemea Serikali hii ya CCM inayotoa ahadi hewa katika kulinda usalama wa maisha yao au watafute njia nyingine mbadala? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ranchi ya Kitengule inapakana na vijiji sita vya Kishoju, Kihanga, Katanda, Kibwera, Mushabaiguru na Mulamba vyenye jumla ya wakazi wanaozidi 20,000. Cha kushangaza wakazi hao wote walipewa jumla ya hekta 2,000 tu, huku ikijulikana wazi kuwa mahitaji halisi ya wanavijiji hao ni zaidi ya hekta 20,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vitalu vya Ranchi ya Kitengule viligawiwa kwa wawekezaji wadogo wadogo kwa wastani wa kila mwekezaji alipata hekta 2,000 na 3,000. Lakini cha ajabu ni kuwa Kiwanda cha *Kagera Sugar* kilipewa hekta zaidi ya 45,000, wakati kiwanda hakina mifugo kwa kisingizio tu cha kutaka kulima miwa ndani ya eneo hilo la ufugaji. Hata hivyo, hadi sasa Kiwanda hicho kinatumia eneo hilo kukodisha kwa wafugaji kutoka Rwanda na Uganda ilhali wafugaji wetu wakikosa eneo la kulishia mifugo yao. Je, ni hatua gani zinachukuliwa kwa mwekezaji anayeshindwa kutumia mali aliyopewa kwa matumizi kwa kadri ya makubaliano ya mkataba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo wa asili na ufugaji wake una mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa. Zaidi ya 98% ya ng'ombe, 99% ya mbuzi na kondoo na mifugo wengine kwa zaidi ya 90% ni wa asili ambao una ustahimilivu mkubwa dhidi ya magonjwa na mazingira magumu ya Kitropiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo hawa huchangia 99% ya uzalishaji wa mazao yatokanayo na wanyama kama nyama, ngozi na mauzo ya mifugo hai; 70% ya uzalishaji maziwa na mayai. Aidha, rasilimali hii ya asili imeajiri zaidi ya kaya milioni 1.7 za wafugaji na wafanyabiashara (viwanda, mabucha, na kadhalika), inaongeza tija katika kilimo kwa kuzalisha samadi (mbolea) na kutumia wanyama kazi, ni mitaji na mabenki kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali hii kwa kiasi kikubwa imewezesha uchangiaji katika utekelezaji wa sera za Serikali hasa ujenzi wa shule, zahanati za kata na kulipa kodi mbalimbali kwa Serikali. Tunapenda kuutambua mchango mkubwa wa wafugaji wa asili wa Kitanzania, ambao kwa jitahada zao, weledi-asilia na uzoefu wa ufugaji kutoka kizazi hadi kizazi umeendelea kutuwezesha kuneemeka na rasilimali hii mifugo. Wote tunatambua umuhimu wa sekta hii kwani siku haiwezi kuisha bila kutumia rasilimali hii, hususan nyama na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri shahiri, sekta hii ikiendelezwa itatoa mchango maradufu kwa nchi na wafugaji kwa ujumla. Nchi ya India ambayo inazalisha maziwa kutokana na mifugo wa asili (ng'ombe na

nyatimaji) pekee imepiga hatua kubwa hadi kufikia kuwa mzalishaji mkubwa wa maziwa duniani. Lakini maendeleo hayo yametokana na jitahada za makusudi kwa kuendeleza sekta ya asili ya mifugo. Hapa kwetu, bado ipo dhana inayoutukuza ukoloni mamboleo kwa kuthamini vya kigeni na kubeza cha kwako cha asili. Aidha, ikumbukwe kuwa, hata hao mifugo wa kigeni huko itokako ni wa asili pia, hivyo hakuna sababu ya sisi Watanzania kubeza chetu cha Kitanzania badala ya kukiendeleza kwa kuboresha mbegu kama wenzetu wanavyofanya kwa vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya uendelezaji ufugaji wa asili. Pamoja na umuhimu wake bado Serikali haijautambua umuhimu wa sekta ya asili kwa kutoipa kipaumbele katika maendeleo ya sekta nzima ya mifugo. Hii inadhihirika hata kwenye fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara hii. Katika maombi yake, Wizara hii imetenga 1.77% (sawa na takribani shilingi milioni 718 tu) ya bajeti yake, yaani jumla ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa mwaka 2012/13 kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yenye mifugo ya asili yanahitaji miundombinu ya ufugaji ikiwemo majosho, malambo na mabirika ya maji, minada ya kuuzia mifugo, vibanda vya kukaushia ngozi, vituo vya kukusanya maziwa na miundombinu mingine muhimu. Aidha, ufugaji wa asili unahitaji huduma muhimu ikiwemo ya afya ya mifugo, upandishaji kwa chupa *(artificial insemination*) na huduma ya ugani kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na mchango mkubwa wa sekta hii ya ufugaji wa asili, ni dhahiri kuwa kiasi cha fedha kilichotengwa ni kidogo. Bajeti hii inadhihirisha jinsi ambavyo Serikali hata katika mipango yake isivyoyapa kipaumbele maendeleo ya ufugaji wa asili na wafugaji kwa ujumla. Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kupata maelezo ya kina ni kwanini sekta ya ufugaji wa asili haikutengewa fedha za kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutenga maeneo ya malisho. Nchi yetu ina maeneo makubwa ya takribani hekta milioni 60 zinazofaa kwa ufugaji. Hata hivyo, pamoja na ukubwa huo ardhi inayofaa ufugaji ni 40% tu ndiyo inayotumika kwa sasa kutokana na kukosekana kwa miundombinu muhimu katika ufugaji na uvunaji mifugo na huduma za kijamii ikiwemo maji na afya katika maeneo hayo. Aidha, kasi ya upimaji wa maeneo ya malisho bado ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hekta milioni 60 zinafaa kwa shughuli za ufugaji, lakini katika mwaka mzima wa 2011/2012 ndani ya Wilaya 67 ni hekta milioni 1.26 tu zimeainishwa hii ni 2.1% tu ya eneo linalofaa ufugaji. Kasi hii ni ndogo, hairidhishi katika kuleta maendeleo ya ufugaji wa asili. Hata hivyo, inatia shaka kwa maeneo ya jumla Wilaya 67 kuwa na hekta milioni 1.26 tu za ufugaji. Hii inaonyesha ni jinsi ufugaji wa asili usivyothaminiwa. Tunashuhudia wawekezaji wa kigeni wakigawiwa maeneo makubwa ya nchi yetu na kwa mchakato wa haraka lakini inapokuwa kwa

wawekezaji wa ndani hasa katika ufugaji wa asili fursa hiyo hawaipati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu huu wa Serikali unasababisha wafugaji kuendelea kuonekana kuwa wavamizi na wavunjifu wa sheria. Hii dhana hasi dhidi ya wafugaji si sahihi kwani Serikali inachelewa yenyewe kutenga maeneo, hali inayosababisha uvunjifu wa sheria. Je, inakuwaje Serikali inayosimamia utekelezaji wa sheria ndiyo inajenga mazingira ya uvunjifu wa Sheria? Tunaitaka Serikali iongeze kasi ya kupima haya maeneo na iyape kipaumbele yale maeneo ambayo tayari hawa wafugaji wa asili wanaendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wakulima na wafugaji. Tumeshuhudia migogoro mikubwa baina ya wakulima na wafugaji kuongezeka na kwa sura tofauti siku hadi siku. Kwa mfano, mgogoro uliotokea Wilayani Rufiji mwezi Mei 2012 ambao ulisababisha kifo cha Mtanzania mwenzetu (Mungu ailaze roho yake mahala peponi – amina), majeruhi na uharibifu wa mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara yanayotakana na migogoro ya aina hii ni makubwa kiasi cha kuathiri ustawi wa kiuchumi na kijamii kwa ujumla. Chanzo kikubwa cha migogoro hii ni ardhi. Je, hili linawezekanaje kwa nchi kubwa kama Tanzania, ambako 60% ya eneo linalofaa kwa ufugaji halitumiwi na hata eneo kubwa linalofaa kwa kilimo nalo pia halitumiki? Je, haya makundi ya wakulima na wafugaji yanafarakana kwa nini? Suluhisho hapa ni kushirikisha

makundi yote ya kijamii na kuweka bayana mipango ya matumizi ya ardhi za vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile uiainishaji na utengaji wa maeneo ya malisho yafanywe kwa kasi. Aidha, mamlaka ziache kufanya maamuzi kwa upendeleo uliojikita kwenye misingi isiyo ya utawala bora, hasa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya Kikatiba, nchi yetu imejengwa na waasisi wa Taifa letu katika misingi ya utawala bora na kuthamini utu wa raia wake. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania toleo la 1977; Ibara 2 (1-2) inataja maeneo ya nchi na pia kumpa Rais madaraka ya kuigawa katika Mikoa na Wilaya bila kuzingatia ukabila au shughuli za kiuchumi zinazofanyika. Ibara 12 na 14 zinatoa na kulinda haki na usawa wa Mtanzania na kusisitiza kuthamini utu wake na Ibara ya 14 inampa Mtanzania haki ya kuishi na hifadhi ya maisha yake. Aidha, Ibara ya 17(1) inampa haki Mtanzania ya kwenda popote katika eneo la nchi. Mfugaji Mtanzania anastahili haki hiyo ya Kikatiba. Wafugaji tunaowazungumzia hapa wamezaliwa Tanzania na Katiba ya nchi inatawambua na kulinda haki zao kama ilivyo kwa Watanzania wengine. Kambi ya Upinzani inataka maelezo ni lini Serikali itakamilisha jukumu lake la kupima maeneo kati ya wakulima na wafugaji ili kuondoa migogoro hii ambayo inawaumiza Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya uagizaji wa nyama ya kuku toka nje ya nchi. Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2011 imeonyesha kuwa nchi yetu

ina kuku takribani 58 milioni ambao wanafugwa hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuku wote hao bado Wizara hii inaendelea kutoa vibali ya kuagiza nyama ya kuku kutoka Brazil, jambo ambalo ni kinyume cha sheria zetu na matamko mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa na serikali hapa Bungeni mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 5/4/2012, Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Mifugo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Dr. E.J.Sekidio) alitoa kibali cha kuagiza nyama ya kuku kutoka nchini Brazil kwa Kampuni ya *Frostan Ltd*, ya Jijini DSM kibali chenye namba 000551 cha kuagiza kiasi cha kilo 27,100 au tani 27.1 ya nyama za kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 20/7/2012 Mkurugenzi Mkuu huyo huyo alitoa kibali kingine chenye namba 00000409 na *code* namba 0655 kwa Kampuni ya *Malik Faraj Company Limited* cha kuagiza nyama ya kuku kutoka Zanzibar kiasi cha katoni 10,000 zenye kilo 10 kwa kila katoni moja na hivyo ni sawa na kuagiza kilo 100,000 au tani 100 za nyama ya kuku kwa ajili ya migodi ya kuchimba madini ya *Barrick*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata majibu ya kina kuhusiana na vibali hivi na kama ni sahihi kuendelea kuagiza nyama ya kuku kutoka nje wakati wapo wafugaji wa kuku hapa nchini. Aidha, tunataka kujua nyama za kuku kiasi cha tani 100 zilizoagizwa kutoka Zanzibar ni kutoka nchi gani? Au ni

kutoka Zanzibar? Na kama ni kutoka Zanzibar wanahitaji kibali cha kusafirisha nyama kuja Bara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la magonjwa ya milipuko limekuwa hadithi ya mara kwa mara ndani ya nchi yetu. Kwa uhakika hatutaweza kufikia kwenye "mapinduzi meupe" na ufugaji wa kibiashara kama suala la magonjwa ya milipuko halitapewa kipaumbele na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Magonjwa kama Homa ya Midomo na Miguu (*Foot and Mouth Disease-FMD*), Homa ya Mapafu (*Contagious Bovine Pneumonia – CBPP/CCPP),* Kimeta (*Anthrax)* yamekuwa magonjwa tishio kwa wafugaji na taifa kwa ujumla. Kwa mfano *FMD* kwa miaka ya nyuma ilikuwa inashambulia makundi ya mifugo mara moja tu kwa mwaka; kuanzia miaka ya 1999 hali ya kushambulia hadi mara tatu zizi moja imekuwa jambo la kawaida. Ni vema Wizara ijue sababu za hali hii inayokwamisha maendeleo katika sekta hii na kuendelea kuleta umaskini ndani ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ya mifugo yaenezwayo na kupe yamekuwa tatizo sugu kwa taifa hili. Serikali kwa kupitia Wizara hii imekuwa ikijaribu bila mafanikio makubwa kupunguza tatizo liletwalo na kupea kwa kutoa ruzuku kwenye dawa ya kuogeshea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza pamoja na ruzuku kwenye madawa ya kuogeshewa, ruzuku kubwa sasa ilekezwe kwenye chanjo ya magonjwa kama Ndigana Kali (*East Coast Fever –E.C.F)* kwani ugonjwa huu ndio hatari kupita

yote yaletwayo na kupe na kwa bahati chanjo yake inapatikana, ila kwa bei kubwa sana; hivyo, wafugaji wengi kutoweza kumudu kuinunua kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo kwa muda mrefu wataalamu na wadau wengi wamekuwa wakilikwepa ni suala la Bima ya Mifugo ili kuwakinga mifugo dhidi ya majanga na matokeo mbalimbali ya mabadiliko ya tabianchi kama ukame wa mara kwa mara, magonjwa ya mifugo na madhara yatokanayo na wanyama wakali wa pori kama simba na fisi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba ili kuweza kuwashawishi wafugaji kuongeza ubora wa mifugo na kupunguza madhara ya magonjwa, Serikali kwa kupitia wizara hii ianzishe mkakati wa Bima ya Mifugo ili kukinga wafugaji na majanga na ajali mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia kwa waathirika wa ugonjwa wa mifugo Kyengenge. Mwishoni mwa miaka ya themanini palizuka ugonjwa wa midomo na mapafu kwa mifugo, ambapo mifugo wengi walikufa na kuwaacha wafugaji hao katika hali ya umasikini wa kutupa. Kwa kuwa Serikali imetambua kuwa ni muhimu kuwasaidia wafugaji waliopatwa na majanga kwa mifugo wao, kama Rais Kikwete alivyofanya kwa wafugaji wa Longido na Monduli hivi karibuni, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwafidie wafugaji wa Kyengenge ili waweze kuanza kufuga kama ambavyo walikuwa wakifanya miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usindikaji masoko na ulaji wa nyama. Hapa nchini kuna zaidi ya minada 300 ya

awali, 13 ya upili na sita ya mipakani. Minada yote ya awali inasimamiwa na Halmashauri za Wilaya ambapo minada ya upili na ya mipakani inasimamiwa na Wizara. Minada michache ya awali inafanya kazi ila mingi ni mibovu. Aidha, vipo viwanda sita vya kusindika nyama na machinjio za kisasa saba. Kwa sasa, ulaji wa nyama kwa mtu kwa mwaka ni kilo 11 kiasi ambacho ni chini ya kiwango cha kilo 50 kinachopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (*FAO*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo upungufu wa miundombinu kwa ajili ya usindikaji na masoko ya mifugo na mazao yake. Pia, kumekuwepo na uingizaji wa mazao ya mifugo yenye ruzuku kubwa kutoka nje ya nchi ambayo hukatisha tamaa wawekezaji pamoja na kuleta ushindani usio sawa kwa mazao ya mifugo yanayozalishwa au kusindikwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ikijibu Swali Namba 76 Februari 4, 2009 kuhusu kujenga Viwanda vya Nyama kwenye Mikoa inayofuga kama vile Arusha, Manyara, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Morogoro na kadhalika, Naibu Waziri alisema:-

*"Katika kutimiza azma hii, baadhi ya wawekezaji kutoka sekta binafsi wamejenga machinjio na viwanda vitatu (3) vya kisasa vya kusindika nyama vya Sumbawanga Agricultural and Animal Feeds (Sumbawanga, Rukwa). Tanzania Pride Meat (Mvomero, Morogoro) na Mkuza Chicks (Kibaha, Pwani). Aidha, Serikali imeuza asilimia 51 ya hisa za machinjio ya kisasa ya Dodoma kwa Kampuni ya National Investment Company Limited (NICOL) na*

*asilimia 49 zimechukuliwa na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO). Vile vile, Wizara imebinafsisha Kiwanda cha Kusindika Nyama cha Shinyanga kwa Kampuni ya Triple "S" Beef Limited".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wafugaji katika Mikoa ya wafugaji ni kwa nini viwanda vya kusindika nyama havijengwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kumekuwepo na upotoshaji mkubwa unaofanywa na Serikali kuwa kuna ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo, lakini ukweli ni kuwa ujenzi huo ni wa machinjio (Ruvu, Shinyanga na Dodoma) na siyo viwanda vya kusindika. Je, bila viwanda vya kusindika nyama na kuuza na kusafirisha nyama nje ya nchi tunawezaje kutumia mifugo yetu kuinua uchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sekta binafsi bado haina uwezo wa kutosha wa kuwekeza katika viwanda vya kusindika mazao, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ijenge viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na baadaye viwanda hivyo viendeshwe kwa utaratibu wa ubia kati ya Serikali na sekta binafsi. Kadhalika, Serikali ihakikishe viwanda vilivyobinafsishwa vinafanya kazi zilizotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usindikaji, masoko na unywaji wa maziwa. Tanzania ina ng'ombe milioni 21.3 na kati ya hao 680,000 ni wa maziwa na wanazalisha jumla ya lita milioni tano (5) kwa siku na tunasindika takriban lita 105,000 kwa siku. Inasikitisha ongezeko la

uzalishaji haliendi sambamba na uongezaji thamani wa zao la maziwa. Takwimu hizi zinaonyesha bado kuna lita nyingi sana ambazo hazijakusanywa wala kusindikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Sekta ndogo ya maziwa kwenye pato la Taifa kwa nchi tatu za Afrika ya Mashariki kwa mwaka 2009 ni: Maziwa: 1.2% Tanzania, 1.5% Kenya, 4.1% Uganda, Jumla ya Wafugaji waliokuwepo kwa mwaka 2009 ni 1,764,000. Hii ni kwa mujibu wa *MLFD (2010), ASDS (2010), UBOS (2010).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007, nchi za Afrika ya Mashariki zote zilizalishwa lita bilioni sita (6) za maziwa, na hizo zilikuwa ni sawa na 25% ya uzalishaji mzima kwa bara la Afrika, na kati ya hizo Kenya ilitoa asilimia (58%), Uganda (25%), Tanzania (14%), Rwanda (5%), Burundi (0.28%).

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizopo. Viwanda vingi vimeshindwa kuendelea kusindika kutokana na mazingira magumu ya biashara hapa nchini. Hasa uwepo wa gharama kubwa za uzalishaji na uendeshaji wa biashara katika sekta ya Maziwa. Maeneo makubwa yanayoonekana kuathiri sekta ni:-

(i) Uwezeshaji Mdogo wa mamlaka husika ya kuendeleza na kusimamia secta (Mf. Bodi ya Maziwa);

(ii) Serikali kutoweka mpango maalum kwa kufuata mlolongo wa thamani wa kuendeleza ufugaji wenye tija;

(iii) Uhamasishaji Mdogo wa kutumia bidhaa za maziwa zitokanazo na Maziwa (Mpaka sasa kila Mtanzania anakunywa takribani lita 41/ mwaka chini ya kiwango cha lita 200/kwa mwaka kinachopekezwa na *FAO*; na

(iv) Kutokuwepo kwa vituo vya kukusanyia maziwa (*milk collection centers*) kwenye maeneo yenye wafugaji wa ng'ombe wazalisha maziwa ambayo ni malighafi muhimu inayoweza kutumika kwenye viwanda kwa kusindika maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda ina ng'ombe milioni 6.8, lakini wanazalisha lita 3.2 milioni za maziwa kwa siku na wanasindika wastani wa lita 394,520 kwa siku. Msindikaji mkubwa, Sumeer, anasindika lita 120,000 kwa siku ambacho ni zaidi ya kiasi cha usindikaji wa viwanda vyote vya Tanzania kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa Sekta ya Maziwa imeendelea kukua taratibu sana hapa nchini ukilinganisha na wenzetu katika nchi jirani. Hii imetokana na kutokuwepo kwa sera muafaka za kodi, mathalani Kenya ambapo maziwa ya maji hayatozwi kodi, jambo ambalo limewezesha ukuaji wa sekta ya usindikaji maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hizi za Afrika ya Mashariki kwa mwaka 2009 zilikuwa na viwanda vya usindikaji maziwa kama ifuatavyo: Tanzania (35), Kenya (27), Uganda (16). Uwezo wa viwanda hivyo kusindika

maziwa kwa siku ilikuwa Tanzania lita 394,600, Kenya lita 2.9 milioni na Uganda lita 448,200. Lakini hali halisi ya uzalishaji kwa viwanda hivyo ni kuwa Tanzania inasindika lita 105,380, Kenya lita 2,484,000 na Uganda lita 204,100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya maziwa kwa nchi hizi takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania ni aslimia 26.7%, Kenya asilimia 85.7%, na Uganda ni asilimia 45.5%. Kwa takwimu hizi inaonyesha kuwa Tanzania ndio nchi ya mwisho katika matumizi ya maziwa japokuwa ni nchi inayoongoza kwa kuwa na mifugo mingi kulinganisha na nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 inaonyesha kuwa Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 13.839 tu; kati ya fedha hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni nne (4) na fedha za kutarajia toka kwa wahisani ni shilingi bilioni 9.839.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo huu kwa Wizara hii unaonesha kuwa Serikali bado haijakuwa na nia ya dhati kuwekeza katika sekta hii na pia ni kwenda kinyume kabisa na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kama ulivyopitishwa na Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kigezo gani zaidi ya Mpango wa Miaka Mitano kinafuatwa katika kupanga miradi ya maendeleo kwa Wizara hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumesema hapo juu, sekta hii kama uwekezaji katika sekta hii utafanywa kwa kadri ya mpango ulivyo ni dhahiri mchango wake kwenye pato la taifa utakuwa ni mkubwa kwa kulinganisha na sekta zingine za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maoni hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kumbukumbu zote ziandikwe kama zilivyo kwenye kitabu, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kasulumbayi kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi kwa kweli ameisoma hotuba yake kwa kukandamiza kabisa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa tuingie kwenye hatua inayofuata ya kikanuni na hatua inayofuata ya kikanuni sasa ni kuruhusu Waheshimiwa Wabunge waweze kuchangia hoja hii. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Saleh Pamba atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Chatanda.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali yayote, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru

kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru Waziri, Mwenyekiti wa Kamati kwa hotuba zao nzuri ambazo zimejaa maelekezo mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijachangia katika hotuba hii, kwa vile ni mara yangu ya kwanza, napenda nichukue nafasi hii nizungumzie kidogo masuala ambayo yanahusu maendeleo ya Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala makubwa matatu katika Jimbo langu ambayo Serikali ya Chama changu cha Mapinduzi, inayatekeleza. Suala la kwanza ni kuhusu barabara ya Tanga - Pangani hadi Bagamoyo. Barabara hii usanifu wa kina umekamilika na sasa hivi Serikali ipo katika hatua ya kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Sisi Wanapangani tunaliona suala hilo ni kubwa sana kwa sababu litatusaidia sana katika kufungua Wilaya yetu hasa kwa maeneo ya kiuchumi. Kwa hili, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Pangani tunayo maeneo mazuri sana ya vivutio vya utalii. Tumekubaliana na Serikali kwamba maeneo yote haya ya Ushongo, Mkwaja, Kipungwi, yataunganishwa kwa barabara za lami ili kuhakikisha kwamba zinapitika kwa urahisi zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, naomba uingie kwenye hoja, hoja hizo zote tulishazimaliza.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka tu.

**MWENYEKITI:** Hapana! Tunaomba ujikite kwenye hoja iliyoko mbele yetu.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hoja iliyopo, nataka nizungumze yafuatayo. Sekta ya uvuvi ni sekta muhimu sana hapa nchini. Jana nilikuwa naangalia takwimu mbalimbali zinazohusu sekta hii kwa nchi mbalimbali duniani. Nikajaribu kuangalia umuhimu wa sekta hii kwa nchi kwa mfano Vietnam ambayo kwa mwaka 2009 peke yake waliuza samaki nje ya nchi wenye thamani ya dola bilioni 4.3. Mauritius ambayo ni nchi ndogo inafanana sana na Kisiwa cha Zanzibar waliuza samaki wa dola bilioni 1.5. Mozambique ambayo ni nchi jirani waliuza samaki wenye thamani wa dola milioni 574. Tanzania tumeuza samaki dola milioni 145 na Kenya dola milioni 57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande ufugaji wa samaki, wenzetu wa Vietnam mwaka 2009 walizalisha samaki jumla ya tani 2.8 milioni. Uganda ambayo ni jirani zetu wamezalisha samaki kutoka kwa wafugaji tani 80,000. Kenya jirani zetu wamefuga au wamezalisha samaki wa tani 12,000 na sisi Tanzania tani 7,000 na nchi ndogo ya Myanmar Mashariki ya Mbali wamevuna samaki au ufugaji wa samaki wa tani 800,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii inaonyesha nini? Inaonyesha kwamba bado Serikali yetu haijatilia mkazo sana katika sekta hii. Kwa hiyo kuna haja kwa Serikali yetu kuweka mkazo sana katika sekta hii. Tunayo mito, bahari kubwa, maziwa makubwa, kwa hiyo kuna haja ya kutilia mkazo katika sekta hii. Tunalo eneo la bahari la ukanda wa *EEZ* wa maili 300 na sasa hivi Serikali yetu

imeshaomba kwenye Umoja wa Mataifa kupata zaidi ya *square kilometer* 60,000. Kwa hiyo, hii yote inatuonyesha kwamba ni lazima tujipange vizuri katika kuhakikisha kwamba tunatumia rasilimali hizi ili kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika mipango mizuri ya Wizara hii, napenda nichukue nafasi kuwapongeza sana, kwamba wameanzisha *Fisheries Development Plan* ya mwaka 2012 hadi mwaka 2016. Mpango huu wa *Fisheries Development Plan* unahitaji jumla ya shilingi bilioni 320 kwa miaka mitano ili uweze kutekelezwa lakini kwa bahati mbaya kwa mwaka huu na mwaka jana ambapo mpango huu ungeanza, hakuna fedha ambazo zimetengwa hata senti moja. Mwaka huu peke yake katika *Fisheries Development Plan* tulihitaji shilingi bilioni 44 ili tuweze kutekeleza masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona mpango huu ni muhimu sana, kwa sababu katika mpango huu iwapo Serikali itatoa fedha za kutosha matatizo mbalimbali ambayo yamezungumziwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo na Kilimo ni matatizo ambayo yanaweza kupatiwa ufumbuzi wa haraka. Ni matumaini yangu kwamba tunao mpango wa kupitia bajeti *(budget review)* inapofika Desemba kila baada ya miezi sita, napenda kuchukua nafasi hii kuiomba Serikali kwa dhati kabisa wakati tunapofanya *budget review* angalau nusu ya fedha ambazo tumezitenga katika *Fisheries Development Plan* basi fedha hizo zipatikane ili wenzetu waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi katika Bahari kuu, tunazo meli nyingi zinazovua katika bahari kuu, lakini sasa hivi tunaendelea kukatisha leseni tu hatupati faida za uvuvi wa bahari kuu kwa sababu meli nyingi zinavua bahari kuu na samaki wote wanaondoka bahari kuu hukohuko. Kwa misingi hiyo, ili tufaidike na uvuvi huu wa bahari kuu, naiomba Serikali kwa dhati kabisa sasa ianzishe bandari ya uvuvi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mpango wa Serikali wa kuimarisha Bandari ya Dar es Salaam, nafikiri wakati umefika wa kuongeza ki-*component* cha bandari ya uvuvi. Faida zake ni nyingi, kwanza ni kwamba tutahudumia meli zote kwa kuzipatia mafuta, chakula maji na kadhalika. Pili, tunapata *royalties* ambazo sasa hivi hatuzipati kwa sababu samaki wote huwa wanasafirishwa katika bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni suala ambalo linahusu wavuvi wadogo wadogo. Wavuvi wadogo kwa bahati mbaya wamekuwa kama watoto yatima. Kwa sababu ya unyonge wao hawapati nafasi ya kuweza kupata mikopo. Hawawezi kupata mikopo kwa sababu ya *vulnerability* yao. Kwa hiyo, ni vizuri tukawa na utaratibu ambao tutawasaidia wavuvi wadogo wadogo waweze kupata zana, waweze kupata nyavu, waweze kupata boti za kisasa. *SACCOS* zao hizi bado ni dhaifu sana, wavuvi wadogowadogo wana vyombo ambavyo si imara sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili tuwasaidie wavuvi wadogo wadogo, nina mapendekezo yafuatayo.

Katika Wizara ya Kilimo, wenzetu wana *Agricultural Inputs Revolving Fund*. Naamini kwamba sasa wakati umefika kwa Wizara hii ya Mifugo kuanzisha *Fisheries Input Development Fund.* Zipo nchi ambazo zitakuwa tayari kuisaidia Serikali na kuisaidia Wizara hii. Hapo zamani walikuwa wakiisaidia Serikali na Wizara hii, nchi ambazo zinahusika sana na masuala ya uvuvi. Nchi kama Japan, Korea, Norway wako tayari kama wataona Serikali tayari imeanzisha mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ni kengele ya pili.

**MHE. SALEHE A. PAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi name niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nawapongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri na Watendaji ikiwemo Kamati ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa namna walivyoandaa bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nisije nikasahau, naomba niunge mkono hoja ya bajeti hii asilimia mia moja ingawaje bajeti hii haikidhi kabisa mahitaji yaliyopo. Bajeti hii ni ndogo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utekelezaji wake wa ahadi ya kuwapatia mifugo wafugaji ambao walikuwa wamepoteza mifugo yao. Wafugaji wa Wilaya ya Longido, Monduli, Ngorongoro wanakiri wazi kwamba haijapata kutokea wafugaji kufidiwa mifugo pale inapokufa. Hivyo jambo hili limetokea na kuijengea heshima Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo baadhi ya watu ambao walikuwa wakichochea kwamba kauli ya Rais ilikuwa ni ya kisiasa, lakini naomba niwaeleze tu kwamba wananchi wa Wilaya ya Londido, Monduli na Ngorongoro kwamba ahadi ya Rais haikuwa ni ya kisiasa na imeweza kutekelezwa hivyo waendelee kuamini kwamba Serikali yao inawajali na wataendelea kupata ile mifugo ambayo Rais

amewaambia kwamba Serikali itakuwa ikiwapa kila mwezi mifugo ile 500 kwa kila Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala zima la wale watendaji wa ugani. Wapo watendaji wa ugani ambao wanashughulikia pamoja na masuala ya kilimo, lakini ukiangalia watendaji wengine wanaegemea zaidi kwa upande wa kilimo lakini kwa upande wa mifugo hawategemei zaidi huko. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali izalishe zaidi watendaji wa mifugo ili kusudi waweze kuwasaidia wafugaji katika kuhakikisha kwamba wanaboresha mifugo yao ili waweze kujiinua kiuchumi na hatimaye kuiletea Serikali yetu mapato ambayo yanaweza yakasaidia katika kuendesha shughuli zetu za maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la migogoro ya ardhi. Suala la migogoro ya ardhi limekuwa likiletwa katika Bunge hili, kila siku tunazungumza suala la migogoro ya ardhi lakini ufumbuzi wake haupatikani. Naiomba Serikali kwa sababu jambo hili limekuwa likizungumzwa sana hapa Bungeni na migogoro imekuwa ikiendelea kuwepo kila kukicha, ikiwezekana Bunge lijalo tupatiwe Mikoa ile ambayo inahusika na suala la wafugaji na wakulima kwenye migogoro hiyo. Watuletee taarifa ambayo inaonesha kwamba wameshapima maeneo mangapi ambayo ni ya wafugaji pamoja na wakulima. Kuliko kuendelea kusikiliza kila siku taarifa zinaeleza tu kwamba tunao mpango, tunaendelea kupima. Ni vizuri sasa wakatuletea taarifa ambayo inaonesha kabisa kwamba tumeshapima kwa kiasi Fulani, Mikoa fulani

kwa ajili ya wafugaji na kiasi hiki tumetenga kwa ajili ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii sasa nizungumzie suala la soko la wafugaji. Ni kweli kabisa kwamba wafugaji wamekuwa wakifuga mifugo yao lakini masoko yamekuwa ni tatizo. Hata hivyo, kama watapata masoko kutokana na tatizo la kutokuwa na watalaam ambao wanawasaidia kuhakikisha kwamba wanaboresha mifugo yao basi imekuwa ni vigumu sana wafugaji hawa wakipeleka mifugo yao wanapata bei ambazo hazikidhi kabisa kulingana na mifugo ambayo wanaiuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kuchangia hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mary Chatanda kwa mchango wako. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Rashid Ali Omar, naona hayumo ndani ya ukumbi wa Bunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Asaa Othman Hamad atafuatiwa na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana.

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nakushuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kusema machache kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii ya kumpongeza sana Waziri pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara hii. Nachukua fursa hii ya kuwapongeza kwa dhati kwanza kutokana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imezaliwa kutoka Wizara ya Kilimo na Mifugo iliyopita. Kama tulivyoshuhudia mwaka jana, fungu walilopewa kutoka Serikalini na wenyewe wakitegemea kwamba ndiyo hapo wasimame kwa miguu yao watembee, tulilalamika ni dogo mno. Ni bahati mbaya mwaka huu limeshuka zaidi. Matarajio ya Wizara hii kufanya vizuri kwenye mchango wa Taifa itabaki ni ndoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi ni Mjumbe wa Kamati inayoshughulikia Wizara hii, kwa hiyo nazungumzia uhalisia kwa kadri nilivyoshuhudia. Ripoti ya Kamati yetu imejikita zaidi kuyaeleza yale ambayo tumeyakuta na maboresho gani tumeshauri yafanyike ili dhana nzima iliyotarajiwa ya Wizara hii ya kuwapatia tija Watanzania na mchango kwa Taifa la Tanzania itekelezeke. Hali kadhalika, tunatarajia ajira ipo tena kubwa endapo tutajipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo; waliotangulia kuchangia wameeleza umuhimu wake, lakini bado inakwazwa na changamoto ambazo nadhani Serikali ingechukulia kama ni suala la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi ni changamoto ambayo kila anayesimama nadhani anataja ardhi ni tatizo. Lakini si tatizo kwamba Tanzania hatuna ardhi, tuna tatizo hatujajipanga kusema eneo hili ni la wafugaji na eneo hili ni la wakulima, eneo hili ni

makazi ya watu na kadhalika. Namna tunavyokwenda tunasababisha mizozo ambayo haileti faida kwao wafugaji wala wakulima, lakini pia ni sifa mbaya kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyopo, leo tunazungumzia hamsini na nne bilioni lakini deni la Wizara hii kwa wafugaji kupata malambo, visima, upimaji sijui kama na wao fedha ni hii lakini fedha ya maendeleo tunategemea zaidi wahisani. Hapa ndipo kwenye tatizo. Wahisani hawatatujengea viwanda, wahisani hawatajenga miundombinu. Ni juu ya Serikali kujenga mazingira mazuri kuwavutia wawekezaji. Hapa tunazungumzia wawekezaji wazalendo, umuhimu namba moja, wawekezaji wa nje umuhimu namba mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyang'anyiro cha malisho ya mifugo na na maji binadamu na mifugo si jambo la kupendeza hata kidogo. Unapopita huko vijijini ukawakuta Watanzania wanafukuzia maji na punda wanafukuzia maji kwenye bwawa moja si jambo jema. Hii inatokana na fedha ndogo Wizara hii inayoipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwa haraka sekta ya uvuvi. Kila Taifa Mwenyezi Mungu amelijalia rasilimali yake, Tanzania imebahatika, tunazungukwa na bahari, tuna maziwa, likiwemo Ziwa Nyasa, tutabanana hapohapo na wenzetu, lakini hatujafanya vizuri kwenye maeneo haya kwa tija kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali sasa tuipatie Tanzania mafanikio kupitia rasilimali hizi.

Wenzetu Wachina rasilimali watu wameitumia ipasavyo na leo China tunaisifia hapa. Sisi tuna bahati mbili, tuna rasilimali watu, tuna rasilimali *natural*, ni suala la kujipanga tu. lnawezekana, tutimize huo wajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la uvuvi haramu. Mbunge wa Pangani amesema, nadhani hatutawafanyia vema wavuvi wadogowadogo, sheria hizi tunazozitunga hapa, lakini hebu tujiulize tumewawezesha vipi wavuvi wadogo halafu tukawatungia sheria? Maana yake tusitunge sheria kama tunawakomoa, tutazame mazingira halisi ya maisha. Maisha yao yanategemea maziwa yale wanamoishi au kandokando ya bahari inayowazunguka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hiyo ni kengele ya pili. Naomba nimwite msemaji anayefuata Mheshimiwa Pindi Hazara Chana atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa hii. Kwanza nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Mathayo David Mathayo na Mheshimiwa Ole-Nangoro, mfugaji maarufu kabisa na wote wanatoka maeneo ya ufugaji, nawapongeza sana kwa kazi zao nzuri. Nina imani kubwa sana kwao, lakini safari hii nimekuja na *style* tofauti na-*criticize* mfumo, ndiyo *style* yangu ya kuchangia kwa Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama nilivyoanza kwa Wizara zingine, watalaamu mjiandae, chukua *pen,* karatasi, andaa majibu, muwape Mawaziri wetu wanapo-*wind* waje na majibu muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inaitwa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara zingine zinaitwa jina tu, Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Katiba na Sheria, hapa kwa nini mnatuitia maendeleo, mna maana gani? *Concept* ya maendeleo, tunataka maelezo. Maendeleo maana yake ni *development* lakini hayo maendeleo sisi Watanzania lazima tuwe mashahidi, uvuvi unaendelea, mifugo inaendelea, ardhi ya kutosha ipo? Kwa hiyo, mimi naanza na jina la Wizara, wanishawishi kwamba maendeleo yapo na yanatosha*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna nchi nyingine ni *desert,* hawana maji, sisi Tanzania tuna Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, *Indian Ocean,* Ruaha, Mtera, Mindu – Morogoro, unaambiwa kuna mito 30 ya maji, lakini kuna nchi haina, inaitwa *desert,* huko ni jangwa kwenda mbele. Kutokana na hii mito ambayo Mungu ametuletea maana yake ni utajiri tayari. Watu wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa mito na maeneo haya na bahari na kadhalika, hawapaswi kuwa maskini. Sasa hayo maendeleo, ndiyo hoja iko hapo, nataka wanishawishi kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti imeombwa hapa shilingi bilioni 54 *current*, mishahara shilingi bilioni 40, miradi shilingi bilioni 13. Hizi shilingi bilioni 13 majibu ya Waziri yakinishawishi, nakupeni pesa lakini hizi shilingi

bilioni 40 hazina mjadala zinaitwa ni *compulsory expenses,* lazima watu wapate mishahara, hii nakupa sasa hivi, hamna shida. Hapa kwenye maendeleo, shilingi bilioni 13, naomba uniambie Wizara hii inaingiza kiasi gani? Leo nitajikita kwenye uvuvi, kabla sijakupa shilingi bilioni 13 tukubaliane kule *TRA*, Bwana Kitilya anakusanya kiasi gani cha uvuvi mpaka leo unatuomba shilingi bilioni 13. Wizara hii inabidi ichangie sana katika nchi yetu siyo tukamate meli, wageni wanakuja wanachukua samaki zetu halafu tukiwaweka magereza, mimi Katiba na Sheria natoa hela za kwenda kuwalisha wale wageni wanaokamatwa wakati samaki ni zetu, wanatuingilia, tunakuja tunaruhusu kienyeji, hapo kwa kweli inabidi tuongee Daktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu wengi wamezungumzia kuhusu wavuvi wadogowadogo na nitazungumzia kule Njombe, Makete, Ludewa kuna eneo linaitwa Manda, mto Ruhuhu, kweli kabisa maeneo yale ukienda ni changamoto, inabidi wawe matajiri sana. Lakini kuna changamoto kwanza utalaam, Bwana Samaki Halmashauri ya Ludewa mimi sijamuona. Halmashauri ya Njombe na Makete si kwamba hakuna mito, ipo Delto Ruaha inapita, maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kuna Mtera, Afisa Samaki wa kuelekeza utalaam kwenye Halmashauri zetu, hawa watu wanapungua sana kila iitwapo leo. Kwa hiyo, nataka *statistics,* Halmashauri ngapi zina Afisa Samaki, wanaotoa elimu ili tuone namna gani maendeleo yapo, maendeleo ndio hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa elimu imekuwa ni changamoto, wengine wengi wamezungumzia vitendea kazi, wengine watumia neti, tunaambiwa wanatumia neti zinanyang'anywa, zinachomwa suala siyo kuwanyang'anya, *you give them the alternative*, chukue ile mpeni ile muafaka. Kwani neti ni shilingi ngapi hizo ambazo ni muafaka, nyavu za kuvulia, mbona kilimo tunatoa ruzuku, mbolea, *voucher*, hawa wavuvi wanapewa nini? Lakini pia vitendea kazi hivi havipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napita sana, kila nikienda Iringa napita pale Mtera watu wanavua samaki, tume-*legitimatize* wanalipa na kodi maskini ya Mungu. Naongelea katika eneo ambalo nimepita achana na maeneo makubwa ya *Indian Ocean* na wapi huko, wenzetu wa Zanzibar wanajua zaidi. Lakini vitendea kazi, wanasema Mheshimiwa tulitee nyavu muafaka, nauliza duka gani, *TFA* sizioni, yaani vitendea kazi tu vyenyewe vinavyotakiwa vile muafaka vya kitalaam ni changamoto. Vinapokuwa vinaingizwa nchini hata hiyo kodi tupunguze kama tunavyofanya upande wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu maeneo mengi sana ya pembezoni wanaishi akina mama ambao ndio wameniingiza humu Bungeni, wale akina mama wa pembezoni ndio wamesema niwe Mbunge wao wa Viti Maalum na Mjumbe wa *NEC* kupitia UWT. Sasa wakasema sisi akina mama wakati mwingine hata kile wanachovua ni gharama kubwa, *cost overhead* ya kuvua samaki, gharama inakuwa kubwa kiasi kwamba hata wakati mwingine kula zile

samaki anakuwa anakula mtaji. Anavua maskini samaki inabidi ajikamue kwenye matenga, auze pale kwake, kula inakuwa ni kazi, kwa sababu gharama ni kubwa. Kwa hiyo, wakati mwingine wanawatuma vijana, wale vijana wanawalipisha wale akinamama hela nyingi. Lakini pia vikundi hivi vya akina mama maeneo ya pembezoni havijawa-*recognize,* wakienda benki hawakopesheki, wengine hapa wameshazungumza ni benki zipi zinawakopesha wavuvi hawa maeneo ya Mtera, Manda, kule wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu, utalaam wakienda Halmashauri wanaomba utalaam, tunaomba masoko, Bwana Samaki kwanza hayupo. Maafisa wakifuatwa, wanasema mimi ni mtaalam wa Injinia. Sasa huyu jamani mwananchi, jamani wavuvi hawa kweli kabisa haya maendeleo ya mifugo na uvuvi, tunataka maelezo hayo maendeleo yako namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hawa samaki kwa kweli ambao tumekuwa tukiwavua na na kadhalika ipo haja ya kufikiria namna ya kuwafuga. Wanajua mimi siyo mtalaam, mimi ni Mwanasheria kwa taaluma, *nutrients* yaani usisubiri samaki mkubwa amtafune mdogo halafu waendelee kuzaliana, tunaweka *nutrients* za aina gani ku-*make sure* kwamba hawa samaki wanazaliana kwa kasi tunayoitaka? Huwezi ukaacha tu *nature* i-*take its cause,* lazima uweke utaratibu, eneo hili mkiweka majani haya, mkalima mle ndani, samaki wengi wanasogea, wanazaliana, wanakuwa na afya na kadhalika. Watalaam wanajua, kuna lile Shirika la Utafiti, TAFIRI,

TAFIRI bwana mko wapi? Tunataka tuone maendeleo ya mifugo na uvuvi, tukija hapa tunapiga makofi, mapato ya Wizara hii ni makubwa sana, hata kiwango wanachokiomba kwa kweli ni kidogo ikilinganishwa na hela mnayotuingizia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, naomba sana maeneo hayo niliyosema muyazingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija upande wa mifugo, kuna mashirika kama *NARCO* lazima lipewe uwezo. Kuna maeneo kama *ranch* za taifa, kule Makete kuna Kitulo na maeneo mengine kwa majina yao. Haya maeneo yanatakiwa yatunzwe, tulisema tusibinafsishe yabaki kwa Serikali kwingine tulibinafsishwa imekula kwetu. Haya ambayo hatujabinafsifisha, tunayatunza namna gani yaendelee kuwa ni shamba darasa? Watu wakajifunze ufugaji, watu wakajifunze mambo mbalimbali, lazima pia yawe yanaingiza wafugaji wanakwenda pale, wanalipia kutoka eneo moja, Halmashauri zinawapeleka wakajifunze. Mimi nimeona juzi Nanenane pale Morogoro wamefanya vizuri sana alikuwepo Waziri Mkuu lakini maeneo kama haya yawe ya kudumu, siyo tu Nanenane unasubiri tena Nanenane tunapeleka hela nyingi kwa siku nane, sijui wiki moja, tunaweka mabanda, hapana siku nane tu mnaweka hela nyingi, tunasafiri tunakwenda pale *perdiem*, wekeni shamba darasa la mifugo na uvuvi vya kudumu, endelevu hata *cost* zinakuwa za chini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba ufafanuzi wa maeneo hayo niliyozungumzia. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nikushukuru sana pamoja na Wabunge wenzako walioshiriki katika mazishi ya marehemu mama yangu. Mmekuja kunifaraji wengi, pamoja na Wabunge wote mlionipa pole. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme kama alivyosema Mbunge aliyetangulia kwamba nataka kufahamu mfumo wa Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kwa sababu ni jina tu kwamba maendeleo ya mifugo, lakini kinachofanyika sikioni kwa sababu Wizara yenyewe haina fedha za maendeleo. Fedha mnaziona shilingi bilioni 13, nadhani ni za utafiti, siyo fedha za maendeleo. Kama hawana fedha za mabwawa, hawana fedha za majosho, hata *crush* hawana fedha, ukiwaambia Wizara hii wachimbe kisima kimoja cha shilingi milioni 20 watasema hatuna fedha. Sasa maendeleo haya ya mifugo itawezekanaje kwa Wizara ambayo haina fedha za maendeleo ya mifugo, fedha za maendeleo ukisema mabwawa unaambiwa kwamba nenda TAMISEMI, majosho nenda TAMISEMI, kwa nini basi hii Wizara ipo? langaliwe tena upya kwa sababu siyo kwamba tunataka tu Wizara inayoitwa Wizara ya Mifugo ambayo haina msaada wowote kwa mifugo. Nataka jibu leo kwa sababu niliuliza katika Bajeti uliyopita Waziri hakunijibu, kuna maana gani kuwa kwenye Wizara ambayo haisaidii mifugo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kwanza kuishukuru Serikali kwa kutupa madawa ya ruzuku lakini kuna madawa ambayo hayapo kwenye ruzuku. Madawa ya *IVF* na magonjwa ya miguu na midomo, hayana ruzuku, naomba madawa ya magonjwa yawekwe kwenye ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kulizungumzia ni mgogoro kati ya wakulima na wafugaji. Wafugaji wa Kilosa, Mbeya, Mpanda wamenyanyasika sana katika nchi yao, wamenyang'anywa mifugo lakini mpaka leo Serikali inatuma Tume tu, Tume ambayo haileti taarifa. Tunaomba Serikali ifanye utafiti wa kutosha wa namna ya kuwasaidia wafugaji hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni *ranch*, nashukuru Serikali kutugawia maeneo katika *ranch* ya *West Kilimanjaro* lakini katika *Ranch* hiyo, maeneo mliyogawia Wilaya ya Longido hayapo katika Wilaya ya Longido, yako katika Wilaya ya Arumeru. Naomba tupewe maeneo katika maeneo tunayopakana nayo. Msituletee mgogoro kati ya Arumeru na sisi hata Ngaboboko wamepewa eneo ambalo haliko katika kijiji chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala *Ranch* ya Kongwa. Kwa masikitiko makubwa, hiyo ranchi, siyo ranchi ya mifugo tena ni *ranch* ya kilimo, nashangaa kabisa *ranch* ya mifugo kuwekwa kilimo ndani. Ukiuliza wanasema eti wamevamia, wananchi wanavamiaji na kukata maeneo na kwenda kuanza

kulima katika *ranch* ya taifa? Ukipita barabarani huoni lakini ingia ndani. Mheshimiwa Waziri kama ukitaka kuthibitisha nenda siyo nyaraka ambayo utaambiwa kwamba leta ushahidi, ukitaka nenda leo katika *ranch* hiyo. Ranch hiyo ni kilimo tupu. Kama ni hivyo basi hiyo *ranch* igawanywa kwa wananchi, wananchi wafuge mifugo yao. Hiyo *ranch* akipita kesho wewe huna kazi kwa sababu ni mashamba tu, tena mashamba ya kulimwa na trekta, mashamba makubwa. Kwa hiyo, naomba hiyo *ranch* kwanza madume yaliyoko pale yasambazwe kwa wananchi wapate mbegu bora na igawanywe kwa wananchi wafugie siyo walimie, wafugie na waweze kufaidika katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la fedha za *PEDAP.* Hizi fedha nazungumzia kila wakati kwa sababu ukiangalia huko ndiko kuna miradi inayoitwa ya mifugo. Lakini ukikuta mradi fedha za ununuzi na gharama ndio matumizi makubwa kuliko fedha za mradi wenyewe. Serikali sijui kwa nini isifuatilie hizi fedha za *PEDAP,* ni fedha zinazoingia kwenye matumizi mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia na mimi nirudie kushukuru sana Serikali kwa kutupa mifugo na nina hakika kwamba watazidi kutupa mifugo ambayo bado inahitajika kugawanywa kwani bado mifugo mingi na wananchi kwa kweli wameathirika mpaka sasa kuna wengine ambao hawawezi kununua chakula wala kuwasomesha watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kulizungumzia suala la Ngorongoro. Serikali iangalie Ngorongoro kwa sababu Ngorongoro siyo ya wakulima, lakini ni wananchi wanaohitaji nao wawe na makazi bora. Mpaka leo Ngorongoro wanaambiwa kwamba wasijenge, kama wananyimwa kulima waruhusiwe basi wajenge nyumba nzuri za kuishi, wasikae kwenye karne ya 18, wengine wameendelea mbele, wana makazi mazuri. Ukimnyima kilimo, umnyime na kujenga nyumba bora ambayo itakuwa kwa kweli hata hii Katiba sasa haiwatendei haki. Naomba sana Serikali iliangalie suala hilo la Ngorongoro, waruhusiwe nao wajenge makazi, siwatetei kwenye kilimo sana, lakini kwa makazi, sidhani kama makazi yataharibu hifadhi. Kama yataharibu hata hoteli kubwa zilizoko pale ni makazi. Hata ofisi yenyewe ya Ngorongoro imejengwa *block* nzuri sana, inafanana tu na Bunge hili lakini ikisemekana makazi ya wananchi yanapigiwa kelele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia suala la mgogoro wa wafugaji na wakulima inawezekana kabisa likatafutiwa ufumbuzi. Mbona kule Kaskazini kwangu hakuna mgogoro na tuna wakulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa kweli tunakupa pole kwa msiba mkubwa uliokupata wa mama mzazi.

**MHE. NAMELOK E.M. SOKOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuamua kwa makusudi kabisa kuwafidia wafugaji wa Wilaya ya Longido, Monduli na Ngorongoro mifugo yao. Hili ni kutokana na ukame mkali uliotokea mwaka 2008/2009 na kusababisha kaya 6172 kupoteza mifugo yao yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzinduzi huo umeshafanyika katika Wilaya ya Longido tarehe 19 mwezi wa pili kwa kuwapatia ng'ombe 500 na kubakia na ng'ombe 11,408, Wilaya ya Monduli tarehe 2 mwezi wa 8 kwa kuwapa ng'ombe 500 na kubakiwa na ng'ombe 6,127 na Wilaya ya Ngorongoro kwa kuwapa ng'ombe 500 na kubaki na mifugo 7,463. Kwa namna ya pekee na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Arusha, tunashukuru, hili halijawahi kutokea. Hiki ni kielelezo kwamba Rais wetu na Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi anawajali wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ajuaye yanayoweza kutokea kesho. Hatuombi majanga kama haya yaendelee kutokea lakini nilikuwa naishauri Serikali iangalie namna ya kuanzisha Bima ya Mifugo na Mazao ili yanapotokea majanga kama haya wafugaji, wakulima waweze kufidiwa badala ya kuendelea kusubiri huruma*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni ya tatu Barani Afrika kwa kuwa na mifugo mingi lakini pato linalochangiwa na sekta hii halifiki hata asilimia nne (4%). Hii ni kutokana na changamoto nyingi zinazoikabili sekta hii. Kwanza kabisa, upungufu mkubwa wa bajeti. Mwaka 2010 bajeti katika Wizara hii ilikuwa shilingi bilioni 57, mwaka 2011 shilingi bilioni 54, fedha hizi hazitolewi kwa wakati. Tulikuwa tunaomba Serikali ni namna gani sekta hii inaweza kuongezewa bajeti yake. Pili ni migogoro mikubwa kati ya wakulima na wafugaji na chanzo chake ni kwa kushindwa kusimamia na kupanga matumizi bora ya ardhi. Tatu, ni ukosefu mkubwa wa masoko ya nyama na maziwa kwa bei nzuri itakayomsaidia mfugaji. Nne, ni bei kubwa ya chanjo za mifugo ambazo wanakumbukana nazo wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo chanjo ya mifugo ya Ndiganakali. Chanjo hii inapatikana, chanjo hii inatibu mifugo kwa asilimia 90 lakini bei yake ni ghali mno. Dozi moja inauzwa kati ya shilingi 8,000 mpaka 13,000. Tunaomba Serikali iangalie ni kwa namna gani dozi hii inaweza ikaanza kutolewa kwa ruzuku ili nao wafugaji

waweze kufaidika kama inavyofanyika katika Kilimo Kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la tano ni ukosefu wa wagani katika Wilaya. Tunaomba Serikali iangalie ni namna gani sasa wagani wanaweza kufikishwa hadi Wilayani na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko changamoto nyingine lakini hapa natoa ushauri tu wa Serikali kufanya mambo mawili, kwanza kuwezesha shirika la *NARCO* kwa kuwapatia fedha ili waweze kuwasaidia wafugaji kwa kutoa mbegu bora za mifugo. Lakini pia nashauri Serikali iwekeze katika sekta hii, iwekeze katika malambo, iwekeze katika majosho, iwekeze katika machinjio ya kisasa, pia iwezeke katika viwanda vya maziwa. Lakini mwisho kabisa iwekeze katika vituo vya afya vya mifugo ili wafugaji waweze kufuga mifugo bora yenye afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kufanya hivyo pia Serikali iwahamasishe wananchi ili waweze kula mazao yatokanayo na mifugo kwani takwimu za *WHO* zinaonyesha Tanzania tuko chini ya viwango. Kwa mwaka mzima mtu anatakiwa kunywa lita 200 za maziwa na hapa kwetu inaonyesha mtu mzima anakunywa lita 45 za maziwa na nyama inaonyesha kilo 50 na hapa kwetu inaonyesha mtu mzima anakula kilo 12 za nyama hali kadhalika mayai na maziwa. Nashauri Serikali iweze kuwahamasisha wananchi ili

wao wenyewe waweze kuchangia katika sekta hii hata kwa kuvaa viatu, *handbags* na kadhalika ambavyo vinatokana na mazao ya mifugo. Sisi wenyewe tunaweza kukuza pato la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuchangia bajeti hii ya mifugo na uvuvi, lakini kabla sijaanza, nichukue fursa hii kuwatia imani watu wenye mapenzi mema walioingiwa na wasiwasi baada ya mtu mmoja kumsingizia Mheshimiwa Spika, kwamba amenifukuza Bungeni kwa sababu nimekula rushwa, waamini kwamba niko Bungeni na sauti ni ile ile *Panasonic*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu wa pili nimpongeze Mheshimiwa Mwendapole kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM wa Kata ya Rutoro kwa sababu kwa kuchaguliwa Mwendapole, Serikali imetoa tamko zuri sana kuhusu migogoro ya Rutoro iliyodumu takribani miaka saba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naupongeza msimamo wa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi na nawaambia wananchi wasihangaike, rangi ya kijani ni matumaini, migogoro yote tutaisuluhisha. Migogoro ya Rutoro imekaa miaka saba, baada ya watu wa Rutoro kufanya maamuzi, wakanituma mimi *entumwa erahuka*, nimefanya kazi ya Rutoro. Nawashukuru sana

Mheshimiwa Mathayo, Mheshimiwa Ole-Nangoro, Dokta Mwakyusa, Dokta Kamani na Mama Waride wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Rutoro limeacha makovu, naiomba Wizara ya Mifugo, waharakishe wao na Wizara ya Ardhi, watafute maridhiano na watakapokuwa wamemaliza, sasa wale watu waliobaki, wasiwaache na wao wawe wachungaji, wawafundishe wawe wafugaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba tunawaacha watu wanakuwa wachungaji, wawe wafugaji muwafundishe hizi mbinu za kisasa zinazozungumzwa. Lakini niiombe Serikali yangu kwa sababu kwa miaka saba Kata yangu ya Rutoro iliachwa bila msaada tukiwa katika kupigana na kukimbia, basi Serikali yangu kupitia Waziri Mkuu, mnisaidie katika miundombinu ya barabara, elimu, lakini kama nilivyowaahidi wananchi wangu, nakwenda na *environment,* siwezi kwenda na jembe la mkono. Nashukuru tena Wizara, lakini walichokiahidi katika makaratasi yao, wakitekeleze kabla ya mwezi wa kumi.

Mheshimiwa Waziri wa Ardhi amesema kwamba Bwana Mayunga, Mkurugenzi wa Upimaji atashirikiana na Wizara ya Mifugo kwenda kupima, ningependa hayo yatimizwe kusudi bendera ya Chama cha Mapinduzi iendelee kupepea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ufugaji Kagera si la kuzungumza. Unahitaji moyo wa jiwe kuuzungumza, sasa dawa ni moja, Mheshimiwa Mathayo nina imani

na wewe, Mtumishi wa Mungu Mzee Ole-Nangoro nina imani na wewe, msimame kidedea. Mkikutana na Malaika wa Mungu akawauliza kazi gani mlifanya katika Wizara yenu? Semeni kumaliza matatizo ya mifugo Misenye, mtaingia peponi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la uvuvi. Suala la uvuvi lina kitendawili, ninao uhakika kwamba watu kutoka nchi za nje Uganda, wananunua katika Visiwa vyangu kilo moja ya samaki kwa shilingi elfu nne, wakiwa Mazinga, wakiwa Bumbire. Kwa nini watu wa Mwanza wanunue bei ndogo? Kuna kitu pale, nendeni mkaangalie, msisubiri kuambiwa, huenda kuna njama za kuua viwanda vyetu na viwanda vikifa hatuwezi kupata ajira, vijana watakosa ajira, lakini viwanda vikifa tutakosa ushuru, naogopa, lichunguzwe hilo jambo, lichunguzwe kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini uvuvi katika Ziwa Victoria limewaacha ndugu zangu wa Bumbire Abaganga, limewaacha watu wa Kerebe, Goziba bila kipato chao walichokizoea. Ile sehemu ilikuwa na Vijiji, ninachoiomba Serikali yangu mnisaidie kusudi wale wananchi waliokuwa wazawa wa sehemu ile, wawe na zana za kisasa, waweze kushindana na watu wapya wanaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawawezi kuwa watazamaji katika ardhi ambayo waliachiwa na wazazi wao. Kama hawawezi kuvua kwa zana za kisasa, ndiyo maana wanakwenda kwenye uvuvi haramu. Mheshimiwa Waziri alipokuja Bukoba, aliambiwa juu ya utendaji wa watendaji wake. Kuna

mtu mmoja sitaki kumpandisha chati alisemwa sana. Huyu mtu amwondoe, kama mtu analalamikiwa aondolewe. Nazungumzia, wafugaji hasa wa asili na wavuvi wale wa asili, wananyanyaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitendo vya rushwa, lakini ni kutokana na wale watu kwamba wanalazimika kwenda kwenye uvuvi haramu ambao mimi naupinga kwa sababu wana nyenzo duni. Wapeni nyenzo zinazofaa kusudi muwanyang'anye zile nyenzo ambazo hazifai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nizungumzie ufugaji wa viumbe maji au samaki. Tulishafika mbali, nimesikitika sana sikusikia ukizungumzia hatua tuliyofikia Mheshimiwa Matayo, wafugaji wangu wa samaki wananchi wameshatengeneza vikundi, wanajiandaa kufuga, sijui hiyo umeiweka upande gani, watu wa Ruhanga, Izigo wanajianda kufuga, sijaona umeweka wapi. Kama utaniita kando na kuniambia fungu lako ndiyo hili, tatizo la ufugaji Wabunge wenzangu ni namna ya kutengeneza mashine ya kutengeneza chakula, *the competitive advantage* ya ufugaji wa samaki ni namna ya kutengeneza kile chakula cha samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki kuna umri fulani anapenda chakula kinachoelea, mwingine *sub-immerse*d. mwingine kinachokuwa chini ya sakafu ya maji, mwananchi wa kawaida hawezi kutengeneza na kama alivyosema Mbunge mwingine kuna *ingredients* zinazopaswa kuingia mle kusudi samaki aweze kupendeza. Mtupeleke kule, tufuge kwa ajili ya

kuongeza lishe, tufuge kwa ajili ya kubadilisha mazao ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwetu tuna matatizo, mazao ya kahawa yanakwisha nguvu, twende kwenye samaki na hii haiwezi kuonekana mpaka Wizara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mifugo isaidie. Sasa maendeleo yatakuwepo kama sisi tutaweza kuelekezwa kule ni kazi kubwa inahitaji mkono wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie *NARCO*. Wakati tunagawa vitalu, naiomba Serikali yangu iisaidie *NARCO*. *NARCO* ni chuo, ni darasa, lakini si darasa la kawaida, ni darasa analoweza kuingia mtoto wa Mtanzania yeyote. Hawa watu wa kuja, hawa mnaowaita wawekezaji, mkiwaachia hizi *block* zote na mashamba wayachukue, mtoto wa mkulima hawezi kwenda kuwa *General Manager*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda maeneo ya *NARCO* yabaki, vijana watoke Sokoine waje wafanye kazi pale, mtoto yeyote bila upendeleo aweze kupanda kuwa *Chief Executive*, lakini ni sehemu ambayo sisi wazazi wao tunaweza kuingia kwa uhuru na kwenda kujifunza nini kifanyike. Nashukuru mmeleta mwekezaji wa Kiwanda cha Nyama kule Kagera. Nina imani kuwa huyu mwekezaji mbali na kuchinja ng'ombe, atawafundisha wananchi namna ya kufuga ng'ombe wa nyama sio yule ng'ombe anayeishi miaka kumi na nne, kufuga ng'ombe anayeishi miezi kumi na nane mpaka ishirini na nne amekwenda sokoni. Hiyo ndiyo tunataka kujua,

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafuga hivi, tunalalamikiana, tunakimbizana nchi nzima kwa sababu tuna nyenzo duni, ufugaji na ukulima wa kisasa unahitaji nyenzo. Serikali tujifunge mkanda kama ambavyo tunasema tengenezeni bajeti ya dharura kusudi muiweke pale iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti na mwisho nahitimisha kuwaambia wapiga kura wangu kwamba niko, sauti yangu *Panasonic*, sina tuhuma yoyote, niko pale pale na zaidi naitetea Serikali ya Chama changu ndiyo maana naunga mkono. Wanaonipiga mawe ni kwa sababu mimi ni jembe na nakitetea Chama changu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawatakia utekelezaji mwema. (*Makofi*)

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii nzito na nzuri kwa ajili ya Jimbo la Nkenge. Naomba tu nipongeze Serikali kwa jitihada kubwa inazofanya kwa ajili ya kutatua hili tatizo kwa kweli kama alivyosema msemaji aliyetoka. Tatizo la Nkenge la vitalu limekuwepo kwa miaka mingi, lakini namshukuru Mungu sasa kwamba tunaanza kuondoa tatizo hilo. Kwa kweli Mungu awabariki sana kwa kututendea haki. Labda niseme tu kuna jambo moja ambalo nataka kuiasa *NARCO*. *NARCO* ndiyo imekuwa tatizo kubwa la kusababisha haya yote tunayoongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo, NARCO ilipokuwa inagawa vitalu, iliweza kuuza vitalu na watu ndani na watoto ndani na maduka ndani na hata shule zimeuzwa kwa watu binafsi. Kitendo hicho ndicho kimesababisha vurugu hii yote kutokea. Kama wangefuata mipaka yao, kama wangefanya kama ambavyo wamekuta watu Vijijini, wakaachia kwenye sehemu ya *NARCO* kusingekuwa na tatizo lolote. Tatizo kubwa ni kuuza watu pamoja na ardhi, pamoja na hospitali zao, pamoja na maduka yao na watoto wao. Kwa hiyo, hilo ndilo lilikuwa tatizo kubwa na namshukuru Mungu sana nilikuwemo katika hiyo Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwatia moyo Wanankenge kwamba kwa kweli Serikali yetu ni sikivu na wakati umefika kwamba kama mtu una pesa, tunaomba usitumie pesa zako kununua watu, utumie pesa zako kununua ardhi na ile hali ambayo inakubalika kwa Watanzania wote. Kwa hiyo, naomba kurekebisha kidogo, muda ni mdogo lakini naomba tu ninukuu kwa sababu kuna kitu nakiona hapa kimekosewa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa namba 24, ukiangalia namba mbili (2) imeandika kwamba, kubadilishwa kitalu namba 287/3 kitakwenda kuwa pamoja na 287/6, si kwamba kumweka mwekezaji, huyu mwekezaji yupo, lakini amechukua ardhi kubwa kuliko uwezo alionao, tulishauri kwamba namba tatu (3) na namba sita (6) wakae kitalu kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, tuliongelea kitalu namba 11. Hiki kitalu kinamilikiwa na wafanyakazi wa *NARCO* waliamua na wao kujimegea kipande, wamejimegea kipande, lakini kutwa kuchwa wanapeleka Serikali Mahakamani. Lakini na wao hawana haki ya kujipa ardhi bila kuangalia utaratibu. Wameingia kwenye Kijiji na wananchi hawana nafasi. Tulishauri hiki Kitalu kichukuliwe na Serikali. Kwa hiyo, ningeomba hata kama wanaendelea kushtaki sio halali, tunaomba wajue kwamba, huwezi kuwa mwenyewe unagawa na wewe ukajigawia na wakati watu wana malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba muda hautoshi. Ukiangalia kitalu namba 17, tuliishauri Serikali irudi kwa wananchi kwa sababu ni mali ya Kijiji, huyu mtu hajafanya kitu chochote, anachukua watu kutoka Uganda wanachungia mle na matokeo yake Watanzania wanakosa mahali pa kuchungia. Tulishauri kirudishwe kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Namba 14 ni kijana ambaye alikuwa anapenda kufanya kazi, lakini kwa kuwa walimpa sehemu ambayo sio yenyewe, wamempa mali ya Kijiji, wanakijiji wamempiga na wamemtoa kwenye Kijiji, hiyo *block* iko tupu. Tumeshauri irudi kwa Kijiji na hatimaye huyu kijana kwa kuwa ameshaleta wanyama wake wamerudi *NARCO*, tunaomba *NARCO* impatie nafasi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu nishauri katika haya au niwatie moyo wananchi wa Misenyi kwamba tulichokiahidi na nimshukuru Rais

wakati nagombea alinisimamisha na akasema nina uhakika tatizo hili Mama Mshama atalimaliza, nataka kuhakikisha kwamba sitalimaliza pekee yangu lakini Wizara yetu ambayo tunaiamini italimaliza na Taifa letu litaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya machache, naomba Wanankenge mwendelee kusubiri hata haya ambayo ni madogo tukiyamaliza, nina hakika nitamshauri vizuri Waziri na tutakwenda pamoja. Wananchi mtakaa vizuri na wawekezaji mtakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, Mungu awabariki sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunakwenda vizuri na naomba tu niseme kwamba, mchana tukirudi kuchangia kama nilivyosema Mheshimiwa Mkiwa alikuwa anahitaji apate dakika zake zote kumi, kwa hiyo, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Makilagi, atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Ignas Mlocha. Tutajitahidi tupate angalau wachangiaji wengine kadhaa kabla hatujaingia kwenye hatua nyingine ili kwa kweli hoja hii iweze kupata wachangiaji wa kutosha.

Kwa hiyo, hapa tutashirikiana sana na meza ya Makatibu kupima dakika zetu za mtoa hoja za kupata nafasi, lakini kuongeza Waheshimiwa Wabunge wengine angalau tuweze kupata nafasi ya kuendelea kuchangia kwenye mada hii. Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

*(Saa 7.15 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa ratiba yetu tunaendelea na shughuli yetu ya leo na sasa nitamwita mchangiaji wetu wa kwanza Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu na uhai kwa siku ya leo nami nikawa mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpa pole Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afrika Mashariki, familia yake pamoja na dereva wake kwa ajali iliyowakuta tarehe 7 Agosti, 2012, tunaomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na kuwaponya ili arudi katika shughuli tuweze kuwa naye pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwapa pole wote walioondokewa na ndugu zao katika ajali mbaya iliyotokea Mkoani Tabora, Mwenyezi Mungu awape subira katika wakati huu mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuongelea zaidi zana za uvuvi. Kumekuwa na tatizo la zana za uvuvi kwa muda mrefu sana, wavuvi wadogowadogo

wakinyang'anywa nyavu zao na kuchomwa moto, lakini nyavu nyingine zinaponyang'anywa hazichomwi moto, Maafisa uvuvi baadhi yao huzunguka na nyavu hizi wakaziuza tena kwa wavuvi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inaonekana wazi kabisa, tatizo la kutumia nyavu haramu halitakwisha. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri akae na kuliangalia hili vizuri na aweze kuongea na wavuvi vizuri ili waweze kumueleza ni Maafisa uvuvi gani wanaofanya mchezo huo kwani sasa umekuwa ni mchezo wa kudumu. Tangu Bunge la tisa mimi nikiwa Mbunge suala hili nimeliongelea sana lakini ufumbuzi wake sijauelewa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aweze kuwaangalia Maafisa uvuvi hawa ni jinsi gani ambavyo wanaweza wakawa waaminifu kwa sababu baadhi yao wamekuwa si waaminifu kwa Serikali hii na kuwatia wananchi hasara siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye kilimo wanapeleka pembejeo za kilimo, namwomba Mheshimiwa Waziri haiwezekani wavuvi nao wakapelekewa pembejeo za uvuvi ili waweze kununua zana za uvuvi moja kwa moja kutoka Serikalini bila kupitia kwenye maduka yanayouza zana za uvuvi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naongea hivi? Zana za uvuvi zimefutiwa kodi lakini baadhi ya wavuvi walio wengi hawalifahamu hili kwamba zana hizi zimefutiwa kodi na bado wanauziwa na wenye maduka bei ile ile ya zamani. Kwa hiyo, naomba kwanza kabisa Wizara ifanye kuelimisha kutoa matangazo kwenye redio na kwenye *TV* ili wananchi

waelewe kwamba zana za uvuvi zimefutiwa kodi na waelewe kabisa wazi kwamba, wanapaswa kununua zana hizo kwa bei nafuu siyo bei wanayonunua sasa hivi. Kwa hiyo, katika kuondoa kodi kwenye zana za uvuvi hazimneemeshi sana mvuvi bali zinawaneemesha wenye maduka kama siyo wenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia pia kuhusiana na uvuvi hasa katika nchi yetu. Kuna nchi ndogo kama *Seychelles* wanatumia kuvua kwa kutumia mishipi mirefu sana ambayo wanachomeka ndoano na meli hizo zinakwenda kuvua katika maji marefu ili kuondokana na tatizo la kufukuzana na wavuvi kwa nyavu haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini tusiwachukue wataalam wetu hasa wa Halmashauri kwa sababu ndiyo wako karibu sana na wavuvi na siyo wanaokaa maofisini, kwa sababu mtaalam anayekaa ofisini hajui mvuvi anatumia nyavu gani, hao waliopo katika Halmashauri ili waweze kupata ujuzi na tuweze kuondokana na uvuvi wa kizamani wa kuendelea kufukuzana na wavuvi na kuwanyang'anya nyavu zao na kuwachomea moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wananchi wa Jibondo Mafia walinyang'anywa nyavu zao na hawana kazi nyingine ya kufanya zaidi ya uvuvi. Leo hii 98% mpaka 99% wamenyang'anywa nyavu zao na hawana njia ya kujikimu mpaka wavuvi hao sasa wamekuwa ombaomba mpaka inashangaza kwamba hivi mtu ukiwa mvuvi ni kosa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mtu ukiwa mvuvi huthaminiwi na nchi hii, wanajali tu uvuvi unawazalishia asilimia ngapi, lakini hawajali mvuvi huyu ni kitu gani anakipata ndani ya uvuvi wake. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, tumeona wafugaji wamesaidiwa ng'ombe, naomba wavuvi wa eneo la Jibondo na wao wasaidiwe nyavu kama si nyavu angalau nyingi hata za kuweza kuanzia maisha yao ili waache kukimbiakimbia na kuhamahama, mwisho wake watahama kijiji kizima kibaki hakina watu.

Mheshimiwa Waziri, kama mliweza kwenye ng'ombe kuwafidia wananchi waliofiwa na ng'ombe zao pia naomba kwenye nyavu hasa wananchi wa Jibondo, Mafia muwafikirie ili na wao waweze kujikimu maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia kidogo upande wa Viwanda vya Samaki. Ni wazi kabisa kwamba wananchi wanaozungukwa na migodi kuna asilimia fulani wanapata wanaboreshewa maendeleo yao zikiwemo shule na zahanati. Pia tumeona na wenzetu wanaozunguka Mlima Kilimanjaro wana ushirikiano wa kuweza kuwasaidia kuwaboresha angalau shule, hospitali na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwenye mifugo kuna nini? Mwanza kuna viwanda vingi sana lakini ningependa Mheshimiwa Waziri akija ku-*wind up* aniambie viwanda vya Mwanza kwa ujirani mwema je wanaboresha kiasi gani shule na zahanati zinazowazunguka na zilizo karibu? Kwani tukichukulia

mfano, Wilaya ya Ilemela Kata zaidi zipo kandokando ya Ziwa Victoria. Kwa hiyo, napenda nijue aidha, kama si hata shule je katika tozo hilo asilimia ngapi inarudi kwenye Serikali za Mitaa ili na wao waweze kujikimu na kuweza kuboresha maisha ya shule zao kama ambavyo wanafanya watu wa migodi na watu waliopo karibu na Mlima Kilimanjaro wanavyoboresha shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia suala la mifugo. Mifugo Tanzania imekuwa ni adha, wafugaji wana matatizo, Mheshimiwa Rais alisema ng'ombe anakonda na mfugaji anakonda. Hii ilikuwa ni dhana wazi kabisa kuonesha ni jinsi gani ambavyo Serikali itaweza kukidhi haja ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukichukulia mgogoro ambao unaendelea sasa hivi katika Wilaya ya Rufiji, napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba alifuatilie suala hili kwa kina ili wananchi isifikie sehemu mpaka tupate mauaji ya watu zaidi ya 1,000 au 1,500 ndiyo tuanze kuchangamka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamesema hili ni bomu linakuja lakini mimi ningependa Mheshimiwa Waziri baada ya hapa aende Rufiji akafanye utafiti, je, Wilaya ile ina uwezo wa kuchukua ng'ombe wangapi? Kwa sababu wafugaji wetu tunawapenda na wakulima pia tunawapenda lakini suala hili lichukuliwe kwa msingi na isifanywe suala hili kuwa kama ni suala la kisiasa kila siku ikawa maneno ya siasa na utekelezaji ukawa haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi bora ni yule anayetekeleza matakwa ya wananchi, kiongozi bora ni yule anayesikiliza shida za wananchi na kiongozi bora ni yule anayefuatilia masuala ya wananchi kwa karibu zaidi kuliko kuwa mbali zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameongea wenzangu saa hivi kuhusu malambo kwa wafugaji. Kule kwetu Usukumani.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ambayo ni nyeti sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Lakini vile vile nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mungu, Mungu wa rehema, Mungu muweza wa yote aliyeniwezesha jioni ya leo kuweza kusimama na kuzungumza katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niungane na Watanzania wote kuwatakia kila la kheri Watanzania wote hapa duniani kwa mfungo mzima wa Ramadhani na naomba Mwenyezi Mungu awakubalie swaumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze sasa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa sababu

kwanza mimi ni mdau wa Kamati ya Mifugo na Uvuvi, lakini vilevile ni mdau wa mifugo kwa sababu mimi ni mfugaji na lakini vile vile ni mvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunga mkono naomba niende moja kwa moja kuchangia mambo machache ambayo nimeyachagua kuyatilia mkazo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na ufinyu wa bajeti kusema ukweli pamoja na kwamba dhamira ya Serikali na mipango ya Serikali ni kuifanya Wizara ya Mifugo na Uvuvi iweze kuchangia pato la Taifa ili kuongeza uchumi wa Taifa letu, lakini bado kuna tatizo kubwa sana la Wizara hii kila mwaka bajeti yake kushuka. Ukiangalia kwa mujibu wa taarifa tulizonazo na taarifa ya Waziri pia imeonesha kwamba kila mwaka wanapopanga bajeti Wizara ya Mifugo imekuwa kwa kweli inashuka kabisa katika fedha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, Wizara hii ni Wizara nyeti sana na ni Wizara muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ijitahidi kufanya kila inaloweza itafute fedha hata kama ni za dharura au hata kama ni za mkopo ili katika malengo yaliyowekwa na Wizara ya mwaka huu yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama tutazungumzia migogoro ya wakulima na wafugaji au tutazungumzia miundombinu ya maji au tutazungumzia miundombinu ya malambo na majosho bila bajeti hii kuboreshwa tutakuwa tunazungumza kitu ambacho

hakiwezekani. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ijitahidi sana, itafute fedha za dharura, iweze kuhakikisha bajeti hii inaendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mwaka mwingine wa fedha yaani mwaka 2013/2014, nawaomba sana mnaopanga vipaumbele bajeti hii pia iwekwe katika maeneo ambayo ni kipaumbele kwa sababu ni Wizara nyeti sana kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo naomba niungane na wenzangu kueleza kwamba lipo tatizo kubwa sana la migogoro ya wakulima na wafugaji katika nchi hii. Mbunge mmoja amezungumza na ametolea mfano wa Rufiji, lakini kuna Kilosa na maeneo mengine Misenyi. Ninachoomba ni kwamba, sasa Serikali pamoja na jitihada zake iongeze kasi zaidi katika kuhakikisha migogoro ya wakulima na wafugaji inaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri sana Serikali kwamba wanapojiandaa kumaliza hii migogoro naomba wajielekeze katika mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nafikiri Waheshimiwa Wabunge na hata Watanzania wanaonisikiliza wanajua kwamba, mwaka 2006 Serikali ilifanya kazi nzuri sana ya kuhamisha mifugo katika bonde la Ihefu na kuipeleka katika Ukanda wa Pwani. Kwa bahati mbaya sana wakati zoezi lile linafanyika

maandalizi ya kutosha hayakufanyika na nitatoa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaozunguka Mikoa ya Pwani wao wamezoea kulima na kuvua, suala la ng'ombe na mbuzi kwao ni wadudu na wanawaogopa. Sasa wamepelekewa mifugo mingi zaidi karibu 150,000 bila kuwaandaa wananchi kujua namna ambavyo wanaweza wao wakawa wanalima na wanachanganyika na wafugaji. Kwa hiyo, naomba jambo la kwanza katika kuondoa migogoro hii ni elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya ziara kama mjumbe wa Kamati Rufiji na tulionana na wananchi wa Ikwiriri walituambia kabisa kwamba hawana shida kabisa na hawakatai mifugo katika Wilaya yao kwa sababu kwanza mifugo imewasaidia hata kuimarisha uchumi wa Wilaya yao. Lakini walichokuwa wanasikitika wanasema sisi hatukuandaliwa kupewa hata elimu ya ufugaji ili na sisi tuweze kufuga na tuweze kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu Mikoa ya Mara, Mwanza na Shinyanga hakuna migogoro ya wakulima na wafugaji, ni kwa nini haitokei? Ni kwa sababu Mkurya anafuga na analima, Msukuma anafuga na analima, ni tofauti na wenzetu wa ukanda wa Pwani wenyewe kazi yao ni kulima. Sasa kama analima halafu unampelekea mfugaji, mfugaji ambaye pia na mwingine halimi halafu unamwambia wachanganyike. Kwa hiyo, naomba Serikali itafute fedha za haraka kwenda kutoa elimu

katika ukanda walikopeleka mifugo na siyo Pwani peke yake ni pamoja na Tanga, Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba, migogoro ya wakulima na wafugaji inatokana na nini? Inatokana na miundombinu ya mifugo bado ni hafifu pamoja na jitihada tunazozifanya na hata kuhamahama kunatokana na wafugaji wanakoishi. Kwa mfano, Wasukuma wa Mwanza wanaondoka Mwanza kwa sababu hakuna malambo, majosho wala malisho, lakini pia wanaondoka Mara wanakwenda Katavi, wakifikiri kule kuna ardhi nzuri na yenye rutuba ya kulisha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba ili kuondoa hili tatizo la wafugaji kuhamahama kwenda kutembea nchi nzima na mahali pengine mazingira yanaharibika. Naomba Serikali sasa na najua Serikali haishindwi kitu, ijaribu kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hasa majosho, malambo na mambo mbalimbali yanayohusiana na mifugo. Tukifanya hivyo, tatizo la wafugaji kuhamahama litakuwa limeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji. Nimetolea mfano katika Ukanda wa Kanda ya Mashariki na Pwani. Tulipokuwa tunahamisha mifugo kutoka Ihefu hata katika maeneo mengine ambayo wakulima wanakwenda kwa bahati mbaya sana Serikali haikutenga fedha za kutosha hata kwa ajili ya kupima ardhi ambayo wakulima watakwenda matokeo yake mifugo inaanza kushushwa barabarani kuanzia Morogoro, Chalinze, Kibaha mpaka

wameingia Rufiji wanashusha na kila wanapokutana na majani wanashusha ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi mifugo imeshushwa mpaka kwenye bonde la Rufiji, sasa kama tumezuia bonde la Ihefu halafu tunakwenda kupeleka mifugo bonde la Rufiji, tunafanya kitu gani? Naiomba sana Serikali, nilifanya utafiti nikaongea na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ambazo kunakwenda mifugo, wakaniambia Mama hatuwezi kutenga fedha kwa ajili ya kupima ardhi kwa sababu mapato yetu sisi ni kidogo na mahitaji ya ardhi kwa ajili ya wafugaji na wakulima ni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wakawa wamenituma nije niombe sana na niiombe Serikali ambayo ni sikivu kwamba, sasa Serikali Kuu ibebe hii dhamana, ijaribu kutafuta fedha kokote kama ambavyo tumetafuta fedha kokote tukazipata kwa ajili ya kupeleka mifugo Arusha, basi tujitahidi kupata fedha ili sekta ya ardhi iende ikapime ardhi katika yale maeneo, kwa sababu bila kufanya hivyo itakuwa ngumu sana na itaendelea kuleta matatizo kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie jambo lingine ambalo ni suala la uimarishaji wa uchumi kupitia sekta ya uvuvi na mifugo. Sekta hii kama nilivyosema mwanzo ni sekta muhimu sana, sekta hii haiwezi kuimarika kama nchi yetu tumeruhusu viwanda tunawaachia watu binafsi. Mafia kuna kiwanda ndiyo wawekezaji wetu, kiwanda kipo na kweli kinafanya kazi nzuri na hata Mwanza vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishauri Serikali kwamba tujaribu sasa kutumia fedha zetu za ndani kujenga viwanda vyetu na nasema inawezekana na naomba niiombe Serikali kwamba wahamasisheni *NSSF, PPF* na Mifuko mingine yote ya Jamii waje kuwekeza katika viwanda vyetu kwa sababu wakiwekeza katika viwanda tutaweza kusindika minofu ya samaki na tutaongeza ajira, lakini vile vile samaki watapata soko na pia tutauza hata ndani ya nchi na uchumi wa Taifa letu utaongezeka. Lakini vile vile tutasindika minofu ya nyama, wafugaji badala ya kubaki kuwa wachungaji, ng'ombe watawasaidia kuboresha maisha yao na siyo peke yao na hata ajira katika nchi yetu zitaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nizungumzie suala la kuwawezesha wanawake na vijana kupitia uchumi wa bahari na ziwa. Kama unavyojua wazalishaji wakubwa na wafanyakazi wakubwa wa kazi ni wanawake na vijana. Katika baadhi ya maeneo wanawake na vijana wanaozunguka kanda ya bahari, kanda ya Ziwa Victoria, kanda ya Ziwa Manyara, Kanda ya mashariki na maeneo mengine ambapo maziwa yapo. Kwa kweli wanawake na vijana wa maeneo hayo wamekalia uchumi, wanahangaika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongea na vijana katika ukanda wa Pwani wananiambia Mama sisi tupo tayari kufanya kazi lakini hatuna uwezo wa kwenda katika kina kirefu cha maji, matokeo yake tunakwenda katika maji mafupi, hatupati samaki wa kutosha, matokeo yake tumewaachia watu wengine

kabisa ndiyo wanakuja kuchukua uchumi wa nchi yetu. Naiomba sana Serikali, tuwawezeshe vijana na wanawake ili waweze kupata zana za kisasa za kuvulia samaki, waweze kupata zana za kisasa za za kuhifadhi samaki. Niliongea na akinamama na wapo tayari kabisa kwa biashara lakini shida yao ni majokofu, basi Serikali tujitahidi kuwawezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni suala la kutunga sera ya namna tutakavyoendesha huu utaratibu wa kuwa na mifugo. Tuwe na sera, maana haiwezekani wewe mfugaji mmoja una ng'ombe zaidi ya 2,000. Ni kweli kama alivyosema Rais wa nchi wewe mwenyewe na familia ni maskini huna kitu, ng'ombe wanazidi kuharibu mazingira. Ifike mahali tutengeneze sera kwamba ukifikisha ng'ombe kadhaa ukauze ili uweze kupeleka watoto shule na uweze kuboresha maisha yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge busara yangu inanituma nimwite Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Lakini pia nitamwita Mheshimiwa Rose Sukum kwa sababu toka tumeanza mchango huu sijapata mchangiaji kutoka upande wa chama kingine. Pia kwa dakika chache sana mwishoni nitampa Mheshimiwa John M. Cheyo nafasi kwa kutumia Kanuni ya 60 nadhani ili awe mchangiaji wa mwisho.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama katika Bunge lako Tukufu. Pili, nakushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Lakini kabla ya kuchangia kwanza niwaombee Waislam wote ambao wamefunga katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Mwenyezi Mungu azikubali amali zao na saumu zao ambazo zina mtihani kidogo kutokana na mchanganyiko zilionao. Mwenyezi Mungu azikubali swala zao za suna na faradhi, witri na *taraweh*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nakumbusha kwamba hii ni wiki ya tatu na ya mwisho ambapo ndani ya wiki kuna *Laila tul-kadiri* yaani usiku wenye cheo. Katika usiku huu ambao Mwenyezi Mungu kwa hekima yake ameuficha haujulikani uko tarehe ngapi, lakini katika siku mbili za mwisho, amali unayofanya kama amali moja, basi inalipwa mwa muda wa miaka 83.333. Nadhani hakuna binadamu yeyote kutoka sasa hivi ambaye ataishi kwa miaka 83. Kwa hiyo, naomba tujipinde zaidi katika wiki hii ya mwisho ili tupate fadhila za Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa nichangie bajeti. Kwanza nianze na ufinyu wa bajeti. Kama tujuavyo ni kwamba, sekta ya mifugo ilikuwa katika Wizara ya Kilimo na sekta ya uvuvi ilikuwa katika Wizara ya Maliasili. Lakini kwa hekima ya Mheshimiwa Rais Kikwete alitaka hizi sekta zipewe umuhimu mkubwa wa maendeleo na ndiyo maana akaziundia Wizara maalum. Lakini cha kusikitisha ni kwamba ndani ya miaka mitatu mfululizo bajeti ya

Wizara hii imekuwa ikirudi chini. Kwa mfano, mwaka 2010/2011 bajeti ilikuwa shilingi bilioni 58.8, mwaka 2011/2012 ilikuwa shilingi bilioni 57.2 na mwaka huu ni shilingi bilioni 54.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta imekaa kama taa ya koroboi vile imepata mafuta na kidogo kidogo inashuka. Mimi naona kuletwa kwenye Wizara hii basi sekta hizi za uvuvi na mifugo zinakufa kwa sababu kwa mfumo huu haziwezi kutekeleza lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu ni kwamba, kwa sababu tunaongeza bure gharama za Serikali kwa kuongeza Wizara, sasa hivi tuna Wizara 31. Kwa kuwa kila siku tumekuwa tukipiga kelele kwamba Serikali inaingia gharama kubwa kwa kuongeza Wizara, basi Wizara hii ivunjwe na hii sekta ya mifugo ilirudishwe Kilimo na uvuvi irudishwe Maliasili au zote ziende kilimo, *otherwise* hapa tutakuwa tunafanya kazi ya bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi haya hapa kwa nia ya kuwakosesha Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ulaji, hapana, isipokuwa katika hali halisi ya maendeleo ya nchi yetu lazima tupange kwa kuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uvuvi; wavuvi wetu ni wavuvi wadogo wadogo ambao kipato chao ni cha chini kabisa. Wanatumia zana duni za uvuvi na umaskini kwao hauwezi kuondoka. Wakati mwingine hawana hata uhakika wa chakula cha siku moja na vile vile hawawezi kuchangia katika pato la Taifa au kama wanachangia ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya wavuvi wetu wamekosa msaada wa Serikali. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu Serikali imeshindwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kununua zana za uvuvi ziwawezeshe kuvua katika bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tujuavyo katika maeneo ambayo tunavua sasa hivi samaki wamekwisha na wako katika bahari kuu, sasa huwezi kupata samaki. Kwa mfano, sasa hivi hapa Dodoma samaki kilo moja ni shilingi 6,000/=. Lakini bahari kuu samaki ni wengi, inasemekana wanazaliwa mpaka wanakufa bila kuvuliwa. Kwa hivyo, Serikali imewaacha mkono wavuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hiyo haitoshi ni kwamba, wavuvi hawa wameambiwa wasalimishe nyavu na zinachomwa kwa sababu wanaharibu mazingira ya samaki. Nakubaliana na hilo kabisa, lakini baada ya kuchoma nyavu kwa sababu zinaharibu mazingira ya samaki ni nini kinafuata sasa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Wizara wanasema wanatoa shughuli mbadala kwa wavuvi yaani badala ya kuvua sasa walime mbogamboga au mwani au wafuge nyuki. Sasa kweli utamtoa mvuvi aliyebobea ambaye toka azaliwe anavua, ameoa kwa uvuvi, amesomesha kwa uvuvi, leo unamwambia akalime mbogamboga, akafuge nyuki au akalime mwani! Hiyo inaingia akilini kweli? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Haiingii! *(Kicheko)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kitu cha msingi cha kufanya ni kwamba, Serikali ihakikishe inatoa mikopo kupitia benki za raslimali mfano *TIB* ambayo itatumika kununua zana za uvuvi. Nina hakika tukianza kuwapa zana hizi basi hatutamuona mvuvi yeyote ambaye anavua katika maeneo ambayo yanahatarisha usalama wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba, ili tuwasaidie wavuvi wetu siyo kuchoma nyavu bali ni kuwapa vitu mbadala, na siyo kwenda kulima mwani au mbogamboga kwa sababu mvuvi hawezi kufanya kazi kama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita Wizara ilisema inaandaa andiko ili kutoa fursa kwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi. Nataka Mheshimiwa Waziri aje aseme hapa kwamba hilo andiko ambalo linawapa fursa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi hii kujua manufaa ya sekta ya uvuvi limekwishaandaliwa kwa sababu sisi kama Kamati hatujaliona mpaka sasa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika hili ni kwamba, wavuvi wadogo wadogo wameandaa waraka wao huu ambao umeeleza kero zao, hususan kutoka Kisiwa cha Kibondo kule Mafia. Naomba muusome waraka huo kwani nafikiri Waziri anao. Katika waraka huo kuna *research* ambayo inafanywa na wanasayansi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Norway. Utafiti huu unaitwa “Uvuvi wa mwambao wa

Tanzania na changamoto za utandawazi katika usimamizi wa rasilimali, maisha ya watu na utawala.” Nadhani hii ni *paper* muhimu hivyo waisome ili waone kero za wavuvi wetu na nini wanataka wafanyiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka niende katika mifugo. Katika mifugo naanza na viumbe ambao wameanza kutoweka hapa katika nchi yetu. Kuna viumbe ambao sasa hivi wanaanza kupungua. Kwa mfano, kasa na nyangumi. Najua kwamba kuna sheria inayomlinda Kasa kwa mfano huruhusiwi kuonekana ukiwa na nyama ya kasa, wala mayai au mafuta yake. Lakini bado viumbe hawa wanaendelea kupungua. Sasa labda tuelezwe, ama hizi sheria hazifanyi kazi au zinataka zirekebishwe kidogo hapa Bungeni! Lakini kuna haja kabisa ya kuhakikisha hawa viumbe muhimu wanaendelea kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni magonjwa ya wanyama ambayo vile vile yanaathiri binadamu. Kuna magonjwa mfano kichaa cha mbwa ambacho kinaathiri binadamu. Waswahili wanasema kinga ni bora kuliko tiba. Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuhakikisha mbwa wetu wote wanachanjwa? Kwa sababu kichaa cha mbwa kinga yake ni kuchanja mbwa. Mfano mwingine, mafua ya ndege; Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba ugonjwa huu hautokei, au ukitokea unadhibitiwa kwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika mifugo ni kwamba nchi yetu kama walivyosema Wabunge wengine ina eneo kubwa (hekta milioni 94) ambazo zinafaa kwa kilimo na mifugo, lakini cha

kushangaza ni kwamba wafugaji wetu wengi wanatangatanga kutafuta malisho. Nasema jambo moja kubwa ambalo linasababisha hili ni tatizo la maji na malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo kwa nini Wabunge wote wanalalamika kuhusu maji, anasema waulize Halmashauri kwa sababu wao ndiyo watekelezaji. Sasa unajiuliza kwa nini Halmashauri hawatekelezi hili? Hawatekelezi upatikanaji wa maji katika mifugo yetu kwa sababu kama wanapata maji ya kutosha, basi mifugo haina haja ya kutangatanga katika maeneo makubwa. Lakini vile vile kuna umuhimu wa kuwa na malisho ya kutosha. Tuna matatizo ya malisho ya wanyama.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofi*)

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ambayo mimi pia ni mjumbe wa Kamati inayoisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelekea moja kwa moja kwenye suala la bajeti kwa kuiambia Serikali kwamba bajeti ya mifugo ni ndogo. Nasemea hivyo kwa sababu shilingi bilioni 13.8, sehemu kubwa imekwenda kwenye suala la kuendeleza mifugo ya kisasa. Lakini ng'ombe

wa asili kwa kweli hawakujitokeza hata kidogo. Nasema hivyo kwa sababu fedha za *DADPs* zimeelekezwa kwa TAMISEMI na Halmashauri ndizo zinazoweza kuangalia suala la malambo machache tu na wala siyo mengi kwa upande wa ufugaji wa ng'ombe wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bajeti iliyotengwa nadhani ndiyo maana ubora wa ng'ombe wa asili unasuasua. Unasuasua kwa sababu wafugaji hawana maeneo na huduma muhimu kwa mifugo yao. Hivyo, basi wafugaji wanahitaji kauli ya Serikali kupitia Waziri Mkuu. Leo tunaomba kukwambia kwamba jambo hili la ng'ombe wa asili liangaliwe na kutengewa fedha za kutosha. Hizi ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa maeneo ya malisho. Naomba kulizungumzia hilo kwa kirefu. Ng'ombe wa asili wana uwezo wa kuleta kipato. Kuna Mheshimiwa Mbunge asubuhi alihoji akasema hivi mifugo wana kipato gani? Nataka kumweleza kwamba mifugo wana kipato kikubwa hasa ng'ombe wa asili kwa sababu mwaka 2011/2012 ng'ombe milioni 1.1 waliingia sokoni na kati ya hao ng'ombe wanaotoka kwenye ranchi walikuwa 5,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ina maana kati ya ng'ombe hao wote waliooingia sokoni takribani 1,095 ni wa asili. Hao ndiyo walioingia kwenye soko la nchi hii na ambao wanaleta pato la Taifa hili. Sasa Serikali haioni kuna umuhimu wa kuelekeza fedha kwenye sekta hiyo ya ng'ombe wa asili ili waweze kupatiwa huduma bora? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nyama tani 503,496, maziwa lita bilioni 1.5 na ngozi vipande milioni 2000.8 ziliingia kwenye soko na ng'ombe hawa wote ni wa asili siyo wa kisasa. Je, hamuoni kwamba wana pato? Sasa nasema tangu tulipopata uhuru ikiwa ni miaka 50 hadi hii leo kati ya hekta milioni 60,000 zilipopangwa kutengwa kwa ajili ya mifugo, ni hekta milioni 2000.3 zilizotengwa, lakini hawa wafugaji hawakugawiwa. Sasa Serikali iwaambie wananchi hawa kwamba ni lini watagawiwa maeneo hayo ili waweze kufuga kwa amani na utulivu bila kuwa na migogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa kwa nini wakati huo huo sekta ya wanyamapori inagawiwa ardhi kubwa sana, kilimo wamegawiwa ardhi kubwa sana, lakini wanyama hawa wa asili wanaonekana hawafai. Nina usemi wangu ambao naurudia kila wakati kwamba, "Mnaona hawa wanyama hawafai na wafugaji wao hawafai kwa sababu hawakai karibu na nyie na wanaleta migogoro wanaharibu ardhi yenu. Lakini nyama kwenye masoko yenu au bucha zenu zote nyie wakubwa ndiyo wanunuzi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili liangaliwe sasa kwa undani ili tuone tunawatetea vipi hawa wafugaji kwa asilimia mia moja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga fedha lakini malambo hayo yanayojengwa ni hewa na ardhi inaleta utata. Naomba nizungumzie suala la ardhi. Suala la ardhi ya wafugaji limekuwa mtambuka kwa

sababu Wizara ya Ardhi ndiyo inayogawa ardhi, Wizara ya Mifugo imo humo ndani, Wizara ya Maliasili imo humo ndani, Mazingira imo humo ndani, TAMISEMI wamo humo ndani na kadhalika. Sasa ni nani atakayehusika kugawa hiyo ardhi ya wafugaji? Sisi tunapenda kufahamu hilo kwa sababu migogoro imetutia hofu sana sisi wananchi wote ambao ni wafugaji. Wafugaji wako hapa wanasikiliza kwa sababu wanaona kila mwaka wanarudi kutaka kujua ni lini wanagaiwa hiyo ardhi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia Mvomero ni kero. Kwenye vitabu vya hotuba ya Waziri wameeleza kwamba watatua matatizo na wamewaagiza Halmashauri. Halmashauri hawawezi chochote. Msituhamishie kwenye Halmashauri wakati wao wanasema hawawezi kugawa na hawakugawa mpaka leo. Sasa tunaomba Serikali yenyewe kupitia Wizara za Ardhi, Mifugo na TAMISEMI waende kugawa hiyo ardhi ya wafugaji ili waweze kuishi kwa amani na utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna migogoro Kilosa, Kilombero, Meatu, Rufiji, Igunga, Loliondo, Mikumi, Tarangire, Vilima Vitatu na Hanang. Hawa watu ni lini watapata ahueni ili waweze kuishi kwa amani na utulivu kama siyo Serikali hii kufanya hiyo kazi? Tunaanza kutupa mizigo kwa Halmashauri, Wakurugenzi wamepigika hawawezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali inaweza kugawa ardhi ya kilimo basi yale maeneo yote waliyoyagawa kwa ajili ya kilimo wafugaji warudi

kwenye maeneo hayo kwa sababu yalikuwa ya kwao ili wasihangaike. Tumekwenda Rufiji, wananchi wa Rufiji pamoja na Wabunge wao wanasema wafugaji waondoke, waende wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametolewa Ihefu wakapelekwa Rufiji, huko Rufiji wanasema waondoke. Wizara inasema Halmashauri igawe ardhi, itagawa ardhi gani mbona hamkuionesha? Tunaomba hii ardhi ambayo ni hekta milioni 60 iko wapi kwa hapa Tanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwenye sehemu ya soko. Mifugo inaweza kuleta maendeleo bila matatizo yoyote kwa sababu nimeelezea hapa mwanzoni kwamba iliingia kwenye soko. Je, ni lini sasa Serikali itajenga viwanda vya kuongeza thamani ya mazao kwa sababu bila kujenga hivyo viwanda bado hayo mazao ya mifugo hayana faida yoyote. Hata tukikaa tuangalie mambo yote hatutasaidia chochote kama hatutaongeza thamani ya mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi zinajitahidi lakini hawana uwezo kwa sababu pia wanalipa kodi kubwa. Mlikubali kwamba tutafuta kodi lakini mpaka leo kodi haijafutwa. Hii tasnia ya maziwa itawezaje kuleta maziwa mengi hapa Tanzania na kuwafanya watu wote wakanywa maziwa kama hawatafutiwa kodi? Kwa nini tunafuta kodi ya madini, tusifute kodi kwenye tasnia ya maziwa? Nadhani sasa ifike mahali tuamue kwamba tunafuta kodi kwenye tasnia ya

maziwa ili Viwanda vya Maziwa viendelezwe na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye suala la viwanda Serikali ihusike kwa asilimia mia moja kujenga Viwanda vya Ngozi na Nyama ili wananchi waweze kuuza mifugo yao kwa urahisi na kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, Serikali imesema kwamba wana viwanda: Kiwanda cha Shinyanga cha Mbeya kimekufa, lini watafufua hivyo viwanda viwili? Tunaimba tu, tunapiga wimbo wa Taifa hatusaidiwi chochote. Ni lini sasa sisi wafugaji tutasaidiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimsaidie Mheshimiwa Waziri kwamba, wafugaji sasa tusaidiwe na Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha kwa kupewa fedha za kutosha ili kuiwezesha sekta hii iendelee vizuri na iweze kuchangia katika kuleta pato la Taifa kwa ujumla. Kama nchi za jirani wenzetu wanaweza kupata pato kutokana na ng'ombe wa asili, nyie mnasubiri eti mpaka waletwe ng'ombe wa kisasa, lini hao wa kisasa watatosheleza? Tuwaboreshe hawa hawa wa kienyeji waliopo kwa kuwapa wafugaji malambo, maji, majosho na maeneo ya malisho na wao wenyewe watajua ni namna gani wanaweza kuendeleza nchi hii kwa pato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wameshukuru sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge tulisema hapa tumebakiwa kama na dakika tano au sita hivi, Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza moja kwa moja kwa kwenda kwenye hoja. Kwanza, nataka kuwatoa wasiwasi Wabunge wote ambao wamo katika Bunge hili wakisema eti wafugaji ni maskini, wao wamekonda na ng'ombe wao wamekonda. Hakuna mtu tajiri katika nchi hii kama mfugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimefurahi Mheshimiwa Waziri ametuletea takwimu ambazo zinaonesha kwamba biashara ya ng'ombe sasa hivi ni trilioni moja. Idadi ya ng'ombe milioni 18 zidisha mara shilingi 300,000 wewe mwenyewe utajua hesabu na huo ndiyo utajiri tulionao katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tuliyo nayo, tunashindwa kuongeza utajiri huu, tunashindwa kuutumia utajiri huu, tunashindwa kuhamasisha hawa watu wawe na maisha ambayo yanafanana na jinsi mnavyofikiria ninyi kwamba ni matajiri. Wote walio juu pale ukiangalia katika Mifuko yao unaweza ukakutana

na shilingi laki tatu au nne ziko humu humu kwenye nguo ambazo wamevaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia kati ya Wabunge, ukimwomba sasa hivi akupe mkopo wa shilingi laki tano, atasema nenda kwa Spika na kadhalika hamna ndani ya Mifuko yetu. Kwa hiyo, ondoeni hiyo dhana, hatushughuliki na watu maskini, tunashughulika na watu matajiri na tunachopaswa kufanya ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nimeangalia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ni kidogo sana mazungumzo juu ya chakula cha ng'ombe. Ukitaka ng'ombe hawa wasitangetange basi tupe chakula cha ng'ombe. Katika sehemu nyingi Amerika na kadhalika hiki chakula wanatuletea hapa kinaitwa *corn* hicho ni chakula cha ng'ombe, watu wanalima mahindi kwa ajili ya ng'ombe na ng'ombe hawatangitangi wanakula palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nimeangalia nini kinafanyika katika Wizara hii juu ya chakula, hamna na uwezo wa kupata chakula kizuri upo. Kwanza tuna alizeti kibao, pamba kibao na pamba mwaka huu itatoa karibu tani laki 355, asilimia 66 hiyo inaweza kuwa ni mashudu, ukiweka kwenye mashudu ng'ombe watanenepa na watu hawatahamahama kwa sababu chakula chao kipo palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtazamo wa Wizara lazima ugeuke sio uwe mtazamo kwamba ng'ombe watajilisha jinsi wanavyotaka wenyewe.

Ng'ombe wajitafutie wao wenyewe, wachungaji watajitafutia wenyewe, sasa Serikali iingie katika kutengeneza chakula cha ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumalize migogoro. Leo hapa nimepata taarifa mara sijui Kilosa Kijiji cha Ng'aite wanafukuzwa, sijui watu wanafungiwa kilimo chao kwa sababu kuna mwekezaji, kule kwenye hifadhi ya Mikumi ng'ombe 200 wanapigwa. Haya mambo yatatuletea matatizo ya kutokuwa na amani katika Taifa hili. Hebu Serikali mwangalie hao wafugaji, mtamaliza hii migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, Ngorongoro ng'ombe pamoja na wanyamapori wanalisha pamoja kwa nini sisi kule Ng'wag'wali, kwetu sehemu ya Meatu, Nkuyu kwa nini ile *Game Reserve* ambayo tumewapa watu kuua, tumewapa watu *hunting blocks,* kwa nini ng'ombe na mifugo na wanyamapori wasiweze kuchunga pamoja. Sasa hivi wanachunga kweli, lakini wanachunga kwa rushwa na kila wakati wanakamatwa na kila wakati wanapigwa na ng'ombe wao wanachinjwa kwa nguvu kwa bunduki, kwa nini tusianze kufikiria vingine na tukahakikisha kuwa ng'ombe wetu wanalisha katika mahali ambapo kama vile vile Ngorongoro wanavyofanya pamoja na wanyamapori. Namwomba Mheshimiwa Waziri azungumze hili jambo pamoja na Waziri anayehusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hapa mmesema mizani, sawa lakini mizani inatumika. Sisi tunachotaka tufike mahali ambapo ng'ombe kwa

*book* au *book* nne kwa kilo au tano kwa kilo, ndiyo utaratibu mzuri unaofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, dakika hazikutosha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa John Cheyo, lakini ujumbe umefika.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana Serikali kutoa kifuta machozi kwa wafugaji wa athari za ukame. Je, Serikali ni ini italipa fidia kwa wafugaji ambao wameathirika na *operation* hatarishi za haki kwa wafugaji wa Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inahimiza mipaka kwa mbuga za Wanyama na nyingi zimepanuliwa na kumeza huduma jirani za maji ambayo yalitumika kwa mifugo na kwa wanyamapori. Je, huduma hii kwa maji itarejeshwa vipi katika maeneo yaliyomezwa na upanuzi wa Hifadhi za Wanyamapori katika Mikoa ya Tabora Shinyanga, Meatu, Bariadi, Mbeya Morogoro na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo haijapewa kipaumbele pamoja na kuwa Tanzania inashika nafasi ya tatu katika Afrika kuwa na mifugo mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuchimba malambo; kwa kuwa kuhamahama kwa wafugaji ni kwa sababu ya kutafuta maji, ni vyema Serikali iwe na mpango maalum ili kuwa na maji ya kutosha na ya karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujenga majosho; katika afya ya mifugo suala la majosho ni vizuri lipewe uzito wa kipekee na litasaidia kuboresha afya ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza maeneo ya malisho; ni vyema suala hili liangaliwe upya.

**MHE. MWIGULU L.M. NCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa jinsi unavyomudu majukumu ya Wizara yako. Nimpongeze pia Naibu wako kwa jinsi mnavyotekeleza majukumu kwa ushirikiano. Nimpongeze kipekee kwa kuwakumbuka Kihistoria wafugaji kwa kuwafidia kwa kuwapa ng'ombe. Hii imesaidia sana kuwajenga wafugaji kuwa Serikali inawajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali ifufue malambo na kujenga mapya ili yaweze kutumika kuendeleza ufugaji. Maeneo mengi ya nchi hii ni kame, lakini maji mengi hupotea tu mvua inaponyesha. Vile vile naomba Wizara ifufue majosho na madawa yawafikie wafugaji ili kuosha mifugo yao kuendana na sera ya ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imalize migogoro ya ardhi ili ufugaji uweze kufanyika bila ugomvi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niiombe Wizara iwakumbuke wafugaji wa Jimbo la Iramba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri na watendaji wa Wizara kwa hotuba nzuri, naomba nichangie hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii za wafugaji sasa hivi wanahamahama kutafuta malisho nchi nzima, hii inatokana na ongezeko la idadi ya watu na mifugo yao, lakini rasilimali ya ardhi imebaki hiyo hiyo. Ni vizuri sasa Serikali kupanga mikakati maalum ya kutenga na kupima maeneo maalum kwa ajili ya kuchungia. Ardhi ya wafugaji iwe kwa ajili ya kufuga tu, hili ni jambo muhimu sana Serikali ilitatute kwani baada ya miaka 10-15 hivi litakuwa ni tatizo lisilotatulika. Serikali (Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Ardhi) shirikianeni kutatua matatizo haya, ni bomu kubwa la siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iongeze juhudu ya kujenga mabwawa na majosho ya kuogesha mifugo, kwa sasa hali ilivyo wafugaji kwenye maeneo yenye mifugo mingi wanataabika sana na magonjwa ya mifugo yanayosababishwa na kupe. Jimbo la Igunga kwa mfano, linao uhaba mkubwa wa majosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ijipange sasa kuendeleza biashara ya nyama ya ng'ombe. Mipango itayarishwe kuanzisha machinjio ya kisasa kwenye miji yetu ili nyama iweze kupata soko la uhakika. Kwa mfano, migodi ya madini na uwekekezaji mwingine, wananunua nyama nje kutokana tu na utayarishaji mbaya wa nyama. Tulete mapinduzi ya mifugo na mazao yatokanayo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro kati ya wakulima nchi hii bado halijapatiwa majibu. Lipo tatizo la wafugaji kuhamahama kufuata malisho na maji, pia wafugaji hawana maeneo maalum ya malisho. Nashauri wafugaji watengewe eneo lao la malambo, majosho yajengwe ili kumaliza migogoro iliyopo sasa.

Mheshimiwa Spika, kulitokea zoezi la kuhamisha wafugaji kutoka Ihefu, mifugo mingi ilikufa kutokana na *DC* Hawa Ngulume kufungia mifugo hiyo kwenye mazizi bila kupata chakula na hivyo kusababisha hasara kubwa kwa wafugaji waliohama kutoka Mbarali Ihefu. Niliwahi omba Serikali iwalipe fidia, nataka kujua ni lini Serikali itawalipa fidia wafugaji hawa? Naomba kupewa majibu kwa niaba ya wananchi wa Mbarali.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu wengi wao ni wadogo wadogo ambao hawana zana za kisasa na

imepelekea mapato yao kuwa madogo madogo, hivyo ushauri wangu kwa Serikali ni kuwapatia wavuvi wadogowadogo zana za kisasa ili waweze kwenda katika bahari kuu na waongeze kipato chao.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, kuna meli za mvuvi toka nje ya Tanzania zinavua katika Bahari kuu na Serikali imekosa mapato. Naishauri Serikali kutumia Wanajeshi kikosi cha Wanamaji *Navy Command* ili kudhibiti uvuvi unaofanywa na wageni toka nje.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna ngombe wengi na nchi yetu ni ya tatu kwa kuwa na ng'ombe wengi ikiwa nyuma ya Sudan na Ethiopia, lakini ng'ombe wetu hawana ubora wa kutosha kwani hawakunenepeshwa inavyohitajika. Hivyo nashauri Serikali kuongeza kazi ya kunenepesha ng'ombe ili kuweza kupata ng'ombe wenye ubora na nyama bora ili tuweze kuuza nyama nje ya nchi ili kuongeza pato la wafugaji kupambana na umaskini na hatimaye Serikali kuongeza pato la Taifa kwani Botswana imepiga hatua katika sekta hii na hawana mifugo mingi kama Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya machinjio ya kisasa ni kidogo, havitoshi hapa nchini kwetu Tanzania, ni vyema viwanda hivi vikaongezwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kuwasilisha.

**MHE. NAMELOK E.M. SOKOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naipongeza

Serikali kwa kuandaa mipango ya kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi. Hata hivyo, sijaona bajeti maalum kwa ajili ya utekeleza wa mipango hii. Sasa na hii inaweza kufanywa kama mipango mingi ya Serikali inayoishia kwenye makaratasi. Naishauri Serikali itafute fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango hii.

Mheshimiwa Spika, Viwanda vya Samaki, katika nchi yetu vinakabiliwa na changamoto, zikiwemo kodi ambazo siyo za kiushindani, matokeo yake nchi inapata wawekezaji wachache katika sekta ya uvuvi, Serikali iziangalie upya kodi za viwanda ili iweze kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji siyo ishara nzuri katika nchi yetu, lakini hatuoni hatua za makusudi zinazochukuliwa na Serikali kumaliza tatizo hili. Migogoro hii inawafanya wafugaji wajione kama wakimbizi katika nchi yao. Nashauri Serikali sasa ipange na kusimamia matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iwekeze katika sekta hii, iwekeze kwenye Viwanda vya Kusindika Maziwa, machinjio ya kisasa, majosho, malambo lakini pia kwenye vituo vya afya vya mifugo ili kuweza kukuza pato la sekta hii kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itoe ruzuku kwa chanjo za mifugo mfano, chanjo ya ndigana kali ambayo kwa asilimia 90 inasaidia, lakini bei yake ghali mno. Chanjo hiyo itolewe kwa ruzuku kama inavyofanyika kwa pembejeo za kilimo.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuaminiwa sana na Mheshimiwa Rais akawateua kuendelea kuongoza Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ukame mwaka 2005/2006-2008, Ukanda wa Kati, Mikoa ya Singida na Dodoma ilikumbwa na ukame mkali sana hadi kupelekea kufa kwa mifugo mingi. Ilikuwa ni kawaida wakati huo kuona mizoga mingi barabarani na mifugo minadani haikuwa na thamani yoyote hadi kufikia Tshs. 5,000/= kwa ng'ombe na wakati mwingine wafugaji hawakupata hata sauti moja na kuacha mifugo yao kwa sababu isingeweza kurudishwa nyumbani kwa sababu ya kudhoofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ni kwa nini Serikali imechagua Wilaya za Longido na Monduli tu kuwalipa fidia maalum na kuacha Wilaya zingine ambazo nazo ziliathirika sana. Ni kigezo kipi hasa kilichotumika kuja na sera hii ya ubaguzi wa wafugaji? Hivi kazi ya ufugaji ni ya kabila la Wamasai tu? Naomba jibu juu ya vigezo vilivyotumika. Naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kufidia Wilaya zingine zilizoathirika ili kuondokana na dhana hii ya kibaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Manyoni Magharibi linakabiliwa na ukame wa mara kwa mara na mifugo hulazimika kuhamahama kutafuta maji na malisho. Kata za Idodyandole, Ipande, Aghondi, Sanjaranda na Kitaraka zimekuwa zikiathirika sana na tatizo la ukame, njia muafaka ya kukabiliana na tatizo hili ni uchimbaji wa mabwawa na malambo. Naiomba

Wizara hii itusaidie kwa hili, aidha kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa Maafisa Ugani, madawa, majosho bado ni kitendawili. Katika hali ya upungufu huu huduma haitolewi kwa haki, hutolewa kwa upendeleo au kwa rushwa. Naiomba Wizara itathmini tatizo hili kwa kina na ije na jawabu la kukomesha matatizo haya hasa pale Maafisa Ugani wanapokataa kwenda kutoa huduma vijijini na kung'ang'ania kukaa au kutoa huduma mijini. Mara nyingine hata mabucha vijijini yamekosa wataalam wa kukagua nyama na hivyo watu wengine wasio na ujuzi kufanya kazi hiyo *at the risk of the customers*.

Mheshimiwa Spika, majosho bado ni machache sana na vijiji viwili, vitatu, hata vinne hulazimika kuchangia josho moja. Mifugo hulazimika kutumia safari siku nzima kwa ajili ya kwenda kuogeshwa tu. Naishauri Serikali ifanye jitihada za kusambaza majoso kila kijiji ili kazi ya uogeshaji iwe rahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani nyingi kwa Mungu wangu aliyenijalia afya njema hata leo hii nimeweza kuja Bungeni na kuchangia kwa maandishi. Natoa pongezi kubwa kwa Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Wanakamati wa Kamati ya Maendeleo ya Mifugo na

Uvuvi katika kulisemea suala la uhaba wa wataalam katika sekta ya mifugo na uvuvi, kwani ndiyo sababu kubwa ya mchango mdogo sana wa sekta hii katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, sekta hii ni muhimu sana, hivyo, tunaomba Serikali iongeze bajeti ili kuendeleza sekta hii ya uvuvi na wafugaji wanahitaji kupewa elimu ya ufugaji bora na kutafutiwa soko la uhakika la bidhaa zao kusudi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, Serikali isomeshe wataalam wengi zaidi ili waweze kufanya utafiti na kutoa ushauri unaofaa kwa wavuvi na wafugaji, inasikitisha sana kuona wafugaji Mkoa wa Geita ni wengi sana hasa wafugaji wa ng'ombe, hivyo maziwa, nyama na ngozi ingeweza kabisa kuwasaisaidia Wanageita kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwasaidie wafugaji wanaoishi karibu na migodi wapewe tenda ya kuuza maziwa na nyama kwa wawekezaji badala ya kuagiza kila kitu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwa heshima kubwa ombi langu Waziri wakati wa majumuisho aseme lini wafugaji wa Geita watasaidiwa kupata nyama na maziwa vizuri ili wawekezaji hawa wanunue badala ya kuagiza nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji katika Wizara hii. Pamoja na pongezi hizi napenda kuchangia machache hususani ni Kituo cha Utafiti katika Wilaya ya Misungwi kiitwacho Mabuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabuki ina eneo lenye zaidi ya hekta 8000. Eneo hili limeanza kuvamiwa na wenyeji na kusababisha ugomvi wa mara kwa mara kati ya wafanyakazi wa kituo na wanavijiji vizungukavyo kituo hiki. Hii inatokaa na kupungua kwa maeneo ya malisho ya ng'ombe kwa wanavijiji. Ombi langu ni kukiwezesha kituo hiki kuweka uzio katika eneo lote la kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba Wizara iweze kujenga nyumba za wafanyakazi kwani hivi leo wengi wanakaa Kituo cha Utafiti Ukiliguru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile maji kwa ajili ya wafanyakazi na mifugo kwenye kituo hiki ni tatizo kubwa, naomba Wizara iweze kukisaidia kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namwomba Waziri na Naibu Waziri tutembelee kwa pamoja shamba la Mabuki kuona *potential* iliyopo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mungu kwa neema na rehema zake nyingi kwangu. Ni wajibu wangu kutamka *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Spika, mifugo na uvuvi ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu, jambo la kusikitisha ni kuwa Serikali hijaipa umuhimu wowote! Kibaya zaidi ni kuwa pamoja na uwiano wa idadi ya watu na ng'ombe ni 2:1, yaani kila watu wawili ni ng'ombe mmoja. Lakini hata kilo 50 tu za nyama Mtanzania hawezi kula kwa mwaka mzima! Huu ni msiba kwani hata afya za watu wetu zinadorora kwa kukosa protini ya kutosha! Pia ni hivyo hivyo kwa maziwa, samaki na mayai!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iache sasa kuongea tu bila ya vitendo vya kuboresha ufugaji na uvuvi. Serikali itumie Balozi zetu kutangaza nyama ya ng'ombe na mbuzi katika nchi za nje ili tupate masoko. Serikali iimarishe uvuvi wa kisasa kwa kuwahamasisha na kuwasaidia wavuvi ili waweze kuvua samaki wengi kwa soko la ndani na la nje pia.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipambane na uvuvi haramu kwa kuwashughulikia wazalishaji bidhaa za uvuvi haramu badala ya kuwachomea nyavu wavuvi tu. Serikali iimarishe sekta ya maziwa kwa kuondoa urasimu usio wa lazima kwa uwekezaji wa Viwanda vya Maziwa. Pia ipunguze kodi ya usindikaji maziwa ili maziwa yawe bei nafuu na Watanzania wengi wamudu kunywa maziwa ili tupate kuimarisha afya za watu wetu kwa maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa bahari kuu ni utajiri ambao sisi bado tunauona kama kuku anavyoangalia kipande cha almasi! Kuku huiacha almasi na akadonoa pumba, mtama au mchele! Wakati umefika Serikali kuacha mzaha na iweke mkazo na mkakati imara kwa uvuvi wa bahari kuu, rasilimali samaki tuliyonayo ni kubwa sana kwenye bahari kuu, ushahidi ni samaki wa Magufuli. Lakini tunawaacha wavunwe kiholela na majangiri kwa kuwapa posho kidogo watendaji wa Serikali ili wafumbe macho! Hii ni hatari kwa maendeleo na mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi zenye nia njema ya kuja kushirikiana na Serikali katika uvuvi wa bahari kuu, lakini bado Serikali haijakuwa tayari. Hivi ni bora rasilimali samaki iibiwe na majangiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kusisitiza kuwa Serikali itumie balozi zetu kuitangaza nchi yetu na ubora wa nyama za mifugo yetu. Nasisitiza kwa sababu nchi nyingi wanaamini kuwa nyama ya mifugo yetu si salama! Wanaamini kuwa mifugo yetu ina maradhi ndio maana hawataki nyama ya mifugo ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuwasilisha.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa namna ya utendaji wao katika Wizara hii, pia naipongeza Wizara kwa namna ilivyoshiriki katika Maonyesho ya Nane Nane, Dodoma ambapo tuliweza kutembelea banda hilo tulijifunza mengi. Naiomba Wizara kuendelea kuwasaidia wajasirimali wanaojishughulisha na suala zima la miradi ya maziwa, samaki bali pia mtengeneze *incubator* inayotumia mafuta ya taa kwani huyu ni mkombozi kwa wasiojiweza kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magonjwa ya wanyama/mifugo; mbwa ni mnyama ambaye naye hufugwa na wanadamu ama kwa ajili ya ulinzi au hata wengine husema anatumika kama kitoweo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa ambao humpata mbwa yaani kichaa cha mbwa imekuwa ni tatizo kubwa kwa binadamu, mifugo na hata kwa wanyama wadogo wadogo. Ugonjwa huu ambao unapompata mwanadamu au mnyama anaweza kupoteza maisha kama hatapatiwa chanjo ya haraka, kuna taarifa ya kwamba hivi sasa nchini kwetu ugonjwa huu umeshika kasi sana na kwa mujibu wa ripoti za kidunia watu takribani 50-100 hufa hapa Tanzania kutokana na gonjwa hili la kichaa cha mbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa kuwa kupata chanjo ni ghali na upatikanaji wake vijijini ni wa dhiki, Serikali ifanye msako maalum wa kusaka na kuwangoa mbwa wote ambao tayari wameathirika au wanaoonesha dalili za ugonjwa huo, pia iweze

kuwadunga chanjo wanyama wengine wote ambao wameng'atwa na mbwa kichaa kuwajua wale wote ambao tayari wamengatwa kwa upande wa wanadamu ili na wao waweze kupata msaada wa chanjo hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, homa ya mafua ya ndege ni homa ambayo ni mbaya kuliko homa nyingine zote ambapo huambukizwa kutoka kwa wanyama kama ndege kwenda kwa ndege wenzao au kwa wanadamu hasa wanapowatumia kama chakula. Homa hii husambaa kutoka nchi za mbali na kuingia hapa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ituambie imejipangaje kukabiliana na tatizo hili ambalo ni hatari sana kwa raia wetu na hata wanyama wetu. Maradhi yote niliyoyataja yanahitaji kufanyiwa tathmini ile tuweze kujua ukubwa wa maradhi. Naomba Waziri atakapo-wind bajeti yake atueleze ni kwa namna gani Wizara yake kwa kushirikiana na *WHO (Wolrd Health Organization)* wamejiweka tayari iwapo tatizo hilo litatokea.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja, napenda kutoa ushauri kwa Serikali kwa kuipa kipaumbele Wizara hii kwa kuiongezea au kuipa bajeti inayotosheleza ili iweze kukidhi haja ya wananchi wengi walio na kipato cha chini ambao ni wafugaji na wavuvi, kwa bajeti hii ndogo sana, haiwezi kuendesha shughuli za Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kutafuta fedha ya mkopo kwa ajili ya Shirika la Mifugo la *NARCO* ambalo linashindwa kujiendesha kibiashara na kiufugaji kama ilivyokusudiwa. Hivyo, Wizara ione *NARCO* ni sehemu ya Shirika lao, hivyo wasaidie kutafuta fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianzishe Viwanda vya Ngozi ili ngozi yetu iweze kutumiwa hapa nchini na kuongeza ajira kwa vijana wetu na kuthamini biashara ya vitu vinavyotokana na ngozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isimamishe kubinafsisha Kiwanda cha Tanganyika *Packers* kule Mbeya ili kiwanda hiki iwe na ubia baina ya Serikali na *NARCO* kuliko kuuzwa baadaye Serikali iingie hasara ya kujenga kiwanda kingine kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe fedha za kutosha kwa Chuo cha Mbegani ili chuo hiki kiweze kujiendesha na kuzalisha wataalam wengi wa ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ipunguze kodi nyingi za Viwanda vya Maziwa ili wananchi waweze kujiimarisha katika sekta ya maziwa na tuache kuagiza maziwa kutoka Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iangalie kupunguza kodi kwa Viwanda vya Samaki ili wawekezaji waweze kupandisha bei ya samaki aina ya sato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa bahari kuu umekuwa na matatizo makubwa kwa wawekezaji wa

Kitanzania kwa kuwa na kodi nyingi za uendeshaji wa meli za kuvulia, kama ongezeko la bei ya mafuta. Hivyo, kufanya wavuvi wetu kushindwa kukaa kwa muda mrefu baharini na kushindwa kuvuna samaki aina ya Tuna na kufanya meli za kigeni kuvua samaki hawa kwa wingi. Nashauri Serikali iwekeze kwa kununua meli kubwa za kuvulia katika bahari yetu ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Ni vizuri sasa Wizara hii ikafikiria Maafisa Samaki waliopo kwenye Halmashauri kwa mafunzo zaidi, kwani hawa ndio watu walio karibu zaidi na wavuvi, ili waweze kutumia ujuzi zaidi walioupata wa uvuvi uwe wa kisasa na wenye tija kwa wavuvi na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kwani kuna Maafisa uvuvi ambao sio waaminifu, hukusanya nyavu ambazo hazifai na baadaye kuziuza tena kwa wavuvi wengine, hapo ni wazi uvuvi wa nyavu haramu hautakwisha kwa kuwa na watendaji ambao sio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Serikali kusema kuwa, wameondoa ushuru/kodi kwenye zana za uvuvi, lakini wavuvi hawanufaiki na hili wanaonufaika ni wenye maduka kama si wenye viwanda, lakini wavuvi hawanufaiki kabisa na hili. Kwanza wengi wao hawana habari kama wanatakiwa kununua vifaa huku ikiwa kodi imeondolewa. Ni vema basi, sasa Wizara ikafanya kazi hiyo ya matangazo

kwenye redio na hata *TV* ili wavuvi wapate habari nao waweze kutumia nafasi hiyo na waweze pata maisha bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi na *SUMATRA* wamekosa umahiri wa shughuli za uvuvi kwa wavuvi wadogo wadogo, hatimaye kuwalazimisha wavuvi kutumia maboya ya kujiokoa huku shughuli ya uvuvi huo ni kuwa majini wakati wa uvuvi. Wangekuwa na umahiri wa shughuli za uvuvi wasingefananisha uvuvi na vyombo vya usafiri wa abiria na mizigo. Ukizingatia aidha, unapotaka ufafanuzi na maelekezo kunapelekea mara nyingi wavuvi kunyimwa ukaguzi vyombo vyao vya uvuvi na kunyimwa leseni za vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora sasa idara ya uvuvi ikafanya shughuli hiyo ya ukaguzi kuliko kuwaachia *SUMATRA* kufanya kazi hiyo, huo ni kuwadhulumu wavuvi pesa nyingi bila sababu kwani wavuvi ndio wanaolazimishwa kuwalipia gharama ya *Taxi*, chakula na posho nyingine bila ya ufafanuzi wa malipo hayo, wala kuwapa risiti ya malipo hayo. Huo ni wizi wa macho macho, kwani *SUMATRA* hawana bajeti ya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema sasa wavuvi nao wakapata zana za uvuvi na mifugo kwa njia ya pembejeo za uvuvi, kama ilivyo kwenye kilimo ili waweze kupata zana za uvuvi kwa gharama nafuu na pia kwa mkopo kama wakulima kupitia *BMU*.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu watu wote pasipo ubaguzi, nampongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa hotuba yake nzuri ambayo imegusa sehemu nyingi muhimu za maendeleo ya watu na nchi. Pia nampongeza Naibu Waziri kwa kazi nzuri na mashirikiano mazuri anayompa Waziri wake katika kufanikisha majukumu ya shughuli za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze na mchango, nazungumzia Minada, tunayo minada mingi Tanzania ambayo ipo katika mazingira magumu kiafya. Mnadani ni sehemu ya mkusanyiko wa watu wengi ambapo huhitajika huduma za lazima za kibinadamu kama huduma za kula na kwenda haja. Minada mingi shughuli hizi zinapatikana kienyeji sana, biashara za vyakula zinafanywa chini ya miti, ndani ya mavumbi yaliyochanganyika na kinyesi na mikojo ya wanyama. Kutokana na kukosekana vyo, binadamu (watu) wanakwenda haja ovyo, hivyo afya za watu kuwa hatarini.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa kuwa mnada ni sehemu ya biashara na panatozwa kodi kwa mauzo yote. Kwa nini Serikali ishindwe kuweka mazingira bora katika minada yetu. Naomba Serikali iboreshe huduma hizi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wetu wa ng'ombe, mbuzi, kondoo hauzingatii mazingira na kwa kiasi kikubwa ufugaji huu unachangia uharibifu wa

mazingira ufugaji huu unasababisha migogoro ya (ardhi) kati ya wafugaji na hasa wakulima. Pamoja na Tanzania kuwa na sehemu kubwa ya ardhi lakini migogoro kila siku inazidi. Wafugaji wapewe elimu ya ufugaji bora na wenye tija, wanyama kidogo mapato makubwa, ufugaji bora utawawezesha wafugaji kumudu kutoa huduma za malisho, josho na matibabu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia uvuvi, kama Serikali ingepanga mipango mizuri na kusimamia ipasavyo. Uvuvi ungesaidia Taifa letu sehemu kubwa ya ajira kwa vijana wetu na mapato. Wavuvi wengi wanavua kwa vyombo na zana duni. Wanavua uvuvi wa zamani ambao umepitwa na wakati, ndio utakuta pamoja na bahari, maziwa na mito tuliyonayo samaki hawatoshi, vibua na samaki wengine tunanunua kutoka Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii si kwamba Tanzania samaki hakuna, la hasha! Uvuvi duni ndio unachangia Tanzania kukosa samaki wa kutosha. Nashauri Serikali iwe na nia thabiti kuwekeza hasa katika bahari kuu kwa kuwawezesha wavuvi kwa zana za kisasa, elimu bora ya uvuvi wa Sayansi ili wawafikie samaki katika bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, tukifanya haya wananchi wetu watapata ajira na Taifa litapata mapato. Ahsante.

**MHE. DKT. SEIF S. RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kupongeza uwasilishwaji wa hotuba iliyoelezea maendeleo ya mifugo na uvuvi kwa

ufasaha na upana wake, pamoja na juhudi za dhati za kuendeleza mifugo kwa wingi wake na utunzaji wa Kimataifa na uvunaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maamuzi ya Serikali kuachia mamlaka za chini kabisa hata katika ngazi ya Mitaa, Kitongoji na Vijiji kwa nionavyo ni kasoro moja kubwa sana na ambayo inazipa shida mamlaka mbalimbali bila ya sababu kabisa. Mamlaka hizo za chini zinaachiwa kutenga maeneo kwa ajili ya mifugo na kufanya maamuzi ya kupokea mifugo bila ya uwezo wa kusimamia misingi, sheria na kanuni za matumizi bora ya ardhi na hivyo kuwa ni chanzo kikubwa cha migogoro mikubwa nchini kote.

Mheshimiwa Spika,kutokana na kosa hili la msingi lilitufikisha katika hali ya mifugo kuhamia popote na kufanya shughuli za mifugo kila mahali hata ndani ya mashamba na maendeleo yaliyotengwa kwa kilimo ni udhaifu mkubwa katika usimamizi wa shughuli hii muhimu ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yaliyopo Rufiji na kwingineko ni moja ya mifano hai ya kasoro ya kushindwa kupanga kutokea ngazi ya juu kabisa ya Serikali katika kuainisha maeneo ya kutengwa kwa kazi hii, kuweka miundombinu ya kuwezesha wafugaji kubaki katika maeneo yao na wakulima na wavuvi wote waendelee kwenye maeneo yao bila ya mwingiliano wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linawezekana kabisa ikiwa Serikali katika ngazi ya juu itasimamia mipango ya

Kitaifa kutenga maeneo kwa kushirikisha Halmashauri zote nchini, itenge maeneo kwa matumizi ya wafugaji. Kwa kushirikisha wafugaji husika na Taasisi za fedha na utaratibu wa mikopo kulinda maeneo ya wafugaji na kuwekeza katika miundombinu rafiki kwa wafugaji. Hii naamini itapokelewa na kila mtu na itaondoa kero hii ya kupatanisha wafugaji na wakulima na hata kuhatarisha maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuona hali ilivyo mbaya Rufiji na kwa haraka na umakini kulishughulikia hili kwa vile athari zake zitakuwa kubwa kuliko inavyoonekana migogoro ya wafugaji na wakulima, naliona hili litachangia kuongeza athari inayohusiana na bonde na Mto Rufiji kwa pande zote mbili kubwa, nazo ni mafuriko na ukame utakaokandamiza maeneo, mashamba, nyumba na maisha ya watu wengi kuliko miaka yote ya Historia ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikifika hapo na tunaomba Mungu asitufikishe hapo, bado Serikali na hasa Wizara hii itakuwa mmoja wa wanaochangia kutokea kwa hatari hii. Lazima hatua zichukuliwe sasa na kwa haraka kuondoa mifugo katika bonde la Mto Rufiji kama Serikali ilivyokiri kwamba hiyo ndiyo nia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tunaposema kuwawezesha wavuvi, naomba niambiwe ni juhudi zipi zinazofanywa na Serikali kuhamasisha uvuvi Wilaya ya Rufiji ambayo wamekuwa watazamaji wa fursa nzuri ya kuwekeza kwenye uvuvi? Naamini tunahitaji kwa

uwiano uwekezaji wa wastani kwa wavuvi katika Wilaya ya Rufiji kuliko sehemu nyingine na ikiwezekana ufugaji wa samaki kibiashara ungeweza kutufikisha mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia hili, naomba nirudie kimsingi kuiomba Serikali kusimamia changamoto ya uwekezaji wa mifugo na migogoro na wakulima Wilaya ya Rufiji. Naiomba Serikali ibebe jukumu la kusimamia hili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN M. WASSIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini natoa maoni na maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itilie mkazo ujenzi wa viwanda/machinjio ili kupunguza uuzaji wa mifugo, nchi jirani ya Kenya ina viwanda mpakani ili kufaidi ng'ombe wanaovushwa kwa magendo na hata wizi. Napendekeza *NARCO* kwa kushirikiana na sekta binafsi kuanzisha kiwanda/machinjio katika eneo la *EPZ* la Mkoa wa Mara lililoko Bunda. Naomba suala hili lipewe kipaumbele ili ng'ombe wanaosafirishwa toka Simiyu wauzwe na kusindikwa hapo Bunda badala ya Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu biashara ya ngozi; bado hakuna mfumo wa kuridhisha wa soko la ngozi, mfumo uliopo ni wa magendo, Viwanda vya Ngozi

viongezwe badala ya kutegemea kiwanda kimoja kilichoko nje ya eneo la wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi; wakati umefika tutilie mkazo ufugaji wa samaki badala ya wataalam wa uvuvi kuwa wakaguzi, waanze kutoa elimu kwa wafugaji wa samaki.

Mheshimiwa Spika, suala la maji ni tatizo kubwa kwa wafugaji, tuwe na *multipurpose dams* kwa ajili ya mifugo, umwagiliaji na maji ya kunywa.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Taasisi kwa maandalizi ya hotuba ya Bajeti ya 2012/2013 ya mfano wa pekee inayogusa maeneo yote muhimu katika sekta ya mifugo na uvuvi. Pamoja na hayo napenda kutoa ushauri, maombi na mapendekezo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuainisha na kutenga maeneo ya wafugaji; ili kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji, Wizara isimamie uanzishaji na kutenga maeneo ya wafugaji nchini. Eneo la Rufiji ambapo mifugo imeingia bila usimamizi mzuri umechangia migogoro, vita mauaji ya wanachama na mifugo.

EMheshimiwa Mwenyekiti, eneo ni kubwa na Serikali kupitia Wizara inaweza kusimamia kutenga maeneo na kutoa elimu ili kupunguza migogoro. Ni juu ya Wizara kubuni sera, mfumo na kuomba fedha ndani ya Bajeti kuu ili kuweza kusimamia kazi hiyo Kitaifa.

Watendaji waandae utaratibu wa utekelezaji, tathmini ya gharama na kuomba fedha za usimamizi 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mamlaka ya Mifugo; zamani kulikuwepo Mamlaka ya Mifugo *LIDA (Livestock Development Authority)*. Je, mamlaka hii imefutwa? Iwapo imefutwa ipo haja ya kuwa na chombo hicho kwa kuzingatia ukubwa wa eneo la ufugaji na uvuvi nchini. Ni vema ukaundwa upya ili kusimamia ufugaji na uvuvi na sekta mtambuka, pia zilikuwepo kampuni za *DAFCO (Dairy farming Company)* (kampuni ya ng'ombe Tanzania) na *NARCO* ambayo bado ipo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la kukausha samaki Kasanga *Port,* Sumbawanga. Bandari ya Kasanga *Port* kusini mwa Ziwa Tanganyika inakuwa kwa kasi na kuimarisha biashara kati ya Tanzania na DRC – Kongo. Eneo hilo pia ni muhimu sana kwa uvuvi wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo ni kwamba, wavuvi wananchi wa Tanzania wamewezeshwa na wawekezaji toka Zambia na hivyo kuwapa masharti ya kupeleka mazao yote ya uvuvi Zambia na hivyo kuboresha soko la Zambia. Wahisani walisaidia kikundi cha Watanzania kujenga eneo kubwa sana na kuwezesha kukausha samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hilo limekuwa halifanyi kazi kutokana na masharti ya uvuvi kwa wawekezaji wa nje ya nchi. Nashauri Wizara iingilie kati kuona inawawezesha wavuvi wa Tanzania eneo hilo na hatimaye kuwezesha mradi wa kukausha samaki

kuanza na kuendelezwa badala ya kuangalia majengo ya gharama kubwa kukaa bure!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnada wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imeanzisha mnada eneo la Ngomeni/Mkanyageni Muheza, lengo ni kuboresha mfumo wa uuzaji wa mifuko ili kuboresha hali za wafugaji na wafanyabiashara kwa jumla. Nashauri Wizara isaidie kuwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuboresha mnada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya *MACEMP;* miradi hii imekuwa ikisaidia miradi ya jamii katika ukanda wa Pwani. Hata hivyo, kwa mwaka 2011/2012 uwezo wa fedha kwa utekelezaji wa miradi hiyo ya Jamii umepungua sana. Wizara inasema nini juu ya kuendelezwa kwa miradi ya *MACEMP* kwa mwaka wa fedha 2012/2013, na hata utekelezaji wa maombi kwa miradi iliyopo sasa ambayo bado haijapatia fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kiwanda cha Tanga *Fresh* kupata eneo la hifadhi ya ng'ombe wa Maziwa; Wizara ya Maendeleo ya mifugo na uvuvi inatambua yafuatayo:-

(i) Tanga *Fresh* ni kiwanda muhimu kwa uchumi wa Taifa na maendeleo ya wafugaji hasa katika Mkoa wa Tanga na hasa Wilaya za Tanga, Muheza, Mkinga Pangani na Korogwe.

(ii) Tanga *Fresh* imekuwa na tatizo la eneo la kufuga ng'ombe hasa baada ya Serikali kuwataka Tanga *Fresh* kupisha eneo la shamba la Buhuri eneo la Jiji la Tanga ili kuwezesha Tanga *Fresh* kuendelea Wizara inaombwa kusaidia na kuendelea kusaidia Tanga *Fresh* kuwa na eneo la karibu kwa ajili ya ufugaji wa kuendeleza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hifadhi ya maeneo ya bahari kutokana na mabadiliko ya nchi na kiuchumi, Kitaifa na Kimataifa, Tanzania sasa ni lazima iongeze nguvu katika kuhifadhi maeneo tengefu ya Bahari lengo kuu ni:-

(i) Kuhifadhi mazingira.

(ii) Kuwezesha mabadiliko ya kukua kwa utalii katika maeneo ya bahari.

(iii) Kuwezesha kuboresha, kukuza na kuhifadhi mazalia ya samaki maeneo ya Pwani.

Kwa msingi huo na kwa lengo la kukuza uchumi wa Taifa Serikali lazima iwezeshe uwezo wa Wizara kuhifadhi na kuwekeza katika maeneo ya hifadhi ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mahitaji ya wafanyakazi kuboresha sekta ya uvuvi na hifadhi ya maeneo ya Bahari; pamoja na kuwepo nia ya kuwa na chombo/Mamlaka sekta ya mifugo, pia sekta ya uvuvi na hifadhi ya maeneo ya bahari ni lazima iwe na mamlaka yake. Mkakati ulioanza kubuniwa lazima uendelezwe na kukamilishwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo ni lazima kuwezesha sekta na Taasisi zake kuwa na wafanyakazi wa kutosha na kuandaa mfumo wa kuwezesha watendaji wapya kupatikana kabla ya kustaafu kwa watendaji wa muda mrefu ambapo wamekuwepo bila kutolewa kwa ajira mpya. Maombi rasmi yalifikishwa kutoka Wizarani kwenda Idara ya Utumishi, tunaomba utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukusanyaji wa ngozi za ng'ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika. Uuzwaji wake unakuwa ni nchi za nje ambapo Mtanzania hanufaiki na mazao yake yanayotokana na nchi yake na Mtanzania kuendelea kuishi katika hali ya umaskini hata japokuwa ana mifugo mingi lakini kwa sababu hana elimu ya kutosha bado ataendelea kuthamini mifugo kuliko maisha ya familia yake mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na mfumo wa kutoelimishwa vya kutosha watu utakuta hawajui kuthamini mali walizonazo na kujikuta wakiendelea kuwa kero kwa majirani zao wanaoharibiwa mazingira yaani yakiwamo na mazao yao kwa sababu ya mifugo kukaa bila mpangilio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuna ngozi zetu za ng'ombe, mbuzi, kondoo, samaki wakati mwingine hata ngozi za mamba na vijana wetu wanahangaika na maisha, ni lini Serikali itajipanga

kuhakikisha vijana wetu wanatumia malighafi kuwanufaisha watu wengine. Ni lini Serikali itanenepesha ng'ombe za watu binafsi hasa Sumbawanga, Vijiji vya Kwela na Wilaya ya Kalambo ambapo hakuna ranchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kutenga maeneo kwa ajili ya ufugaji kama maeneo ya Jimbo la Kwela na Wilaya mpya ya Kalambo kwani nako Wasukuma wenye mifugo wameshaanza kuvamia katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu ambacho sikielewi katika nchi hii pamoja na kuuza nyama, ngozi na pembe za ng'ombe wetu nazo zinapelekwa wapi? Mbona sijaona jalala la pembe? Pembe za ng'ombe hukusanywa na baadhi ya watu wengi kutokea Kenya kwa ajili ya kwenda kuuzia nchi zinazotengeneza vishikizo. Je, ni lini Serikali itaweka viwanda vya kutengeneza vishikizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana niliulizia juu ya ufugaji wa samaki wa mabwawa katika Mkoa wa Rukwa ambapo nilitaka kujua kama Serikali iko tayari kutoa mafunzo kwa wafugaji wao ili waweze kutunza samaki na kuvua kwa muda muafaka ili kuwa na ufugaji wenye kuleta tija katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niliomba utaratibu wa makusudi ufanyike ili samaki wanaotoka katika Ziwa Tanganyika ambao wanapelekwa Zambia, Burundi na Zaire kwa njia za vichochoro wathibitiwe ili Serikali ipate haki yake ya msingi (kimapato).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Rukwa kuna mfugaji ambaye mifugo (ng'ombe) wake wamekuwa wakishinda kwa kuwa na uzito mkubwa katika sherehe za nane nane na hata nane nane ya tarehe 8/8/2012 yaliyofanyika Dodoma, ng'ombe kutoka Rukwa mwenye uzito wa kilo 900 (mia tisa) alikuwepo na alikuwa mshindi. Ng'ombe huyo ni Dume! Je, Serikali inamweka katika mazingira gani au inamsaidiaje kwa maumbile hayo manene yenye uzito mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hawezi kupanda ng'ombe wa kawaida, je, mna maandalizi gani ya kumtengenezea jike bandia? Je, mbegu zake haziwezi kuwa na soko? Kama mbegu zitapata soko je mwenye ng'ombe atakuwa na hisa gani?.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfugaji huyu mwaka jana alikuwa mshindi na mwaka huu amekuwa mshindi, je, Serikali ya Tanzania imempa tuzo gani na amepewa kipaumbele gani katika jamii? Naomba maswali ya ng'ombe na mfugaji huyu yajibiwe hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Wilaya ya Nkasi ni mdau mkubwa wa Wizara hii kutokana na kuwepo mambo yafuatayo:-

(1) Mtandao mkubwa wa Ziwa Tanganyika.

(2) Ranchi ya Kalambo na vitalu vya wafugaji waliopewa vitalu wakati wa sera za ubinafsishaji.

(3) Shamba la mwekezaji Saafi lililopo Nkundi lenye mifugo mingi na eneo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mambo tajwa hapo juu, wananchi wa Wilaya ya Nkasi hasa Jimbo la Nkasi Kusini wanatakiwa wawe wananufaika na sera zote zinazoendelezwa na Wizara jambo ambalo bado kumfikia mwananchi wa kawaida kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Tanganyika eneo lote la mwambao katika Wilaya ya Nkasi na Jimbo langu la Nkasi Kusini, wananchi wanaoishi maeneo hayo wamebaki maskini wa kutupwa, huku wakizungukwa na utajiri wa asili wa samaki na dagaa, lakini hawawezi kuzitumia rasilimali hizi kuondoa umaskini uliowabobea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ione hili kwa namna ya pekee sana kutoa mikopo kwa wavuvi wadogo wadogo. Iwepo sera kama ile ya pembejeo za kilimo kupata ruzuku na kuwa na mawakala wa kuzisogeza pembejeo.

Mheshimiwa Spika, vile vile pawepo na mikopo midogo midogo na mikubwa yenye mfumo unofanywa na *DADEPs* kudhamini kulipia zaidi ya asilimia 80 ya miradi inayohamasishwa ya uvuvi mkubwa na mdogo.

Uwekezaji ufanyike mwambao mwa Ziwa ili tupate Viwanda ya Kusindika Minofu ya samaki maarufu kama *migebuka* sangara, kuhe na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kuona wavuvi wote wa Wilaya ya Nkasi wakipanga foleni kwenda kuuza samaki wabichi nchini Zambia ambapo wengi hupata hasara kwa samaki wao kuoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwezeshe jambo hili kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi ili kuondoa changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme upelekwe hadi Kirando Mji Mdogo uliopo mpakani kwenda Zaire ili kituo hiki kitumike kujenga miundombinu ya usindikaji samaki na uhifadhi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo Ranchi ya Kalambo inaendelea vizuri hasa baada ya kupata mkopo toka *TIB*. Nilipoitembelea Ranchi hii inaonesha inafanya vizuri na hapajakuwa na changamoto kubwa za kuzuia maendeleo yake isipokuwa nashauri yafuatayo:-

Pawepo utaratibu wa kuzitaka Halmashauri kuchukua mifugo *NARCO* (Kalambo) na kusambaza kwa wakulima ni ajabu kuona Halmashauri za mbali zimekwenda kununua na kusambaza mifugo bora huku Halmashauri ya Nkasi ikiwa haijafanya jambo hilo.

Serikali itoe ruzuku kwa Kalambo Ranchi ili iweze kuboresha na kufikia malengo yake mpaka sasa Kalambo Ranchi inajiendesha yenyewe kama ingepewa ruzuku ingeweza kufikia malengo yake ya

kuanzisha mafunzo kwa wafugaji wa maeneo yale kwa wananchi wanaozunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko limekuwa siyo tatizo kutokana na Saafi kuwa mnunuzi wa ng'ombe wanaonenepeshwa na kuuzwa, tutumie fursa hii kuwapatia ruzuku ili wajenge nyumba za watumishi na ofisi yenye hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchhi wanaonesha kuitikia wito wa ufugaji bora na ambao wanauhitaji kwenye ranchi wawe wanatembelewa ili kubaini na kuwasaidia wale ambao wanalegalega washauriwe na kupewa msaada.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la ardhi katika Vijiji vya Nkana, Sintali, Mkomanchindo na Kasopa. Naomba Serikali irekebishe mipaka ili kuwasaidia wananchi wa vijiji hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifugo nchini, Wizara lazima ije na sera ya ufugaji usioharibu mazingira unaofanywa na wafugaji wakubwa, linafumbiwa macho hasa. Kuna nini? Waziri halioni janga linalosababishwa na sera mbovu za ufugaji wetu. Je mifugo inawasaidia kweli au ni adhabu kwa Watanzania hawa wanaokosa fursa za elimu, wanakosa fursa za afya huku wakiwa na mifugo mingi.

**MHE. ABDULASALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali nampongeza Waziri kwa kuteuliwa tena katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Pamoja na

kuwapongeza kwa hotuba yenu ya bajeti kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013. Nikiwa kama mmoja wa Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge katika Wizara yako, naomba sana kwa heshima na taadhima kuwa suala la wafugaji wa Kitongoji cha Ngaire, wafugaji hao walikusanyika na kuomba kuwa na makazi katika eneo hilo na Serikali na Wilaya ikawaruhusu. Baada ya kupewa eneo hilo wao kwa umoja wao na kuona umuhimu wa elimu kwa watoto wao, walijenga shule ya msingi na makazi yao ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, eneo hilo Serikali ikabinafsisha kwa wawekezaji Watanzania na wafugaji pia. Cha kusikitisha na kuhuzunisha, wananchi hao hawakupewa kipaumbele katika kubinafsishwa kwa maeneo hayo. Naomba katika majibu yake Mheshimiwa Waziri aweze kunipa majivu yatakayoridhisha ili wananchi nao wajue hatma yao.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu ndorobo katika baadhi ya maeneo Wilayani Kilosa. Kuna usumbufu wa ndorobo katika eneo la Mfilisi ambalo Halmashauri ya Wilaya imetenga kwa ajili ya wafugaji, ndorobo ni wengi sana hadi Kijiji cha Madizui kata ya Kisanga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali yetu kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima, eneo hili la wafugaji la Mfilisi wafugaji wengi wamekimbia kutokana na usumbufu wa mbung'o katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaelekeza hapo nyuma nikiwa mmoja wa

wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Kilimo/Maji na mifugo. Naomba sana sana wafuatilie masuala haya kwa faida ya wafugaji katika Wilaya yangu ya Kilosa. Serikali inatilia mkazo suala la ufugaji.

Mheshimiwa Spika,naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hatua zilizochukuliwa na Serikali kwa kuziagiza Halmashauri mbalimbli kutenga maeneo na kuwaka miundombinu kwa ajli ya ufugaji. Hata hivyo taarifa ya Serikali inaonyesha kwamba ni hekta milioni 2.3 tu katika Wilaya 66 ndio zimetengwa kwa ajili ya ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idadi kubwa ya mifugo tuliyonayo Mijini/Vijijini bado kuna haja kwa Serikali kutoa maagizo kwa kila Halmashauri (yenye maeneo) kuhakikisha kwamba katika mipango yao ya matumizi ya ardhi, wanatenga maeneo kwa ajili ya wafugaji. Usisubiri migogoro itokee ndipo tufanye maamuzi. Ni muhimu ikaeleweka kwamba kwa kasi hii ya kuongezeka kwa mifugo kusipokuwa na hatua madhubuti kuna hatari kubwa sana ya kuwa na machafuko! Baina ya wafugaji na makundi mengine ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo kwa madhumuni ya kuweka mazingira bora ya uwekezaji na miundombinu ili kuwa na uvuvi endelevu na wenye tija.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Kawe liko kwenye ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi, shughuli za uvuvi ni sehemu ya maisha ya Watanzania wanaoishi katika maeneo haya (Kata za Kawe, Msasani, Kunduchi na Mbweni). Halikadhalika wavuvi wameunga mkono juhudi za Serikali kwa kuainisha *BMU'S* kwa madhumuni ya kuzilinda na kuzisimamia rasilimali za uvuvi. Hata hivyo, bado wavuvi hawa wadogo wadogo wanaofanya kazi katika mazingira mgumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata taarifa toka Serikalini, ni lini itakuwa na mkakati mahsusi wa kusaidia wavuvi wa ukanda huu ambao wamesahaulika kwa kipindi kirefu?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwamba bajeti yake sasa ikubaliwe. Sekta ya mifugo na uvuvi ni muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi wa nchi hii. Pamoja na changamoto mbalimbali zilizopo, naishauri Serikali iendelee kuipangia fedha za kutosha kwa ajili ya kuwasaidia kwa karibu zaidi. Yapo mambo mengi ya msingi ambayo yanapaswa kutiliwa maanani katika sekta zote mbili za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, changamoto kwa upande wa mifugo kuna ongezeko kubwa la mifugo wakati maeneo ya malisho yakiendelea kupungua. Aidha, ongezeko la watu nchini pia ni kikwazo kikubwa kwani

maeneo ya uzalishaji mali hasa shughuli za kilimo na makazi, zimekuwa zikongezeka kwa kasi kubwa matokeo yake imekuwepo migogoro isiyokwisha baina ya wakulima na wafugaji, migogoro hii imefikia hatua ya kumwaga damu kwa wakulima na wafugaji kupigana hadi kuuana.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia Wizara pamoja na wadau wengine kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uzazi wa mpango ili kudhibiti ongezeko holela la watu. Kwa upande wa mifugo ni kwamba, Serikali iweke vivutio vyenye kuwza kuwashawishi wafugaji kuvuna mifugo yao ama kwa kuwauza mifugo yao wakiwa hai au kwekeza katika sekta ya viwanda vya nyama vitakavyokuwa vinatoa fedha nzuri ili kuwatenga wafugaji waone umuhimu na kuwapunguzia mifugo na kuboresha maisha ya wafugaji kwa kujenga nyumba ya kisasa zaidi na kwa jinsi hiyo kuokoa uharibifu wa mazingira unaokwenda sambamba na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Viwanda vya Ngozi kutachangia sana katika pato la Taifa. Sekta ya uvuvi inakabiliwa na uvuvi haramu kwa kutumia sumu katika maziwa, mito pia uvuvi wa kutumia baruti ni tishio katika Taifa letu kwa sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iiwezeshe sekta ya uvuvi kwa kununua vifaa vya kisasa hasa meli na boti za kurahisisha shughuli za doria kwa lengo la kukabiliana na tishio la uvuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukame kwa maeneo mengi ya wafugaji, limesababisha kuwepo kwa uhaba wa maji kwa ajili ya mifugo. Hivyo, ni vema Serikali ikatenga fedha za kutosha kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa ili kukabiliana na tatizo hili linalowafanya wafugaji kuhamahama na wakati wakifanya hivyo wamekuwa wakilisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima na kuzua migogoro, tuliyokwishaishuhudia.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine naishauri Serikali ione uwezekano wa kuiongezea fedha ya bajeti katika Wizara hii ya maendeleo ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kusimamia vyema utekelezaji wa sera, mipango na mikakati ya nchi katika sekta hii muhimu katika maisha ya Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, wakati nikitambua jitihada mbalimbali zinazofanywa na Wizara katika kuendeleza wafugaji, jitahada hizo hazionekani kupewa uzito kwa upande wa wavuvi. Je, ni asilimia ngapi ya bajeti ya maendeleo imetengwa kwa sekta hii ya uvuvi kwa mwaka 2012/2013. Nipate majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha ya Watanzania wengi wakiwemo wa Vijiji vya Mwambao wa Bahari ya Hindi katika Wilaya za Tanga, Mkinga, Pangani na Muheza yanategemea uvuvi. Ningependa kuelezwa ni

mikakati gani imewekwa ya kuboresha uvuvi katika Wilaya hizi za Mkoa wa Tanga? Ningependa kuishauri Wizara kuwawezesha wavuvi wadogo katika masuala ya nyenzo na vifaa vya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinaonesha kuwa mikoko ina faida kubwa sana. Je, Wizara haioni, sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha parogram maalum ya upandaji mikoko? Ni vyema sasa wananchi wa maeneo ya Mwambao wa Bahari ya Hindi kuwezeshwa kuanzisha Vitalu au mashamba ya mikoko si tu kwa ajili ya kulinda mazingira bali pia iwe ni chanzo cha shughuli ya kujiongezea kipato? Naomba nipatiwe majibu.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhus Sekta ya Mifugo; sekta hii ina changamoto nyingi kwanza kuhakikisha wafugaji wana maeneo ya malisho na maji kwa mifugo yao. Hivyo, Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa kuna mpango mkakati wa makusudi kwa wafugaji na kutenga maeneo ya kutosha ya malisho, maji, majosho na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye kila linalowezekana kuondoa migogoro kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihamasishe wafugaji kufuga kwa tija, pia kuangalia ufugaji wa *Zero Grazing* na hii ikizingatiwa na kusimamiwa vizuri

itamkomboa mfugaji kwa haraka sana - nyama na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe kuwa na mpango wa makusudi kuongeza thamani kwa mazao ya mifugo, nyama, maziwa, ngozi na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kuhusu sera ya mifugo itolewe vya kutosha kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ranchi za mifugo ziendelezwe na wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke bayana Sera ya Mifugo ili kuondoa migogoro ya mara kwa mara hapa nchini kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Uvuvi, naishauri Serikali iwe na mkakati wa makusudi katika kukabiliana na wavuvi haramu katika bahari na maziwa yetu. Aidha, Serikali idhibiti nyavu zisizo na viwango kutumika kuvulia samaki katika maziwa yetu (watengenezaji wa nyavu hizo wadhibitiwe) na nyavu hizo zisiwe sokoni.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLACK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa rasilimali za ardhi, maji na malisho ya mifugo. Kumekuwa na tatizo kubwa la migogoro isiyokoma kati ya wafugaji na wakulima kitu kilichopelekea kupoteza hata maisha kwa baadhi ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa dhati itenge maeneo rasmi ya wafugaji ili wasiingilie maeneo ya wakulima na mifugo hiyo kuharibu mazao ya wakulima na kuwasababishia hasara kubwa ya kukosa chakula, kuishi kwa hofu na kukata tamaa ya kutekeleza mpango wa kilimo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa wafugaji kutokuwa na maeneo wamekuwa wakilisha mifugo yao hata katika hifadhi za Taifa katika mbuga za wanyama kwa kutojua mipaka na haki zao. Serikali iwaelekeza wafugaji na siyo kuwaadhibu bila wao kuelewa tatizo kama vile kupiga risasi mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itueleze inatumia mbinu gani ya kuwapa elimu wafugaji waliozagaa vijijini nchi nzima ili waelezwe mipaka yao ya kuchungia mifugo yao bila kusababisha migogoro? Pia kumekuwa na matatizo kwa wafugaji kunywesha mifugo yao katika visima vya maji, visima vifupi wanavyotumia wanadamu wakichangia na mifugo kama ng'ombe na mbuzi, Wizara inasemaje katika hilo ili kulinda afya za wanadamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa magonjwa ya mifugo, Serikali inapanga mipango mizuri, lakini utekelezwaji utekelezwe kwa kufuatilia mapungufu. Maeneo haya ya kunenepesha ng'ombe yachimbwe mabwawa kwa ajili ya maji ya mifugo tu na siyo kuchanganya na shughuli za binadamu. Kumekuwa na matatizo ya uchafu wa mazingira sehemu wanapolishwa ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanatumia maji ya mabwawa au dimbwi wanapokunywa ng'ombe kwa kufulia nguo na kuweka sabuni mle na uchafu wa aina nyingi vikiwemo vinyesi, mifuko ya rambo na vinginevyo. Hivyo, basi kwa maeneo kama hayo ya malisho ya mifugo na manywesheo ya maji Serikali ipige marufuku binadamu kutumia maji hayo ili kuepusha madhara pande zote kwa mifugo na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la magonjwa ya mlipuko pamoja na mpango mzuri wa Serikali wa kuzuia magonjwa ya mlipuko kwa mifugo. Usimamizi mzuri uzingatiwe kwani mifugo imekuwa ikipata dawa za chanjo, lakini magonjwa yamekuwa yakisakama mifugo kama ng'ombe, nguruwe, kuku, mbuzi na mingineyo kwani madawa mengi yananunuliwa huku yamepitwa na wakati na kutokinga magonjwa kwa mifugo na hatimaye mifugo inapukutika sana kama kuku na ng'ombe na kusababisha magonjwa kuonekana ni sugu. Serikali inatoa elimu gani kwa wafugaji hasa wa vijijini wanaonunua dawa na kuwatibu wenyewe bila kuwa na elimu ya kuchunguza kama dawa zile zimekwisha muda wake?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mathayo David Mathayo, Waziri; Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro, Naibu Waziri; Dkt. Charles Nyamrunda, Katibu Mkuu; Dkt. Yohana Budega, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara na vitengo pamoja na Wenyeviti wa

Bodi na watendaji wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa jitihada kubwa wanazofanya kusimamia utekelezaji wa sera na sheria za sekta za mifugo na uvuvi. Nawatakia baraka za Mwenyezi Mungu ili waendelee kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nathibitisha kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni au mapendekeo yangu katika maendeleo ya mifugo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008/2009, wafugaji wengi katika Mkoa wa Arusha walipoteza mifugo karibu yote kutokana na ukame. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kitendo alichokifanya kwa kutoa kifuta machozi kwa wafugaji wa Wilaya tatu kati ya zile zilizoathirika. Wilaya ya Arumeru ni moja ya Wilaya zenye wafugaji wengi kwani Kata za Oldonyosambu, Olkokola, Musa, Kisongo, Bwawani, Mateves na Oljoro zina sehemu kubwa ya wakazi wao ambao ni wafugaji tu na hawafanyi kazi nyingine.

Kwa masikitiko wao wamebaguliwa kwa sababu waliathirika sawa na wale wa Longido, Monduli na Ngorongoro, ieleweke kuwa Wilaya yangu inazungukwa na Wilaya za Simanjiro, Monduli na Longido hivyo athari zozote za kimazingira kwenye Wilaya huathiri pia Wilaya yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba uhakiki wa athari za ukame kwenye Wilaya ya Arumeru ufanywe upya na waathirika watendewe haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uandaaji wa mazingira ya ufugaji endelevu. Athari za ukame uliotokea mwaka 2008/2009 hadi 2009/2010 kwa wafugaji kwenye Mikoa ya Arusha na Manyara zingeweza kupunguzwa kama Serikali ingechukua hatua zifuatazo:-

Kwanza, kufufua malambo yaliyojengwa enzi za mkoloni na miaka michache baada ya uhuru wa Tanganyika kwenye Wilaya zote za uliokuwa Mkoa wa Arusha. Ziko ishara ya kuwepo kwa maeneo yaliyokuwa malambo huko Kisongo, Oldonyosambu, Musa, Mteves, Ikokola, Bwawani, Mwandet na Oljoro ambayo yaliteketezwa na udongo kujaa hivyo kupotea. Nashauri Serikali kupitia Wizara hii isaidie kufufua malambo hayo ili pamoja na mifugo kupata maji, wakazi wa maeneo hayo watumie maji hayo kuzalisha mboga na kufuga samaki.

Pili, kuboresha malisho, Wizara iwasaidie wafugaji kupanga matumizi ya ardhi kwa kuigawa katika kujenga uzio ili malisho yafanyike kwa mzunguko *(rotation)* ili kupunguza uharibifu wa mazingira na kufanya nyasi kutomalizika kabisa eneo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji wa samaki, vijana wengi nchini hawana ajira kama wangepata ushauri sahihi na kufundishwa kwa vitendo faida za ufugaji wa samaki wangeweza kujipatia ajira

na kipato endelevu kupitia sekta ya uvuvi. Katika Jimbo langu changamoto hii ya vijana kukosa ajira ni kubwa, naomba msaada wa Wizara kuanzishwe mabwawa ya mfano ili kushawishi vijana kuanzisha ushirika wa ufugaji ili kupunguza kero ya ukosefu wa ajira na kugeuka ombaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. TEREZYA L. HUVISA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha mifugo tuliyonayo Tanzania ni hazina kubwa ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia, nawaomba wataalam waendelee kuwahamasisha wafugaji wapunguze mifugo yao kwa kuuza ng'ombe na mbuzi au nyama ili kupunguza idadi ya mifugo ambayo inakuwa kero kubwa kwa sababu ya kuhama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwahamasishe wafugaji kufuga mifugo inayoweza kubebeka kwenye maeneo yao. Tukiacha wafugaji waendelee na ufugaji wa kuhama hama, uharibifu wa mazingira utaendelea kuwa mkubwa na migogoro kati ya wafugaji na wakulima haitakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna wimbi kubwa la wafugaji kuhamia kwenye mabonde makubwa kama Kilombero, Ihefu, Rufiji, Ruvu na kadhalika. Mabonde hayo ni vyanzo vikubwa vya maji

vinavyotegemewa na Taifa hili kwa ajili ya uzalishaji wa maji mijini na vijijini, uzalishaji wa umeme na utekelezaji wa kilimo cha umwagiliaji na ufugaji bora. Kuwaachia wafugaji wavamie maeneo hayo ni kujiletea janga la Taifa la ukaukaji kwa vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara iweke utaratibu wa kuelimisha wafugaji kuhusu uvunaji wa mifugo ili wanufaike na mifugo yao, lakini vile vile kupata elimu ya ufugaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAHRA ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukamatwa na kufilisiwa wafanyabiashara wa zana za uvuvi. Kuna ukamataji kwa wauzaji wa zana za uvuvi madukani na zinapokamatwa huangamizwa kwa kuchomwa moto na wauzaji huchukuliwa hatua za kisheria Mahakamani hata kama uingizaji wake ni kutoka nje ya nchi kupitia katika ukaguzi unaokubalika wa kitaalam wa viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vinapoingizwa nchini kwetu vinalipiwa kodi na ushuru, vipi zana hizo ziwe ni haramu kuuzwa na kutumika kwake. Pia kumkamata mvuvi ikiwa vimeingia kwa kuzingatia viwango vya uingizwaji, ni kwa nini Serikali isipige marufuku uingizaji wa vifaa hivyo vya uvuvi na kukamatwa vifaa hivyo vinapoingia tu nchini badala ya kusubiri kufika madukani au kwa wavuvi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vipi tunawasaidia hawa wavuvi wadogo kuwapatia vifaa vinavyofaa,

ukizingatia kuwa wananchi wanaoishi kando ya bahari au maziwa uvuvi ndio njia pekee ya kuwaendeshea maisha katika mahitaji yao muhimu ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini sera ya uvuvi? Kwa sababu wavuvi wana malalamiko na *SUMATRA* wamekosa umahiri wa shughuli za uvuvi kwa wavuvi wadogo, hatimaye kuwalazimisha wavuvi kutumia maboya kujiokoa huku shughuli ya mvuvi huyo ni kuwa majini wakati wa uvuvi. *SUMATRA* ingekuwa na umahiri wa shughuli za wavuvi wasingefananisha wavuvi na vyombo vya abiria na mizigo. Wavuvi hao wanapotaka ufafanuzi hupelekea kunyimwa leseni na ukaguzi wa vyombo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wavuvi pia wana malalamiko kwa *SUMATRA* wanapohusika na ukaguzi wa vyombo vya uvuvi na wanaporidhika ndipo, Idara ya Uvuvi hutoa leseni. Kwa mawazo ya wavuvi walio wengi, wanaona kazi hii ibakie kwa Idara ya Uvuvi wenyewe ili kuondoa urasimu na usumbufu na utumiaji wa fedha nyingi kwa wavuvi wetu wakati kipato chao kidogo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi katika Ziwa Tanganyika umetokea uvuvi haramu wa kutumia nyavu ambazo hazistahili kabisa kutumika katika Ziwa Tanganyika. Hizo nyavu inasemekana zinatoka Burundi zinakuwa kama zina sumu au zinabadilika, zimetengenezwa maalum kumaliza

samaki Ziwa Tanganyika, zinaharibu samaki kuliko hata kokoro.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa wafanyakazi wachache wa Idara ya Uvuvi pia hawana hata mafuta ya kufanyia doria, inakuwa taabu sana kudhibiti uvuvi huo haramu wa kuangamiza samaki maana haijatokea kwa *makira* kuvua samaki aina ya *migebuka* ila kwa hizo nyavu haramu. Naomba operesheni maalum ifanyike katika Ziwa Tanganyika kabla hawajamaliza samaki, pia kudhibiti wavuvi toka nchi za jirani hasa kutoka DRC na Burundi wanakuja na nyavu haramu.

Mheshimiwa Spika, hata vikundi vya *BMU* vilivyopewa mafunzo maalum havisaidii kabisa kuzuia uvuvi haramu huo, wao kazi yao ni kutafuna pesa zinazotolewa kuvisaidia, mfano, kikundi cha *BMU* cha Kirando hakifanyi kazi ya kudhibiti uvuvi haramu huo. Wao walipewa pesa Sh. 25,000,000 wakanunua *Generator* na eti kusambaza umeme Kirando na kununua vitu ambavyo havina msaada wa kudhibiti uvuvi haramu au hata kuelimisha wavuvi, huo ni ubadhirifu wa pesa za Serikali na kodi ya wananchi wetu. Nimewahi kulalamika hata katika kikao cha Bunge, lakini hakuna chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, hizo Sh. 25,000,000/= kinajinufaisha kikundi cha wajanja tu wachache ambao wanatafuna kodi ya wananchi wetu, hakuna kazi yoyote wanayofanya. Hii ni kama pesa za yatima au sadaka kama kundi linapewa kiasi hicho cha shilingi millioni 25 na hawashughuliki na kudhibiti uvuvi haramu

ambao unaendelea mpaka leo naomba suala hilo lichunguzwe maana mimi ni Mbunge wa Jimbo ambalo Kijiji hicho kipo na siwezi kuona ubadhirifu unatendeka nikawa kimya, itaonesha na mimi nashiriki huo ubadhirifu.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika hoja zifuatazo:-

Mbeya vijijini hususani katika maeneo ya Ilungu, Igoma, Ulenje kuna tatizo la maeneo ya kulishia mifugo. *TANAPA* wamechukua maeneo yote ambayo wafugaji waliyatumia kwa miaka yote. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maeneo mbadala wafugaji hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya kufufua Kiwanda cha Nyama cha Mbeya zimekuwa zikitolewa kila Bunge la Bajeti, lakini bado hatuoni utekelezaji wowote. Je, Serikali imejipanga vipi katika kufufua kiwanda hiki ambacho kilitengwa miaka zaidi ya 40 iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro mingi kati ya wakulima na wafugaji. Je, Serikali imejipanga vipi katika kupunguza migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu imejaliwa kuwa na mifugo mingi, je, ni kiasi gani cha nyama kimewahi kuuzwa nje ya nchi hadi sasa kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inasadikika kuwa na mifugo mingi kuliko nchi nyingine zote katika ukanda wa Afrika Mashariki. Jimbo langu la Kibaha vijijini ni mojawapo ya maeneo yenye mifugo ya kutosha. Tatizo kubwa limekuwa ni namna ya kutumia rasilimali hii kunufaisha wananchi na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka hamsini sasa tangu tupate uhuru na tumeshindwa kufaidi rasilimali hii ya mifugo. Sababu kuu ni kukosekana viwanda vihusuvyo sekta ya mifugo ili kutengeneza samadi na vinginevyo. Wenzetu wa Kenya wana mifugo wachache lakini wamefanikiwa sana kiasi cha kuweza kuwapa wanafunzi wa shule maziwa badala ya uji. Ni lazima tubadilike.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali na Wizara kujizatiti kuwawezesha wananchi hasa Jimboni kwangu ili waone fahari ya kuwa na mifugo hii.

Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi liangaliwe kwa jicho la pekee, sekta ya uvuvi ina manufaa mengi, mfano, kitoweo, biashara na vinginevyo. Serikali iendelee kuweka mazingira wezeshi kwa wavuvi wadogo kwa kuwapa zana bora ili kuepuka kutumia zana haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na naiomba iendelee kupiga vita uvuvi haramu katika bohari na maziwa yetu ili kuwakomesha wanaohudumu ustawi wa uchumi wetu. Wavuvi katika

Jimbo langu la Kibaha vijijini hasa kando kando ya Mto Ruvu nao wanahitaji sana mkono wa Wizara na Serikali ili wainuke kiuchumi na kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niendelee kusisitiza umuhimu wa Serikali kuwatumia wataalamu wetu wa mifugo hasa wa *SUA* kutoa elimu ya namna bora ya ufugaji, elimu inayotolewa katika Taasisi hii isiwe ya kwenye vyeti pekee bali ionekane ikifanya kazi katika maendeleo ya mifugo nchini. Msisitizo uwe kwenye kuondoa dhana potofu ya kila msomi kutaka kukaa Ofisini badala ya kujikita katika maeneo ya ufugaji *(field)*.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wa kuwafidia ng'ombe, wafugaji waliopotelewa na ng'ombe wao kutokana na ukame. Nimwombe akumbuke na maeneo mengine kama Jimbo langu lenye wafugaji wengi. Hata hivyo, nitoe tahadhari kuwa mabadiliko ya hali ya hewa duniani kote umepelekea kudidimika kwa mvua ambayo ni nguzo muhimu kwa ajili ya maji na malisho ya mifugo (majani). Wafugaji hawa bila kubadili mfumo wa ufugaji ni sawa na bure, kwani ukame ukija tena wanaweza kufa. Ni muhimu wafugaji wakahimizwa kubadili utaratibu wa kuwa na mifugo mingi isiyo na tija.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja na kumpongeza Waziri pamoja na wasaidizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 80 au 90 ya mwambao vijijini na kiasi kidogo kilichopo/kinachobaki ndio kipo Manispaa ya Mtwara-Mikindani, lakini cha kushangaza katika ugawaji wa rasilimali za uwezeshaji hasa katika shughuli za uvuvi kupitia *MACEMP* kiasi kinachopelekwa Mtwara Vijijini hakilingani na ukubwa wa eneo la bahari yanayohitaji kuhifadhiwa badala yake fedha nyingi zinapelekwa kwenye eneo la Mjini ambapo ni wananchi wachache sana wanaotegemea bahari kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Vijiji vya Mgau, Naumbu, Kisiwa Pemba Pwani, Msangamkuu, Sinde, Ng'wale, Mkungu, Mayanga, Mahurunga, Mngoji, Nalingu, Mnete, Mnazi, Kilambo, Mpapura, Ndumbwe, Msimbati, Mtandi, Tangazo, Litembe, Mngoji, Imekuwa, Majengo, Msijute na Mbuo ni vikundi vichache sana toka baadhi tu ya vijiji ndio wamenufaika na miradi ya *MACEMP*. Wananchi kutoka vikundi vilivyobaki wanauliza watanufaikaje na huu mradi upo na wao watanufaika au mradi umeshafika mwisho?

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika sekta yenyewe ya uvuvi haijapewa umuhimu unaostahili na hivyo kuifanya sekta hii kuonekana kwamba haina umuhimu wowote juu ya uchangiaji wa pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, laiti Serikali ingetoa umuhimu kwa sekta hii, naamini kwamba, pato kubwa la uchumi

wa nchi lingepatikana kutokana na mazao yatokanayo na bahari ukiwemo uzalishaji au uvuvi wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufugaji wa vifaranga vya samaki unaofanywa sasa, bado umuhimu wa ufugaji huo haujapata baraka stahiki kutoka Serikalini isipokuwa vikundi vingi ambavyo huwa vinafanya kazi hiyo kujitegemea lakini ikiwa Serikali inatilia maanani ufugaji huo itueleze ni vikundi vingapi ambavyo vimepokea misaada ya zana na kifedha za kusaidia ukuzaji wa ufugaji huo wa vifaranga vya samaki.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna bahari na maziwa, ni neema na baraka kutoka kwa Mungu, tuna wajibu wa kuyatumia kwa uzalishaji. Bahari tunayo, mito tunayo, uwezo wa kuzalisha tunao, tunaomba Serikali iwawezeshe Watanzania.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maoni yangu kwa kuchangia katika Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wengi katika nchi yetu wameendelea kufanya ufugaji wa kizamani, hivyo kuendelea kuleta mmomonyoko wa udongo na uharibifu wa mazingira katika maeneo yale yanayotumika kwa ufugaji. Ni kwa nini elimu ya ufugaji wa kisasa isitolewe redioni ili wafugaji wetu waelimike, wafuge kisasa na hivyo wajikwamue kimaisha, kuliko ilivyo sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji walio wengi hasa walioko Morogoro, Arusha, Mwanza na Shinyanga wanafuga mifugo mingi isiyo na malisho bora. Mambo mawili yanajitokeza; moja, mifugo mingi isiyo na malisho bora na pili, wafugaji wenye hali mbaya ya maisha/umaskini uliokithiri mfano nyumba mbovu, lishe duni, mifugo iliyokonda kutokana na wingi wake na malisho mabaya kutokana na ukosefu wa maji ya kutosha na majani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kwa nini elimu isitolewe kwa wafugaji li wajue kwamba madhumuni ya kufuga ni ili kuwa na maisha bora na sio kujilimbikizia mifugo huku hali yao ya maisha ikiwa hairidhishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kwa nini wafugaji wasielimishwe umuhimu wa kuwa na mifugo michache yenye afya nzuri kuliko kuwa na mifugo mingi sana yenye afya mbovu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeandikwa kwa utaalam sana lakini katika hali halisi, sivyo ilivyo, ukifika huko kwa wananchi. Bado kuna matatizo makubwa ya majosho ya mifugo, bado kuna upungufu mkubwa wa wataalam wa mifugo katika vijiji vyetu. Bado madawa ya mifugo yanauzwa katika baadhi ya maduka ya madawa, madawa hayo yamekwisha muda wake. Hakuna juhudi zozote zinazofanywa na Wizara hii za kudhibiti dawa za mifugo. Wafugaji wengi wa kuku mijini wanalalamika kuuziwa dawa za kuku ambazo zimekwisha muda wake wa kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za ufugaji na uvuvi hapa nchini bado hazijapewa kipaumbele katika kuziendeleza ili kufikia viwango vya Kimataifa. Katika benki zetu na vyombo vingine vya fedha vinavyotoa mikopo, hatujasikia hamasa yoyote ya mikopo kutolewa kwa ajili ya wafugaji na wavuvi wetu. Hata wale wanaojitahidi kufuga au kuvua bado upatikanaji wa soko umekuwa sio wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mkazo katika kuendeleza wafugaji na wavuvi kwa kuweka mazingira bora na upatikanaji wa soko ili kuondoa vikwazo vilivyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Wizara hi kama ifuatavyo:-

Kwanza, nampongeza Waziri, Serikali na watendaji kwa kazi nzuri wanazozifanya. Pamoja na pongezi hizo naanza kuchangia kwa kumtaka Mheshimiwa Waziri kuongeza juhudi ili kuhakikisha zao la nyama linauzwa nje ya nchi na kuingizia Taifa pato la fedha za kigeni. Pamoja na kuwa na mkakati huo naomba aje na mkakati wa kuwawezesha wafanyabiashara wanaosafirisha nyama kwenda nchi za Morocco, Mauritania na kwingineko wanaolalamikia ukiritimba na kucheleweshwa kupata vibali vya kuwawezesha kufanya biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kichaa cha mbwa, kumekuwepo na matukio ya watu kung'atwa na mbwa wenye kichaa. Pamoja na mikakati mizuri ya kuwachanja mbwa, bado kuna wananchi wengi ambao hawawachanji mbwa wao na kuwaachia wakizurura barabarani bila kujali usalama wa wapita njia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atoe tamko la kulazimisha wananchi kufunga mbwa hasa nyakati za mchana na kuwachanja kila mara. Hata hivyo, kuwepo na mkakati wa kuwa na mbwa wote wanaozurura mchana au watu hao kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na magonjwa mengi yanayosababishwa na ulaji wa nyama nyekundu. Mfano, magonjwa ya kuumwa na viungo na mengineyo. Hata hivyo, kumekuwepo na ushauri toka kwa Madaktari kwa wagonjwa wao hasa wenye umri mkubwa kuacha au kupunguza ulaji wa nyama nyekundu. Naomba Waziri awaeleze wananchi kama kuna njia mbadala ya kuzitengeneza nyama hii ili kuliwa kwa usalama na kundi hilo. Hii ni pamoja na maziwa ya ng'ombe, mbuzi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na tatizo hilo kumekuwepo na bidhaa hii ya nyama kupanda bei sana kitu kinachofanya Mtanzania wa kawaida kushindwa kula nyama. Kwa mfano, kwa Mkoa wa Dar es Salaam nyama huuzwa kwa Sh. 5,000/= mpaka 6,000/= kwa kilo moja. Naomba Waziri aje na sababu

za msingi za kufanya nyama nchini kuuzwa bei ghali kiasi hicho ikiwa ni pamoja na maziwa, nyama ya kuku samaki na kadhalika.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuchangia bajeti ya Wizara ya Mifugo na uvuvi, sekta hii ni muhimu na ikisimamiwa kikamilifu inaweza kuchangamsha uchumi wa nchi hii kwa kasi kubwa zaidi. Eneo la kwanza ni shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli hizi zimekosa msimamizi makini na hatimaye kutuweka njia panda. Kwanza, uvuvi wa kisasa umewaacha wananchi wazawa waishio visiwani na kando kando ya ziwa kubaki yatima, wameporwa rasilimali zao walizopewa na Mwenyezi Mungu. Hoja hapa, ni Serikali kuja na mipango na mikakati itakayowezesha uwepo wa uvuvi wa kisasa endelevu, lakini kwa wakati huo huo kujenga ustawi wa wananchi wa maeneo asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ni soko la samaki wanaovuliwa kwa zana za kisasa-viwanda, kuna dalili za kuwepo njama miongoni mwa wenye viwanda kupanga bei ya samaki. Baya zaidi ni kuwa bei inayotolewa ni ndogo sana, haikidhi gharama za uzalishaji. Baya zaidi bei hiyo kwa Mwanza ni ndogo kuliko inayotolewa na wanunuzi toka Uganda na Kenya huko huko visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la bei hizi ni kuwa samaki watanunuliwa na viwanda vya nchi jirani. Hatua hii kwa hesabu za haraka itaua viwanda vyetu, kuathiri ajira, kuikosesha Serikali yetu kodi na ushuru

utokanao na shughuli za viwanda hivi. Undani wa hali hii ni kuwa, huenda wenye viwanda kwa upande wa Tanzania hawadhuriki na ustawi wa viwanda upande wa nchi jirani tunazochangia Ziwa. Tafakari ya kina ipelekee Serikali kujiuliza kwa nini wenye viwanda nchini walikuwa wanapendelea kupeleka kontena za samaki Nairobi, Kenya ili isafirishwe nje badala ya ndege kuja Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mbaya zaidi ni pale wavuvi watakapobanwa na ukiritimba wa wenye viwanda kwa kuwapa bei ndogo ilihali wenzao wa nchi jirani wananunua kwa bei kubwa na soko lao ni moja huko Ughaibuni. Hoja hapa ni Serikali kuingilia kati kwa kuwalinda wavuvi wazawa ambao shughuli zao zimebeba mikopo mikubwa nyuma yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu katika kusimamia shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria tumekuwa na utendajji usioridhisha. Uvuvi haramu bado unaendelea na jitihada zia wadau kukomesha tatizo hili hazijaleta mafanikio yanayotegemewa. Tatizo hapa ni kutokuwa na mipango na mikakati sahihi, udhaifu mwingine ni umaskini wa hasa wazawa ambao hawawezi kuvua kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kwa shughuli hizi za uvuvi haramu kunashamirishwa na watendaji wa Serikali kushiriki moja kwa moja au kushiriki kwa kula rushwa kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Dkt. Mathayo alielezwa wakati wa ziara yake Mjini Bukoba. Wapo watendaji wanaoshiriki kula rushwa. Matendo hayo mimi kama Mbunge nimeyapokea toka kwa

wananchi wasio na maslahi. Baya zaidi udhalimu huu umekuwa ukifanyika kwa Afisa Samaki kusimamiwa na Askari Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la ranchi za Kagoma, Misenyi, Kitengule mpaka eneo la Karagwe, chonde chonde Serikali yangu isirudi nyuma ifuate ushauri wa Kamati huru ya mwaka 2010 iliyotumwa na Mheshimiwa Magufuli pamoja na kazi iliyofanywa na Kamati ya wataalam wakiwemo Wabunge, mimi na Mheshimiwa Asumpter Mshama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasoro ya taarifa ya timu ya pili ni kwa sisi Wabunge hatujaiona *final* ripoti tunayonasibishwa nayo. Suluhu ni moja Serikali ihusishe Wizara zote mtambuka katika kuleta suluhu. Hakuna haja ya kutuma kikosi kingine, nyaraka zilizoko mezani zinatosha kumwongoza mtu makini kutoa maamuzi. Hapa dawa ni kwenda haraka sana kwa kuhakikisha kuwa wananchi wakulima na wafugaji wadogo wamepatiwa maeneo yao na wawekezaji wamepewa maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Rutolo, unyama mkubwa ulifanyika kwa mali na utu wa Mtanzania. Serikali inapaswa kuandaa mpango wa kuwarejesha wahanga katika hali ya kawaida. Serikali ijipange kuwaongoza wananchi kwa kuwaelekeza kufuga si kuchunga. Ni dhahiri Rutolo sehemu zake ni nyingi zinafaa kufuga, sawa, basi wawezeshwe wakulima wadogo wadogo kufuga ng'ombe wa nyama na maziwa kwa mtindo wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara makubwa yamefanyika kama nilivyosema. Serikali iende zaidi kwa kuwaangalia kwa jicho la huruma watu hawa katika sekta za afya, elimu, miundombinu na kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namalizia kwa kueleza kuwa Serikali isafishe taswira yake kwa wana Kagera kwa kumaliza migogoro ya ranchi zote mwaka huu.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Waziri kwa hotuba ya bajeti yenye mwelekeo na uwasilishaji mzuri. Pia nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara na watumishi kwa kuandaa Bajeti nzuri na yenye mwelekeo wa kuifungua sekta ya mifugo na ile ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kusimamia kwa umahiri utekelezaji wa sera zinazosimamia maendeleo ya mifugo na uvuvi. Tumeanza kuona mafanikio kadhaa katika ubora wa mifugo na ukuaji wa biashara ya mifugo, nyama, maziwa na mazao mengine ya mifugo na samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana bado Wizara inahitaji iongeze juhudi katika mambo yafuatayo ambayo yanachangia kurudisha nyuma maendeleo ya mifugo:-

(i) Kudhibiti ufugaji wa kuhamahama ambao unasababisha kueneza magonjwa ya mifugo nchini.

(ii) Kuimarisha huduma za mifugo mfano malambo, majosho, madawa, chanjo na kadhalika. Huduma bado haziridhishi kwa maendeleo yenye tija ya mifugo. Hata Maafisa Ugani katika mifugo ni watu adimu na kazi yao haionekani kwa uwazi kwa wananchi wengi.

(iii) Kuimarisha miundombinu ya masoko/minada ya mifugo. Hali litachangia kuhamasisha wananchi kuvuna mifugo yao, kuuza mifugo ndani ya nchi na kuupata bei nzuri kwa thamani ya mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamaji holela wa mifugo umeleta madhara makubwa katika Jimbo langu la Bagamoyo, Bagamoyo limevamiwa na mifugo mingi inayotoka maeneo ya kaskazini ya nchi. Jambo hili limeathiri kilimo katika Jimbo langu na Wilaya nzima ya Bagamoyo kama wanavyofanya katika maeneo mengine, wafugaji hawathamini mimea/mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameendelea na tabia ya kuingiza mifugo katika mashamba ya wakulima. Hata shambani kwangu, mifugo ilivamia wiki chache zilizopita na kuharibu mazao! Jambo hili linalalamikiwa sana maana, nami kama Mbunge nashindwa kujua nichukue hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuchangia ukosefu wa chakula kwa wananchi wa Jimbo langu, tabia hii pia inapelekea mahusiano mabaya kati ya wananchi wa nchi moja. Wizara lazima itoe

kipaumbele katika kutatua tatizo hili kwa maendelo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri. Aidha, nawapongeza wao pamoja na watendaji wao wote kwa hotuba nzuri, nawatakia utekelezaji wenye mafanikio wa bajeti ya 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi, naomba kuzungumzia yafuatayo kwa nia ya kuboresha:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Migogoro ya wafugaji na wakulima katika Wilaya ya Morogoro vijijini, nashauri Wilaya isaidie kutengeneza mfumo wa *ranch* ndogo ndogo na hizi *ranch* zijengwe lambo la kunyweshea wanyama wao. Aidha, naomba Serikali idhibiti uhamiaji holela wa wafugaji kutoka Mikoa yenye ng'ombe wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahamiaji wamekuwa wengi katika maeneo ya mapori tengevu na Selous hadi kusababisha wanyama kama tembo kukimbia na kuvamia makazi ya binadamu pamoja na kuharibu mashamba. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili kwamba, wana mkakati gani wa kudhibiti nchi hii mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uboreshaji wa wanyama wadogo hususani kuku wa kienyeji katika

maeneo ya vijijini. Inasikitisha sana kuona kuku wengi wanakufa kutokana na magonjwa yanayozuilika kwa kutumia chanjo. Changamoto kubwa hapa ni ukosefu wa chanjo, ukosefu wa elimu kwa wananchi na watendaji kutotimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iwezeshe upatikanaji wa chanjo na pia Maafisa mifugo wahimizwe wajibu wao wa kutoa elimu na kuchangia kuku kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba, ufugaji wa kuku wa kienyeji ni fursa kubwa ya kuondoa umaskini miongoni mwa wananchi hususan Morogoro Vijijini. Aidha, wananchi wengi Morogoro wanapenda kufuga sungura, lakini tatizo ni upatikanaji wa sungura, elimu ya ufugaji pamoja na soko la uhakika. Nawakumbusha sana wataalam wa Wizara hii kumuunga mkono Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki na kuhamasisha ufugaji wa sungura kwa ajili ya kitoweo na biashara.

Mheshimiwa Spika, tatu, soko la maziwa katika eneo la Tarafa ya Ngerengere. Wananchi wengi wa eneo hili wana ng'ombe wengi, lakini soko la uhakika kwa ajili ya maziwa halipo, naomba Serikali isaidie mkakati wa kusindika maziwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, fursa ya kufuga ng'ombe wa maziwa katika maeneo ya Tarafa za Mkuyuni, Mikese na Matombo. Maeneo haya yanayo fursa kubwa ya kufuga ng'ombe wa maziwa kwani

wananchi wanapenda kunywa maziwa lakini hayapatikani. Naomba Serikali ianze mradi wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa mtindo wa *zero grazing* kwa sababu majani ni mengi sana.

Mheshimiwa Spika, tano, ufugaji wa samaki katika Tarafa za Mkuyuni na Matombo; wananchi wa maeneo haya wapo tayari kufuga samaki lakini wanaomba elimu, mwongozo na vifaranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili kuna maji mengi kwa mwaka mzima, hivyo mradi wa samaki utaongeza uchumi pamoja na kuboresha lishe. Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini Serikali itaanza mradi huu ambao wananchi wanasubiri kwa ari kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuijulisha Wizara kwamba, katika Wilaya ya Morogoro kunajengwa Bwawa la maji la Kidunda. Naomba kujua Wizara hii imejipangaje kutumia bwawa hili kuboresha ufugaji wa samaki kwa ajili ya kuondoa umaskini pamoja na kuongeza ajira kwa wananchi wa Kidunda? Naomba iwepo mipango endelevu ya kuwaelimisha kuhusu uvuvi bora pamoja na kuwapatia nyenzo ambazo hazitaharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nikiamini kwamba Mheshimiwa Waziri atajibu hoja zangu.

**MHE. DKT TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa hotuba ya bajeti ya Wizara yenye mipangilio makini. Hata hivyo,

napenda kusisitiza Serikali kuchukua juhudi za makusudi kutenga maeneo kwa ajili ya mifugo kwa kupanga matumizi bora ya ardhi ya vijiji. Kutofanya hivyo sekta ya mifugo itaendelea kunyang'anywa maeneo kwa matumizi mengine kama vile kilimo cha mazao na makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaona tayari baadhi ya mashamba ya *NARCO* wakipewa wananchi kuweka makazi vile vile kwenye vijiji vingi, muda wa kilimo ukifika ng'ombe wanakosa mahali pa kulishia. Hakuna mtu atakayewaongoza wanavijiji kutenga maeneo bila mwongozo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana elimu ya ufugaji samaki itiliwe mkazo na kwa Jimbo langu la Busega, naomba ipatiwe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aliwahi kujibu swali langu Bungeni kuwa Kituo cha Madawa bora cha Igalukilo kitafufuliwa na kuwa kingewekewa uzio. Hata hivyo, hadi sasa hakuna kinachoendelea, naomba Waziri uwe unafuatilia ahadi zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Busega tuna bahati ya mnada wa mifugo wa Mwasamba ambapo wanunuzi huja kununua mbuzi toka nchi jirani ya Kenya. Naomba mnada huu uingizwe kwenye mpango wa kuboresha minada ya mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kuwa mmoja wa wachangiaji katika Wizara hii. Nawapongeza pia viongozi wote wa Wizara hii akiwemo Waziri na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara na Wakurugenzi wote. Pamoja na ufanyaji kazi mzuri wa Wizara hii, bado kuna chagamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ili Wizara ifanye kazi zake kwa ufanisi na wananchi wafugaji waone kazi hizo na kuwapa matumaini ndani ya sekta hii, ni lazima ifanye kazi na Halmashauri zetu kwa karibu sana na kuhakikisha zinafanya kazi ambazo Wizara imezipa kipaumbele. Kwa maana hiyo, Wizara ni lazima izisimamie Halmashauri kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu tumekuwa na maneno mengi mazuri na takwimu nyingi kutoka Wizarani ambazo hazina msaada wowote kwa wafugaji wadogo na wa kati na ndio walio wengi ndani ya nchi hii. Leo nachangia kwa maandishi, lakini naomba Mungu mwaka ujao nione mabadiliko na nipate nafasi ya kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimoja kinachonikera ni majosho na mabwawa (malambo) katika Wilaya mpya ya Gairo. Katika Wilaya hii ya Gairo, kuna wafugaji wengi wadogo, lakini hakuna majosho wala malambo. Hasa katika Vijiji vya Chogoali Ndogomi, Idibo, Talagwe, Mkalama, Meshugi, Majawanga na Leshata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu wakati Wilaya ya Kilosa kabla haujagawanywa kuwa na Wilaya mbili

za Gairo na Kilosa ilitolewa tenda kujenga lambo katika Kijiji chenye wafugaji wengi ni Kitaita. Lambo hilo lilichukuliwa na maji hata kabla ya kazi hiyo kwisha, pamoja na juhudi zangu zote mpaka leo hakuna matumaini yoyote ya kumaliza lambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi hasa toka Kilosa wajue kuwa Gairo imekuwa Wilaya, pamekuwa na upendeleo wa eneo la Wilaya ya zamani kwa Miradi yote na kuiacha miradi yote ya Wilaya mpya. Je, Wizara hii pamoja na sisi kama Madiwani ndani ya Wilaya zetu, lakini si wataalam, wanayaonaje haya yakifanyika kwa nia ya kudhoofisha miradi ya Wilaya mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba Wizara ifahamu na iweke upendeleo katika Wilaya mpya na ijue kuwa miradi yote iliyotolewa katika kipindi cha miaka mitatu ya nyuma toka Gairo ijulikane Wilaya itakuwa haijafaidika na mradi na hasa malambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuunga mkono hoja ya hotuba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa majumuisho ya hotuba kwa niaba ya wananchi wa Korogwe Mjini kupata majibu ya uvamizi wa wafugaji wanaoharibu mazao na kuleta hasara kwa wakazi wa Lwengera, Kwamsisi, Kwamdulu, Ngombezi na Kwamugumi vitongoji vilivyo Korogwe Mjini. Aidha, Serikali itujibu

wakazi wa Korogwe je, imeshindwa kudhibiti kiburi cha wafugaji wahamaji? Kiasi cha kupelekea mauaji ya raia pale Lwengera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaelekea kauli za Serikali hazitekelezeki je, tuwaambie nini wakazi wa vitongoji hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika Wilaya ya Korogwe ni eneo mahsusi la mnada wa mifugo kwa miaka mingi pamoja na Korongwe kuwa na idadi ndogo ya makazi ya wafugaji, kuna changamoto ya josho na machinjio. Je, ni lini Wizara kupitia miradi ya *DADPs* itajenga josho pale Korogwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Taifa hili sasa lina vijana wengi Mjini na Vijijni. Je, nini sera ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu kutoa elimu ya ufugaji na uzalishaji kwa vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, si vema sasa Wizara kuwa na mpango kazi na mkakati wa kutoa elimu ya uvuvi, ufugaji na uzalishaji mazao yatokanayo kwa kuajiri wataalam wa kutosha kila Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mungu kwa kuniweka hai hadi leo ninapofikia kupata fursa ya kutoa mawazo yangu juu ya bajeti hii ingawa ni kwa maandishi. Nachukua nafasi kubwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na jopo lake zima linalompa ushirikiano mkubwa uliomwezesha

kutoa hotuba nzuri na hata utendaji wa ufanisi wa kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza pamoja na Wizara kwa juhudi zinazofanyika za kutoa mafunzo ya Mifugo na Uvuvi pia utaratibu wa kutoa mafunzo hayo kwa wataalam na kwa wafugaji na kwa wavuvi pia. Hii inaonesha ni kwa jinsi gani ilivyo makini kwa kazi yake. Vile vile nazidi kuipongeza Wizara kwa hatua ya kutoa vitendea kazi kwa wahusika na wakufunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi iliyopita tumekuwa na wataalam hewa wa vitengo hivyo hasa Vijijini hata katika Kata, naamini hata Wilayani pia. Nasema hivyo kwa vile hapakuwa na vitendea kazi ikiwa ni pamoja na madawa ingawa sijahakikisha kama uwepo huu wa vitu hivyo umeshafikishwa katika maeneo niliyoyataja. Kama bado kama ninavyojua basi Serikali ione haja na umuhimu wa kupeleka huduma hiyo haraka kulingana na taarifa iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na utaratibu wa Serikali au sijui ni *NGOs* fulani zilikuwa na utaratibu au mpango wa kopa ng'ombe au mbuzi ulipe mbuzi. Mpango ule ulikuwa ni mzuri kwani ulikuwa unamwezesha mwananchi wa hali duni kupata mfugo kwa urahisi, sijui ni kwa vipi mpango ule hauonekani siku hizi kama kuna unakoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ningeomba uendelezwe kwa hasa sehemu zile ambazo ufugaji na mifugo ni haba kama vile Mikoa ya Kusini maana

Mheshimiwa Rais katika kampeni alihimiza na kuhamasisha wananchi kula nyama na kunywa maziwa, jambo ambalo kwa kuwa mifugo haipo ya uhakika ya kukidhi mahitaji, ni vigumu kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile itakuwa ni jambo la busara endapo Serikali itatoa mikopo ya kuwawezesha hasa vikundi ili wajenge mazizi ya kisasa na mbegu za ng'ombe na mbuzi wa kisasa. Pamoja na madawa pia katika kufanya hivyo kutawawezesha wananchi wengi kujiinua kiuchumi. Pia hiyo azma ya Rais kutimizwa kwani nyama na maziwa vitapatikana kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi ni muhimu katika uchumi kwa wavuvi ila sekta hii bado haijatazamwa vizuri kwani kwa muda mwingi wavuvi walikuwa wanavua bila utaratibu mzuri. Serikali hivi karibuni imeamua kuwakamata kwa ule uvuvi haramu, jambo ambalo ilibidi wapewe elimu mapema kabla ya hatua inayochukuliwa. Kwa hivi sasa Wizara ilivyofungua vyuo, ni vizuri kwani watafanya kinyume wakati watakapotambua sheria inayotakiwa katika uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo Viwanda vya Kusindika minofu ya samaki ni vichache. Ingekuwa ni vema miji mikuu iliyopo kando ya Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu vijengwe viwanda hivyo ili ajira pia zipatikane kwa vijana na ikibidi wapewe wawekezaji ili kufanikisha hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya uvuvi itolewe zaidi hasa vijiji vyote vilivyo kando ya bahari na mabwawa, kwa vile watu hawa tangu enzi za mababu mashamba yao ni maeneo hayo. Sasa hali ya kuwapa wawekezaji bila kutengewa eneo au maeneo ya wao kupata samaki kunapelekea kufanya uvuvi haramu. Hivyo, Serikali iliangalie hilo kwa makini na kwa manufaa ya umma huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kuchangia hotuba ya Wizara ya Mifugo kwa kutounga mkono hoja. Nina sababu ya kutounga mkono hoja baada ya kutoridhishwa na mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina mifugo mingi, lakini haileti tija kwa wafugaji na hata kwa Serikali. Taifa limeendelea kuwa na wafugaji wengi wanaofuga kienyeji kwa kuhamahama bila kuzingatia ufugaji na kisasa wa kuwa na Ranchi. Serikali ina mpango gani wa kuwa na ranchi za kutosha kwenye maeneo yenye wafugaji wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ndani ya Jimbo langu kulikuwa na ranchi ya Ngongo ambayo imeuawa bila maelezo ya kina na sehemu ya ranchi imejengwa sekondari. Kwa kuwa kwenye ranchi hiyo kulikuwa na mtambo wa kuzalisha chakula cha mifugo, haijulikani baada ya kufa kwa ranchi mashine hizo za uzalishaji chakula cha mifugo ziko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro kati ya wafugaji na wakulima kutokana na ufugaji wa kuhamahama maeneo mengi yanakabiliwa na ukame na mmomonyoko wa udongo inayosababishwa na uwingi wa mifugo. Serikali imekuwa ikiwahamisha wafugaji na kuwapeleka kwenye maeneo mengine, kwa mfano, kundi la wafugaji wamepelekwa maeneo ya Kusini kama vile Rufiji. Wafugaji hao wamesababisha mapigano baada ya kuingiza mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepuka mapigano ambayo husababisha uharibifu wa mali na hata vifo ni budi Serikali ikaandaa mpango kabambe kuelekeza ufugaji wa kisasa na kuwaandaa kwa mafunzo wafugaji ili waepuke ufugaji wa kuhamahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa za mifugo yetu hapa nchini inatoa malighafi kama ngozi, pembe, mifupa na kwato, pamoja na kuhamasisha uwekezaji kwa Viwanda vya Ngozi. Serikali haioneshi kwenye hotuba ya bajeti popote inapozungumzia uwekezaji kwenye viwanda vinavyoweza kutumia malighafi ya pembe za ng'ombe na mbuzi. Ambazo zinaweza kutumika kutengeneza vifungo vya nguo. Pia kwato kwa viwanda vya gundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatakiwa iwe makini inaposimamia ufugaji wa nguruwe, hata kama Mheshimiwa Waziri amefurahishwa na ongezeko lao ni vyema afahamu kuwa kuna jamii hairidhishwi na mnyama huyo. Hivyo, wanaofuga wawe waangalifu ili kuepuka mapigano ya wafugaji na walaji wa nguruwe

dhidi ya wale wasiofuga na kula nguruwe kwa mujibu wa imani ya dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi haramu kwa kutumia zana zisizofaa bado unaendelea kwenye maeneo ya maziwa na baharini. Sababu kubwa ni wavuvi kukosa uwezo wa kulipia gharama za zana za uvuvi, kuwa na vyombo hafifu kama mitumbwi ambavyo haviwezi kuwapeleka mbali ili waweze kuvua samaki watakaoleta tija kwa wavuvi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri hazina boti za kisasa za doria jambo ambalo husababisha matumizi ya silaha za moto na kusababisha vifo kwa kushindwa kuwakamata wavuvi haramu pindi wanapowabaini. Nina mfano wa wananchi tisa waliouawa kule Geita eti kutokana na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri imezungumzia Viwanda vya Samaki, Kanda ya Ziwa, lakini ukanda wa Pwani hakuna pamoja na uwingi wa samaki wa baharini ambao huishia kuibiwa na Serikali ikiwa haina tija kwa samaki hao. Wizara inatakiwa kuboresha vikundi vya wavuvi kwa kuwapatia boti na meli za uvuvi na kuhamasisha wawekezaji ili wajenge viwanda vya samaki kwa maeneo ya Pwani ya Mikoa ya Kusini ikiwemo Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zipatiwe boti za doria na wahimizwe kutoa leseni za uvuvi kwa wavuvi wadogo bila urasimu kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Mathayo kwa kazi nzuri anayofanya katika Wizara hii. Pia nampongeza Mheshimiwa Ole Nangoro Naibu Waziri kwa ushirikiano mkubwa sana. Bila kuwasahau watendaji wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa pale ambapo nimehitaji msaada kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ni Wizara muhimu sana hasa kwa maeneo ya Kanda ya Ziwa ambapo wananchi wake walio wengi hutegemea uchumi wao kutokana na mifugo na wengine kutegemea shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti nilioufanya unaonesha kuwa Mkoa wa Mwanza na Geita ikiwa Wilaya ndani yake unaongoza kwa kuwa na mifugo wengi ikifuatiwa na Mkoa wa Shinyanga na Mikoa mingine. Pamoja na kuongoza kwa kuwa na mifugo mingi hasa ng'ombe, lakini Mwanza, Shinyanga hakuna Kiwanda cha Nyama. Matokeo yake wafugaji wanauza mifugo yao kwa bei ya chini sana kwa kuwa hawana soko la uhakika la kuuzia mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, naomba Serikali iweke mkakati madhubuti wa kuanzisha Viwanda katika Kanda ya Ziwa ili kuwezesha kuwa na soko la uhakika kwa mazao ya mifugo. Vile vile Serikali iwekeze katika kuimarisha majosho ya mifugo na mabwawa ya maji ili kuwasaidia wafugaji kuboresha ufugaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uvuvi katika Jimbo la Busanda ninavyo vijiji vilivyoko kandokando ya Ziwa Victoria ambavyo ni Vijiji vya Bukondo, Kageye, Kasanghwa na Nungwe. Wananchi katika vijiji hivi wanategemea sana shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto yao kubwa ni mtaji. Ili kuimarisha sekta ya uvuvi ni hakika wananchi wanahitaji kuwezeshwa katika kupata vifaa vya uvuvi. Naomba Serikali iweke kipaumbele katika kuwawezesha wavuvi hasa wadogo ili waweze kuendelea zaidi na kuimarisha vipato vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Waziri au Naibu Waziri afike Jimboni kwangu Busanda ili ajionee hali halisi ya wavuvi wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa ya kuchangia hoja katika Wizara hii muhimu kwani ndio uti wa mgongo wa wananchi wengi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa jambo la kawaida sasa, mambo mengi sana kama Mbunge wa Jimbo nimeshauri, kuhusu suala la Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kugawa upya maeneo kwa wafugaji wa asili katika vijiji na vitongoji vyetu. Lakini mpaka sasa hakuna lililofanyika kiasi

kwamba sasa wafugaji wamepoteza imani kwa Wizara hii, pia hata kwa Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuwa ni jambo la kawaida kuona wafugaji hawa wakihangaika kupata maeneo mazuri ya kufugia wakati wafugaji ambao si wazawa wakizawadiwa maeneo makubwa ya misitu ya hifadhi au maporomoko ya akiba. Wakiishi humo kwa raha na neema nyingi wakati wazawa wanahangaika na mifugo yao katika maeneo finyu ndani ya vitongoji na vijiji vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona hata Kamati zinazoundwa kushughulikia suala hili hatuoni maamuzi na utekelezaji wa dhati unaofanywa na Serikali katika mapendekezo yanayotolewa na Kamati hizi ili kurekebisha adha hii kwa wananchi. Kamati zinazoundwa, aidha zinaishia mikononi mwa hawa wageni wabadhirifu wa maeneo na pia mijini pasipo kwenda vijijini na kuwafikia hawa walengwa au wahanga wa maeneo ya malisho!

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kila mara Kamati hizi zinapotembelea maeneo haya haziwakutanishi wakulima na wafugaji au Wabunge wa eneo husika kwani Mbunge kama mwakilishi wa wananchi lazima ayajue maeneo ya wananchi wake. Mara nyingi Kamati hizi haziwahusishi Wabunge wala kuwataka Wabunge maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa rai kuwa sasa Serikali ione umefika wakati suala la migogoro ya wakulima na wafugaji linapata suluhu mara moja. Suala hili ni suala mtambuka na kuna kila sababu ya

kulifanyia kazi kwa haraka mno. Suala la wazawa kunyimwa fursa hii na kuzawadiwa kwa wageni ambao hawana uchungu kabisa na ardhi yetu, hawana uchungu kabisa na wazawa hawana chochote cha kupoteza kwa yale wanayoyafanya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona mpaka baadhi ya wananchi wanafanywa kuwa watumwa, wanapigwa na wafugaji wasio wazawa na kusababisha vilema vya miili yao. Wapo wazawa wamepoteza maisha na kesi kuishia kutojulikana. Jambo la kusikitisha mbona Bunge hili halijawahi kupata taarifa ya Watanzania wanaofugia nchini mwao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Watanzania wanaofugia Rwanda, Watanzania wanaofugia Burundi au Uganda? Hivi iweje leo kwetu kuwa ndio sehemu ya malisho na sehemu ya kunenepesha mifugo yao wakati faida ya mifugo hiyo na mazao yatokanayo na mifugo hiyo yanafaidisha nchi zao na watu wao! Haikubaliki hata kidogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Waziri mwenye dhamana, sasa ni muda muafaka kwake na watendaji walioko chini yake kutoka ofisini na kwenda kushughulikia suala hili kwa uhalisia wak, vinginevyo watakuwa wanazidi kuchochea bomu linalotegemea kulipuka kwa kulisogezea moto wa petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ya Mkoa wa Kagera isimame imara na iwajibike ipasavyo nina imani ufumbuzi utapatikana na amani itapatikana.

**MHE. AGGERY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wanachi wa Jimbo langu la Siha naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza wenzetu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara na hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Nampongeza pia Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri anayoifanya na hivyo kuwa msaada wa hali ya juu kwa Mheshimiwa David Mathayo David kama yeye mwenyewe alivyokiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Siha ni Wilaya ya Mifugo, naamini Wizara itatukumbuka hasa katika eneo la malambo na majosho ya kuoshea mifugo. Tukiangalia takwimu Wilaya ya Siha ni miongoni mwa Wilaya ambazo mchango wake wa mazao ya mifugo ni wa hali ya juu. Aidha, tunaomba tusaidiwe kujenga eneo ambalo litatumika kama eneo la mnada ili Halmashauri ya Wilaya ya Siha iweze kunufaika kutokana na mapato yatokanayo na mauzo ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imekuwa kila mwaka bajeti yake inapungua na kuifanya Wizara hii isitekeleze majukumu yake kisawasawa. Naiomba Serikali ielekeze nguvu zake nyingi kuhakikisha tengo la Wizara hii linapata fedha nyingi zitakazowezesha Wizara hii kuwasaidia wafugaji walio wengi hasa ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wakiwezeshwa kwa kuandaliwa miundombinu muhimu kama maji kwa kuwachimbia mabwawa malambo na majosho kunaweza kuwawezesha kuwasaidia sana hawa wafugaji wengi wanaohamahama kwa kufuata malisho na maji. Ni vizuri Serikali ikaliangalia hili kwa umuhimu wa aina yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wakulima na wafugaji, isipoangaliwa kwa makini tutaleta vita kubwa kati ya wakulima na wafugaji, kila kundi lina umuhimu wake katika nchi hii. Ni vyema Serikali ifanye mchakato wa haraka wa kutenganisha maeneo ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya uvuvi, uvuvi ni eneo muhimu sana katika nchi yetu kwani tuna bahati ya kuwa na maji ya mito, maziwa na bahari ambavyo vyote tumezungukwa navyo. Ni vyema Serikali ikajikita kuhakikisha inaandaa kujenga mazingira ya wavuvi wanaotumia zana ndogo za uvuvi na duni ambazo haziwasaidii wananchi walio wengi wanaishi kando kando ya Bahari na Maziwa na Mito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwasaidie wavuvi hawa ambao watasaidia kukuza kipato cha Taifa na kupata fedha za kigeni na kuleta ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi katika Ziwa Tanganyika, katika eneo la uvuvi ambalo halijapewa kipaumbele ni Ziwa Tanganyika kwani hakuna mradi mkubwa ambao unafanya kazi wala kuwawezesha wavuvi walio katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma kuwasaidia wavuvi wa Ziwa hili la Tanganyika ambalo ni ziwa lenye kina kirefu kiasi kwamba kama hawajawezeshwa na Serikali kwa kupata dhana bora za uvuvi zinazofanana na mazingira ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuishauri Serikali iandae chombo cha doria katika eneo la Ziwa Tanganyika ambako usalama wa wavuvi sio salama kutokana na kuwepo kwa mwingiliano wa mpaka na nchi jirani. Wavuvi wetu wa Ziwa Tanganyika wamekuwa wakinyang'anywa nyavu na mitumbwi na maharamia. Ni vizuri Serikali ikatoa majibu vipi kitafanyika kuwaokoa wavuvi hao kuwa kama watoto yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja hii baada ya kupewa majibu.

**MHE. ABAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri natoa pongezi zangu binafsi kwako

wewe na Naibu Waziri pamoja na watendaji wako wote kwa kazi nzuri mnazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hoja moja katika Jimbo langu la Temeke, nina wavuvi wengi kuanzia Kurasini maeneo ya Shimo la Udongo Kijiji cha Wavuvi na maeneo ya Mtoni, lakini Mheshimiwa Waziri wavuvi hao wamesahaulika, sasa nataka uniambie wakati ukijibu hoja wavuvi kwa miaka saba yangu niliyokuwa Bungeni walisaidiwaje na sasa watasaidiwaje?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTHER L.M. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Waziri kwa hotuba yake Dkt. David Mathayo David aliyoisoma hapa Bungeni. Pili, namshukuru Waziri kwa kusema Kiwanda cha Nyama, Mkoa wa Shinyanga tayari kimeshaanza kufanyiwa ukarabati. Hiyo itakuwa ni njia pekee ya kuwainua kiuchumi wafugaji wa Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kuchangia katika Mkoa wa Simiyu, asilimia kubwa wananchi wa Simiyu ni wafugaji. Wafugaji hao wanapata shida sana kuhusu soko la kuuzia ng'ombe, wanunuzi wakija kununua wanawanunulia kwa bei ya chini sana. Ng'ombe ananunuliwa kwa bei ya sh. 300,000/= wakati Dar es Salaam ng'ombe huyo anauzwa kwa bei ya sh. 800,000/= huoni kwamba wafugaji hao wanapata hasara na kuwanufaisha

wanunuzi ambao ni walanguzi, wananunua kwa bei ya chini na kwenda kuuza kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ijenge Kiwanda, Mkoa wa Simiyu hiyo ndio itakuwa njia pekee ya kuwasaidia wafugaji ili waweze kuongeza kipato, lakini pia naiomba Serikali ijenge Kiwanda cha Ngozi na cha maziwa hiyo itakuwa njia pekee ya kuwakomboa kiuchumi wafugaji wa Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wote kwa kuwasilisha bajeti nzuri yenye mwelekeo na iliyosheheni takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upungufu katika bajeti hii hususan kiasi cha fedha kilichotengwa na kiasi cha bajeti inayoshuka kila mwaka, bado naunga mkono bajeti hii nikiamini kwamba Serikali yetu katika miaka ijayo itaongeza bajeti katika sekta hii ili kutekeleza azma ya Serikali kama iliyotamkwa katika Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi 2010/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi kati ya watumiaji imezidi kuongezeka kwa sababu kubwa zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya watu imeongezeka kutoka milioni tisa (1961) kufikia milioni 45 (2012) na inategemewa kufikia milioni 65 (2025). Idadi

ya mifugo hususan ng'ombe kutoka milioni tisa (9) (1961) na kufikia milioni 22.8 (2012) licha ya mifugo mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mabadiliko ya tabianchi na baadhi ya maeneo kwa sasa hayafai kwa kilimo na ufugaji, kumekuwepo ufyekaji wa misitu kwa ajili ya mkaa kwa wastani wa hekta 450,000 kwa mwaka na hivyo kuzidi kupunguza maeneo ya kilimo na ufugaji. Idadi ya wanyamapori kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni dhahiri kwamba eneo la kilimo la hekta 44 milioni na umwagiliaji hekta 29.4 milioni na za ufugaji linazidi kupungua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwepo na mpango kabambe unaohusisha Wizara mbalimbali ili kuja na mkakati wa kuondoa tatizo hili.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana tena kwa mara ya kwanza siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za msingi imekuwa ni tabia ya baadhi ya Mawaziri kuwa na mazoea ya kufanya kazi kwa mazoea ya upendeleo kwa baadhi ya maeneo na kuona baadhi ya maeneo katika nchi kuwa si sehemu ya Tanzania. Ni hii yote inatokana na baadhi ya Mawaziri kufanyia kazi mezani au sehemu fulani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawastahili kabisa kuwa viongozi katika kipindi hiki ambacho Serikali yetu inashambuliwa sana na Upinzani. Wanachangia sana kupanua Upinzani na kufanya wananchi waichukie Serikali yetu kumbe tatizo kubwa linatokana na ubaguzi wa waliopewa dhamana hiyo kutotenda haki kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi, ukisoma kitabu chote cha bajeti cha Wizara hii hakuna sehemu hata moja inayoelezea namna gani Serikali inaendeleza rasilimali za Ziwa Rukwa. Je, Rukwa siyo sehemu ya nchi ya Tanzania? Naomba nijibiwe. Je Wavuvi wa Ziwa Rukwa siyo Watanzania walio na haki kama wavuvi wa Maziwa mengine? Naomba nijibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ubaguzi na unyanyasaji mkubwa kwa wananchi wa Jimbo langu na wananchi wote wanaotegemea Ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefika Ofisi ya Mifugo na Uvuvi na vile vile nimemwona Waziri kumweleza changamoto na matatizo ya Ziwa Rukwa, bado hadi leo hii nashangaa kuona hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hajagusa kabisa Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitoe mchango wangu kwa kifupi, Ziwa Rukwa linakabiliwa kuwa na mifugo mingi kuliko wastani wa eneo na kusababisha mmomonyoko wa udongo, tope kujaa Ziwa Rukwa, mazalia ya samaki kuharibiwa huko nyuma, Ziwa Rukwa lilikuwa na kina cha wastani mita

nane au kumi hivi sasa wastani wake ni mita nne tu. Je, Mheshimiwa Waziri hayaoni hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la shughuli za uvuvi ambao hauzingatii matumizi endelevu ya rasilimali za Ziwa Rukwa. Mheshimiwa Waziri hajayaona haya?

Mheshimiwa Spika, kutofanyika kwa tafiti ambazo zingeweza kuonesha kiasi cha rasilimali iliyopo ndani ya Ziwa Rukwa, tujifunze mafuta yaliyogunduliwa katika Ziwa Albert Ziwa ambalo jiografia yake inafanana na Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo dhamira ya pamoja ya kuhifadhi mazingira baina ya Wilaya zinazozunguka Ziwa Rukwa kama vile Wilaya za Sumbawanga, Mpanda, Chunya na Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo mdogo wa Halmashauri za Wilaya katika kusimamia uhifadhi wa Ziwa Rukwa. Hii ni pamoja na uhaba wa watumishi ufinyu wa bajeti kukosekana kwa vitendea kazi, gari, *boats* na pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uelewa mdogo wa elimu ya uhifadhi wa mazingira miongoni mwa wananchi kuchangia uharibifu wa mazingira ya Ziwa Rukwa elimu itolewe, fedha itengwe ya kuhifadhi mazingira ya Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wa Ziwa Rukwa kuendelea kutumia zana duni na kushindwa kupanuka kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali za majini katika Ziwa Rukwa, Serikali iweke vyombo vya kuokoa wavuvi *boats* na maboya okozi kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, viongozi waliopewa dhamana watembelee Maziwa yetu yote ili kuona changamoto zilizopo na kutafuta utatuzi kutokana na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa jitihada zao za kuimarisha sekta hii kwa kiasi kidogo sana kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ya Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa kuwa na mifugo mingi, lakini bado sekta hii haijachangia ipasavyo kwenye pato la Taifa. Ifike wakati sasa sekta hii ichangie zaidi ya sekta ya kilimo katika pato la Taifa. Tukidhamiria tunaweza pamoja na mifugo mingi bado hatuna Viwanda vya Nyama, hatuna Viwanda vya Ngozi wala hatuna Viwanda vya Maziwa vya kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Utafiti wa mifugo havipati fedha za kutosha kwa ajili ya utafiti.

Mikakati na mipango ya utafiti inayopangwa na watafiti haiwezi kufanikiwa, nchi haiwezi kuendelea bila tafiti mbalimbali ikiwemo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba makubwa ya kuzalisha mifugo inaweza kabisa kuanzisha Viwanda vya Nyama na Maziwa, tunashindwa nini katika hili? Hati Miliki ya mashamba hayo yanaweza kutumika kupata mikopo benki kwa ajili ya kujenga viwanda na badala ya mashamba hayo kuuza ng'ombe, mbuzi na kadhalika yakauza mazao yatokanayo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tupange kusonga mbele na siyo kusimama kama tunavyofanya leo. Kiko wapi Kiwanda cha Nyama, Shinyanga? Tanganyika *Packers* iko wapi? Kiko wapi Kiwanda cha Nyama, Ngozi, Samaki na kadhalika. Tumesimama katika sekta hii amini ninalolisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sekta ya maziwa iweze kukua bidhaa zitokanazo na maziwa ziondolewe *VAT* ili wananchi wamudu kununua maziwa yanayozalishwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile nchi yetu haina mifugo na samaki, makampuni ya kigeni yanayochimba madini yanaagiza nyama, samaki na kadhalika kutoka nje ya nchi. Je, Serikali yetu inasema nini katika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CYTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri pamoja na kazi nzuri, Wizara hii inavyojitahidi kuimarisha sekta ya Mifugo na Uvuvi kwa ujumla. Pongezi hizi ni pamoja na kwa Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi inayoendelea kuboresha mifugo ili kupata kizazi bora cha mifugo ya aina mbalimbali kama vile ng'ombe, mbuzi, kuku na kadhalika. Kwa kuwa mifugo mingi imekuwa ikiathirika sana kwa ukame unaoikumba Mikoa ya wafugaji wa ng'ombe kama Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma na kadhalika, ufanyike utaratibu wa kuhakikisha Wizara inashirikiana kwa karibu na Wizara ya Maliasili na Mazingira na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kutunza mazingira na vyanzo vya maji ili mabwawa na malambo yaweze kuchimbwa kwa wingi ili mifugo isikose maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile bado elimu kubwa iendelee kutolewa kwa wafugaji ili waweze kupunguza mifugo yao. Kwa njia hii wataweza kumudu kuihudumia mifugo yao na kuweza kupata uchumi wa kutosha kwa kupata nyama bora au kuiuza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Nyama cha Mbeya, bado juhudi ya kukipatia Kiwanda hiki mwekezaji wa kudumu hazijazaa matunda. Je, ni nini kinachoendelea hivi sasa na hatima yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu kuna mipango gani ya kuendeleza sekta ya uvuvi hasa kuboresha uvuvi wa kisasa kwa wavuvi wadogowadogo katika Ziwa Nyasa na Ziwa Rukwa.

Kuna miradi inayoendelea katika Maziwa mengine kama Ziwa Victoria na Tanganyika, lakini katika Ziwa Nyasa hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake uvuvi unaofanyika katika maeneo hayo bado ni ule ule ya Kizamani sana, hakuna mabadiliko yoyote. Kinachoendelea ni kukamata nyavu zenye ukubwa mdogo bila elimu yoyote ile. Nashauri sasa Wizara ielekeze juhudi zake katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti, lakini Wizara hii sasa itekeleze ahadi ambayo Mheshimiwa Magufuli aliiweka pale Mchinga. Kuvipa vikundi ng'ombe wa maziwa ili viache uvuvi haramu. Sasa suala hili ni kero kwangu na wapiga kura wangu. Tafadhali naomba bajeti hii itatue kero hii ambayo mwaka jana mlikubali kuimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwahamasisha wavuvi wa Vijiji vya Mchinga, Maloo, Kijiweni, Mvuleni, kuacha uvuvi haramu kwa ahadi ya kuwapatia nyavu na boti za kisasa, ahadi hii haijatekelezwa na Chama cha Mapinduzi imekumbwa na dhoruba ya kutokubalika katika maeneo hayo. Kiokoeni chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi na usalama katika ukanda wa Bahari ya Hindi, maeneo ya ufukwe toka kijiweni hadi Lindi ni madogo, kuwe na boti ya *patrol*.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora una maeneo makubwa ya Hifadhi lakini kiuhalisia maeneo yote yameshavamiwa na wafugaji kutoka Mikoa mingine, jambo ambalo linasikitisha na linajenga chuki kwa wanavijiji ambao wanazunguka maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Maafisa wetu wa Maliasili ngazi ya Mkoa na Wilaya husika wanalijua hilo, lakini wameunda mtandao wa ulaji, kwani kila wakipita kukagua maeneo ya hifadhi wanawakuta wafugaji ambao wamo na wanaendelea kuishi ndani ya hifadhi na kuharibu mazingira lakini Maafisa hawa wanapatana nao kisha wanapewa rushwa na kuwaacha kuendelea kuishi na kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itusaidie kuokoa maeneo yetu ya hifadhi, lakini pia itafute namna bora ya matumizi ya ardhi na wakulima na wafugaji wote wapate maeneo yao. Pia idadi ya Watanzania imeongezeka sana na maeneo mengi ya hifadhi yameshaharibika kupita kiasi. Kwa hiyo, Serikali ikague maeneo hayo na ikiwezekana kiasi kidogo cha ardhi ya hifadhi itolewe kwa wananchi ili wanufaike na ardhi ya ziada, lakini pia wawezeshwe kulinda maeneo ya hifadhi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo na uvuvi zina uwezo wa kutoa

mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi na kuboresha maisha ya wananchi. Hata hivyo, mchango wa sekta zote mbili kwenye pato la Taifa unaendelea kushuka. Katika mwaka 2011 sekta ya mifugo ilikuwa kwa asilimia 3.9 ikilinganisha na asilimia 3.4 mwaka 2010. Huku sekta ya uvuvi ikikua kwa asilimia 1.2 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa kasi ya ukuaji wa sekta za mifugo na uvuvi kunafanya maelezo yanayotolewa na Wizara husika kuwa: "Kupungua wa mchango wa sekta hizo kwenye pato la Taifa ni matokeo ya kukua kwa sekta nyingine." Yanapaswa kutolewa maelezo ya ziada ya sababu zingine za kudidimia kwa sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye majumuisho, Wizara ieleze kwenye mwaka wa fedha 2012/2013, imeweka malengo ya kuongeza kwa asilimia ngapi kasi ya ukuaji wa sekta za mifugo na uvuvi na mchango wa sekta husika kwenye pato la Taifa. Aidha, imeweka mfumo gani wa tathimini na utekelezaji kuhakikisha malengo yanafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya mifugo, naomba kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2012, Serikali irekebishe kodi katika bidhaa zitokanazo na mifugo zinazozalishwa nchini ikiwemo kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwa kipindi maalum. Uchumi wa nchi unaathiriwa kwa bidhaa za mifugo kama maziwa, nyama, ngozi na kadhalika. Zikienda kuuzwa nje ya nchi zikiwa ghafi

huku matumizi ya bidhaa hizo nchini yakiwa chini na kupoteza, pia mapato ya pamoja na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii iende sambamba na mkakati wa haraka wa kuweka mazingira bora ya uzalishaji na usambazaji kwa viwanda vya usindikaji wa mazao ya mifugo nchini. Serikali ione kuwa sekta ya mifugo kama ilivyo kilimo ina mchango katika kupunguza mfumuko wa bei na ongezeko la gharama za maisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam naomba katika shule zitakazowekwa kwenye mpango wa maziwa shuleni kwa mujibu wa aya ya 116 pawepo pia shule mojawapo kutoka Jimbo la Ubungo. Aidha, napendekeza kwamba Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na Manispaa za Jiji la Dar es Salaam kuwa na mkakati wa kuhamasisha ufugaji wa mbwa katika kaya za pembezoni kama sehemu ya utekelezaji wa mpango wa ulinzi shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya uvuvi; pamoja na kauli iliyotolewa na Serikali Bungeni na hatua ambazo zimeendelea kuchukuliwa katika Kanda ya Ziwa kuhusu kushuka kwa bei ya samaki, bado malalamiko toka kwa wavuvi yanaendelea. Serikali ieleze hatua za ziada za kuboresha bei kama ilivyo kwa upande wa Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvuvi katika Bahari Kuu lichukuliwe kama mojawapo ya vipaumbele vya kimkakati vya kupanua wigo wa mapato kwa nchi. Mamlaka ya kusimamia uvuvi eneo husika *(DSFA)*

iombe nguvu za ziada za vyombo vya dola katika doria ili kulinda rasilimalli hizi muhimu.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuwa wafugaji wa Mkoa wa Rukwa, wamekuwa wakifuga kwa staha kwa kulinda mazingira bila kukata miti hovyo kwa kuwa wanajua fika kuwa kwao kukata miti na kuharibu mazingira kwa kuwa na mifugo mingi pia hupelekea mmomonyoko wa udongo na uharibifu wa ardhi (mazingira). Wafugaji hawa pia ambao ni wakulima wameheshimu mazingira na ndiyo maana ukulima wao umekuwa wa tija na Watanzania wengine wakajipatia chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kwamba, Serikali kupitia Kamati ya Ulinzi na Usalama za Mkoa, Wilaya, Kata, mpaka Vijiji wasimamie wafugaji wahamiaji kutoka Mikoa mingine ili waige mfano mzuri wa wafugaji wa Rukwa wanaofuga kwa tija bila uharibifu wa mazingira. Ikibidi yatengwe maeneo haraka sana kwa ajili ya wafugaji na wakulima na wafugaji wafuge kwa tija ili isije ikazalisha kutokuelewana na migogoro inayopelekea ugomvi. Wanarukwa ni watulivu, wapole na wakarimu sana, lakini hilo la kuharibu mazingira hawatakubaliana nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rukwa ina maziwa makubwa ya Tanganyijka na Rukwa. Natoa rai yangu kuwa wavuvi wa maziwa haya walindwe kwani wanavamiwa sana na wavuvi haramu toka nchi jirani za DRC, Burundi na Rwanda. Wavuvi walindwe

wahamiaji haramu ni wengi mwambao mwa Ziwa Tanyanyika hata Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maziwa haya yanatoa samaki wengi wazuri na watamu wenye lishe. Hivyo, Viwanda vya Kukausha Samaki na Kusindika vinahitajika ili kuinua uchumi wa Rukwa na Tanzania nzima. Pia Viwanda vya Kuchinja na Kusindika Nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uvuvi haramu, kumekuwa na wavuvi haramu wanaotumia baruti, nyavu zisizostahiki kuvua samaki (nyavu haramu). Nyavu hizi zimekuwa zikivua mpaka mazalia madogo madogo ya samaki. Uvuvi huu wa kutumia baruti huathiri viumbe vidogo vidogo na pia huaribu matumbawe. Hii ni kutokana na wavuvi wengi kutokuwa na elimu ya viumbe wa habarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na Wizara iwaangalie sana wavuvi wadogo wadogo na wapatiwe mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kununulia zana bora. Mheshimiwa Waziri haoni wavuvi hawa kutopatiwa elimu ya mara kwa mara ya viumbe vya baharini ndio chanzo cha kuharibu mazalia na matumbawe? Uvuvi huu haramu unapelekea bahari zetu na maziwa kukosa samaki wa kutosha, ni lini Serikali itawadhibiti wavuvi haramu na ni wavuvi

wangapi haramu mpaka sasa hivi wamekamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchafuzi wa mazingira kwenye bahari; kumekuwa na uchafuzi mkubwa ndani ya bahari na kwenye fukwe za bahari. Wananchi ambao wamejenga kando kando ya bahari, wamekuwa wakitumia bahari kwa haja kubwa na haja ndogo. Baadhi ya wananchi wanatupa mifuko ya *plastic* na kadhalika wananchi hawa hawajengi choo kwa matumizi yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia baadhi ya viwanda mitaro mingi ya maji machafu imejengwa kwa kuelekezwa baharini na maji machafu hayo yana kemikali. Uchafuzi huu wa mazingira unasababisha viumbe vingi vya bahari kufa na hata matumbawe kuharibika. Je, Serikali na Wizara haioni kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa wananchi waliozunguka bahari ili kuepusha uchafuzi huu wa bahari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko la samaki, wavuvi wengi wamekuwa hawanufaiki na soko la uuzaji samaki. Hasa wavuvi wadogo wadogo, ambao wamekuwa wakinufaika na biashara hii ni wale wafanyabiashara wakubwa wakubwa. Wamekuwa wakiwalangua wavuvi wadogo wadogo na kuwapangia bei ndogo sana na wao kunufaika kwa kupitia migongo ya wavuvi wadogo wadogo. Serikali na Wizara ina mikakati gani kuhakikisha wavuvi hawa wadogo wadogo wananufaika na soko hili la uuzaji wa

samaki na wao kupatiwa bei ya uhakika ambayo inakwenda na wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro baina ya wafugaji na wakulima. Wafugaji wengi hawana maeneo ya kufuga. Mifugo yao mara kwa mara imekuwa ikiingia kwenye mashamba ya wakulima na wamekuwa wakiingia migogoro na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu wa Serikali kuiongozea fedha Wizara hii ili kukidhi haja ya kuwapatia wafugaji na mifugo yao mahitaji muhimu kama vile majosho na maji kwa njia ya malambo, mabwawa, visima na maeneo ya malisho. Lakini pia ubora wa mifugo utaongezekia na hii itaepusha wafugaji kuhamahama mara kwa mara na itawapelekea kutokuwa wakimbizi katika nchi yao.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Wafugaji wengi hawana maeneo maalum ya kuchungia mifugo yao hivyo kupelekea mgogoro usio wa lazima. Wizara ilitizame kwa upya jambo hili na kuweka mkakati thabiti ya kuainisha maeneo maalum kwa wafugaji ili kuondoa matatizo yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa mifugo, kuna uhaba mkubwa wa wataalam hawa katika Halmashauri zetu katika ngazi za kata hivyo wafugaji hawapati ushauri wa uhakika wa jinsi ya kukabiliana na changamoto wanazopata hivyo mifugo mingi kufa na mfugaji kutokuwa na uhakika wa ustawi wa mifugo

yao. Hata hivyo, baadhi ya wataalam hawa wanapoenda kutoa huduma kwa wafugaji hutoza ada mbalimbali kama za chanjo, mafuta ya pikipiki na kadhalika. Wizara ituambie gharama hizi anazolipishwa mfugaji ni halali? Je, viwango halisi ni ngapi (kama vipo) badala ya kumuondolea mfugaji unafuu anazidi kunyonywa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa asali, nchini Tanzania kuna asali nyingi huzalishwa lakini hakuna viwanda vya ku-*process* na kupaki asali hizi ili kuuzwa nje. Serikali ni vema itazamie jambo hili na kuanzisha viwanda vya kufungasha asali hizo ili kuinua mapato ya nchi lakini kumwezesha mfugaji huyo kuuza asali kwa uhakika na kumpatia mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya uagizaji wa nyama ya kuku toka nje ya nchi. Tanzania inao kuku wengi wa kutosha ambao wataweza kutosheleza mahitaji ya nchi, haiingi akilini kuku kuagizwa toka nje. Hii ni aibu kwa nchi yenye rasilimali nyingi. Wizara iweze kuanzisha viwanda vya kusindika kuku ili kuwawezesha kina mama kuwa na soko la uhakika la kuku wanaofuga. Haya yanawezekana kama Serikali hii ina dhamira ya kweli na ya dhati kusimamia jambo hili. Waziri atupe majibu ya mkakati gani alionao kuinua soko la kuku nchini? Tunaomba majibu ya uhakika wakati wa majumuisho.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri,

Katibu Mkuu na Watendaji/Watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni kwa namna gani Wizara inapambana na changamoto ya miundombinu ya maji taka inayochafua na kuingiza sumu baharini (Bahari ya Hindi), Maziwa kama vile Victoria, Tanganyika, Nyasa na kadhalika na hivyo kuathiri viumbe waishio majini kama vile samaki. Kwa kiasi kikubwa maji taka ya Jiji la Dar es Salaam, Jiji la Mwanza, Tanga, Manispaa ya Kigoma Ujiji na kadhalika yanaishia Bahari ya Hindi au kwenye maziwa tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki wadogo wana tabia ya kula kemikali (Zebaki) ziingiazo majini na samaki wakubwa hula samaki wadogo hatimaye binadamu hula samaki wakubwa. Athari zake kwa afya ya binadamu ni kubwa sana, (ugonjwa kama wa minamata uliowahi kutokea Japan miaka ya huko nyuma).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba kujua hatua iliyofikiwa na Wizara hii kuhusu utekelezaji wa lengo la saba la milenia la uhifadhi wa mazingira na uendelezaji wa mazingira endelevu katika sekta ya mifugo na uvuvi, *sustainability and environmental protection.*

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wakuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri aliambie Bunge lako Tukufu kwa nini sekta ya Mifugo na Uvuvi mchango wake katika *GDP* ni mdogo sana? Nchi yetu inao ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku kwa mamilioni lakini pamoja na ukweli huu sekta hii haichangii vya kutosha. Naomba Waziri aniambie ni sababu zipi hasa za msingi ambazo zimeifanya sekta hii isiwe mchangiaji katika uchumi wa nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchi yetu inatekeleza Mkakati wa Kupunguza Umaskini na Kukuza Uchumi (MKUKUTA), sekta ya Mifugo na Uvuvi zimeajiri Watanzania wangapi? Aidha, napenda nijue mikakati inayolenga sekta ya uvuvi kuboreshwa na hivyo kuwa mojawapo ya mhimili wa kuchangia ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inapakana na Bahari, inayo Maziwa na Mito mikubwa ambayo ndio maeneo mahsusi kwa mazalio ya samaki. Hata hivyo ni ukweli usiopingika kwamba wavuvi wetu bado wanatumia zana duni kabisa za uvuvi. Wavuvi wetu hawawezi kwenda kuvua maji makuu *(deep sea waters).* Je, Serikali ina mpango gani kuwawezesha wavuvi kupata zana za kisasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja hii kwa kuanza

kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na uongozi wote wa Wizara hii na kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo la muda mrefu kuhusu namna ya kugawa ardhi ya wafugaji na ile ya wakulima. Wafugaji pamoja na kupewa maeneo yao lakini hayana mabwawa ya maji pamoja na malisho. Tatizo la wafugaji kuhama halitaisha kama maeneo wanayopewa hayana malisho au maji, tutatue kwanza mahitaji ya mifugo hiyo. Baada ya Serikali kuwekeza kwenye maeneo hayo ni vizuri sana tujielekeze kuhakikisha mifugo inatoa mchango kwenye uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mazao ya mifugo kama nyama, maziwa na ngozi, tuwekeze kwenye viwanda vya mazao hayo ili tuone sekta hii inaendelea kwa kuonyesha ongezeko la pato kwa uchumi wa Taifa hili. Kama maeneo haya hayajashughulikiwa itakuwa vigumu kwa sekta hii kuonekana ni ya muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo ranchi za Taifa, hivi kweli kwa aina ya ufugaji uliopo una tofauti na ule wa kawaida? Ranchi kama ya Kongwa, sijaona kuna tofauti, ni kubwa, kama tumepata pato kubwa kwenye mfuko wa Serikali basi, kama sivyo naomba nijulishwe Serikali inapata kiasi gani kwa mwaka? Nadhani kuna tatizo kubwa la kiuongozi wa ranchi hii ya Kongwa. Waziri afuatilie na kuchukua hatua.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mathayo David Mathayo, Naibu Waziri, Mheshimiwa

Benedict Ole-Nangoro, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti ya Wizara yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inazo changamoto nyingi ambazo ningependa kuzichangia. Kwanza ni migogoro kuhusu wafugaji na wakulima. Sasa hivi kumekuwepo na migogoro mikubwa sana katika karibu Mikoa yote ya nchi hii na migogoro hiyo inaongezeka siku hadi siku na kusababisha mpaka wananchi kupoteza maisha yao, uharibifu wa mali ambayo madhara yake ni kuathiri hata ustawi wa kiuchumi na kijamiii na kuleta uadui baina ya makabila ya wafugaji na wakulima. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja, atueleze ni mikakati gani watakayotumia kumaliza migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, vibali vya uagizaji wa nyama ya kuku toka nje ya nchi. Serikali ingeacha kutoa vibali vya uagizaji wa nyama ya kuku toka nje kwa sababu nchi yetu kwa sasa ipo juu sana hasa ukizingatia kuwa elimu ya ujasiriamali imetolewa kiasi kwamba wananchi wengi sana wamejiingiza katika biashara hii na inawasaidia wananchi wakiwemo kina mama kukuza vipato vyao na uchumi wa nchi hii lakini uangizwaji wa nyama ya kuku toka nje ya nchi kunafanya kukosekana kwa masoko ya nyama ya kuku hasa kwenye maduka ya *super market* na mahoteli makubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha ufugaji wa kuku na ili wananchi waweze kufaidika na hata kukuza pato la nchi hii, Serikali ingehakikisha kila Halmashauri

inakuwa na wataalam wa Idara ya Mifugo na hata Halmashauri zilizopo mijini. Wataalamu hao wasikae tu ofisini, waende kukagua miradi na kutoa elimu kwa ajili ya ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, machinjio, Serikali iangalie pia uboreshaji wa machinjio zetu hapa nchini. Katika Mkoa wetu wa Iringa Halmashauri ya Manispaa upo mradi wa machinjio ya kisasa, tayari tumepata wawekezaji ambao wameahidi kufunga vifaa vipya vya kisasa kwa mwaka huu lakini tatizo Serikali imekuwa ikisuasua kuleta pesa kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa machinjio hayo. Naomba sasa mradi huu upatiwe kipaumbele wa kupatiwa pesa shilingi milioni 200 tu ili mradi huu ukamilikie na wananchi waweze kufaidika na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie kuna baadhi ya machinjio hapa nchini hasa machinjio ya Mkoa wa Dar es Salaam ni machafu sana hasa wakati wa mvua machinjio zilizopo Manispaa ya Ilala ile ya Mazizini ni chafu sana. Naomba uwepo ukaguzi wa mara kwa mara. Mazingira machafu katika machinjio yanaweza hata kusababisha magonjwa ya kuambukiza kama kipindupindu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wawepo Madaktari wa kutosha kwa ajili ya kupima nyama ili iwe yenye ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha 2012/2013 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mathayo David kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana katika kutusaidia sisi kama Wabunge lakini pia katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku kiutendaji kwa Serikali na wananchi kwa ujumla bila kuchoka na bila woga. Nampongeza pia Naibu wake Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri niliyoanisha, naomba nitoe mchango wangu katika maeneo machache kuwiana na hali halisia ya Jimbo la Kilwa Kaskazini na Wilaya ya Kilwa kwa ujumla. Hotuba ya bajeti imezungumzia mapinduzi ya ufugaji kwa kuweka miundombinu katika maeneo yote ya ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilwa ni miongoni mwa maeneo ambayo wamepokea wafugaji wengi sana pamoja na Serikali kujenga josho lakini eneo la Puyu, Kata ya Miteja halina lambo na mara zote wataalam wamekuwa wanakuja kuchukua vipimo na tafiti bila utekelezaji kwa muda mrefu sana. Katika hotuba ya mwaka huu, Waziri ameitaka Halmashauri itenge bajeti ili kutekeleza uchimbaji wa

lambo kinyume na ahadi yake ya mwaka jana kuwa Wizara yake itatenga pesa ili kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sasa ni wakati muafaka wa kuangalia namna ambavyo wananchi wanaoishi ukanda wa pwani na maziwa kupata gawio kutokana na mauzo ya samaki na mazao mengineyo kama wale wa maeneo ya migodi yanavyopata (*royalties*). Hii itasaidia sana kuinua jamii husika pamoja na kusaidia wavuvi wadogowadogo kupata dhana bora za kuvulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya uvuvi yamepewa kipaumbele ila napenda Serikali ichukue hatua zaidi kuimarisha ulinzi baharini kwa maana mpaka sasa hali ni mbaya na wananchi wazuiwa kuvua katika baadhi ya maeneo huku wengine (wageni) wanavua na kuondoka na rasilimali hizi bila kuzingati malipo au athari zozote ambazo zinajitokeza baadaye. Ni kheri wananchi wanaozuiwa kuvua basi wapewe mbinu mbadala ili kujiendesha katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia zipo meli ambazo zinavua katika eneo la Somanga hadi Masoko ambapo baada ya kuvua huchambua samaki na kuwatupa baadhi kufuatana na mahitaji yao kwa kuwafunga kwenye mifuko, kwa nini wasiwagawe kwa wavuvi wadogo? Lakini hakuna mwenye hakika kama wamelipia leseni na mazao waliyovua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza uzalishaji na upatikanaji wa kutosha wa samaki, naishauri Serikali ianzishe na kutoa elimu ya kutosha katika ufugaji wa samaki kwenye mabwawa na uanzishaji wa mashamba ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mgawanyo wa ardhi baina ya wafugaji na wakulima katika nchi yetu ni kubwa sana na ipo haja sasa ya Serikali kuangalia upya namna ya kuboresha eneo hili kwa maana waathirika wakubwa ni wananchi wa kipato cha chini. Naishauri Serikali iendelee kuboresha na kuanisha mipaka ili kusiwe na mwingiliano lakini pia itolewe elimu ya kutosha nini umuhimu wa kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea na mkakati wa kuimarisha soko la bidhaa za mifugo na samaki (maziwa, ngozi, nyama na kadhalilka) lakini pia tuangalie namna ya kudhibiti bidhaa zinazotoka nje kwa maana zinatoa ufinyu wa soko kwa bidhaa zetu. Pamoja na mpango huu, tuhakikishe tunapata namna bora zaidi kwa kufufua viwanda vyetu bila kutegemea wawekezaji wa nje ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa mzigo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla na hii pia inapelekea kelele nyingi kwa wasiofahamu maana ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali ya ukame, ipo haja sasa ya Serikali kuelimisha na kuweka mkakati wa kutumia mabaki ya mazao kama mabua ya mahindi na mabunzi yake, mtama, mashudu, majani ya maharage, majani ya migomba na

kadhalika ili wanapovuna wahifadhi na kuwa akiba wakati wa ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali iliyopo sasa, suala la kilimo ni muhimu sana na kama hotuba ilivyoainisha ni vema tukatilia mkazo zaidi katika dhana bora. Napendekeza tuyatumie vizuri Majeshi yetu (JKT, MAGEREZA, JKU) kwa kuyapa teknolojia na pia tuwaongezee mtaji ili wafanye ufugaji wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ichukue jitihada za makusudi kuelimisha jamii katika ufugaji wa kuku wa kienyeji ili kuinua kipato cha watu wa hali ya chini lakini pia kuongeza mapato ya Serikali katika ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili yote haya yafanikiwe na kupata ufanisi wa kutosha, naishauri Serikali iharakishe mpango wa uanzishwaji wa Benki ya Kilimo ambayo itabeba pia Wavuvi na Wafugaji kama alivyoainisha katika hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba Serikali iweke kipaumbele cha pekee kwenye mifugo na samaki haswa ukizingatia umuhimu na mchango wake mkubwa kiuchumi haswa kipindi hiki ambapo kuna shughuli nyingi za uchimbaji madini na gesi nchini. Njia ya rahisi ya kuwanufaisha wananchi ni kuweka mfumo wa kusaidia ushiriki wao kwa kupata kipato cha mazao ya mifugo na bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote. Baada ya hapo nakushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi katika bahari kuu, ni chanzo kimoja cha kuwapatia vijana wetu wanaoishi katika sehemu za pwani za nchi yetu ajira. Ikiwa Serikali itajipanga vizuri kuwawezesha wavuvi wetu kwa kuwapatia vyombo vya kisasa na vifaa vya kutosha wataweza kujiajiri na pia wataondokana na umaskini na pia Serikali itapata kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina vyanzo vingi sana vya kuongeza mapato lakini imeshindwa kwa mfano Ziwa Tanganyika kuna samaki wengi sana, tulifika kwenye Bandari ya Kasanga, tukashuhudia maboti yanayovua samaki na kwenda kuuza Zambia. Hii yote inatokana na ukosefu wa umeme katika sehemu ile na miundombinu mibovu ya barabara ya kutoka Kasanga kwenda Sumbawanga Mjini. Naishauri Serikali iwawezeshe hawa wavuvi wa Kasanga kwa kuwapatia umeme japo wa jenereta wa kuweza kuhifadhi samaki wao ili Serikali iweze kupata mapato na watu wetu waweze kujiajiri na kuondokana na umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina maeneo mengi ya kuweza kufuga mifugo lakini kwa nini kila siku ugomvi hauishi kati ya wafugaji na wakulima? Naishauri

Serikali isimamie sana haya maeneo ya mifugo ili hii mizozo kati ya wafugaji na wakulima iwezekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kiangazi mifugo mingi sana inakufa kwa ajili ya kukosa maji hivyo basi kwa nini Serikali haijengi mabwawa ya kuhifadhia maji ya mvua ili wafugaji wetu waondokane na dhiki ya kutafuta maji kwa masafa marefu ya kunyweshea mifugo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie namna gani inaweza kusaidia wafugaji kupata chanjo kwa ajili ya mifugo yao kwa sababu mifugo mingi inakufa kwa ajili ya kukosa chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe taaluma kwa wafugaji kwa sababu wafugaji wengi hawana taaluma ya ufugaji ili waweze kupata uzoefu wa ufugaji wa kisasa na kupata maslahi makubwa na nchi yetu iongeze kipato.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013 bajeti iliyotengwa ni ndogo sana. Fedha za Maendeleo shilingi 13,839,483,000 hazikuelekezwa kusaidia au kutatua migogoro na upimaji wa ardhi ya mifugo ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ya asili, bajeti iliyotengwa ni ndogo sana nadhani pia utekelezaji wake hautakuwa na ubora. Hili linaweza kuwa sababu ya kusuasua kwa wafugaji asili kukosa maeneo na huduma muhimu kwa mifugo yao. Wafugaji wanahitaji kauli ya Serikali kupitia Waziri Mkuu juu ya jambo hili la

kutengewa fedha kidogo na migogoro yote ya ukosefu wa maeneo ya malisho yatatatuliwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ikiwemo ng'ombe wa asili milioni 1.1 imeingia sokoni mwaka 2011/2012 kati ya hao ng'ombe wanaotoka ranchi hawazidi 5,000 na wa asili ni ng'ombe 1,095,000. Je, ni kwa nini muelekeze fedha kwa ranchi wakati ng'ombe wa asili huwaingizia kipato kikubwa na lishe? Aidha, nyama tani 503496, maziwa lita bilioni 1.7, ngozi vipande milioni 2.8 vimetokana na ng'ombe, mbuzi na kondoo wa asili. Je, Serikali ina mpango gani kwa wafugaji wanaoleta maendeleo na kipato cha Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa miaka 50 ya Uhuru kati ya hekta milioni 60 ni hekta milioni 2.3 zimetengwa. Kwa kipindi hichohicho tumeshuhudia maeneo makubwa yakitegwa kuwa hifadhi za Taifa za wanyamapori, misitu na mashamba makubwa ya Serikali ambayo yaliwashinda na kuwapa wawekezaji. Zoezi hilo pia lilihusisha kuondolewa wafugaji asili ambao wanatupatia nyama, maziwa na ngozi. Mfano Wilaya ya Hanang, kuondoa wafugaji na kufungua mashamba ya ngano matokeo yake kubinafsishwa kwa wawekezaji bila tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utashi wa Serikali na viongozi juu ya upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ufugaji wa asili uko wapi? Ardhi kwa shughuli nyingine ipo. Suala la ardhi ya wafugaji ni la mtambuka kwa kuwa lipo Wizara ya Ardhi, Mifugo, Tamisemi, Mazingira na kadhalika na hili linaweza kuwa sababu ya kusuasua kwa wafugaji asili. Kukosa maeneo ya ufugaji, mifugo

haiwezi kuendelea bila kuwa na masoko bora, viwanda vya kuongeza thamani ya mazao na masoko ya bidhaa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi inajitahidi kuzalisha lakini Serikali bado haijaweka mazingira wezeshi ya biashara. Kenya ambayo imepiga hatua kubwa hususani katika tasnia ya nyama na maziwa, Serikali inastawisha sekta binafsi. Mfano kodi nyingi ambazo ni kero na zinaongeza gharama za uzalishaji na bei ya bidhaa zimeondolewa. Kwa kuanza, tunaitaka Serikali iondoe ushuru wa forodha kwenye vifungashio, vifaa na mashine katika biashara ya maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilinde soko la bidhaa za maziwa za ndani kwa kuongeza ushuru wa forodha wa bidhaa zitokazo nje. Iondoe *VAT* kwenye maziwa na bidhaa zake ili kupunguza bei kwa walaji na gharama kwa msindikaji yaani *VAT* itozwe kwa kiwango cha 0%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, utendaji wa matumizi wa fedha za *DADPS* kwa ajili ya maendeleo ya mifugo vijijini. Halmashauri nyingi hutumia fedha hizo kwa matumizi mengine au ujenzi wa malambo, majosho, minada, dawa. Kwa kuwa kiwango cha chini yaani ubadhirifu ni mkubwa sana hasa Wilaya ya Hanang. Kuchimba malambo hewa majosho hewa na kadhalika. Ukaguzi maalum ufanyike.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wa Wizara hii kwa umakini wa utekelezaji wa majukumu makubwa waliyonayo katika Wizara hii maalum kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwapatia wananchi wa Mikoa ya Arusha ng'ombe ikiwa ni msaada kutokana na athari walizozipata kutokana na ukame mkubwa uliopelekea kupoteza mifugo zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuomba Mheshimiwa Waziri kulifuatilia kwa makini suala la wavuvi wa Manispaa ya Tanga. Wavuvi hawa wanne waliotii agizo au amri ya Waraka wa Serikali wa kusitisha uvuvi wa kutumia nyavu za *ring net* kupitia Waraka huo Na.KA/594/01/87.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Waraka huo kutolewa, wavuvi hawa kwa uhakika kabisa walitiii amri hiyo na walipandisha vyombo juu pamoja na nyavu zao. Wakitafakari ni nini watafanya kutokana na amri hiyo lakini kwa bahati mbaya sana Maofisa waliokuwa katika operesheni hii walichukua vifaa vyao vikiwa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tatizo linakuja pale ambapo watu hawa hawakushtakiwa kwa sababu hawakuwa na hatia yoyote, leo iweje tuambiwe vifaa vile vimeteketezwa kwa amri ya Mahakama? Hivi Mahakama gani inaweza kutekeleza hukumu isiyo na mshtakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Waziri aliyotoa kwamba watu hawa walikimbia sio kweli. Hivi iweje watu waliokimbia wapeleke barua za maombi ya kurejeshwa vifaa vyao katika ngazi tofauti za Serikali ikiwemo ofisi ya Wizara, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Halmashauri ya Jiji la Tanga na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uongo mkubwa uliotolewa na Maafisa wa Wizara juu ya kadhia hii. Naomba uonane na wavuvi hawa kupata suluhisho la jambo hili.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi unaofadhiliwa na *ADB* wa *Lake Tanganyika* ambao upo katika nchi zinazozunguka Ziwa hilo yaani Tanzania, Congo, Zambia na Burundi. Mradi huu ulichelewa kuanza kwa kuwa DRC walichelewa ku-*sign* sasa tayari umeanza lakini bado wavuvi waliambiwa wajitenge kwenye vikundi wapewe mafunzo ya uvuvi bora watakopeshwa vifaa bora vya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hakuna kitu lakini pia wanawake na vijana wanaofanyabiashara ya mazao ya *Lake Tanganyika* waliahidiwa mafunzo na vifaa bora vya kukaushia samaki lakini wengi hawajapata mafunzo hayo wala vifaa. Mradi uliahidi kujenga mialo na masoko ya samaki na vitu vingine, je, Serikali inasemaje juu ya maendeleo ya mradi huo, umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uingizaji wa mazao ya mifugo kama maziwa, mayai, kuku wa nyama, nyama ya ng'ombe *especially from South Africa* na Kenya, naomba kufahamu kwa nini tusiboresha mifugo yetu ili izalishe maziwa, mayai na nyama nzuri na bora ili tusiruhusu mazao hayo kutoka nje? Hii itasaidia kuongeza pato la wafugaji lakini pia pato la Taifa kwani viwanda vitakua na kuongezeka, vya kusindika nyama na maziwa. Nafahamu tuko kwenye soko huria lakini tukiboresha mifugo yetu na viwanda vyetu tutapunguza kiasi cha uingizaji wa mazao na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ugani bado ni duni, wananchi hawapati huduma hiyo. Serikali iongeze juhudi za kusomesha wataalam wa ugani. Lakini na waliopo waende *field* wasibaki maofisini tu ili tufuge kisasa na tupate mazao bora.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nakushukuru na kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mungu muweza wa yote kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwatakia Waislam wote Ramadhani iliyo Makuburi pia nampongeza Waziri na timu yake kwa kuandaa maelezo ya ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba sasa nijielekeze katika masuala machache ambayo nimechagua kuyatilia mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti ya mifugo na uvuvi. Pamoja na jitihada na dhamira ya Serikali za kuhakikisha sekta ya mifugo na uvuvi inakua miongoni mwa sekta zinazotoa mchango mkubwa wa Taifa, dhamira na jitihada za Serikali hazijazaa matunda mazuri kwa sababu malengo yanayopangwa hayatekelezwi kwa kiwango cha kuridhisha kwa sababu bajeti ya sekta hii ya uvuvi imekuwa inapungua mwaka hadi mwaka. Hivyo inaathiri utekelezaji wa mipango mizuri ya sekta hii na kusababisha kutoleta tija kwa Taifa. Naishauri Serikali ione uwezekano wa kutenga fedha za kutosha katika sekta hii ili iweze kutoa mchango kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wakulima na wafugaji. Pamoja na dhamira njema ya Serikali ya kuhakikisha wakulima na wafugaji wanaishi na kufanya kazi za kilimo na mifugo kwa amani na utulivu, bado tatizo la migogoro ya wakulima na wafugaji halijapatiwa ufumbuzi kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali itenge fedha za kutosha za ndani kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima na wafugaji jinsi wakulima watakavyonufaika watakapoishi pamoja na wafugaji na wafugaji watakavyonufaika watakapoishi pamoja na wakulima. Kipaumbele kitolewe kwa wananchi ambao asili yao si wafugaji bali ni wakulima na wafugaji ambao si wakulima. Kipaumbele kiwe katika maeneo ya Mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutenga maeneo ya kilimo na mifugo. Serikali itenge na kuweka bayana

maeneo ya kilimo na mifugo ili kuepusha migogoro ya mara kwa mara. Kazi hii ya kutenga maeneo naomba ipewe umuhimu wa kipekee tena kazi hii Serikali Kuu, Wizara ya Fedha pia iwe mtekelezaji namba moja. Wasiache Halmashauri za Wilaya kutenga fedha kutokana na mapato yao ya Halmashauri, uwezo wao ni mdogo wa kuweza kumudu gharama za kupima ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya mifugo, pamoja na jitihada za Serikali za kuboresha miundombinu ya mifugo, lipo tatizo la miundombinu ya mifugo, mabirika ya maji, naiomba sana Serikali itenge fedha za kutosha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kujenga miundombinu ya mifugo, malambo, majosho na malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa uchumi kupitia sekta ya mifugo na uvuvi. Sekta ya mifugo, ni sekta muhimu sana kwa uchumi wa Taifa lakini mchango wa sekta hii haujaonekana bayana kwa kiwango cha kuridhisha. Naishauri Serikali ihamasishe mifuko ya Taifa ya *NSSF, PPF, PSPF* na kadhalika kujenga viwanda vya kusindika minofi ya nyama, samaki na maziwa badala ya kutegemea sekta binafsi ambao wanajitokeza kwa kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutunga sera ya mifugo. Usindikaji, masoko na unywaji wa maziwa, nashauri Serikali ifanye yafuatayo ili rasilimali ya maziwa iweze kuchangia pato la Taifa. Serikali itoe elimu kwa wanawake wa Tanzania kuhusu umuhimu wa kunywa

maziwa. Pia itayarishe vituo vya kukusanyia maziwa na kuyafikisha sokoni na viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwezesha wanawake vijana kupitia uchumi wa bahari na maziwa, ili kuwawezesha vijana wetu wengi kupata ajira ya uhakika. Naiomba Serikali iongeze kasi ya kuwakopesha vijana vitendea kazi vya kisasa vya kuvulia samaki ili waweze kukabiliana na ushindani uliopo wa uvuvi wa kisasa. Nashauri katika mpango huu kipaumbele kiwe ni kwa vijana na wanawake wanaoishi kandokando ya Bahari ya Hindi, Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Manyara, Ziwa Singida na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi katika bahari kuu. Kwanza, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba kutamka kuwa uvuvi wa bahari kuu haujasaidia uchumi wa Tanzania. Bado meli za kigeni ambazo zinavua bila ya kibali zinaonekana zinavua katika bahari ya Tanzania. Ili kudhibiti hili, lazima nchi ipate helikopta na boti zenye kwenda kwa mwendo wa kasi kwa ajili ya kulinda bahari yetu na wavuvi wa kigeni wanaopora samaki wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli hizi huonekana na wavuvi wetu hasa wakati wa usiku na kama hatua za dharura hazitachukuliwa, samaki wengi watapungua na pengine kutoweka kabisa. Kwani meli hizi hutumia

nyavu ambazo zinaharibu matumbawe, masalio ya samaki na kuvua samaki wadogo.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja, pia napenda kumpongeza Dkt. David Mathayo David, Waziri wa Wizara hii na Naibu wake Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro kwa utendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mpango gani kurudisha Chuo cha Mafundi Sanifu Maabara (Liti – Temeke) kwani chuo hiki ni muhimu sana kwa utafiti wa magonjwa ya wanyama na hasa wakati huu ambapo Sheria ya Utafiti kwa Mifugo Tanzania 2012 imepitishwa na kuwa sheria. Aidha, *VICS* zetu zitapata wapi wataalam kama hakuna *Technician* (*Laboratory*) wakati hawazalishwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka mzima sasa, Wilaya ya Tandahimba imekuwa ikipoteza mbuzi na kondoo kwa wingi kwa vifo kwa ugonjwa ambao haujathibitika kuwa ni sotoka. Wataalam wa *VIC*-Naliendele walifanya utafiti dhidi ya vifo hivyo lakini si *VIC* wala Wizara wametoa majibu kwa wananchi na hivyo wataalam wa ugani kushindwa kutoa elimu kwa wananchi juu ya nini kifanyike ili kudhibiti tatizo hili. Napenda kuijulisha Wizara ya Mifugo kuwa utendaji wa aina hii (*slowly*) kwa tatizo la Wilaya moja tu unatoa dalili kuwa tukipata tatizo kubwa kwa eneo kubwa tunaweza kuathirika sana kwani hakuna '*seriousness'* ya kushughulikia matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Manispaa ya Mtwara eneo la Mikindani kulikuwa na kiwanda cha maboti siku za nyuma. Je, ni nini hatma ya kiwanda hicho kwa sasa hasa ukitilia maanani ukuaji wa nyanja ya uwekezaji Ukanda wa Kusini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo ina mpango gani kuanzisha kituo cha uzalishaji mitamba Wilayani Tandahimba kufuatia kituo cha Ngongo - Lindi na kile cha Nachingwea kufungwa na hivyo kubakiwa na kituo cha Ngaramo pekee ambacho hakiwezi pekee yake kukidhi mahitaji ya Kanda ya Kusini?

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kupenda wafugaji na wakulima wa nchi hii. Wakati tunachangia hoja hii ni siku mbili au tano zimepita ametoa kifuta jasho kwa wafugaji waliofiwa na ng'ombe zao kutokana na ukame uliotokea mwaka jana Wilayani Simanjiro na Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuthibitisha upendo wa Mheshimiwa Rais kwa wafugaji, alipoingia madarakani mwaka 2005 aliagiza Wizara kumfanya mchungaji ambaye tunamwita mfugaji kutoka uchungaji na kuwa mfugaji ili afaidike na mifugo yake badala ya kuwa mtumwa wa mifugo yake. Dhamira ya Mheshimiwa Rais kutaka wachungaji kuwa wafugaji ni kutaka kuinusuru nchi katika jangwa, kuepusha migogoro ya wakulima na wafugaji wanaohamahama na mwisho ni kumfanya mfugaji huyu afaidike na mifugo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejipangaje katika kutekeleza agizo hilo la Mheshimiwa Rais? Nadhani imefika wakati sasa kwa Wizara kuwa na Sera ya Mifugo ambayo itaainisha maeneo ya mifugo na kulima. Sera ambayo itamtambua mfugaji kwa eneo, yupi ni mfugaji mdogo, wa kati na mkubwa ili Wizara iweze sasa kupanga mikakati ya kumsaidia mfugaji mdogo na wa kati katika ufugaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipange eneo la ufugaji mdogo na wa kati, kwa kushirikiana na Halmashauri ambazo zina maeneo ya kufugia na kujenga miundombinu yote ambayo itahitajika katika maeneo hayo badala ya kuachia Halmashauri pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na Wizara ipange maeneo ya wafugaji wakubwa kwa kushirikiana na wafugaji wenyewe pamoja na Halmashauri ambazo zitakuwa na maeneo ya kuwapokea wafugaji hao wakubwa na naamini wafugaji wakubwa wapo, wana uwezo wa kujihudumia wenyewe kama Serikali itawaelekeza nini cha kufanya katika ufugaji wao bila kuleta athari kwa nchi au jamii nyingine inayowazunguka. Haiwezekani mchungaji ambaye ana mifugo kati ya 8,000 hadi ng'ombe 20,000 bila kuwa na eneo maalum analomiliki kisheria na kutokuwa na miundombinu inayohitajika kutunza mifugo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mtanzania ana haki kikatiba kwenda mahali popote katika nchi hii. Naomba niwakumbushe pia wananchi pamoja na ruhusa hiyo ya kikatiba ni vizuri tukaikamilisha ruhusa

hiyo ya kikatiba kwa kutovunja sheria za nchi. Bado Serikali inaonekana inasema au inatenda kwa maneno na mipango ambayo siyo sahihi aidha kwa kujua au kwa maslahi ya jamii fulani badala ya kulinda maslahi ya nchi na jamii ya wakulima ambao ndio walishaji wa chakula katika Taifa hili na nchi jirani zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikipinga hoja iliyokuwepo mbele yetu bila kuelekeza Serikali yangu nini kifanyike, nitakuwa sijaitendea haki nchi yetu katika kuinusuru na jangwa, kuzima migogoro ya wakulima na wafugaji lakini vilevile kuwafanya wafugaji wakafaidika na mifugo yao na kuondoa uadui na wananchi wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sera na taratibu ambazo nimeshazielekeza kwa Serikali, ni vizuri sasa tukaanzisha Wakala wa Mifugo ambaye ataainisha maeneo ya ufugaji (wadogo, wa kati na wakubwa); ataainisha idadi ya ng'ombe ambao wafugaji watakuwa wanatakiwa kuwa nao katika makundi yote ya wafugaji; atasimamia minada yote Kiwilaya, Kimkoa na Kitaifa ili kudhibiti ongezeko holela la mifugo isiyoenda sambamba na mipango ambayo Serikali inayopanga. Naamini tukifanya hivi tutashinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii hasa katika suala zima la adha wanayopata wafugaji wetu hasa katika maeneo yanayopakana na hifadhi za mbuga kama Serengeti. Hawa Watanzania wanafuga ng'ombe nyingi ambazo zinalisha Watanzania kwa maana ya mazao

yatokanayo na mifugo kama maziwa, ngozi, nyama na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hulisha nchi ya jirani kama Kenya lakini wafugaji hawa wanakosa sehemu za kulisha mifugo yao maana wameingiliwa na hifadhi na wakienda kulisha wanapigwa risasi na kufa huku wakinyang'anywa mifugo yao, familia inabaki ikiteseka hasa vijiji vya Bondugu. Naomba Wizara au Serikali ishirikiane na Wizara zingine kama ya Ardhi na ya Maliasili na Utalii ili wananchi hawa wawe huru na kuendeleza ufugaji ambao unatoa ajira na kukuza uchumi wetu hasa jamii ya kifugaji waishio Mara na kwingineko nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu juhudi zetu za Wizara kuhakikisha bidhaa za mifugo zinatumiwa kwa wingi hapa nchini hasa viwanda vya ngozi, viwanda vya nyama, viwanda vya kwato na *by product* zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kuhusu zao zima la samaki, naye imesahaulika kabisa, tuna Ziwa Victoria ambalo lipo Mikoa mingi ikiwemo Mara, maeneo ya Bunda, Musoma na Shirati lakini uvuvi haramu ambao unaharibu samaki sababu wanakufa hata samaki wadogo na kuelea ziwani kitu ambacho kinageuka kuwa uchafuzi wa mazingira na ukosefu wa ajira na kudumaza uchumi, tuwe na viwanda hivyo, hata mabwawa ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu na nchi yetu ni ya tatu kwa wingi wa mifugo Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kubwa kwa sababu ya ufugaji wa kienyeji usiozingatia *land use plan*. Wafugaji wa maeneo ya Kanda ya Ziwa Victoria wameufanya Mkoa wa Shinyanga kuwa jangwa. Nashauri Serikali iwe na *control mechanism* ya mifugo. Mifugo itengewe maeneo ambayo yatatumika kwa zamu (*blocks)* katika maeneo wafugaji walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wa eneo la Kanda ya Ziwa Victoria popote wanapopeleka mifugo wanakata miti kwa kuogopa mbung'o lakini pia na hofu ya ushirikina wa ndege watakaotua katika miti hiyo. Nashauri Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wafugaji hawa watumie *protection* ya kutosha kwa ajili ya mbung'o badala ya kukata miti na kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji waelimishwe wafuge mifugo michache iliyo bora. Kituo cha *NAIC* cha Arusha kifanye kazi, mifugo ihilimishwe itoe mazao ya mifugo yaliyo bora. Waelimishwe wafanye biashara na mifugo (wa *diversify* biashara zao)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwasaidia wafugaji, sheria ya *PPP* itumike, viwanda vya nyama vijengwe katika maeneo ya wafugaji (Shinyanga, Arusha, Dodoma) sio lazima Serikali ijenge isaidie kwa kuweka mazingira ya kufaa ili sekta binafsi ijenge viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilinde viwanda na mazao ya mifugo ya wafugaji wetu. Kupeleka maziwa nchini Kenya ni matatizo kutokana na vizuizi nchi hiyo inavyoweka ili kulinda maziwa na wafugaji wao. Nchi za *European Union* wanawapa ruzuku wafugaji wao ili nchi za *ACP (African Caribean and Pacific)* wasiweze kuuza mazao ya mifugo Ulaya ili kulinda viwanda vyao. Serikali iweke mkakati mayai yasiingizwe nchini badala yake wafugaji wa kuku wasaidiwe ili wafuge kuku wa kutosha badala ya kuagiza kuku kutoka nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa kutumia makokoro ufanyiwe kazi zaidi. Bwawa la Nyumba ya Mungu halizalishi samaki kwa sababu ya uvuvi usiokuwa na *control*. Mto Kilombero mwanzoni mwa mwaka mamlaka ilizuia wananchi kuvua kwa miezi sita ili kuwapa nafasi samaki kukua. Amri hii hata katika Bwawa la Nyumba ya Mungu inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikundi vya wanawake popote walipo na vijana wawezeshwe wafuge kuku wa kienyeji, nguruwe, samaki kwa muda mfupi. Ufugaji huu umeonyesha kusaidia makundi haya kupata fedha ya matumizi. Serikali kwa kupitia Wizara hii itoe elimu kwa wafugaji ili watumie fursa za mikopo iliyopo *SIDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mpango wa maendeleo ya samaki. Jumla ya bilioni 200 za samaki zinaibiwa *deep sea,* hawaoni kama hili ni tatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda na masoko. Njia ya kukomesha msongamano wa ng'ombe unaonung'unikiwa na wasio wafugaji ni viwanda vya nyama na ngozi. Uchinjaji ndiyo *(exit)* mwisho wa mzunguko wa ng'ombe na maisha yake. Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake ametupa takwimu kwamba ng'ombe takribani 2.5 milioni zinachinjwa kila mwaka – *ref.* idadi za ngozi za ng'ombe zinazouzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, takribani ng'ombe 18 milioni ni takwimu zinazotajwa kama idadi ya ng'ombe nchini. Kutumia takwimu hizi na kama uzalishaji hauongezeki ndiyo kusema tuna ng'ombe wa kututosha kwa miaka sita. Aidha, biashara inayohusiana na ng'ombe, mbuzi, kondoo ni kama trilioni moja – fedha, karibu watu milioni 20 na ajira kubwa inabebwa na ng'ombe au mifugo. Dhana ya maendeleo ni kuongeza uzalishaji wa ng'ombe na kuimarisha *'exit'* masoko na viwanda. Kwa hiyo, kwa mchango huu, ninaishauri Wizara isimamie kwa nguvu zaidi kufunguliwa kwa machinjio ya Ruvu, ya Shinyanga na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mizani, Mheshimiwa Waziri amesema mizani imenunuliwa lakini itatumika ipasavyo? Tatizo wafugaji ni *conservatives,* hawapendi kugeuka haraka. Hapa nahimiza mizani ikamilike ili

ng’ombe wapimwe na kujenga utaratibu wa kufanya biashara kwa kilo kwani nyama inapimwa na kwa nini ng’ombe, ni vema mfugaji akajua bei ya ng’ombe wake kwa kilo. Mtindo huu utaleta tamaa ya kunenepesha ng’ombe na kupunguza kuhamahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo kulishwa katika kambi na *blocks.* Jambo hili linafanyika Ngorongoro kwa nini hili lisifanyike Ny’wang’wali au *Maswa Game Reserve*, sasa inafanyika lakini kwa rushwa. Tuhalalishe kulisha bila kulima na kukata miti. Sasa wafugaji wanateswa na *Game Rangers* wanaondeshwa kwa rushwa. Jambo hili lizungumzwe kati ya Wizara hii na ya Maliasili.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nyeti na muhimu sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti, napenda kuungana na Wabunge wenzangu kuonyesha masikitiko yangu juu ya bajeti hii ambayo imepungua kwa kiasi kikubwa kulinganisha na mwaka jana, sijui ni kwa sababu gani? Naiomba Serikali kuangalia upya bajeti hii kwa kutafuta kila namna ya kupata fedha za kuiongeza ili iweze kuwa na tija. Nasubiri maelezo ya Serikali yaani Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji kutenga maeneo ya kuchungia mifugo. Bado kuna matatizo ya migogoro ya wakulima na wafugaji kwani vijiji vingi bado havitengi maeneo ya kulishia mifugo hivyo mifugo hushambulia mimea na kuharibu mazao. Ninaiomba Serikali kutoa kauli ya utawala kwa watendaji wa vijiji na kata kutenda maeneo ya mifugo ili kuondoa migogoro isiyokuwa na ulazima, naomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malambo ya kunyweshea mifugo. Bado kuna tatizo la malamiko ya maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo. Hii inatokana na malambo kuchimbwa chini ya kiwango yaani kina kifupi au malambo kutokujengewa kingo na kusababisha udongo kuingia ndani ya lambo na kusababisha maji kupungua kina na kukauka. Ninaishauri Serikali kuweka ukaguzi kabla ya malambo kuanza kutumika. Vilevile kuna vijiji vingine vina mifugo mingi malambo machache au moja tu ni vema malambo yachimbwe kufuatana na idadi ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yenye uvuvi kunufaisha wananchi. Napenda kushauri Serikali kufuata utaratibu wa uwekezaji mfano maeneo ya migodi, vijiji hunufaika na Halmashauri kupata asilimia. Ni vipi samaki wasinufaishe maendeleo ya maeneo husika mfano Mwanza na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupandikiza samaki kwenye maziwa. Naomba kuishauri Serikali kuyatumia maziwa vizuri yale ambayo hayana samaki wengi basi wapandikizwe samaki mfano Ziwa Kindai na Ziwa Singida yaliyojo mjini Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kiwanda cha Ngozi Singida Vijijini, Tarafa ya Sepuka, kiwanda kidogo ambacho kinawamba ngozi na kinatengeneza bidhaa kutumia ngozi mfano viatu, mikanda na kadhalika, kiwe kinatengewa bajeti na Serikali sio kuiachia Halmashauri husika. Vilevile watumishi wenye taaluma wapelekwe hapo na wale ambao hawana taaluma wapelekwe kozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumaliza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia nikitegemea nitapatiwa majibu au mchango wangu kutambuliwa.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono hoja, naomba Waziri aangalie jinsi anavyoweza kuangalia Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kilimanjaro wana uhaba wa ardhi. Kwa hiyo, hawana uwezo wa kufuga mifugo kiholela, mifugo inafungwa katika eneo dogo. Wakulima wa Kilimanjaro wana uzoefu wa kufuga ng'ombe wa kisasa katika eneo dogo, ng'ombe, mbuzi na nguruwe wanafugwa katika mabanda yaliyo nyumbani, wakulima wanakata majani na chakula na kupelekea mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la mkulima na mfugaji wa Kilimanjaro ni jinsi ya kupata ng'ombe wa kisasa. Ng'ombe mmoja wa kisasa anauzwa kati ya shilingi 500,000 hadi shilingi 700,000 tu. Ni dhahiri

mkulima au mfugaji maskini hawezi kumudu gharama ya kununua ng'ombe mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Mifugo na Uvuvi akishirikiana na Halmashauri ya Moshi aangalie uwezekano wa kutafuta fedha katika taasisi za fedha ndani na nje ya Tanzania zitupatie fedha kwa ajili ya kununua mifugo na ikopeshwe kwa wakulima na wafugaji wa Jimbo la Vunjo na Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika wafugaji wakikopeshwa fedha za kununua mifugo hiyo, fedha hizo zitarudishwa vizuri sana.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mungu na pia kuchukua nafasi hii kukushukuru na kutoa pongezi kwa Waziri na Wizara kwa ujumla hasa katika kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inazo changamoto kubwa sana katika kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo ningependa sana kujielekeza ni katika viwanda vya kuchakata samaki vilivyopo Kanda ya Ziwa. Waziri atakubaliana name kuwa wenye viwanda vya uchakataji samaki vilivyopo nchini Tanzania upande wa Kanda ya Ziwa ndiyo wamiliki wa viwanda vya samaki upande wa nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na migogoro ya bei za samaki kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye viwanda hivi na hii ni kutokana na kuwa wamiliki wa viwanda hawa kutoa mikataba ya ajira ambayo upande wa Tanzania hawatoi mikataba ya ajira kwa wafanyakazi wa kiwanda (wachakataji) hii imesababisha wenye viwanda hawa kuamua na kuhakikisha upande wa Kenya unapata (samaki) malighafi ya kutosha ili viwanda vya upande wa Kenya ambavyo vina wafanyakazi wenye mikataba ya ajira huko Kenya vinafanya kazi, huku viwanda vya kwetu ambavyo wafanyakazi wake ambao ni vibarua wa muda mrefu hawana ajira na wanakosa kazi za kufanya ukizingatia wachakataji wa samaki katika viwanda vya Tanzania hulipwa kutokana na kazi wanazopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imewafanya wenye viwanda vya samaki kwa umoja wao (umoja wenye hila) wamekuwa wakitoa bei ya chini sana kwa wavuvi wanaouza samaki katika viwanda vya Tanzania na kutoa bei ya juu katika masoko na viwanda vilivyoko mipakani mwa Kenya na Tanzania ambayo imewavuta wavuvi wa Tanzania ambao ilikuwa wauze samaki wao upande wa Tanzania na kuuza upande wa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara isipoangalia mapungufu haya basi ni dhahiri kuwa mbali na kuporomoka kwa mchango wa kiuchumi katika Taifa kupitia sekta hii basi pia ajira nyingi sana na kipato cha mtu mmoja mmoja kitaathirika kwa kiasi kikubwa sana na pia kuna uwezekano mkubwa sana kwa kutokea

vurugu kati ya wavuvi na wenye viwanda na ni hatari sana kwa uchumi wa Taifa na pia ustawi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhu, ni vyema sana jambo hili kuchukuliwa kwa uzito wa kipekee na pia kuliangalia kwa umakini mkubwa sana kuanzia sasa. Serikali kwa kushirikiana na Wizara zote hasa uchukuzi, kazi na ajira, ujenzi na fedha, wakaweka mkakati wa pamoja na kuamua kujenga viwanja vya ndege vya Bukoba na Musoma ili kuwezesha kutua ndege za mizigo ambazo zimekuwa zikichukua samaki hawa katika viwanja vya Kenya ambapo samaki wake wanatoka Tanzania na kuuzwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ya Viwanda na Biashara wahakikishe soko na bei za samaki Kimataifa zinawekwa wazi kila baada ya miezi mitatu ili wavuvi wenye viwanda na wafanyabiashara wa samaki na wadau wote waijue ili kuepuka biashara ya siri kwa bei za samaki duniani na hii itapelekea kuwavutia watu wengi kuingia katika biashara ya samaki.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa fursa hii ya kuchangia kwa maandishi hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta za mifugo na uvuvi, ni muhimu na ina uwezo mkubwa wa kuliletea Taifa letu maendeleo makubwa ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na ajira, viwanda, chakula na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi iliyo na mifugo mingi sana kuliko nchi nyingi Afrika, mifugo mingi hii bado haijaweza kuliletea Taifa letu tija ya kutosha. Bado kuna mapungufu makubwa sana katika kutumia mifugo yetu kutuletea tija ya kiuchumi. Bado tunauza kwa wingi mifugo iliyo hai, tunauza nje ya nchi nyama iliyochinjwa tu tena kwa mapande bila kuchakatwa viwandani na kupata thamani na kuuza nyama yenye thamani kubwa na ubora wa Kimataifa nje. Nyama iliyochakatwa/*processed* ni wazi ina thamani zaidi ya mara tano ya ile isiyochakatwa, bado tumeshuhudia watumiaji mbalimbali wa nyama wakiagiza nyama toka nje na hata kwa wingi kutoka Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia utakuta ukweli ni kwamba mifugo mingi tuliyonayo haina nyama yenye kiwango cha kuchakatwa, kusindikwa na kutoa nyama yenye ubora, ndio maana hata wawekezaji wengi hawajataka kuwekeza kwenye viwanda hivi. Muda umefika sasa Wizara kwa makusudi iangalie yale mashamba ya mifugo, ya ng'ombe wa nyama yapewe kipaumbele kwa ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa nyama, ardhi kubwa tunayo, wataalamu wapo nini tatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo kubwa la usalama na ubora wa nyama inayotumika nchini. Ukiangalia machinjio mengi katika Halmashauri na Manispaa zetu ni mabovu, machafu na kamwe hayakidhi viwango vya usafi na usalama wa chakula uliowekwa na idara ya afya. Napenda kujua ni hatua

gani zinazochukuliwa na Serikali kuondokana na tatizo hili kubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shamba la ng'ombe la Ruvu, yaani (*Ruvu ranch*) mfano wa shamba ambalo halijaweza kutoa tija kabisa katika soko la nyama Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani mwaka umeisha sasa tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alipoweka jiwe la msingi la kiwanda cha kuchakata nyama pale Ruvu na ahadi kadhaa kwa wananchi ikiwa ni pamoja na ajira kwa Watanzania wapatao 1000 na mengineyo mengi ya kiuchumi na kuwa ujenzi ungekamilika mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi leo hii hakuna kazi au ujenzi ulioendelea, mabati na chuma za ujenzi zinaendelea kuibiwa. Hii ni aibu kubwa kwa Taifa na Serikali yetu kuwa mradi uliozinduliwa na Rais na wenye umuhimu kama huo umeishia kuwa jalala. Naomba Waziri ajibu kuna mpango gani na ni lini mradi huu utaendelea kutekelezwa na ulete tija iliyotarajiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kuwa usalama na afya kwa wananchi kwa kuwa na machinjio ya kisasa na zenye kanuni zote za usalama, ni jambo muhimu maana linagusa afya za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu na kuunga mkono hoja.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hotuba hii na naomba mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya majosho ya mifugo. Nimeshaomba sana hapa kuhusu ujenzi wa majosho kwa wafugaji katika vijiji vya Kambiala, Magimba, Sokoine, Mela, Makuture na Matale. Upatikanaji wa majosho na madawa kutawasaidia wafugaji kuhudumia mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa malambo umechangia kwa kiasi kikubwa migogoro kati ya wakulima na wafugaji kwani utafutaji wa maji umepelekea wafugaji kuingia maeneo ya wakulima na kusababisha uvunjifu wa amani. Naomba sana malambo yachimbwe maeneo yafuatayo Magimba, Kambala, Makuture, Sokoine, Mela, Msongozi na Matale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa minada. Mwaka jana niliahidiwa kuwa Serikali itatenga fedha kuboresha minada kwa kujenga na kuboresha huduma za maji, vyoo katika minada ya Mikongeni, Kambala na Hoza, Kata ya Kibati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwajengea majosho, malambo, kuboresha minada na madawa ya mifugo kutasaidia sana wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri, Naibu wake na watendaji kwa kuandaa bajeti nzuri lakini pia kwa uendeshaji Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza na kushauri kuwa huduma kwa wafugaji ziongezwe na kuratibiwa vizuri na hasa huduma za chanjo na uelimishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa, nashauri Wizara iongeze uratibu wa upatikanaji wa dawa, hasa ya kuogesha, kwa bei inayoridhisha na kwa maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ranchi za Taifa zilizoko zipewe uwezo na kuimarishwa ili ziendelee kuwa za msaada, msimamizi na darasa kwa wawekezaji wadogo wanaozunguka ranchi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini naomba ufafanuzi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini bajeti ya maendeleo ya mifugo inapungua kila mwaka wa fedha ilhali sekta hii haina wawekezaji wa maana kutoka nchi za nje na Serikali nayo haina mikakati madhubuti ya kuendeleza sekta hii ya mifugo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 7/8/2012 nilibahatika kuona zoezi la kushindanisha ubora wa

mifugo (ng‘ombe, kondoo na mbuzi) kutoka kanda zote za nchi yetu katika viwanja vya Nzuguni, Dodoma (Nanenane 2012). Kumbe hakuna haja ya kwenda ziara Botswana au Uganda kuona ubora wa mifugo ya nyama na maziwa kwa sababu wanapatikana hapahapa nchini lengo liwe ni kuwawezesha wafugaji wadogo kupata mbegu bora (madume/na au AI).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo imeendelea kuwa “Malaya” katika Wizara zingine kama Kilimo, Maji, Uvuvi hali ambayo inafanya Wizara hiyo ikose “*Due attention“*toka kwa Serikali na watendaji (wataalam) wa Wizara hii na mara zote Wizara zinazounganishwa na mifugo zinameza sekta hii na matokeo yake hupoteza mwelekeo na kutangatanga kama wafugaji wenyewe wasivyothaminiwa na kuishia kuzurura nchi nzima na kufukuzwa kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza/nashauri Serikali iweke ruzuku katika dawa zote zinazotibu magonjwa makubwa ya mifugo kama inavyofanya kwa dawa ya kuua kupe *(Dips).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iache tabia ya kutwaa maeneo ya wafugaji na kufanya mashamba ya wanyamapori (*National parks/Game reserves/Game Controlled Areas)* na kuwapa wawekezaji/ na au Serikali kuchukua kwa ajili ya miradi mikubwa ya Kitaifa. Ikibidi kufanya hivyo, kwa manufaa ya Taifa lazima yawepo makubaliano na fidia kama walivyofanya Wakoloni walipochukuwa Serengeti na kuhamishia Wamasai Ngorongoro na Loliondo, pamoja

na kuweka miundombinu maeneo hayo kama vile maji, *veterinary services/centres.*

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima na wafugaji wanategemeana sana katika kushirikiana na kutumia rasilimali ardhi na maji kwa ustawi wa mazao na mifugo. Hivyo ni dhahiri kwamba kuna kila sababu ya mipango ya maendeleo ya wakulima na wafugaji kuwa *integrated.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mipango mingi lakini leo nataka kujikita katika haja ya kuwa na mipango ya pamoja katika kujenga mabwawa ya maji ya kilimo cha umwagiliaji, malisho ya mifugo *(irrigated pastures)* na mabirika ya kunyweshea mifugo. Mipango ya pamoja itasaidia sana kuipunguzia Serikali gharama za kujenga miradi tofauti (kama mabwawa) katika maeneo mbalimbali ambayo ingesaidia wakulima na wafugaji kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *National Stock Routes,* usafirishaji wa mifugo kupitia njia zisizo rasmi unachangia kuharibu miundombinu mbalimbali hususan barabara, matuta ya makingamaji na kadhalika. Nashauri Wizara irejee na kufufua *"National Stock Routes"* na kuangalia utaratibu wa kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Nchi, kwa ulinzi anaotoa katika nchi yetu pamoja na watu wake. Nampongeza kwa dhati Waziri wa Wizara, Naibu Waziri wa Wizara, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na watendaji wengine wa Wizara kwa jitihada zao za kuiongoza Wizara kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hoja hii, binafsi nitajikita katika maswali pamoja na ushauri. Maswali haya yakijibiwa yatatoa mwangaza mkubwa wa kusaidia Wizara ili ifikie malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ukame katika Wilaya ya Tarime. Napenda kukujulisha kuwa Wilaya ya Tarime imegawajika katika sehemu kuu mbili za Tarime ya Juu na Tarime ya Chini. Tarime ya Chini ndiyo inayojishughulisha sana na kazi ya ufugaji ambayo inajumuisha kata za Komaswa, Manga, Kibasuka, Nyarukoba, Gong'ora/Gorong'a, Kemambo, Nyangoto na kadhalika. Maeneo ya Kata hizi mengi yapo kandokando ya mto Mara ingawa mengine kutokana na hali halisi ya kijiografia na hali ya nchi yenye milimamilima, yako mbali sana na mto Mara. Hivyo sehemu kubwa ya maeneo haya ni kame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, naishauri Serikali iweze kuchimba visima vya uhakika, malambo ya uhakika, mabwawa ya uhakika pamoja na majosho ya uhakika katika maeneo haya kwa

lengo la kuwasaidia wakazi wanaoishi katika maeneo husika. Maeneo ninayopendekeza malambo yachimbwe ni hasa Kata za Manga, Komaswa, Kemambo, Nyangoto, Nyarukoba, Gorong'a na Nyanungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la kukosekana kwa machinjio ya kisasa katika Wilaya ya Tarime. Naiomba Wizara iwashirikishe wadau wa aina mbalimbali ili kuweza kujenga eneo la kisasa la machinjio Wilayani Tarime pamoja na Mji wa Sirari. Hii ni kwa sababu tangu enzi za ukoloni, uhuru hadi sasa hakuna huduma hii katika mji wenye takribani watu wapatao 400,000 pia katika nchi jirani ya Kenya kuna machinjio ya kisasa lakini kwa upande wa Tanzania ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha Nyama/Maziwa Wilayani Tarime. Kiwanda cha aina hii kilijengwa katika mji wa Sirari ulioko mpakani mwa Tanzania na Kenya kwa hakika kitasaidia sana kuwapatia wafugaji wa Wilaya ya Tarime kipato cha kutosha kutokana na shughuli halali ya ufugaji. Nchini Kenya bidhaa ya maziwa na nyama hutoa kipato kwa wafugaji wa nchi hiyo kwani mahitaji ya bidhaa hizi ni kubwa nchini humo. Hivyo naishauri Serikali kupitia Wizara hii ihakikishe kuwa inashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kujenga kiwanda cha Nyama/Maziwa katika mji wa Sirari, Wilayani Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maswali/ushauri katika sekta hii kwa Taifa. Mfugaji hutumia muda mwingi na hata rasilimali nyingi katika

kutayarisha mifugo yake, ng'ombe, mbuzi, kondoo, bata, kuku, na kadhalika lakini tafiti nyingi zinaonyesha kuwa hakuna soko la uhakika la mifugo na mazao yanayotokana na mifugo hiyo. Je, Serikali ina mpango gani makusudi na wa haraka wa muda mfupi, kati na mrefu wa kumhakikishia mfugaji uhakika wa soko la mifugo na mazao yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini haijengi machinjio makubwa na ya kisasa kwa kila Wilaya ili kumwezesha mfugaji huyo kuwa na uhakika wa soko la ndani la bidhaa hiyo inayotokana na mifugo? Serikali Haioni kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kurudisha Serikalini viwanda vya nyama vilivyobinafsishwa ili kutoa ajira kwa wananchi wazawa na wakati huohuo kuwa na soko la uhakika la mazao ya mifugo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ina mpango gani wa kujenga viwanda vya kusindika ngozi angalau kiwanda kimoja kwa kila Mkoa? Ina mpango gani kujenga viwanda vya maziwa angalau kiwanda kimoja kwa kila Wilaya hasa zile Wilaya za wafugaji kama vile Tarime, Serengeti, Bunda, Monduli na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa wafugaji, ni ukweli usiopingika kuwa wafugaji wetu hawapewi elimu yoyote ile hususan Wilaya za pembezoni. Elimu inahitajika sana kwa lengo la kuwaelimisha wafugaji juu ya ufugaji bora, namna ya kuwekeza katika sekta hii na hata namna ya kujiunga na bima ya mifugo. Je, Serikali hadi sasa imetoa elimu juu ya ufugaji bora kwa Wilaya ngapi hapa nchini? Kwa nini hakuna bima ya

mifugo hapa nchini? Kwa nini mifugo haiwezi kutumika kama dhamana ya kuchukulia mikopo kwenye taasisi za fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ranchi za Taifa *(NARCO) nyingi* zilizobinafsishwa au kuuzwa kwa pupa hadi sasa zimeshindwa kuanza uzalishaji. Je, kwa nini Serikali hairudishi ranchi hizo kwa wananchi wazalendo au kwa Halmashauri ya Wilaya inayomiliki ranchi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa mengi yanayoshambulia wanyama katika nchi yetu bado hayajafanyiwa utafiti wa kutosha. Hata hivyo hakuna wataalam wa kutosha katika fani hii ya mifugo, je, kwa nini Serikali haianzishi vituo vya utafiti wa mifugo kwa kila Mkoa katika nchi hii? Kuna mpango gani mahususi wa kuwasomesha wataalam wengi kwenye fani hii ya mifugo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa kauli gani ya uhakika juu ya migogoro ya muda mrefu baina ya wafugaji na wakulima katika sehemu mbalimbali za nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa mifugo hasa ng'ombe Wilayani Tarime. Suala la wizi wa ng'ombe katika Wilaya ya Tarime ni kero na ndilo husababisha migogoro, mapigano ya koo, uvunjifu wa amani na mauaji ya mara kwa mara. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kukomesha hali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi, kwa nini sekta ya uvuvi haithaminiwi katika nchi yetu? Je, sekta ya uvuvi inalipatia Taifa pato kiasi gani? Je, kuna elimu yoyote imetolewa kwa wavuvi juu ya uvuvi bora? Elimu hiyo imepunguzaje suala la uvuvi haramu? Serikali inatoa ushauri gani juu ya samaki wa Magufuli? Je, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani wa kutoa elimu ya Ukimwi kwenye maeneo ya kambi za wavuvi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikichoma nyavu za wavuvi mara kwa mara, hali hii huwatia umasikini wavuvi. Cha kushangaza ni kwamba hakuna elimu inayotolewa kwa wavuvi juu ya nyavu zipi zinafaa kwa uvuvi. Waziri wa Wizara hii anatoa kauli gani juu ya tatizo hili ambalo limedumu miaka na miaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pia watumishi na viongozi wa mashirika chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara itambue kuwa Jimbo la Hanang ni mojawapo ya Wilaya iliyo na ng'ombe wengi lakini miundombinu yake ni duni sana, hatuna majosho, malambo na hata waganga wa mifugo ni wachache. Ninaomba Wizara itembelee Wilaya ya Hanang kuona tatizo hilo la miundombinu ili hatimaye tuweze kuboresha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawatakia siku njema.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia katika Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la wavuvi Ziwa Tanganyika kwa kuvamiwa mara kwa mara na maharamia wa nchi jirani linazidi kuathiri sekta ya uvuvi Mkoani humo. Mashine zinavamiwa na kuibiwa, wavuvi wanauawa na kujeruhiwa, Halmashauri na Manispaa zinakosa mapato. Hivyo ni vyema Serikali ikajitahidi kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zana duni za uvuvi. Kumekuwa na ukosefu wa vifaa bora vya kisasa hata *nature* ya Ziwa Tanganyika lina kina kirefu hivyo vifaa imara na vya kisasa vinahitajika kwa ajili ya sekta hii ya uvuvi. Napendekeza vijana ambao ndio nguvu kazi kubwa ya Taifa wawezeshwe kwa kuhamasishwa kujiunga katika vikundi hivyo na kupatiwa mikopo ya kununua zana bora za uvuvi na hivyo kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la wanafunzi wa shule za msingi Mkoani Kigoma kujihusisha na uvuvi hivyo kutokwenda shule hasa nyakati za msimu wa samaki wengi Ziwani Tanganyika. Kwa mujibu wa malengo ya milenia ifikapo 2015 inatakiwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule wawe wamepata elimu ya msingi. Serikali ihakikishe utoro wa wanafunzi Mkoani Kigoma kwa kujihusisha na uvuvi unakomeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SELEMANI SAIDI JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara na watumishi wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya, naomba kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara licha ya kusimamia sera, naomba ipewe bajeti ya ujenzi wa mabwawa na majosho ya mifugo ili kuondoa migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Fedha za mabwawa na majosho zikisimamiwa na Wizara husika ya mifugo itasaidia sana kuipunguzia malalamiko Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uwekezaji wa viwanda vya nyama na ngozi upewe kipaumbele ili kuleta ajira kwa vijana na kukuza sekta ya mifugo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba ya mifugo yanayomilikiwa na *NARCO* yajengewe miundombinu ya kutosha na kupatiwa vitendea kazi kama *tractors* ili ranchi hizo ziweze kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu wananchi kutoka Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Geita, Simiyu na Mara, ni wafugaji na wanategemea ufugaji kama chanzo kikubwa cha kipato chao pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji hawa wamekuwa na tatizo la maeneo ya malisho ya mifugo yao jambo ambalo husababisha kutafuta maeneo ya malisho sehemu zingine nchini na kuitwa wavamizi. Endapo Serikali itasaidia wafugaji hawa kwa kuwapatia maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo yao wananchi wa Kanda ya Ziwa wataondokana na tatizo hili sugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa idadi ya watu nchini inaongezeka kila mwaka jambo ambalo ni la kawaida kwa nchi zetu zinazoendelea, ni vema Serikali ifikirie njia mbadala ya kuwawezesha wafugaji kuwa na maeneo ya ziada kwa ajili ya mifugo yao bila kubaguliwa na Watanzania wenzao ambao wamekuwa wakiwalalamikia wafugaji na kuwaita wavamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itumie juhudi za ziada kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi walionyimwa vibali Kibondo. Katika Wilaya ya Kibondo, Mkoani Kigoma, kuna mabwawa saba yaliyoko kwenye Hifadhi ya Moyowosi. Wizara ya Maliasili na Utalii imekuwa ikiwapatia vibali vya kwenda kuvua samaki, lakini ni mwaka wa pili sasa wamezuiwa na hawapewi vibali.

Nimekuwa napata malalamiko kwani Afisa Uvuvi wa Wilaya ya Kibondo amebaki bila kazi. Naiomba Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasli na Utalii ili wananchi hawa waendelee na shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mifugo Wilayani Kibondo. Napenda kupata majibu ya Serikali kwa nini kumekuwa na mifugo kutoka nchi ya Rwanda na Burundi wanaovamia maeneo ya wakulima na maeneo ya Hifadhi Wilayani Kibondo? Lini ng'ombe hawa wataondolewa kwani migogoro inazidi kuongezeka siku hadi siku, katika vijiji vya Kigina, Magarama, Busunzu, Kigendeka, Kisogwe, Kifura na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kupata majibu kwa nini kuna ng'ombe wengi katika Hifadhi/Pori la Mayowosi- Kibondo jambo ambalo linaathiri mazingira na sekta ya utalii, kwani watalii hawapendi kuona ng'ombe kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa ushauri kwa Serikali ifanye uchunguzi/upelelezi dhidi ya tuhuma za rushwa zinazotolewa na wananchi dhidi ya Askari Wanyamapori wanaoruhusu mifugo kwenye hifadhi huku wavuvi na wafugaji nyuki wakizuiwa kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa kisasa na elimu kwa wafugaji. Wananchi wa Tanzania wamegawanyika katika maeneo mbalimbali ya nchi na kufanya kazi kulingana na rasilimali zinazopatikana katika mazingira yao. Maeneo yenye rutuba ya kutosha wanaishi wakulima, maeneo yenye Bahari, Maziwa na Mito kuna wavuvi na maeneo yenye ukame na yasiyokuwa na rutuba ya kutosha wanaishi wafugaji, wafugaji wanafuga kwa ajili ya kulisha familia zao na kuongeza kipato cha familia zao ili kuweza kuwasomesha watoto wao na pia kuongeza pato la taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, wafugaji wamekuwa wakiachwa wakitumia njia za kizamani za ufugaji za kuwa na mifugo mingi bila kuzingatia athari za uharibifu wa mazingira na badala yake wamekuwa wakitangatanga nchi nzima wakizunguka na mifugo yao kutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mapigano makali kati ya wafugaji na wakulima wakigombea ardhi, suluhisho hapa ni kwa Serikali kutilia mkazo wa dhati kwa wafugaji ili kuanza kufuga kisasa. Maana yake wafugaji wote waelimishwe umuhimu wa kufuga mifugo michache kwa mazao mengi na vilevile kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya mazao ya mifugo. Kumekuwa na tatizo kubwa sana la viwanda vya mazao yatokanayo na mifugo katika maeneo ya wafugaji. Tanzania inaagiza nyama, maziwa viatu, mikanda ya suruali, mabegi ya ngozi toka nje wakati ina mifugo mengi na ya kutosha kuweza *ku-supply* malighafi ya ngozi, nyama na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzalisha vyote hivi kuanzishwa kwa viwanda vya kusindika nyama, maziwa na mazao ya ngozi kutawafanya wafugaji kufuga kisasa na kupunguza mifugo yao *automatically* kwani watakuwa na soko la kutosha na hivyo kuongeza pato la Taifa. Ningeishauri Serikali kuanzisha viwanda na sio machinjio ya kisasa pekee hasa katika Mikoa ya Singida, Manyara, Shinyanga, Arusha na Dodoma ambayo inaongoza kwa ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi, ni kwa nini mpaka sasa Tanzania imeendelea kupokea samaki toka nje ya nchi wakati ina samaki wa kutosha kutoka vyanzo vyake vya maji vilivyopo? Tumeshuhudia samaki wanaotoka nje hasa Japan wanaosadikiwa kuwa na madhara na wananchi bila kujua wanakuwa wakitumia kitoweo hicho. Je, ni kwa nini tusidhibiti uagizaji huu wa samaki na badala yake tutilie mkazo kwenye uvuvi wa kisasa na kuwaelimisha wavuvi wetu na hasa tukianzia na ufundishaji wa uvuvi bora mashuleni sambamba na ufugaji bora wa samaki na wanyama wafugwao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala lingine linalojitokeza ni uvuvi haramu unaotumia baruti na

nyavu zilizo chini ya kiwango, je, ni kweli kwamba Serikali imeshindwa kuzuia huu uvuvi haramu unaoendelea kila kukicha au tuamini maneno yanayozungumzwa kwamba wavuvi haramu wana mkono wa wakubwa Serikalini na wanalindwa? Kama hii si kweli, naishauri Serikali ilifuatilie kwa undani suala hili maana linaibua hisia mbaya kwa wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la viwanda vinavyouza nyavu ambazo hazistahili kutumiwa na wavuvi ni kwa nini wanaoadhibiwa kila mara wanakuwa ni wavuvi peke yao ambao hununua nyavu hizo viwandani wakati viwanda vinakaguliwa ubora na *TBS*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini wenye viwanda hivi wasichukuliwe hatua za kisheria ikiwepo ya kufungiwa viwanda vyao na kulipa fidia kwa kusababisha uharibifu wa mazingira na kuharibu viumbe vya baharini kwa makusudi? Kwa nini sheria inaangalia mtumiaji peke yake ambaye anakuwa ni mvuvi maskini anayejitafutia riziki yake na haiangalii yule mzalishaji wa vitendea kazi? Serikali ilifanyie kazi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni wakati sasa kwa Serikali kuanza kutilia mkazo sekta hii ya uvuvi maana imeonesha kuwa ni sekta iliyotelekezwa na haitendewi haki ipasavyo. Vijana wengi wanamaliza shule hasa wanaishi maeneo ya Pwani huishia kwenye uvuvi hivyo Serikali ilitupie eneo hili la uvuvi liwe ni ajira tosha na yenye uhakika na

kuondoa wimbi la vijana kukimbilia mjini na kufanya kazi zinazowadhalilisha. Serikali inatakiwa ianze kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya vijana na kuwakopesha zana za uvuvi za kisasa ili wajiajiri na kujipatia kipato ili kuinua hali zao za uchumi na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kuwa bajeti ya Wizara hii kuendelea kupungua kila mwaka hali hii imefanya sekta ya mifugo kuendelea kushuka na hali za wafugaji kuwa duni kiasi kwamba hawanufaiki na mifugo. Mifugo ina uwezo wa kuleta utajiri katika nchi hii kama ilivyo utalii au madini kwani Tanzania imesambaa katika Mikoa mingi nchini, kama Tanzania isingekuwa na mifugo ingebidi nchi iwe inaagiza nyama kutoka nchi za nje ili kulisha Watanzania milioni 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ilisaidie Shirika la *NARCO* ili liweze kuimarika kwa kulipatia fedha ya kujiimarisha. Uongozi uliopo *NARCO* bado ni mpya sana na siyo vema kulaumiwa kuwa umeshindwa kuifufua NARCO. Naomba shilingi bilioni 10 walizoomba wapewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iongeze bajeti ili kufundisha na kuwawezesha wafugaji wa samaki. Nchi ndogo kama Vietnam inapata fedha nyingi kutokana na ufugaji wa samaki. Tanzania imebahatika kuwa na bahari pamoja na maziwa na bado vingetumiwa vizuri kufuga samaki wananchi wangekuwa na hali nzuri ya kiuchumi na pato la Taifa

lingeongezeka. Mpango wa Serikali wa kuendeleza ufugaji wa samaki utekelezwe na usiishie kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya ufugaji na ukulima v*/s* maeneo ya ukulima (mazao) na ufugaji. Nchi yetu itaendelea kuwa na wafugaji na wakulima katika ardhi yake. Jambo la msingi ni mgawanyo wa maeneo haya kwa kuzingatia mahitaji na uwiano. Wafugaji na wakulima *for ages* wame-*co-exist* katika nchi hizi hapakuwahi katika miaka mingi iliyopita kutokea mizozo ya ardhi baina ya makundi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba yapo mambo mapya yaliyojitokeza mfano kuongezeka kwa mifugo kwa idadi-kiholela bila umakini wa ufugaji bora wa kuzingatia mifugo michache "*optimum*" kwa tija zaidi. Mabadiliko ya hali ya hewa hususan tabia nchi kwa ujumla, kusababisha changamoto ya uhaba wa malisho, kuongezeka kwa mahitaji ya maeneo ya kulima kwa wakulima, ukiukaji wa makubaliano ya sheria zilizopo juu ya maeneo tengefu ya ufugaji na yale ya ukulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na masuala niliyoyaorodhesha hapo juu, ni wazi kwamba ipo haja kwa Serikali kuchukua hatua za makusudi, muafaka na haraka ili kudhibiti mizozo inayoendelea sasa katika maeneo mbalimbali ya nchi. Bila hatua hizo, mizozo

ya sasa inaweza kukua na kuongezeka na hata kusambaa nchini hivyo kuhatarisha amani ya nchi kama ilivyoanza kujitokeza kule Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

(i) Wafugaji wafuge kwa ushauri wa kitaalamu, mifugo michache kwa tija.

(ii) Ufugaji holela wa kuharibu maeneo na kuhamia katika maeneo mengine uachwe. Ni vema maeneo yanayoathirika yafanyiwe kazi ili yaendelee kufaa kwa matumizi ya malisho.

(iii) Maeneo tengefu yaainishwe zaidi na yasimamiwe katika matumizi.

(iv) Maeneo ya wakulima yasiingiliwe.

(v) Utii wa sheria ni lazima uzingatiwe.

(vi) Sensa ya mifugo na uwiano wa maeneo yanayotengwa ni muhimu sana ifanyike ili kubaini utoshelezaji.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua jitihada mbalimbali zinazofanywa na Wizara katika kutimiza wajibu wake. Vijana wengi wa jamii ya kifugaji wamekuwa wakilalamika, kutopewa msaada ili kujikwamua na umaskini. Je, Wizara ina mikakati gani ya kuwawezesha vijana wanaotoka katika jamii ya wafugaji hasa kuhakikisha wanapata mitaji ya kufuga ng'ombe wa kisasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa Mkoa wa Mara wamekuwa wakisikia program za Wizara za kuwasaidia vijana wanaojishughulisha na uvuvi. Binafsi kama Mbunge wa vijana, nimekuwa nikiwahamasisha vijana kujiunga katika kupata nyenzo bora za kuvulia samaki. Je, Wizara hii itawasaidia vijana wa Mkoa wa Mara na kanda ya Ziwa kwa ujumla kwa kuwapa zana bora za kuvulia samaki ili waondokane na uvuvu haramu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inashirikiana vipi na Wizara ya Kilimo/na Ardhi ili kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imeshika kasi na kuendelea kuleta maafa katika maeneo husika?

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono bajeti ingawaje haikidhi mahitaji ya sekta hii ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, suala la wataalamu wa mifugo vijijini, ni vema Serikali ikazalisha zaidi wataalamu hao ili waweze kuwasaidia wafugaji kuhakikisha wanakuwa na mifugo bora na kuwapatia ushauri utakaowawezesha kutunza mifugo yao vizuri kwa kuiboresha ili iwe inapata soko zuri na kuwaongezea kipato chao. Aidha, kuendelea kutumika wataalamu wa kilimo/mifugo wapo baadhi yao wanaegemea zaidi kwenye kilimo na kushindwa kuwahudumia ipasavyo wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, migogoro ya ardhi, ni wakati muafaka sasa Serikali ikaacha kueleza wanaendelea kutenga maeneo ya wakulima na

wafugaji, bali ifike mwisho na kulieleza Bunge hili ni maeneo kiasi gani kila Mkoa wenye wafugaji yametengwa ili kuondokana na migogoro ambayo imekuwa ikizuka mara kwa mara. Hii itawasaidia wananchi wafugaji/wakulima kujiona wapo huru na wanaishi katika nchi yao huru yenye amani tele.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali kwa kazi nzuri inayofanya juu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie, kule Njombe kijiji cha Mhasi, kuna bwawa kubwa na linawasaidia sana wananchi wa maeneo hayo kwa kujipatia kitoweo cha samaki. Kwa nini Serikali isiboreshe ili bwawa hilo liweze kutoa samaki kwa wingi? Pia liko eneo lingine kama hilo kule Lupembe, Juwa na Mahera. Naomba Serikali iyape kipaumbele haya niliyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia machache katika hotuba hii ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na matatizo mengi yanayotokana na migogoro baina ya wafugaji na wakulima kama inavyoendelea katika

Wilaya ya Rufiji katika maeneo ya Ikwiriri, Ngorongo na Maparoni na tatizo kubwa ni wafugaji kukaa katika maeneo ya wakulima ambayo hayajatengwa kwa ajili ya malisho ya mifugo. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa migogoro kati ya wakulima na wafugaji inayoendelea Rufiji inapatiwa ufumbuzi ili kunusuru maisha ya Wanarufiji ambao wanafariki kutokana na kupigwa na wafugaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi mwaka 2011/2012, aliahidi kuchimba mabwawa ya kufugia samaki katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani ikiwemo Wilaya ya Rufiji lakini hadi sasa hakuna hata dalili ya utekelezaji. Je, ahadi ya Serikali kuchimba mabwawa ya kufugia samaki imefikia katika hatua gani ya utekelezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitunga sera na sheria mbalimbali kwa upande wa mifugo lakini sheria na sera hizi hazitekelezwi na hivyo husababisha migogoro baina ya wafugaji na wakulima kuendelea kutokea kila kukicha. Je, Wizara inawaeleza nini wananchi ambao wanaathirika na migogoro hii kwa kupata ulemavu ama wanafamilia ambayo wamepoteza ndugu zao (kufariki) kutokana na migororo hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika (vijiji vya Kalalangabo, Kigalye, Mtanga, Mwangongo, Bugamba, Kiziba, Zashe), wananchi wanategemea uvuvi peke yake kwa ajili ya maisha yao. Wizara

isaidie juhudi za kuboresha uvuvi katika eneo hili kwa kutoa vyombo vya uvuvi vya kisasa kwa njia ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile uchakataji wa samaki na dagaa ufanywe na viwanda vidogovidogo *(cottage industry*) hukohuko vijijini ili kuzalisha ajira vijijini. Wananchi waelimishwe kufanya uchakataji kwa kutumia teknolojia rahisi. Ninashauri Wizara iwe na miradi ya mfano kwa kuchukua kijiji kimojawapo (mfano kijiji cha Mtanga) na kuwezesha uchakataji wa samaki na dagaa na kufanya *packaging*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kuanzishwe Mamlaka ya Uvuvi Tanzania ili kusimamia sekta uvuvi, kusajili wavuvi, kutoa leseni na kuendeleza sekta ya uvuvi nchini. Mamlaka pia isaidie kuendeleza masoko ya bidhaa za uvuvi nchini na duniani.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongoza ujumbe wa Serikali yetu kutembelea China (*PRC)* na washirika walitoka Bara (kilimo cha chai) na Visiwani (uvuvi). Tulitembelea pia chuo kikuu cha Shanghai hasa Idara ya Uvuvi. Taarifa tulizopata Ubalozini Beijing na wanafunzi chuoni hapo wote wanatoka Zanzibar, ingawa Bara pia tulikaribishwa kupeleka wanafunzi na hatukujibu mwaliko huo, je, wataalam wa uvuvi tumejitosheleza Wizarani hadi kukataa *scholarships*

hizo? Nipate majibu maana Igalula tunahitaji wataalam ili tufuge samaki katika mabwawa na mito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuku wa kienyeji ni pato zuri kwa vijiji vyetu Igalula na kwingineko, pia ni lishe bora. Jitihada ziongezwe tupate wafugaji wengi kwa kuwa na Maafisa Ugani kwani masoko yapo, uwezo ujengwe kwa ufugaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Kituo cha Uhamilishaji Mifugo Tabora kituhudumie pia Jimbo la Igalula. Idadi ya mifugo imezidi uwezo wa malisho Jimboni hivyo tufuge kisasa na kibiashara. Mazingira yanathirika hasa sehemu oevu na vyanzo vya maji na mito inakauka. Hivyo elimu itolewe tupate wafugaji na si wachungaji, ng'ombe bora watatoa tija, maziwa mengi na nyama nyingi na bora. Tunahitaji Maafisa Ugani na Mashamba Darasa wenye ng'ombe bora. Kilolo nikiwa Mkuu wa Wilaya nilikuwa na wafugaji wenye ng'ombe mmoja 1000kg uzito na maziwa 35 lts kwa siku, naomba utaalam huu pia uje Igalula, Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa ya kufuga samaki. *DADPS* sawa lakini tangu 2009 bado hakuna bwawa Igalula, Loya tu ndiyo upo mradi wa umwagiliaji. Pato litaongezeka kama mabwawa ya Nsololo, Jirani Nyahua (Sikonge), Kizengi yatafufuliwa tupate maji kwa mifugo, kufuga samaki, matumizi ya watu na umwagiliaji pia visima vichimbwe kwa maji ya mifugo na binadamu. Uyui Mheshimiwa Waziri hakuhitaji ng'ombe kutoka Mwanza, Shinyanga, sasa wapo Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Ilolwansimba Isikizwa, Oktoba 29, 2010 kuwa maeneo ya Igalula yatapandwa majani ya malisho bado haijatekelezwa, lini itatekelezwa?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, machinjio ya ng'ombe, mbuzi, nguruwe na kadhalika. Machinjio nyingi hapa nchini hasa machinjio za Dar es Salaam (Vingunguti) ziko katika hali mbaya sana, mazingira machafu na hata wafanyakazi wa machinjio hizo ambao wanapaswa wawe wasafi wengi wao ni wachafu sana. Hali hiyo ya machinjio hizo inahatarisha hata nyama yenyewe na afya za walaji wenyewe. Nashauri Wizara ihakikishe kwamba inafuatilia hali za machinjio zote nchini kote, hali za watumishi wa machinjio hizo ili kumlinda mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ya mlipuko kwa mifugo. Mwaka juzi ulitokea ugonjwa wa mlipuko katika Mikoa ya Mbeya na Iringa, ugonjwa huo uliua nguruwe wengi sana. Baadhi ya wafugaji walipoteza mifugo yao yote na hivyo kubaki maskini kabisa. Ili kukabiliana na hali hiyo huko mbeleni, naomba Wizara ijiandae vizuri kukabiliana na magonjwa ya mlipuko. Aidha, elimu ya ufugaji bora itolewe kwa wafugaji wote nchini, kwa kufanya hivyo wafugaji watakwepa magonjwa kwa mifugo yao yanayosababishwa na mazingira mabaya ya ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza viongozi wa Wizara kwa kazi nzuri ya kusimamia Wizara hasa katika maeneo ya uvuvi haramu na pia ufugaji wa kisasa hasa kiwanda cha *Tanga Fresh* kupewa eneo la kuendeleza mifugo bora kwa nia ya kuwapatia wafugaji wadogowadogo madume, mbegu bora na mitamba ya kisasa/bora, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika Wizara hii ni katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi, nashauri Wizara isaidie kwa kuwawezesha vijana wetu maeneo ya milimani ambayo kuna uhaba wa ardhi kuelimishwa uanzishaji ufugaji wa samaki kwa kuchimba mabwawa madogo madogo ya samaki. Utaratibu huu utawawezesha vijana kupata ajira, Serikali isaidie mbegu bora ya samaki na mitaji midogomidogo ya kununulia vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la maziwa, kiwanda cha *Tanga Fresh* kwa sasa wanakusanya na kusindika zaidi ya lita 50,000. Ongezeko la ukusanyaji na usindikaji maziwa unaambatana na uwezo wa kuhifadhi maziwa hayo kabla ya kuyafikisha kiwandani. Naomba Wizara iwezeshe vikundi vya ufugaji na uuzaji wa maziwa kwa kuwapatia vifaa vya kuhifadhia maziwa. Katika Wilaya

ya Lushoto vikundi hivyo vipo, maziwa yanayokusanywa ni kidogo sana kutokana na uhaba wa vituo vya kukusanyia maziwa hii husababishwa na uwezo mdogo wa kuhifadhi maziwa katika vituo hivyo, maziwa mengi kukosa soko, maziwa yakikusanywa kwa wingi bei kwa wafugaji itapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uuzaji wa mifugo/ nyama nje ya nchi. Pamoja na juhudi za kuanzisha machinjio mengi kote nchini, bado jitihada zinahitajika katika kukuza soko la mauzo ya mazao ya mifugo nje ya nchi. Kuna umuhimu wa kuongeza maeneo ya unenepeshaji ng'ombe ili kupata mifugo bora ya kuchinja kwa kulenga soko la nje. Naamini juhudi zikiongezeka, mifugo itaingiza fedha za kigeni kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu kuhusu Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Wizara hii ni nyeti sana kwa ustawi wa jamii ya wafugaji na uvuvi. Tanzania ni nchi ambayo imekuwa na mifugo mingi sana Afrika na ikitumika vizuri itainua pato la Taifa na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo ambalo limekuwa likiwafanya wafugaji kutofaidika na mifugo yao. Masoko yao hakuna kutokana na viwanda vya ngozi, nyama na maziwa kutokuwepo kabisa. Hili ni tatizo ambalo linapoteza uthamani wa kuwa na wafugaji wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa inayoongoza kwa ufugaji, kuna tatizo kubwa la vituo vya utafiti, majosho na malisho kwa ajili ya mifugo. Hii inaleta migogoro mingi baina ya wafugaji na wakulima kwa kutokutengewa maeneo ya kulishia mifugo, ni hatari sana kwani Tanzania ina eneo kubwa sana ambalo liko wazi ili kuepukana na migogoro hii Wizara/Serikali ione haja ya kutenga maeneo kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwapo na vituo vichache vya utafiti wa magonjwa ya mifugo, hii inaletea mifugo mingi kupoteza uhai kutokana na magonjwa. Aidha, vituo hivi viko mbali sana na maeneo ya wafugaji. Ninaomba sana Serikali ione haja ya kujenga vituo hivi maeneo yenye mifugo mingi ili kuepusha usumbufu kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya kuwepo na uhaba wa majosho kwa ajili ya kuoshea mifugo ni tatizo linaloathiri kwa kiasi kikubwa mifugo. Wizara/Serikali iweke mkakati wa kuweka majosho *at least* kila kata kwenye maeneo yenye wafugaji wengi hii itaongeza uzalishaji wa mifugo bora na isiyo na maradhi yatokanayo na kupe, viroboto na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi, nchi yetu imejaliwa kuwa na maziwa kila upande na bahari kwa upande wa Mashariki, lakini uvuvi sijaona kama unaleta kipato kikubwa kwa wavuvi na hata kuliingizia Taifa pato. Zaidi ninaona wawekezaji wachache wenye viwanda vya kusindika samaki ndio wanaofaidika kwani wamekuwa miungu watu kwa kupanga bei

wanapojisikia na kuwaumiza wafanyabiashara wadogo wa samaki na wavuvi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi ukizingatiwa nchi hii itafaidika pamoja na kuleta ustawi mzuri kwa wavuvi. Kumekuwa na tatizo la kuchoma nyavu za wavuvi na kuwaacha watengenezaji wa nyavu hizo wakiendelea kutengeneza nyavu hizo. Ninaitaka Serikali iniambie ni viwanda vipi vinavyotengeneza nyavu hizo haramu na vingapi mpaka sasa vimeshachukuliwa hatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba wavuvi wapatiwe zana za kisasa ili waweze kuvua kisasa na kuongezea kipato kwa familia zao pamoja na Taifa kwa ujumla. Pia Serikali ione sasa umuhimu wa kujenga viwanda vya kusindika samaki katika maeneo ya uvuvi ili kuongeza ajira kwa vijana wengi ambao mpaka leo hii kuna idadi kubwa sana ya kundi lisilo na ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nipongeze Wizara kwa maandalizi mazuri ya bajeti. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuandaa bajeti na utendaji wao mzuri katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa katika maeneo yafuatayo; uandaaji mbaya wa nyama katika jijiji la Dar es Salaam, uagizaji (kuingiza) nyama, samaki kutoka nje na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandaaji mbaya wa nyama. Napenda nitoe pongezi kwa Mkoa wa Dodoma kwa kuwa na mabucha mazuri sana yanayozingatia afya ya wananchi wake. Nyama Dodoma inaandaliwa vizuri sana, naomba Serikali tukishirikiana na Halmashauri kufanya juhudi za makusudi kubadilisha Mkoa wa Dar es Salaam nao uwe na mabucha mazuri na zana nzuri za kukatia nyama kama wanavyofanya Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uingizwaji wa nyama, samaki, maziwa na mayai toka nje ya nchi. Serikali idhibiti uingizaji wa bidhaa hizi kutoka nje tutunze soko letu la ndani. Tanzania inazo ng'ombe, samaki na mayai ya kutosha kuna haja gani kupokea kutoka nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi harama. Serikali ifanye juhudi za makusudi kukomesha uvuvi haramu. Samaki zinazopigwa mabomu zinaleta athari kubwa kwa binadamu. Doria ziendelee kufanya kazi na Polisi Jamii kukomesha tabia mbaya kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. RADHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuchangia kwa njia ya maandishi. Pia ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walio wengi wanaendesha maisha yao kwa kutegemea mifugo na uvuvi na kwa maana hiyo Wizara inaonekana haijajipanga vizuri katika eneo lake ili kuwawezesha wafugaji na wavuvi kujitegemea kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za mifugo ng‘ombe (majike) ni kubwa na wafugaji wengi wanashindwa kununua na hivyo wafugaji wengi wanafuga ng‘ombe wa kienyeji kama vile jamii ya Masai na kadhalika. Hivyo, naiomba Wizara iongeze uzalishaji wa ng‘ombe wa maziwa na wa nyama na kupunguza bei ili wafugaji waweze kununua na kuendeleza mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula cha Mifugo (ng‘ombe na kuku). Chakula cha mifugo pia ni ghali, wakulima wa mifugo wanatumia gharama kubwa kununulia chakula cha mifugo na hivyo kushindwa kupata faida inayoendana na kazi zao. Hivyo, naiomba Wizara kuangalia hili kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya ufugaji. Ni jambo lisilopingika kuwa kuna migogoro ya maendeleo ya ufugaji kwa maana ya ardhi na hii inawavunja moyo wafugaji. Kwa hiyo, naishauri Wizara kuangalia vyema kuwapatia wafugaji maeneo maalum ya ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa magonjwa. Wafugaji wengi wanapoteza mifugo yao kutokana na magonjwa mbalimbali. Wizara hii bado haijajipanga upya kukabiliana na matatizo hayo na hii inairudisha

nyuma juhudi za wafugaji Tanzania. Hii inatokea kwa kutokuwa makini kwa mifugo inayoingia nchini, hivyo Wizara hii ni vyema iwe makini katika kudhibiti magonjwa hasa kutoka nchi jirani, hii itawasaidia wafugaji kupata maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya siku ya leo na kuweza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu kumekuwa na matatizo ya wavuvi kutoka Zanzibar hususan Pemba wanapokuja kuvua Tanzania Bara. Wavuvi hawa wanapata usumbufu mkubwa wa kudaiwa na kulazimishwa kuleta leseni za shughuli za uvuvi huku wakiwa tayari wana leseni za uvuvi pamoja na vyombo vyao walivyopatiwa toka Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwalazimisha wavuvi hawa kukata leseni kwa mara ya pili kwa kweli ni usumbufu mkubwa kwa wavuvi hawa hasa ukichukulia vigezo vya usafiri wa juu (yaani gari) dereva anayepata leseni ya udereva Zanzibar halazimiki kukata leseni nyingine Tanzania Bara. Hili ningeliomba lipatiwe ufumbuzi ili kupunguza usumbufu huo kwa wavuvi toka Zanzibar. Aidha, Wizara inaweza ikawasiliana na Wizara ya Uvuvi Zanzibar ili kulitafutia utaratibu mzuri suala hili kwa faida ya pande zote mbili lakini pia kwa faida ya wavuvi wetu ambao ni maskini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu mahusiano na mashirikiano baina ya Wizara ya Uvuvi Tanzania Bara na ile ya Zanzibar. Katika miaka ya 80 na 90 kulikuwa na mashirikiano makubwa baina ya pande hizi mbili za muungano, hasa katika maeneo ya utafiti, elimu na taarifa muhimu. Uhusiano na mashirikiano haya kwa sasa yamepungua sana na hivyo kudhoofisha uimara na umakini katika utekelezaji wa shughuli za Baharini. Tutake tusitake bahari yetu ni moja kwa hiyo ili kuitendea haki katika kuilinda na kuihifadhi rasilimali hii muhimu ni lazima pande hizi mbili zijenge mashirikiano makubwa. Hivyo napenda kushauri kuwa uhusiano uliokuwepo urudi kama zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *MACEMP* ni mradi ambao ulitumia pesa nyingi kwa ajili ya uhifadhi wa rasilimali za baharini. Mradi huu umeleta faida kubwa za kijamii na kimazingira. Hata hivyo, kwa sasa mradi huu umemaliza muda wake, sijui Serikali imejipanga katika kuweka mikakati endelevu ya kuhakikisha kuwa yale yaliyofanyika yanaendelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha, ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Tanzania kuwa nchi ya tatu kwa kuwa na idadi ya mifugo mingi

duniani bado sekta ya mifugo na uvuvi haijaweza kuchangia kikamilifu pato la Taifa. Ni jambo la kusikitisha kuona sekta hii mchango wake kwa pato la Taifa unapungua kila mwaka. Sikubaliani na maelezo ya Waziri kwamba kupungua kwa mchango wa sekta hii kumesababishwa na kukua kwa sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa la msingi la Serikali kutoangalia ufugaji kwa ujumla wake kuanzia ngazi ya kijiji hadi Taifa, maeneo yanayotengwa kwa ajili ya malisho ya mifugo ni kidogo sana hayajakidhi mahitaji ya mifugo iliyopo kwenye maeneo hayo, wataalamu wa mifugo ni wachache sana na hata hao waliopo hawana vitendea kazi vya kusafiria kama pikipiki, magari ili watembelee wafugaji na kuelimisha ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna elimu inayotolewa vijijini, wafugaji waandae vyakula vya akiba vya mifugo kama *silage, hays*, mchanganyiko wa pumba, *cotton seed cake* na kadhalika. Serikali ieleze Bunge maeneo gani, Mikoa ipi, wafugaji wanatengeneza *hays* na *silage* ili kuepuka mifugo kukosa malisho kiangazi?

Mheshimiwa Spika, masoko ya mazao ya mifugo ni tatizo kubwa sana. Mifugo mingi inauzwa Kenya kwa bei ndogo sana. Wao wanasindika nyama, wana-*pack,* wana-*export* maziwa, wanachukua kwa bei ya bure, wana-*pack* vizuri wanaleta kwenye *super market* zetu humu nchini kwa bei ghali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo kuku za kienyeji wengi sana na mayai kwenye Mikoa mingi hapa

nchini, ni kwa nini kwenye mahoteli yote ya kitalii hapa nchini wanaagiza nyama kutoka nje na mayai kutoka nje wakati bidhaa hizo tunazo kwa wingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la Watanzania kutokuwa na utamaduni wa kunywa maziwa kwa afya zao. Serikali ina mpango gani makini wa kuhakikisha kila Mtanzania anakunywa maziwa yanayotokana na mifugo yetu? Hii ni ili tuweze kupata soko zuri kwa mazao ya mifugo lakini pia kuinua kipato cha wafugaji na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupandisha ushuru wa kuuza ngozi ghafi nje kwa 90% bila kufufua viwanda vya ngozi hapa nchini haina tija kubwa kwa Taifa na haitasaidia kuhakikisha ngozi haziozi. Viwanda vya ngozi vilivyoko hapa nchini vyote vifufuliwe kikiwepo cha Kibaha, Moshi, Shinyanga, Arusha, Tabora na kadhalika ili ngozi yote inayopatikana iweze kusindikwa, tutengeneze bidhaa, tuuze nje na ndani siyo kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kuweka kodi kwenye vifaa, *equipment* za madokta wa mifugo, hatukubaliani nalo. Hili litarudi kuleta ugumu kwenye huduma za mifugo. Madaktari wa mifugo wako wachache na wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Badala ya Serikali kuangalia jinsi ya kuwasaidia, wanaongeza ugumu. Hivi kweli Serikali ina mpango thabiti wa kuinua sekta hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza ushuru kwenye vyombo vya uchimbaji wa visima na malambo, ni

kutoona umuhimu wa malambo kwa maendeleo ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imeshindwa kuthibiti uvuvi haramu unaofanywa na meli kubwa kutoka mataifa ya mbali katika eneo letu la bahari. Wanavuna na kuondoka na mamilioni ya samaki bila kulipa chochote kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeshindwa hata kuanzisha Bandari ya Samaki anagalu tuuze mafuta ya meli, wavuvi wangelazimika kuja kujaza mafuta kwenye Bandari yetu lakini pia tungeweza kuwafuatilia. Hili ni shamba la bibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwawezeshe wavuvi wadogo wadogo kupata vifaa bora wavue kisasa na waongeze pato.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii ili niweze kutoa maoni yangu katika bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina rasilimali nyingi kwa kuwa na Bahari, Mito na Maziwa, lakini hatujafanya vya kutosha kuhakikisha kuwa nchi inafaidika na rasilimali hizi za maji. Suala la uvuvi bado halitiliwi mkazo kwa kuwekeza vifaa vya kisasa ili kuhakikisha pato la Taifa linaongezeka kutokana na sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mipaka yetu ya majini hailindwi vya kutosha na hivyo kusababisha uvuvi wa wizi katika bahari kuu unaofanywa na nchi

zilizoendelea zaidi katika sekta ya uvuvi. Mfano mmoja ni samaki wanaojulikana kama wa Magufuli, hii ni meli moja tu ilikamatwa ikifanya wizi wa samaki katika bahari yetu. Hivi ni meli ngapi zinakuja kuvua na kuondoka bila kukamatwa? Tumejiimarisha kiasi gani kiulinzi katika eneo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu haina viwanda vya kusindika nyama kama ilivyokuwa miaka ya nyuma. Jambo hili linawanyima wafugaji wetu soko la uhakika la mifugo yao na hasa suala la ufugaji bora linakuwa halizingatiwi sana kwani soko lililopo ni la kienyeji ambapo viwango vya ubora havizingatiwi sana. Ni wakati muafaka sasa Serikali ikafufua viwanda vya kusindika nyama na kuvirejesha vile ambavyo waliuziwa wawekezaji ambao hawajaviendeleza mfano Tanganyika *Packers* ya Kawe jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuwahakikishia wafugaji soko la uhakika pia Wizara iwekeze vya kutosha kwa dawa za mifugo na majosho ili kuhakikisha ubora wa mifugo yetu na mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. VITA R.M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mathayo David Mathayo na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ole-Nangoro, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa kushirikiana kuandaa bajeti yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sekta hii ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu na wananchi wake na imekua mwaka hadi mwaka kwa mfano wa mwaka huu uliopita imekua kwa 3.9% na kuchangia katika pato la taifa kwa 3.7%. Kwa umuhimu wake, hatuna budi tutekeleze mipango tunayoipanga kwa kusimamia utekelezaji wake vizuri na tufikie malengo tunayokusudia mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ahadi za kufufua viwanda vya kusindika nyama na kuanzisha vingine mwaka hadi mwaka. Naomba kuwe na mpango mkakati unaotekelezeka kukabiliana na soko la nyama inayosindikwa kwa viwango ili tuwe na soko la nyama badala ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu pia nauelekeza katika kuwekeza kwenye viwanda vya kusindika samaki katika pwani yetu ya Bahari ya Hindi ili tuweze kuongeza thamani ya samaki wa baharini na hivyo itapunguza kuvamiwa katika bahari yetu na meli za wavuvi haramu ambao wanatupotezea mapato mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutangaze eneo hili kuwa la uwekezaji viwanda vikubwa vya kusindika samaki katika maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi kwa nguvu zote ili wawekezaji wa sekta hii walio katika nchi mbalimbali waweze kufahamu fursa iliyopo na waje kuwekeza. Hii itasaidia kuendelea na kukua kwa mchango wa pato la Taifa na kuondokana na kupanda na kushuka kama ilivyo katika mwaka huu

kuwa 3.7% ikilinganishwa na mwaka 2010 sekta ilichangia asilimia 3.8 katika pato la Taifa. Fursa hii ipo na uwezo wa kuitangaza kwa wawekezaji tunao tufanye kwa kushirikiana na kujiamini tutaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Namtumbo ni Jimbo ambalo tumehamasisha na tumetoa ng'ombe wa miradi ya kopa ng'ombe lipa ng'ombe ili kuwezesha kila kaya kuwa na ng'ombe na kufuga ili kuboresha afya zao na kipato. Pia kuna baadhi ya mifugo iliyohamia kwa wingi kutoka katika maeneo iliyohamishwa na Serikali, tunaomba Serikali ielewe na ituweke katika mipango ya Wizara ya kuisaidia kitaalam na dawa za kusaidia ng'ombe wa kaya na pia kutoa elimu kwa wafugaji wavamizi katika maeneo ya kilimo waweze kuelewa umuhimu wa kuwa pamoja bila mingongano inayoweza kuepukika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mifugo ni sekta muhimu kiuchumi, nashauri:-

(i) Wataalm wa mifugo wawepo katika kila kata, kutekeleza sera na nia ya ufugaji bora.

(ii) Kila Halmashauri itunge *By laws* kwamba wanyama mnadani wauzwe kwa mizani, kilo.

(iii) Wafugaji wa ng'ombe wa Mikoa ya Manyara na Arusha hasa Mbulu, Loliondo na Ngorongoro

wawezeshwe kuwa na machinjio ya nyama za kusafirishwa nje (*export)* kwenda Dubai.

(iv) Mwisho Serikali imekataza ng'ombe kuswagwa kwa miguu kutoka Shinyanga na Mbulu, wabebwe kwa magari hadi sokoni. Ingependeza kupitia barabara za lami.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kutuumba na akatujalia tukawa ndani ya ardhi iliojaa Mito, Maziwa, Bahari kubwa na eneo kubwa la ardhi kwa ajili ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo letu Watanzania ni kutojali na ama kutothamini neema hii ya ardhi na vilivyomo, jambo ambalo linapelekea hata matokeo yake sio mazuri sana kwani neema hiyo hatujaitumia ipasavyo. Kilimo chetu bado sio kilimo chenye tija sana ukilinganisha na hali halisi ya eneo kubwa lenye rutuba tulilonalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,lakini pia tumeshindwa kuyaongezea thamani mazao tunayozalisha kabla ya kuyauza nje jambo ambalo lingeongeza pia ajira kwa vijana wa Kitanzania, pia bado tuna tatizo la viwanda ambavyo vinamsukumo mkubwa katika kuliongezea thamani zao la kilimo pamoja na ajira kwa Watanzania, vilevile kukosekana kwa miundombinu ya uhakika hasa katika yale maeneo ya wakulima, hili pia ni tatizo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiwango tulichonacho cha mifugo katika nchi hii, inashangaza kwamba bado Serikali haijaona kuna haja ya kuwepo kwa viwanda vya nyama lakini pia machinjio ya kisasa lakini pia viwanda vya kukausha ngozi ili bidhaa hizi ziweze kuongezewa thamani lakini vilevile wafugaji waweze kuongeza vipato vyao pamoja na ongezeko la ajira kwa wananchi wetu. Kukosekana kwa vitu kama hivyo hapa kwetu, wenzetu wa Kenya wanachukua nafasi hii na kujifaidisha kwa kuuza nyama ya Tanzania na ngozi walizoziongezea thamani na kulipatia Taifa lao na wananchi wa Kenya fedha za kigeni na kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tungali tuna tatizo la kutotumia vyema Mito, Maziwa na Bahari kubwa iliyotuzunguka. Tatizo bado lipo la kuichezea bahari hii Mungu aliyotujaalia na kwa mwendo huu wa kusuasua tutachelewa sana kuyafikia mafanikio yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa samaki katika bahari kubwa na hata kwenye maziwa bado haujawafaidisha Watanzania hasa ukilinganisha kwamba samaki wengi sana hawajavuliwa lakini pia hata hao wachache tunaovua bado hatujaweza kuwaongezea thamani na tatizo hili linapelekea bado Wakenya kujifaidisha kwa kununua samaki wetu, kuwaongezea thamani na kuwauza nje na kuweza kujipatia fedha nyingi kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la kutoa lawama zaidi lakini hatuangalii ni vipi tutaweza kupiga hatua ya kukabiliana na matatizo yetu. Suala la kukosa kabisa uwezo wa kuvua samaki katika bahari kuu hili ni

tatizo. Hebu Serikali ituambie ina mpango gani wa kuanzisha uvuvi wa bahari kuu na kwamba itanunua meli za uvuvi ili vijana wawe na mategemeo ya kuweza kupata ajira au kazi katika meli hizo lakini pia tuondoe tatizo la kulalamikia wizi unaofanywa na wageni ndani ya maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la unyanyasaji kwa wavuvi wanaotoka Zanzibar katika Bandari za feri Dar es Salaa na Bagamoyo kwa kisingizio cha kukosa leseni, lakini jambo hili halitokei kwa wavuvi wa huku Bara wanapokwenda kuvua na hata kuuza samaki katika eneo la Zanzibar. Jambo hili lina usumbufu mkubwa na manyanyaso kwa wavuvi wa Zanzibar wanapoingia katika bandari za huku Bara. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli juu ya kukomesha unyanyasaji huu kwa wavuvi wa Zanzibar huku Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kuchangia kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara yao. Lakini nina mambo mawili ambayo bado ni changamoto katika Wizara hii, kwanza naomba Wizara hii iangalie kwa kina tatizo la migogoro kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro hii inapelekea mpaka watu kuuwawa, tumeona kule Ikwiriri hivi juzi lakini pia maeneo mbalimbali ya nchi yetu yenye

wakulima na wafugaji bado hali si shwari. Maoni yangu, napenda kuishauri Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI iweze kukaa kwa pamoja na kushirikiana katika kutatua tatizo hili ikiwa ni pamoja na kuwaandalia wafugaji mazingira rafiki ya kufugia mifugo yao pamoja na kuchimbiwa mabwawa na majosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba Waziri akija kujumuisha anifafanulie kwamba hawa Maafisa Mifugo kwenye kata zetu hasa uko vijijini wanafanya kazi gani? Kumekuwa na malalamiko maafisa hawa wanapokwenda kutoa huduma kama ya uchinjaji wa mifugo humtoza mwanakijiji Sh.5,000/= na kilo moja ya nyama, je, huu ndio utaratibu? Naomba majibu toka kwa Mheshimiwa Waziri.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza mchango wangu kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa uamuzi wake wa busara wa kutoa fidia ya ng'ombe kwa wafugaji walioathiriwa na ukame wa 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba kutumia fursa hii kuendelea kuisihi Serikali iwatendee haki wafugaji wa Simanjiro na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Kiteto inayopakana na Simanjiro kwa kupatiwa fidia hiyo kwani wengi wao wameachwa katika umaskini uliotopea kama nilivyowahi kuiomba Serikali 2009/2010 wakati wa Bunge (vikao) la bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziiri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wao kwa kazi nzuri wanayoifanya kulingana na rasilimali kidogo wanayopewa wakati wa bajeti ya kila mwaka. Ni kweli usiyofichika kuwa ufanisi wa sekta ya mifugo unaathiriwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za miundombinu ya ufugaji kuwa ama chini ya TAMISEMI au Wizara ya Maji na mara nyingi hazipewi kipaumbele kutokana na ukweli kuwa Wizara hizo nazo zina vipaumbele vyake na wataalamu wa masuala ya mifugo katika ngazi ya Wizara hawapo TAMISEMI isipokuwa Wizara hii, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa zilizopo kwenye sekta ya mifugo ni pamoja na ukosefu wa maji na malisho ya mifugo kutengwa na kulindwa kwa mujibu wa sheria. Nashauri Serikali ianzishe mpango mahsusi wa maendeleo ya mifugo katika nyanda kame huku ikiweka nguvu kwenye upatikanaji wa maji, utengaji na uboreshaji wa malisho kwenye nyanda hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashauriwa ranchi ya Taifa na mashamba/vituo vya utafiti viwezeshwe kuboresha na kusambaza mbegu bora za mifugo kwa wafugaji ili kuwasaidia kuondokana na ufugaji wenye tija ndogo na kuongeza ufanisi kwenye sekta hiyo. Iwapo Serikali ikiamua leo, upo uwezekano wa Serikali kugawa zaidi madume bora 2000 kwa wafugaji wa jadi. Aidha, suala la uzalishaji kwa njia ya chupa linaweza kuleta mabadiliko ya kasi iwapo Serikali itaamua kuwezesha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuwa *NARCOs* haziwezi kubeba jukumu hilo bila ya Serikali kuwapatia ruzuku. Hivyo nashauri Wizara izungumze na kampuni za ranchi ili kwa pamoja walipatie suala hili ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekuwa ikisumbuliwa na ugonjwa wa Ndigana *(ECF)* kwa muda mrefu lakini kwa muda sasa wataalam wamegundua chanjo ya *ECF* na imethibitisha kuwa na manufaa makubwa kwa wafugaji. Hivyo rai yangu ni kuomba Serikali ione uwezekano wa kutoa ruzuku kwa chanjo hii ili wafugaji waweze kumudu kwani hivi sasa gharama zake ziko juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati sasa wa kumshauri Mheshimiwa Rais aone uwezekano wa kutazama upya muundo na majukumu ya Wizara hii ili iboreshwe kwa kupewa uwezo wa kuboresha miundombinu ya ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mathayo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ole-Nangoro na wataalam wa Wizara kwa hotuba yao iliyowasilishwa vizuri. Naipongeza pia Kamati na Kambi Rasmi ya Upinzani kwa maoni yao ambayo ni ya kujenga na ni muhimu Wizara iyazingatie ili kuimarisha na kuboresha sekta ya Mifugo na uvuvi kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu kwa Wizara hii, nitajielekeza moja kwa moja kwenye Jimbo langu la Bukombe, Jimbo lenye wafugaji wengi wa ng'ombe, mbuzi na kuku, ingawa kondoo na nguruwe wapo pia. Kwa jumla, ufugaji ulio Bukombe ni wa asili, ufugaji shadidi bado haujashika kasi. Hapa nitazungumzia changamoto wanazozikabili wafugaji wa Bukombe katika shughuli yao ya ufugaji wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazowakabili wafugaji wa asili wa Bukombe ni pamoja na hizi zifuatazo; tatizo la maeneo la malisho, tatizo hili liliulizwa kwenye swali Bungeni na pia kuliongelea katika bajeti ya mwaka jana. Hili ni tatizo kubwa kuliko yote yanayowakabili wafugaji. Kutokana na kukosa maeneo ya malisho, wafugaji wanalazimika kuchukua mojawapo ya hatua zifuatazo:-

Kuhamahama, wanahamia sehemu nyingine za Tanzania, jambo ambalo linawaathiri watu ambako wafugaji huhamia, wengine hufugia kwenye hifadhi, hifadhi ya Kigosi kwa Bukombe, wengine hufugia vijijini na hivyo mara nyingine kusababisha migogoro baina yao na wakulima. Jambo hili nimeliuliza kama swali Bungeni lakini Serikali imeishia kuahidi kuwa inaendelea kupima maeneo ya malisho. Swali Serikali itakamilisha lini mchakato wa kupima maeneo ya malisho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la soko zuri la uhakika la mazao ya mifugo. Tanzania inao mifugo wengi sana kuliko nchi yoyote Afrika Mashariki lakini hainufaiki sana kutokana na mazao ya mifugo (nyama, maziwa, ngozi) kwa sababu haina viwanda

vya kutosha vya kusindika maziwa, nyama na ngozi ili kuyaongezea thamani mazao haya kabla ya kuyauza nchi za nje. Swali, Serikali itatekeleza lini ahadi yake ya kuhakikisha viwanda hivyo vinajengwa ili nchi yetu inufaike inavyopaswa kutokana na mifugo yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kubwa kwa wafugaji wa Jimbo la Bukombe na maeneo jirani ni kutokuwepo kwa majosho na malambo. Kwa sababu ya ukosefu huu, wachungaji hutangatanga sana kutafuta maji kwa mifugo wao na tatizo huwa kubwa zaidi wakati wa kiangazi au kama kuna ukame. Wananchi wa Bukombe wanaiomba Serikali kupitia kwenye Wizara hii, iwasaidie katika suala la maeneo ya malisho na majosho na malambo (kama masuala ya haraka) na ijipange vizuri ili viwanda vilivyotajwa vianzishwe (kwa ubia na watu binafsi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nitazungumzia ni ufugaji wa samaki. Ufugaji wa samaki Bukombe haupo, lakini ni sekta inayoweza kusaidia kupunguza au kufuta umaskini kwa vijana wengi vijijini kama kukiwa na mipango mizuri itakayotekelezwa vizuri. Wilaya mpya ya Bukombe haipakani na Ziwa, bali ina Mito midogomidogo na maeneo oevu katika kata kadha wa kadha (mfano Namonge, Nga‘nzo, Uyovu) ambayo kwa msaada wa Serikali, yanaweza kutumika kwa ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweza kusaidia kwa kuhamasisha uundwaji wa vikundi vya watu hadi 10 katika vijiji na kisha ikaandaa mafunzo ya ufugaji wa samaki ambayo yatajumuisha namna ya kuchimba mabwawa ya samaki, muundo wa mabwawa, namna

ya kutengeneza chakula cha samaki masuala ya uvunaji, uhifadhi na masoko. Swali, je, kama Bukombe tukiunda vikundi vya vijana wenye ari na ufugaji wa samaki, Serikali iko tayari kutuletea wataalam wa kuendesha mafunzo ya ufugaji wa samaki?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matatizo makubwa baina ya wakulima na wafugaji katika maeneo mengi ya nchi, Kilwa ikiwa ni eneo mojawapo lililo katika maeneo yaliyochanganyika kati ya wakulima na wafugaji. Tatizo kubwa linalopelekea migogoro iliyopo, inayojitokeza na inayoweza kujitokeza ni kwa kutokuwepo miundombinu ya kuwasaidia wafugaji kufanya ufugaji wa kisasa kwa kuhakikisha hawahamihami. Wafugaji wa Kilwa hadi sasa hawana majosho ya uhakika na ya kutosha, kitu kinachowafanya watembee umbali mrefu kutafuta majosho ambapo huwaingilia wakulima katika mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Kilwa pia hawawekewi miundombinu ya kunyweshea mifugo yao, hakuna malambo ya kutosha na hivyo kuwafanya wahame kutafuta maji, kitu kinachopelekea kuingilia milki za mashamba ya watu na hapo ndipo malumbano yanapoanza. Lakini mpaka sasa Serikali ni kama haina mpango wa kusaidia wafugaji, Tanzania imekuwa haina wafugaji, imekuwa na wachungaji kwa kuwa wafugaji wamekosa utulivu kwa kukosa maeneo maalum kama majosho, malambo na kadhalika ili kuwafanya wasitangetange.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Wizara hii, tunaitaka Serikali ituhakikishie ni lini itajenga miundombinu ya kukidhi mahitaji ya wafugaji ili wasiingilie maeneo ya wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Wizara tuelezwe mkakati uliopo wa kudhibiti migogoro baina ya wakulima na wafugaji isitokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha viwango vya nyama na maziwa vinakuwa na ubora wa viwango vinavyokubalika ili kuingiza ushindani wa soko la bidhaa hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kusini imewekwa kama eneo la ufugaji, kuna mpango gani wa kujenga viwanda vya kusindika nyama na maziwa kwa faida ya wafugaji na pia kutoa ajira kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi, bado uvuvi haramu unazidi kushika kasi kwa kuwa hakuna vyombo vya kudhibiti uvuvi huo katika bahari yetu. Halmashauri kushindwa kukata leseni za uvuvi kwa wakati kutokana na kushindwa kuweka doria kwa kukosa fungu, Sera za uvuvi haziwafikii walengwa (elimu ya namna ya kutumia rasilimali za bahari na kadhalika), wavuvi kutotumia zana za kisasa za kugundua maeneo yenye samaki, vyombo vinavyoweza kuhimili mikikimikiki ya bahari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wavuvi hasa wa Kilwa, ni eneo muhimu kwa uvuvi? Kutodhibiti uvuvi haramu wa mabomu

kunaweza kuathiri hata shughuli za uzalishaji gesi unaoendelea katika Bahari ya Kilwa. Ni lini Serikali itadhibiti na kuhakikisha doria inawekwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kwa wajasiriamali (wavuvi) katika Wilaya ya Kilwa hakuna kabisa. Serikali ina mkakati gani wa kuinua hali ya kipato cha wananchi wa Kilwa kwa kuhakikisha wanapata mikopo kutoka kwenye vyombo vya fedha?

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu ya wataalam kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu ya bajeti ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia Kilimo Kwanza inatakiwa iwe pamoja na mifugo, lakini inaonekana *policy makers* wanafikiria kilimo tu bajeti ya mifugo ni kidogo kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa tufuge kisasa, Serikali haina budi kuwawezesha Wamasai na wafugaji wengine kufuga kwa kutumia njia za kisasa kama uhamilishaji na matumizi ya madume wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ikiboreshwa itasaidia kutoa maziwa ya kutosha, nyama nzuri na samaki au mbolea kwa ajili ya mashamba yetu. Kunywa maziwa kwa wingi kunasaidia watoto kupata lishe nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngara ina ng'ombe wapatao 50,000 lakini wote ni ng'ombe wa kienyeji ambao wanahitaji kuboreshwa kwa njia za uhamilishaji na matumizi ya madume bora. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wawe na mkakati wa kuwasaidia wafugaji wa Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe kutoka Rwanda na Uganda. Wilaya ya Ngara imejaa ng'ombe wa aina ya Ankole wa wahamiaji haramu. Ng'ombe hao ni bora kuliko ng'ombe wa kienyeji wa wananchi wa Ngara, tungeweza kuwa na mchanganyiko wa ng'ombe wa Ankole na wale wa wananchi wa Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maafisa ugani, Ngara ina upungufu mkubwa wa wataalam wa mifugo wa kuwasaidia wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa samaki Ngara, wananchi wa Ngara wanakosa lishe nzuri kwa kutokula samaki. Naamini Wizara ingeweza kuwasaidia wananchi wa Ngara kwa kuchimba mabwawa ya samaki. Kwa kifupi kuna tatizo la ufugaji wa kisasa nchi nzima. Nakumbuka ziara ya Rais wa zamani wa Botwana, Mheshimiwa Matsire alipotembelea Tanzania na akawa anatembezwa na Mheshimiwa Kikwete wakati huo akiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati akipitapita sehemu mbalimbali walikutana na ng'ombe, Mheshimiwa Matsire akauliza hao ni wanyama gani? Aliuliza swali hilo kwa sababu amezoea kuona

ng'ombe wakubwa ya Botwana. Mheshimiwa Kikwete harakaharaka alimwambia kwamba hao ni ng'ombe ila bado wanakua wakati wameshakomaa. Botswana ina ng'ombe takribani milioni mbili na nusu, lakini wanafuga vizuri na wana-*export* nyama na ng'ombe sisi tuna zaidi ya milioni 12 lakini hatufaidiki na ng'ombe hao, *policy makers* sharti wabadilishe *attitude* watoe bajeti ya kutosha.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, naanza kwa kutokuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu. Aidha, baada ya kutokuunga mkono, naomba nichangie baadhi ya maeneo na kubainisha sababu kwa nini siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa ardhi baina ya wananchi wa kijiji cha Katapulo na *NARCO*/Mwekezaji. Sababu ya kutokuunga mkono hoja ni jinsi Waziri wa Wizara hii alivyoamua kwa makusudi kabisa kutomaliza mgogoro huu ambao ni haki ya wananchi wa kijiji hiki kurudishiwa ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Wizara hii mwaka jana nilifanya juhudi za kuonana na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Wizara hii na kwa bahati nzuri hajabadilishwa lakini hazikuzaa matunda na niliposhika kifungu alidiriki kusema "rafiki yangu Kandege, tutamaliza tatizo la mgogoro wa shamba lililoko Kalambo" mpaka nachangia bajeti nyingine ya mwaka huu, nashindwa kuona utashi wa Waziri wa kumaliza mgogoro huu. Sasa naunga mkono

bajeti hii kwa lipi lililotekelezwa kwa wananchi wa Jimbo langu hususani kijiji cha Katapulo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalazimika kumshangaa Mheshimiwa Waziri na Wizara yake ili hali anafahamu ahadi yake kwangu na kwa wananchi wa Jimbo langu alishindwaje kufika Jimboni kwangu kushughulikia mgogoro huu pale Makamu wa Rais alipofanya ziara tena akiwa pamoja na ratiba ya kufungua soko la Kimataifa la Kasange ambalo liko chini ya Wizara yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo jitihada za kumkomboa mvuvi aliye kwenye lindi la umaskini. Ni jambo lisiloniingia akilini namna ambavyo Wizara hii haijaamua kumsaidia mvuvi mdogo aliye Ziwa Tanganyika hususani Wilaya mpya ya Kalambo ambako vijiji vya Kipanga, Samazi, Kasanga, Muzi, Kilewani, Kapele na haswa maeneo yote haya hakuna mwananchi aliyesaidiwa bajeti ya Wizara hii. Je, nina sababu gani ya kuunga mkono bajeti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza zaidi ni baada ya kupata nafasi ya kutembea viwanja vya Nanenane na kutembelea mfuko wa pembejeo na kujionea jinsi ambavyo mfuko huu unavyomtambua mkulima na kumwekea utaratibu wa kukopa pembejeo lakini si kwa mvuvi ni kwamba hatambuliki kabisa, je, ninakuwa na sababu gani ya kuunga mkono bajeti?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sasa tutawaita watoa hoja na kwa mujibu wa muda tulionao tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri, tutampa dakika 20 akifuatiwa na Mheshimiwa Waziri yeye atamalizia kwa dakika 40.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu ambayo ni hoja ya muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi yake ya maisha, zawadi ya afya niliyonayo na kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia katika hoja hii. Nianze tu kwa kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kuiongoza nchi yetu vizuri kwa busara na hekima na kuweza kuiendesha katika hali ya amani, utulivu na kujikita katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge letu

Tukufu, Naibu Spika na ninyi Wenyeviti wetu watatu kwa kuliongoza Bunge letu vizuri na kulifanya lijikite katika shughuli zake za msingi za kutunga sheria, lakini pia kuishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa na imani nami na kuendelea kuniweka katika Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kama Naibu Waziri. Vile vile nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais na kuwaomba kwamba tushirikiane kwa pamoja kufanya kazi tuliyokabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa hivi karibuni na kuwa Wabunge. Napenda kumshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika majukumu ya kuongoza Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kutoka pande zote za Bunge hili na kutoka kwenye vyama vyote vya siasa kwa ushirikiano mkubwa ambao mmekuwa mkinipa ndani na nje ya Bunge. Naahidi kuendelea kushirikiana nanyi hasa katika kuhakikisha kwamba hoja za wananchi, wapiga kura wetu waliotutuma hapa tunazijibu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara yangu Dkt. Charles Nyamrunda na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Yohana Budeba, Wakuu wa Idara na Taasisi pamoja na Wakuu wa Bodi zote zilizoko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Kiteto kwa imani kubwa waliyonayo maana bila ya kura zao nisingekuwa hapa Bungeni na leo nisingesimama mbele yako. Naomba nitumie fursa hii kuwaahidi pamoja na kuwa na majukumu mengi ya Kitaifa yale ya Kijimbo ndio kipaumbele kwangu na nitaendelea kushirikiana na uongozi mwingine uliopo Kiteto kuhakikisha kwamba shughuli zetu za maendeleo zinakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba niishukuru familia yangu kwa upendo na kwa msaada mkubwa wanaonipatia hata ninapokuwa sipo na bila wao nadhani mengi yangenishinda kufanya. Kwa hiyo, kwa namna ya pekee nawashukuru sana nawaambia ahsanteni. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungana na Mheshimiwa Waziri wangu, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi na kuonyesha masikitiko yangu juu ya vifo vilivyowapata Wabunge wenzetu waliofariki katika kipindi hiki Mheshimiwa Mussa Khamis Silima, Mheshimiwa Regia Mtema na Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari. Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia utakumbuka kwamba mnamo tarehe 10 Septemba, 2011 meli ya *Spicer Islander* ilizama na kusababisha vifo vya Watanzania wenzetu wengi. Lakini pia katika mwaka huu tarehe 18 Julai, 2012 meli nyingine ya *MV. Skagit* imezama pia huko Chumbe Zanzibar na kusababisha vifo vya wenzetu wengi raia wa Tanzania na raia wa kigeni. Naomba tu nitumie fursa hii kumwomba Mwenyezi Mungu aweze kuzilaza roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu, sasa naomba nianze kuchangia hoja za baadhi ya masuala yaliyoibuliwa na wenzetu Wabunge. Hoja ni nyingi tutajaribu kujibu kwa muda tulionao. Lakini niahidi tu kwamba, hoja zile ambazo tutashindwa kuzijibu hapa kwa ajili ya muda tutazijibu kwa maandishi. Orodha ya wachangiaji waliochangia kwa kuongea hapa na wale walioandika watatajwa na Mheshimiwa Waziri kama ilivyo jadi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ambayo ningependa kuchangia ni hoja iliyozungumziwa na Wabunge wengi na yenyewe ni hoja ya migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Hoja hii imechangiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Msemaji wa Kambi ya Upinzani amechangia na takribani Wabunge 55 wamechangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonesha tu jinsi hoja hii ilivyo tete na jinsi inavyogusa maisha ya Watanzania wote katika kona zote za nchi yetu. Hoja ilivyowekwa

na Kamati pamoja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, lakini pia na Wabunge 55 waliochangia kwa maandishi ni kwamba, moja, utafiti wa kutosha ufanyike ili kubaini sababu za wafugaji kuhamahama. Lakini pia wengi wamesema kwamba, maeneo yatengwe ya ufugaji na haya yadhibitiwe ili maeneo ya mifugo yasiingiliwe na shughuli nyingine na ili kuweza kudhibiti migogoro hii inayotokana na uhamaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tathmini imeshafanyika na sababu za uhamaji zinajulikana. Hizi ni pamoja na wafugaji kuhamahama ili kuweza kufuatia malisho, maji, chumvichumvi pamoja na mahitaji mengine ya mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhama huku mara nyingi wanatoka katika eneo ambalo kwa sababu ya ukame, sababu ya magonjwa ama sababu ya msongamano hawawezi kupata mahitaji hayo ya mifugo yao. Wanapohama mara nyingi migogoro inakuwepo kwa sababu wanakwenda wanalisha kwenye maeneo yasiyohitajika na mara nyingine migogoro imekuwepo na hata maafa pia kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Matumizi ya Ardhi imehakiki Vijiji 430 vilivyo katika Wilaya 67 ndani ya Mikoa 19 ambavyo hivi vimetenga hekta milioni 1.26 kwa ajili ya ufugaji. Nafahamu Waheshimiwa Wabunge wengi wanasema haitoshi kutenga tu haya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea ushauri uliotolewa na Wabunge wengi waliochangia kwamba

pamoja na kutenga haya maeneo miundombinu iendelezwe, lakini sheria zilizopo zisimamiwe ili kuhakikisha kwamba, migongano haitakuwepo kwa sababu suluhu ni utengaji wa maeneo yawepo ya kilimo tu na yale ya mifugo yabaki ya kufugia tu bila ya kuingiliwa na matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hili pia la kupunguza uhaba wa miundombinu ambayo ndiyo sababu nyingine ya wafugaji kuhama katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu ikishirikiana na TAMISEMI hasa kutumia Mifuko ya *DADP's* ilitumia shilingi bilioni 3.6 ili moja ya kujenga malambo ambayo yamejengwa 53, mengine 45 yakakarabatiwa, lakini pia visima virefu vya maji 18 vimechimbwa kwa ajili ya kutoa maji kwa ajili ya binadamu na mifugo. Kiasi hiki ni kidogo nakubali, lakini ni mwanzo na huenda tutapaswa kuendelea na juhudi hii kuhakikisha kwamba maji yanakuwepo ya kutosha, lakini miundombinu pia iwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba changamoto zinazotokana hasa na migogoro hii ni nyingi, lakini kama Serikali tunaendelea kuomba ushirikiano wenu na hasa kwa kuwa ninyi ndio mnaoelekeza zaidi ili tuweze kujipanga kuhakikisha kwamba kila ardhi kwenye vijiji vyote vyenye wafugaji vinafanyiwa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili maeneo yatengwe, kuwepo na eneo la huduma, eneo la makazi, maeneo ya kilimo na pia yale ya mifugo yatengwe bayana ili kusiwe tena na mwingiliano wa shughuli hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyoibuliwa, Wabunge wengi wamechangia kwamba, dhana ya Kilimo Kwanza bado haifahamiki na haionekani kwamba inazingatiwa sana katika sekta hii ya mifugo. Niseme tu kwamba, mengi yamefanyika na kuna fedha nyingi za *ASDP, DADP's, SAGCOT* pamoja na *TASAF* ambazo zinatumika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba dhana hii inaeleweka kwa watu. Lakini watu pia wanatumia dhamana hiyo ili kuweza kunufaika na mazao haya ya mifugo. Kinachotakiwa nadhani ni kuweka uratibu katika ngazi ya Halmashauri kwa sababu nakubali kwamba, kumekuwepo na udhaifu katika kusukuma na kila kitu kikaonekana kwamba ni kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni uhaba wa wataalam wa ugani. Hili ni kweli limetolewa mara nyingi katika Bunge hili, lakini niwaeleze tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, vyuo vyetu vinavyotoa mafunzo ya mifugo na uvuvi uwezo umepanuliwa kiasi na kwa kipindi kilichopita iliwezekana kuwaajiri wagani 2,616 kwa ajili ya mifugo na 100 kwa ajili ya uvuvi. Idadi hii ni ndogo sana, lakini tutaendelea kujikita katika kuhakikisha kwamba uwezo wa vyuo vyetu unazidi kuongezeka na kupanuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyochangiwa ni hoja ya utafiti. Ni kweli tumeshaunda taasisi mbili za Utafiti moja kwa ajili ya uvuvi *TAFIRI* na nyingine kwa ajili mifugo *TALIRI*. Lakini niseme hoja iliyokuwa inatolewa ni kwamba, taasisi hizi zipatiwe fedha zaidi ili ziweze kufanya kazi na baada ya

matokeo ya utafiti kupatikana, matokeo hayo yawafikie watumiaji wa tafiti hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kwa kupitia *COSTECH* taasisi hizi zimejipa uwezo zaidi maana wameweza kupata fedha nyingine nje ya utaratibu huu wa bajeti. Kiasi cha shilingi bilioni 3.2 mwaka jana na kwa kutumia fedha hizo tafiti nyingi zimefanyika, lakini bado ni lazima tafiti hizi ziwafikie walengwa. Kiwizara tumejipanga vizuri, Idara inayoshughulikia kazi hii ni ile inayohangaika na utafiti, mafunzo na ugani. Kwa sababu wagani wetu ndio wamekusudiwa kupeleka matokeo ya utafiti vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna wazo lililotoka kwa baadhi ya Wabunge waliochangia kwamba baada ya kuwa na Taasisi za Utafiti, kuwepo na *agency* maalum ya kutekeleza matokeo ya utafiti. Pendekezo hili limetoka kwa Mheshimiwa Zitto Kabwe akitaka kuundwe *agency* itakayosimamia uendelezaji wa uvuvi na kwa Mheshimiwa Mbunge wa Morogoro Vijijini amependekeza pia *agency* iundwe kwa ajili ya kutekeleza matokeo ya utafiti wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kama nilivyosema tutajibu hoja kwa maandishi na naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ole-Nangoro, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuanza kutoa ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni sasa bila kupoteza muda, naomba nimwite mtoa hoja Dkt. David Mathayo David ili sasa aweze kuhitimisha hoja yake.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhuhana Wataallah*, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu ili niweze kujibu hoja za Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa mara nyingine kwa michango yao na katika hoja ambazo wamezitoa zenye lengo la kuboresha sekta ya mifugo na uvuvi ili hatimaye ziongeze pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba kumshukuru Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa michango na ushauri alioutoa katika taarifa yake itakayosaidia kuboresha sekta ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru Wabunge wote waliochangia bajeti ya Wizara yangu kwa kuzungumza, na kwa maandishi. Aidha, kwa kuwa hoja walizochangia Wabunge ni nyingi kutokana na muda mfupi niliopewa, sitoweza kujibu hoja zote bali

nitajitahidi kwa kadri nitakavyoweza na naahidi kwamba nitajibu hoja ambazo zitabaki kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii kujibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani zangu napenda niwatambue Wabunge wote ambao wamechangia katika hotuba ya Serikali, hotuba ya Waziri Mkuu, Hotuba za Mawaziri wenzangu zilizotangulia pamoja na hotuba yangu ya siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimtambue Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, Waziri Kivuli wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa michango yao mizuri ambayo nina imani kabisa kuwa itatusaidia katika kuboresha utendaji kazi katika idara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu niwatambue Wabunge wafuatao waliochangia katika bajeti ya Serikali:-

Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Modestus D. Kilufi, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Salvatory N. Machemli, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Eugine E. Mwaiposa, Mheshimiwa Felix F.

Mkosamali na Mheshimiwa Kapteni John D. Komba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani, Mheshimiwa Profesa Peter M. Msolla, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Deusderius J. Mipata, Mheshimiwa Christopher O. Ole Sendeka na Mheshimiwa Herbert J. Mtangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia katika hotuba ya Waziri Mkuu ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Ezekia D. Wenje, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Anthony G. Mbassa, Mheshimiwa Namelok E.M. Sokoine, Mheshimiwa Suzan L. Kiwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Innocent Kalogeresi, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa *Engineer* Mohammed Habib Juma Mnyaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia katika hotuba zilizotangulia za Mawaziri wenzangu ni Wabunge watano ambao ni Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Juma Nkamia na Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliochangia kwa kuzungumza siku ya leo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Titus M. Kamani Mbunge wa Busega, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji; Mheshimiwa Sylvester M. Kasulumbayi, Mbunge wa Maswa Mashariki na Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni; Mheshimiwa Salehe A. Pamba, Mheshimiwa Mary P. Chatanda, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Michael L. Laizer na Mheshimiwa Namelok M. Sokoine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Charles J.P. Mwijage, Mheshimiwa Assumpter N. Mshama, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwaga, Mheshimiwa Amina N. Makilagi, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Rose K. Sukum, Mheshimiwa John M. Cheyo na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa katika orodha yangu niwataje wale ambao wamechangia kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mheshimiwa Silvestry F. Koka, Mheshimiwa Amos G. Makalla, Mheshimiwa Eustace O. Katagira,

Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Selemani S. Jafo na Mheshimiwa Leticia M. Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani, Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Christopher O. Ole Sendeka, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela K. Kahigi, Mheshimiwa Selemani S. Bungara, Mheshimiwa Deogratius A. Ntukamazina, Mheshimiwa Kurthum J. Mchuchuli na Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wapo Mheshimiwa *Engineer* Athuman Mfutakamba, Mheshimiwa Geofrey W. Zambi, Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Mariam N. Kisangi, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Mbarouk Salum Ali, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Hamad Khamis Hamadi na Mheshimiwa Neema H. Mgaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Dkt. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Charles P. Mwijage, Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Kombo Khamis

Kombo, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa Hamoud Abuu Juma, Mheshimiwa Mchungaji Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Ally K. Mohammed, Mheshimiwa Zahra Hamadi na Mheshimiwa Dkt. Terezya Huvisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wamechangia Mheshimiwa Goodluck J. Ole Medeye, Mheshimiwa Anna MaryStella Mallack, Mheshimiwa Mchungaji Israel Y. Natse, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Abdulsalam Amir, Mheshimiwa Deusderius J. Mipata, Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Stephen M. Wassira na Mheshimiwa Dkt. Seif S. Rashidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Waride Bakari, Mheshimiwa Rajabu Mohammed, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Charles Kitwanga, Mheshimiwa Vick P. Kamata, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Namelok E. M. Sokoine, Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby na Mheshimiwa Yussuf Nassoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wamechangia Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, Mheshimiwa Aggrey D. Mwanry, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso**,** Mheshimiwa Abas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Esther Midimu, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Ignas

Malocha, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye na Mheshimiwa Said Mtanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Shaffin A. Sumar, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Cecilia D. Paresso, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Sylivester Masele Mabumba, Mheshimiwa Engineer Gerson H. Lwenge, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mheshimiwa Rukia Ahmed, Mheshimiwa Rose K. Sukum na Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Amina Makilagi, Mheshimiwa Nasib Omar, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Innocent Kalogeresi, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Mussa Zungu na Mheshimiwa Diana M. Chilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Augustine L. Mrema, Mheshimiwa Masoud Salum, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Mwigulu L. M. Nchemba, Mheshimiwa Dkt. Dalaly P. Kafumu na Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema siyo rahisi kujibu hoja zote za Wabunge, lakini naomba kutoa ahadi kwamba, nitatoa maelezo machache

lakini mengine yaliyobaki basi tutajaribu kutoa majibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kubwa kwamba, bajeti ni ndogo, nikilinganisha na bajeti ya mwaka uliopita ni kweli kwamba bajeti ni ndogo, lakini pia nakubaliana na Wabunge kwamba ni ndogo. Lakini tukumbuke kwamba mwezi wa Nne tulikaa tukajadili mipango yetu na vipaumbele vyetu ambavyo tunakwenda navyo kwa mwaka huu kwa maana ya mipango yetu ya kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima tuelewe kwamba, kwa kuwa kupanga ni kuchagua ni lazima kuna maeneo yatapewa vipaumbele na maeneo mengine yatasubiri kidogo. Siyo kusubiri kidogo kwamba haiendelei, lakini kiasi hiki ambacho ni kidogo kimetengwa sisi wenyewe kama Wizara tutakuwa tunatekeleza kutokana na vipaumbele ambavyo sisi tunavyo kwenye Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani kabisa kwamba, miaka ijayo Serikali katika maeneo haya ambayo kwa sasa siyo vipaumbele na yenyewe yatapewa kipaumbele ili tuweze kusonga mbele kwa kasi ambayo Wabunge Wabunge mnaitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, hapa leo tumepewa bilioni 54.6, naomba kukumbusha kwamba tukizungumzia hali halisi ya mchango wa Serikali kwenye sekta hii bado tuna fedha zingine ambazo zinapitia kwa mfano juzi hapa tumeendeleza zoezi la kutoa kifutajasho kwa wafugaji

ambao walipoteza mifugo yao kutokana na ukame wa mwaka 2009/2010 na kifuta jasho hiki thamani yake ni shilingi bilioni 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bilioni kumi na mbili bado inaingia kwenye mchango wa Serikali kwenye sekta ya mifugo. Aidha, katika mwaka huu ambao tunauombea fedha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 13.3 kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Maji na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa shughuli ambazo zinahusu mifugo na uvuvi. Kwa maana hiyo ukipiga mahesabu ya haraka unakuta kwamba fedha ambazo zitakwenda kwenye mifugo na uvuvi ni takribani bilioni 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bilioni 80 siyo kiasi kidogo kwa hali yetu ya uchumi na kwa vipaumbele ambavyo sisi Wabunge tuliviweka. Tuna imani kabisa kwamba zile fedha tulizotengewa kidogo tukifanya kazi kama ilivyotarajiwa na kama inavyotakiwa tunaweza tukapiga hatua kutokana na kwamba, ni lazima tuwe na vipaumbele mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niongeze kama alivyosema kaka yangu Mheshimiwa John Momose Cheyo kwamba, Wafugaji siyo watu maskini. Nakubaliana naye kabisa kwamba katika watu matajiri ni pamoja na wafugaji. Mtu anaweza kuwa na ng'ombe 3,000 lakini anahama anasema kwamba hana maji. Kumbe angeuza ng'ombe 40 au 50 katika ng'ombe 3000 angeweza kujichimbia lambo.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Ndiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndivyo wanavyofanya nchi za Botswana kule mimi nimekaa miaka nane (8), wana mashamba yao wanaita *Cattle Post* kila mfugaji anauza ng'ombe na anaweka miundombinu yake mwenyewe. Serikali haiwezi kutuwekea kila kitu. Kwa hiyo, tusitumie visingizio kwamba Serikali haijatenga fedha, ni lazima na sisi Wafugaji tuangalie uwezekano wa kuuza ng'ombe na kuweka miundombinu ambayo itatusaidia. Hakuna nchi ambayo inatoa miundombinu kwa kila kitu, ni matajiri wafanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani watu wakawa wanaomba fedha Serikalini kila kunapokucha wakati wao wamekalia utajiri. Mimi ni Waziri wa Mifugo nawaambia hivyo kwamba, wauze ng'ombe na wachimbe visima, watengeneze malambo wenyewe. Wasitegemee kwamba Serikali itafanya kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nyuma tulishawahi kutoa mwongozo kuhusu wafugaji wanapotaka kuhamisha mifugo kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Tuliweka mwongozo tukasema mtu anayetaka kutoa mifugo yake Nzega kupeleka Bagamoyo aende kwanza Bagamoyo akaombe ruhusa kwamba kuna eneo la kuleta hiyo mifugo na anapewa kibali cha kuleta au kutokupeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana siyo kupeleka mifugo halafu tunajaza maeneo ambayo watumiaji wengine wa ardhi pia wanahitaji, tunaleta ugomvi. Ni lazima apate kibali kutoka sehemu ambayo anatoka na kibali kule anakopeleka. Bila hivyo tutakuja kuvuruga hii nchi kila mahali tutakuwa tunazagaa. Kwa hiyo ni vema kufuata huo utaratibu. Ni lazima tupate vibali sehemu zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi Mkoa wa Pwani hali yake ni mbaya sana, mifugo ni mingi sana. Nawashauri kwamba, kwa sababu sasa hivi Serikali inaendelea na tathmini kujua wingi wa mifugo kwa kila Kijiji katika Mkoa wa Pwani, tusubiri kidogo kutoa hivi vibali hususani kupeleka Mkoa wa Pwani ili kusudi kutathmini ni wapi ambapo kuna nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu maeneo ambayo yalitakiwa yawe na ng'ombe elfu hamsini sasa hivi kuna ng'ombe laki nne mpaka laki tano. Sasa tutakuja kuharibu kila mahali, tutakuja kukosa hata hayo maji tunayokunywa kutoka Dar es Salaam ambayo yanatokana na vyanzo ambavyo vipo milimani, lakini mifugo inavyoharibu kule Morogoro tutakuja kukosa hata maji ya kunywa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vema pamoja na kwamba tunayo ardhi lakini ni lazima tuitumie vizuri na kuangalia mazingira tusiyaharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ranchi zilizobinafsishwa, kwamba watu ambao wameshindwa kuziendeleza ranchi zilizobinafsishwa wanyang'anywe,

zoezi hilo tunalifanyia kazi na tunaanza Mkoa wa Kagera. Kumekuwa na matatizo kule, watu wamepewa vitalu, lakini hawaendelezi matokeo yake wanaingiza watu kutoka Rwanda na Uganda kuchunga pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeshaanza kazi na nimeshaongea na Waziri wa Mambo ya Ndani na kazi hiyo itaanza kwa kuangalia na kuhakiki uraia wa wananchi wafugaji wanaoishi pembezoni mpaka wa Uganda na Rwanda ili kusudi waweze kurudi kwao Watanzania wafuge kwa wakati na wafuge kwa nafasi kwa sababu hii ni ardhi ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mtanzania atakayetoka Kagera aende Uganda kufuga kule, haiwezekani! Hakuna Mtanzania atakayetoka Shinyanga au Mwanza aende Rwanda na Burundi kufuga haiwezekani! Kwanza wale kule wametunga sheria kwamba mtu haruhusiwi kufuga zaidi ya ng'ombe wawili. Sisi tukizidi kufuga sana utitiri tutaangalia uwezekano wa hiyo sheria angalau kwa kuweka idadi ya ng'ombe ambao ndiyo tutatakiwa tuwe nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kwamba elimu ya ufugaji wa kisasa itolewe, elimu ya unenepeshaji, elimu ya kufuga kutokana na uwezo wa ardhi. Mafunzo haya tunaendelea kuyatoa kuwaelimisha wananchi kupitia televisheni, redio na vipeperushi. *DADPs* inatusaidia kutoa mafunzo, tuna vyuo vyetu Mwanza, Rorya, Kagera vinatusaidia kuelimisha wafugaji wetu kuhusiana na ufugaji bora. Lakini vile vile *NARCO* pia

inasaidia kuwaelimisha wale ambao walipewa vitalu. Vile vile tunazo fedha za *DADPs* ambazo wafugaji 16,500 walipata mafunzo ya aina hiyo ili waweze kufuga kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huu Serikali inajiandaa kukamilisha Benki ya Wakulima, tunawashauri wafugaji na wavuvi wote waweze kupata mikopo kutoka kwenye dirisha lililowekwa katika Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB)*. *TIB* imeshaanza kutoa mikopo miaka mitatu iliyopita ya riba nafuu. Kwa hiyo, nashauri Watanzania wachangamkie fursa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya Mashamba ya *NARCO* yawezeshwe kuzalisha mitamba. Tunayo mashamba ya kutosha kuzalisha mitamba na mwaka huu tumenunua ng'ombe 65 kwa ajili ya mbegu pamoja na madume bora 21 ambao yatapelekwa kwenye mashamba yetu ya Ngerengere, Sao Hill, Kitulo, Nangaramo pamoja na baadhi ya mashamba ya *NARCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni za *NARCO* za Taifa ipewe uwezo wa kifedha. Kampuni ya *NARCO* ilipewa fedha shilingi bilioni 5.8 kwa ajili ya ujenzi wa machinjio ya Ruvu, mwaka huu wametengewa kiasi kidogo. Lakini niseme kwamba kampuni ya *NARCO* ni sawa na *TANESCO,* ni shirika ambalo linajiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mashirika haya ambayo yanajiendesha kibiashara tusiyaendekeza kuwa tunayapatia fedha kwa sababu yana uwezo wa

kutumia rasilimali na kukopa kutoka kwenye mabenki na kufanya biashara. Kwa hiyo, tutatoa kama kuna *special project* lakini siyo kwamba wawe wanapewa ruzuku kila siku wakati wanatakiwa wafanye kibiashara. Haya ni makampuni yanaweza yakakopa na kufanya biashara na kupata faida na kujiendesha yenyewe. Yanaposhindwa kujiendesha yenyewe ni ubovu tu wa uongozi lakini siyo kwamba ni lazima wapate ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kwamba ipewe Kiwanda cha Nyama cha Mbeya. Labda napenda kutoa taarifa kwamba Kiwanda cha Mbeya, sasa hivi mwezi Juni na mwezi Julai Serikali imetangaza zabuni. Kwa hiyo, tunasubiri *process* zingine kusudi tuweze kupata mwekezaji katika kiwanda hicho cha Mbeya. Lakini hata kile Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga ambacho kilikuwa kimechukuliwa na *Triple 'S'* wale *Triple 'S'* wamepatiwa mkopo na *TIB* takribani milioni 900 na kwa sasa hivi wanakikarabati kwa maana ya kuweka miundombinu ya umeme, maji, kujenga sakafu, kuta na baadhi ya mashine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *TIB* imewaahidi kwamba wakitumia mkopo huu vizuri kwa sasa itawasaidia mashine zote za kuhakikisha kwamba kiwanda hiki kinakamilika kabisa kuwa cha kisasa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunatoka Mkoa wa Shinyanga, tusaidiane pamoja tumhimize mwekezaji afuate masharti haya ya benki kusudi aweze kutuokoa maeneo yale mifugo badala ya kutembea huku na kule iweze kuchinjiwa pale pale Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi haramu. Mamlaka kusimamia sheria na zitungwe sheria ndogo ndogo. Ni kweli kwamba, katika Sheria yetu ya Uvuvi namba 22 ya mwaka 2003, Kifungu cha 18 cha Sheria hii kinaruhusu Halmashauri kutunga sheria ndogo ndogo ambazo hatimaye zitatusaidia katika kulinda rasilimali zetu za uvuvi. Pia kwamba wavuvi waelimishwe kutumia zana bora. Ni kweli wakiwa na zana bora hawawezi wakajihusisha kwenye uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya kwamba, wavuvi wapatiwe mikopo yenye masharti nafuu. Kama nilivyosema kwamba, sasa hivi Serikali iko kwenye *process* ya kuanzisha Benki ya Kilimo, lakini sasa hivi kuna nafasi ya kuchukua mikopo hii kwenye Benki ya Rasilimali. Lakini vile vile ni vema wavuvi wakawa na Vyama vyao vya Ushirika pamoja na *SACCOS* ili waweze kuwa na nguvu ya kukopa katika vyombo vya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya sangara, mwezi wa sita mwanzoni tarehe 25 nilitoa kauli ya Serikali hapa kutokana na kushuka kwa bei ya sangara. Napenda kusema kwamba, mazao haya ambayo soko lake liko nje ya nchi wakati mwingine ni vigumu sana ku-*control* na kwa kweli ni vigumu ku-*control* bei ya mazao ambayo tunategemea soko nje ya nchi. Sangara hawaliwi sana Tanzania, hata wavuvi wenyewe wa Mwanza, wa Kagera hawali sangara na wa Mara hawali sangara kama wanavyokula wale wananchi wa Ureno, Italia, Hispania pamoja na Ugiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilichotokea ni kwamba, hizi nchi nilizozitaja Ugiriki, Ureno, Hispania, Italia ni nchi ambazo kwa sasa hivi zina mgogoro wa kiuchumi, yaani uchumi wao umeyumba kwa kiasi kikubwa na nchi hizi *Euro* ile imeshuka. Sasa inaposhuka ni lazima walaji nao wabadilishe chakula kwa sababu sangara kule Ulaya anauzwa ghali kuliko anavyouzwa kuku au nguruwe. Samahani mnisamehe nimetaja nguruwe, lakini ndio hivyo ndio mazao ninayosimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ulaya sasa hivi kuku au *pock* kwa maana ya nguruwe ni jina kali kidogo afadhali niseme *pock*, kuku na *pock* wanauzwa bei zaidi kuliko sangara. Sasa kwa sababu uchumi nao *purchasing power* ya wananchi wale ni ndogo, hakuna ajira, hakuna fedha za kutosha, sasa hivi wana-*opt* kununua vyakula ambavyo ni vya bei rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile wakati wa joto sasa hivi ni *summer* kule Ulaya na wakati wa *summer* wazungu wanasafiri sana, kwa hiyo, hawawezi wakamuacha sangara wakawasha umeme kwa miezi mitatu wanahifadhi sangara kwenye *fridge,* ni gharama. Wakati huu wa joto vile vile kuna samaki anaitwa *cod* anayepatikana Ulaya kwa wingi, kwa hiyo, ndio maana hata mahitaji ya sangara yameshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine kule China wanafuga sana perege *(tilapia), tilapia* wa China wamesaidia kushuka kwa kiasi fulani bei ya

sangara. Kuna samaki mwingine anaitwa *baser* au *pangashars* wao wanafugwa *Far East* kwa hiyo, nao wameshiriki katika kushusha bei ya sangara. Vile vile kuna samaki anatoka kule Australia anaitwa *barramundi* na yeye pia alishiriki katika kushusha bei ya sangara. Lakini nina imani kabisa bei hii kushuka ni *temporary,* yaani ni kwa muda mfupi, kuna siku itapanda itakuwa nzuri, wafugaji wetu nao watafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha mazingira ya uwekezaji katika maziwa yetu na bahari yetu. Mazingira ni pamoja na kujenga miundombinu kama mialo, kukarabati mialo mingine na sasa hivi tuna mialo 28 kwa maana ya Ziwa Victoria na Ukanda wa Pwani. Sasa hivi tunafanya maandalizi ya kujenga mialo mipya minne kwenye Ziwa Tanganyika, ili waweze nao kupata miundombinu ya kuwasaidia kuvua na kuuza vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali katika kuboresha mazingira haya imeondoa *VAT* ya nyumba za kutengeneza nyavu za kuvulia samaki, imeondoa *VAT* kwenye injini za kupachika kwa ajili ya uvuvi kwenye maboti. Vile vile imeondoa *VAT* kwenye vifungashio. Tunawashauri wananchi waendelee kuanzisha Benki za Wananchi pamoja na *SACCOS* ili waweze kupata mikopo katika vyombo vya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu mwaka huu utaanza kwa ajili ya kujenga bandari za uvuvi. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba, baadhi ya kodi kwa mfano kodi za mafuta

katika uvuvi katika maeneo ambayo Watanzania wanaweza wakavua vizuri pamoja na kuangalia baadhi ya kodi zinazotozwa katika Viwanda vya Samaki, hivi labda vingine vingesaidia watu wetu pamoja na miundombinu ya viwanja vya ndege vikiimarishwa, basi Watanzania wengi watakuwa wanatumia viwanja hivyo kuuza samaki nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja imetolewa kwamba je, hivi ni sahihi kuingiza nyama ya kuku? Serikali ilipiga marufuku uingizaji wa mazao ya kuku kwa sababu moja ya tishio la mafua ya ndege. Tishio hilo mpaka sasa hivi halijakwisha, bado lipo. Kwa hiyo, nasema kuna kuku ambao wameingizwa kwa kibali ambacho kinaitwa namba 00551, huyu mwingizaji alifuata taratibu zote za kupata kibali na kuingiza kuku aliingiza kutoka Brazil.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kibali kingine kinaitwa 0000409 kibali hiki kinasema mfanyabiashara alipewa kibali kutoa tani 100 kutoka Zanzibar kuleta Tanzania Bara. Kibali hiki ni *fake* hakijatolewa na Wizara yangu, nimeiagiza Wizara kushirikiana na vyombo vingine vya usalama kuchunguza suala hili kusudi wahusika wote waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme, tunao Watanzania wanaofuga kuku, tunao Watanzania wanaofuga kuku wa mayai, wanazalisha mayai kwa wingi. Sasa pamoja na *threat* hii ya ugonjwa wa mafua ya ndege bado nasema Wizara yangu tusubiri kwanza hakuna tena kutoa vibali kama vipo vilivyokuwa vimetolewa visitishwe kwanza kwa sababu bado tuna

*threat* na bado kuku wanaoza kwenye ma-*fridge* kule Dar es Salaam kwa wafugaji wetu. Kwa hiyo, lazima tulifuatilie hilo mpaka Serikali itakaposema sasa tumeridhika kwamba hakuna tena tishio la mafua ya ndege. Kwa hiyo, sababu ni mafua ya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya fidia kwa wafugaji, Mheshimiwa Mbunge Msemaji wa Kambi ya Upinzani amezungumzia suala la kwamba Serikali iwafidie wafugaji wa Kiengege ambao mifugo yao ilikufa kutokana na ugonjwa wa homa ya mapafu mwaka 1980. Mwaka 1980 nilikuwa darasa la tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwelewesha Mheshimiwa Waziri mwenzangu kivuli kwamba, majanga yanayofidiwa au magonjwa yanayofidiwa ni yale ambayo yanakuja ghafla bila kutegemea na yanaleta athari kubwa kwa lugha za *veterinarian* tunasema kwamba *pandemic diseases. Pandemic* linakuja kwa nguvu halafu haliji mara kwa mara lakini linaleta madhara makubwa kweli kweli. Basi ile inaitwa *pandemic,* hiyo ndio tunaweza tukafidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini homa ya mapafu *(CBPP)* huu ni ugonjwa ambao upo tu, tunaita *endemic* kama vile UKIMWI ulivyo *endemic*, yaani *endemic* maana yake upo tu tunaishi nao. Sasa *CBPP* upo tunaishi nao. Kwa hiyo, hatuwezi tukafidia. Sasa kuna ugonjwa mwingine unaitwa *sporadic, sporadic* ni ule ugonjwa ambao unakuja na kurudia. Unakuja mara moja halafu baadaye unarudi tena, kidogo kidogo. Huo ni kama hii homa ya nguruwe ambao sasa

unatuulia vitoweo kule Iringa pamoja na Rukwa pamoja na Ruvuma. Kwa hiyo, fidia hapo haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie haya machache, ni muhimu kabisa kwamba minada yetu ya upili kuwepo na mizani. Hatuwezi tukaruhusu wafugaji wetu wauze kwa kuangalia kwa macho ama kwa kudanganya, kwa hiyo, lazima kwamba minada yetu yote 12 iwe na mizani kusudi wafugaji wetu wasinyonywe na ili kuepuka wizi na utoroshaji wa mifugo tunaweka minada ya mipakani kusudi kila wanapotaka kutoa kwa mfano kule Longido, wale wote wanaotaka kupeleka Kenya basi wauze kwenye mnada wa Longido. Tumeshatoa vibali huko Mikoani kusudi mtu anayetaka ruhusa ya kuuza ng'ombe afuate utaratibu, aende Mkoani aweze kupata *permit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile katika kuzuia wizi wa mifugo kuna *protocol* ya kuzuia wizi wa mifugo ambayo inaandaliwa kati ya nchi za Afrika Mashariki pamoja na *horn of Africa, horn of Africa* ni pembe ya Afrika, pale Somalia, Ethiopia basi hiyo kuna *protocol* inaandaliwa kusudi kusaidiana katika kuzuia wizi wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika sheria yetu ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo, Sheria namba 12 ya mwaka 2010 vile vile inazungumzia umuhimu wa kuweka chapa na kuweka alama kwenye ngozi ama kwenye masikio kwa ajili ya kuzuia wizi na kutambua mifugo ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji wa samaki, napenda kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge, Wizara yangu ina idara kamili ambayo inashughulika na ufugaji wa samaki na kutoa mbegu nzuri kwa ajili ya watu wanaotaka kufuga samaki. Mwaka huu unaokwisha tumeshazalisha vifaranga 2,600,000 vya perege ambavyo vimegawiwa kwa wananchi na vile vile tumeshazalisha vifaranga vya kambare 800,500 ambao wote wametumika kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa samaki unapunguza nguvu ya uvuvi haramu kwenye maziwa yetu, inapunguza nguvu vile vile hata ya uvuvi halali, lakini inapunguza kwa sababu tukifuga samaki basi tunajipatia kipato tunapata lishe lakini tunaongeza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 99 – Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**

Kif. 1001 – *Admin. and HR Management* Sh. 3,759,832,000/=

**MHE. ZAHRA ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua kuhusu sera ya uvuvi inayohusiana na *SUMATRA* inasemaje, kwa sababu kumekuwa na malalamiko mengi juu ya *SUMATRA* na wavuvi wetu hawa wadogo wadogo kuna urasimu mkubwa ambao unapelekea wavuvi wetu hawa mara nyingi kukosa leseni kwa sababu ni lazima kwanza wakukague *SUMATRA* mpaka waridhike ndio Wizara husika inatoa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kuna manung'uniko ya wavuvi hawa wanahisi kama *SUMATRA,* haina utaalam wa kutosha wa kujua mahitaji hasa ya wavuvi wetu wadogo wadogo ni nini? Kwa mfano, pale *SUMATRA* inapolazimisha wavuvi wadogo wadogo kununua maboya ya kuogelea wakifananisha wavuvi hawa kuwa ni sawa sawa na meli zetu labda za abiria au meli za kuchukua mizigo. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zahra kama ifuatavyo:-

*SUMATRA* inaangalia usalama wa wavuvi na ina-*register* vyombo ambavyo vinafaa kwenda baharini? Kwa sababu kule kuingiza tu chombo baharini ni lazima chombo kile kiwe salama kwa sababu kinaweza kikasababisha ajali kwa vyombo vingine ambavyo ni vizima, kwa maana hiyo ndiyo mahusiano kwamba kikishaonekana kinafaa kuingia baharini ni lazima

kitapewa leseni na Idara yangu na ndiyo maana pamoja na kwamba una gari zuri kwa mfano, lakini huwezi ukapita barabarani kama hujapewa leseni, lazima gari likaguliwe. Kwa hiyo ndiyo maana yake tu. Ni usalama wa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa unisaidie kuwaelimisha wavuvi wako wavae *life jacket*, lakini vile vile waweze kupitisha vyombo vyao vipimwe na *SUMATRA* lakini vile vile wapewe leseni na waandike namba zao kwenye ubavu wa vyombo vile wanavyovitumia. Ni muhimu sana kwa sababu bila hivyo, hata uharamia, watu wengine wanafanya uharamia kwa kutumia vyombo hivyo hivyo ambavyo havijakuwa *registered* na *SUMATRA*.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kujua jukumu la Serikali litakuwa wapi kwenye maji ya mifugo kama wameambiwa wafugaji wajichimbie malambo wenyewe kwa kuuza ng'ombe?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningekuuliza jukumu la Serikali liko wapi kama unaambiwa uchangie ada ya kumsomesha mtoto sekondari. Kwa hiyo, suala hapa ni kwamba, tunachangia, haiwezekani Serikali ikatoa miundombinu yote yenyewe ni lazima tuchangie. Sijasema kwamba tuna-*stop*, sijasema kwamba tunasimamisha, nimesema tunachangia kwa manufaa ya kusogeza ufugaji mbele na mbele.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, katika michango yangu mbalimbali nimeweka msisitizo katika kushauri Serikali kutoa madume wa mbegu kutoka katika *ranches* za Taifa kuongeza ufanisi wa mifugo, lakini msisitizo wangu mkubwa sana upo katika eneo moja la kuhakikisha kwamba, wafugaji wa Simanjiro, Kiteto na maeneo mengine ya Kaskazini kama Mwanga na Same wanapatiwa kifuta machozi katika kile ambacho kinapunguza umaskini unaotokana na ukame wa 2008/2009 kama ambavyo Rais aliamua kuwapatia wenzetu wa Longido, Monduli na Ngorongoro. Nataka kujua nini msimamo wa Serikali katika eneo hili ili kuhakikisha kwamba wafugaji wale walioko katika umaskini uliotopea wanaondokana na adha hiyo kwa wakati huu? Nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sendeka, Mbunge wa Simanjiro kama ifuatavyo:-

Kuhusu mbegu kwa maana ya madume, madume yanapatikana yaliyo bora katika *ranch* zetu, lakini pia ni vizuri niseme kupitia kikao hiki kwamba, Naike ambayo sio mbali kutoka Simanjiro wana uwezo maana wana mbegu kati ya 480,000 mpaka 640,000 na hivyo kwa kutumia uhamilishaji, wafugaji wanaweza wakapata mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hili la kifuta machozi, nimwombe tu kwamba Viongozi, Wabunge wa maeneo hayo wajaribu kujenga hoja maana ni

kweli mifugo ilifariki, mingi ilikufa Simanjiro, Kiteto, Arumeru na Same, lakini ni lazima kujenga hoja tena ili tuweze kuiendea Serikali hasa Ofisi ya Waziri Mkuu inayohusika na maafa na kuona kwamba kutakuwepo pia na uwezekano wa kufanya hilo.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, niliitaka Serikali kuona utaratibu mwingine wa kuelimisha wavuvi badala ya kuchoma nyavu zao. Uwepo wa nyavu zile nilisisitiza kwamba kumekuwepo na sababu ya kutokuwa na elimu ya kutosha ambayo walikuwa na haki ya kuwezeshwa na Serikali yao, lakini badala yake sasa pamekuwa na utaratibu wa kuchoma nyavu. Kwa maoni yangu, ingewezekana kabisa Serikali itafute hela za kuwapa ili kubadilisha nyavu na nyavu, nyavu isiyotakiwa iondolewe na Serikali itoe nyavu mpya ili kuendeleza uvuvi nchini badala ya kuzichoma. Kwani huko ni kuwatia umasikini bila shabby. Nataka kauli ya Serikali. Ahsante.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mipata kama ifuatavyo:-

Sheria yetu ya Uvuvi namba 22 ya mwaka 2003, imetaja zana zinazoruhusiwa kwa ajili ya uvuvi endelevu na zana ambazo haziruhusiwi kwenye maji yetu ama maji ya bahari au maji ya baridi. Sasa Serikali kutokuwa na fedha za kubadilisha nyavu sio kigezo cha kuruhusu watu waendelee kuharibu rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, bado sharti litaendelea lile lile, maana ukifika kwenye maeneo ya uvuvi kwa sababu wanazijua, sio kwamba hawajui, kwamba hawana elimu, elimu wanayo ndiyo maana tukifika kule wanakimbia kabisa na nyavu na makokoro. Kwa hiyo, tutaendelea kuwakamata na kuwafikisha kwenye vyombo vya Sheria na adhabu yake ni kuchoma nyavu, hakuna mbadala mwingine.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kama ambavyo nilikuwa nimeandika kwenye mchango wangu wa maandishi lakini sikupata majibu kwa Mheshimiwa Waziri, najua Serikali inapiga marufuku uvuvi haramu nami pia naungana nao, lakini pia nilikuwa nataka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia vijana wanaojihusisha na masuala ya uvuvi haramu kwa kuwapatia vifaa vya kisasa ili waweze kujikomboa na kupata ajira?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawasaidia namna gani vijana na wavuvi kwa ujumla. Kwanza, tatizo lao kubwa la vitendea kazi vyao kwa mfano nyavu, nyuzi za kutengenezea nyavu, *engine* za maboti yao zilikuwa zinatozwa *VAT* yaani kodi ya ongezeko la thamani, sasa tumeshawasaidia vitu hivyo tumeshavitoa. Kwa maana hiyo bei zimeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachowaomba waunde vikundi vyao vidogo vidogo, Vyama pamoja na *SACCOS* ili waweze kuwa na nguvu ya kukopa kwenye mabenki yanayotoa mikopo. Lakini vile vile nimeelezea kuhusu *TIB, TIB* inatoa mikopo na sasa hivi

tuko kwenye mchakato wa kutengeneza ama wa kuunda Benki ya Kilimo ambapo na wao wafugaji na wavuvi wanaweza wakakopa hapo. Kwa hiyo, naomba kumwomba Mheshimiwa Bulaya aweze kuwashauri vijana, kwamba, wawe na vikundi ili waweze kupata mikopo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa naomba Waziri anisaidie kwa sababu katika suala la ufugaji wa kuku hata jana tumeshuhudia mfugaji bora wa kuku anatoka Mkoa wa Singida, hivyo tunahitaji masoko. Lakini hapa amesema kwamba, katika utoaji wa vibali nimeshtuka kidogo kwa sababu hata yeye anaonekana hana habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ina maana vibali huenda viko vingi zaidi ya hivi ambavyo vimetajwa. Sasa yeye amesema kwamba ameviagiza vyombo vifanye uchunguzi, napenda aniambie ni vyombo vipi ambavyo ameviagiza kufanya uchunguzi na je, atatuletea lini majibu ya vyombo hivyo? Ahsante.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema ni kwamba, kichunguzwe kibali feki ambacho nilikitaja na kwamba tumegundua kuwa, kuna kibali feki ambacho kimeripotiwa na Waziri kivuli. Sasa nikasema, Wizara yangu kwangu ijiridhishe kwanza na iwasiliane na vyombo vya usalama kusudi ichunguzwe hiyo kampuni ambayo ilikuwa inatumia hicho kibali na hicho kibali ni nani amekighushi kusudi hatua za kisheria zichukuliwe.

**MHE. MASOUD ABDALAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie au anieleze kwamba, kwa kuwa nchi za nje unahitaji mifugo mingi zaidi, lakini na nyama nyingi zaidi, lakini sisi uwezo wetu wa kufanya hivyo kusafirisha inakuwa ni tatizo, ni mdogo. Sasa Serikali ina mkakati gani wa kuweza kusafirisha mifugo na nyama ili kuboresha kipato cha wafugaji? Nashukuru.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza Serikali ina mikakati gani, Serikali huwa haifanyi biashara, kwa maana hiyo, haina mikakati ya kusafirisha mifugo, lakini inatengeneza mazingira mazuri ili mfanyabiashara aweze kusafirisha mifugo kwa urahisi zaidi.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza, tufute ile kauli ya Mheshimiwa Waziri ya kutamka nguruwe kwenye mwezi Mtukufu wa Ramadhani. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, niliomba kupata ufafanuzi wa miundombinu ya maji taka iliyoko ambayo yanakwenda moja kwa moja baharini na kwenye Maziwa yetu ambapo kuna zebaki au kemikali ambazo zinaliwa na samaki wadogo na samaki wakubwa wanakula samaki wadogo, halafu kunakuwa na *deposit* ya *chemicals* katika samaki wakubwa na binadamu tunakula wale samaki wa kubwa. Je, Wizara yake ina mkakati gani wa kupambana na hili la uchafuzi wa viumbe hai hivi baharini ambako inaweza

ikasababisha ugonjwa kama wa *minamata* ambao uliwahi kutokea kule Japan ambayo itakuwa ni athari kwetu Watanzania na afya ya binadamu kwa ujumla? Naomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbatia Mwenyekiti wa Chama cha *NCCR*–MAGEUZI na Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria namba sita (6) ya mwaka 1980 ilianzisha *TAFIRI*. *TAFIRI* ni Taasisi yetu ambayo inatumika katika kufanya utafiti, sasa kila mara wanachukua maji, udongo pamoja na samaki kwa sababu ndiyo maana tunasafirisha samaki nje ya nchi lazima wapimwe na *TAFIRI* wakionekana kwamba wako salama basi wanaruhusiwa kusafirishwa. Lakini wanachopima pale ni vimelea vya magonjwa pamoja na kemikali lakini madini tembo, madini tembo ni *heavy metals* ambazo inawezekana zipo kwenye maji ama kwenye viumbe wanaoishi Baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, zoezi hilo linafanywa na *TAFIRI*, linafanywa kwa ukamilifu, lakini pia tuna maabara za kucheki masuala ya *atomic* Dar es Salaam. Kuna maabara kule Nyegezi ya kucheki sumu pamoja na makemikali na madini tembo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbatia usiwe na wasiwasi kazi hiyo inafanywa vizuri na *TAFIRI*.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ili kuboresha mifugo na uvuvi ni lazima tutengeneze miundombinu ya kutosha kwa

wafugaji na wavuvi. Katika mchango wangu wa maandishi nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba kwa nini Serikali imekuwa inatuahidi eneo la Kuyu kuchimbwa Lambo na hata kwenye hotuba yako umeainisha hiyo Wilayani Kilwa na sasa umetoa kauli nyingine tofauti kwamba sasa hatuwezi, lipi ambalo tutashika, kwamba tutachimbiwa hili lambo au ndiyo tuwaambie wananchi wale wajichimbie wenyewe?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwondoa wasiwasi Mheshimiwa Mangungu kwamba nilichosema ni kwamba, tusaidiane wote tuweke miundombinu, sijasema Serikali haitasaidia. Kwa hiyo, lambo ambalo limeahidiwa na Serikali litachimbwa, lakini kwa sababu halitatosha, Mheshimiwa Mangungu *organize* wafugaji wako wachimbe mengine ili kazi iwe rahisi zaidi ya kusaidia mifugo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani, tumezungumzia mustakabali wa ile meli ambayo wavuvi wa Kichina walikamatwa na wakawa na kesi maarufu kama samaki wa Magufuli. Sasa kuna mambo mengi yanasemwa kuhusiana na hali ya ile meli ikiwa sambamba na kuna watu wanahujumu ile meli ambao ni Maafisa wa Bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka tu nipate kauli kutoka kwa Waziri mhusika, mustakabali wa ile meli ukoje na baada ya kushinda ile kesi, meli imebaki kama mali ya Tanzania ama vinginevyo? Kwa hiyo, nataka tu nipate ufafanuzi juu ya mustakabali wa ile

meli na mambo mbalimbali yanayosemwa kuhusiana na hujuma ya hiyo meli.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge wa Kawe, Mdogo wangu na Dada yangu Halima Mdee kama ifuatavyo:-

Kwanza niseme meli hii ilikamatwa mwezi Machi mwaka 2009, kesi hii ilichukua *almost* miaka miwili kwa sababu hukumu imetolewa tarehe 23 mwezi wa pili mwaka huu, wakapatikana wenye hatia, watu wawili, wakachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria. Lakini Rufaa ilikatwa kwa maana hiyo, sasa hivi Rufaa imekatwa na iko kwenye *court*, Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati wote kesi inapoendelea, chombo chochote kilichokamatwa kinaitwa *evidence,* ni kidhibiti, hakuna anayeweza kukitumia, ama aliyekuwa amekamatwa nacho au Serikali. Sasa tulivyoshinda, ingekuwa kwamba hakuna Rufaa, sasa hivi ile meli ningekuwa nimeshaipangia kwamba itusaidie kwenye kufanya doria kwa ajili ya uvuvi haramu kwenye *deep sea*, lakini sasa hivi ile meli iko chini ya Polisi kwa maana ni *evidence* au ni ushahidi. Ile meli haiko chini ya Wizara yangu, iko chini ya Idara zinazohusika kutunza vidhibiti.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni namba 104(2) nawajibika sasa kupitisha bajeti hii kimafungu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*

*ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*Sh. 952,426,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*Sh. 726,264,000/=
Kif. 1004 - *Livestock Research. and Train. Inst... ... ... ...* Sh. 8, 560,028,400/=
Kif. 1005 - *Government Communication Unit... ... ... ... ...* Sh. 149,779,000/=
Kif. 1006 - *National Livestock Inst.- Mpwapwa... ... ...* Sh. 2,229,184,700/=
Kif. 1007 - *Internal Audit Unit...* Sh. 218,417,000/=
Kif. 1008 - *Procurement Management Unit... ... ... ... ...* Sh. 311,236,000/=
Kif. 1009 - *Legal Services Unit* Sh. 108,136,000/=
Kif. 1010 - *Inform. Commun. & Technology... ... ...* Sh. 17, 299,884,700/=
Kif. 7001 - *Veterinary Services ...*Sh. 8,787,313,700/=
Kif. 7002 - *Livestock Identif Regist. And Traceable Unit... ... ... ...* Sh. 0/=
Kif. 7003 - *Pastoral System Development* Sh. 0/=
Kif. 7004 - *Central Veterinary Laboratorie* Sh. 0/=
Kif. 7005 - *Veterinary Council of Tanzania ... ... ...* Sh. 9,005,026,700/=
Kif. 8001 - *Animal Production* Sh. 4,040,244,000/=
Kif. 9001 - *Fisheries Development Division... ... ... ... ...* Sh. 9,324,233,600/=
Kif. 9002 - *Aquaculture Development Division... ... ...*Sh. 1,057,252,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

## Fungu 99- Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

Kif**.** 1003 - *Policy and Planning…*Sh. 1,869,239,000/=
Kif. 1004 - *Livestock Research and Train. Inst. … … … … … …* Sh. 3,254,913,000/=
Kif. 1006 - *National Livestock Inst.– Mpwapwa… … ….* Sh. 1,183,699,000/=
Kif. 7001 - *Veterinary Services* Sh. 3,320,879,400/=
Kif. 7002 - *Livestock Identif Regist. And Traceable Unit… … … … … … … …*Sh. 0/=
Kif. 7003 - *Pastoral System Development…*Sh. 0/=
Kif. 7004 - *Central Veterinary Laboratories…* Sh. 0/=
Kif. 7005 - *Veterinary Council of Tanzania… … …*Sh. 102,799,000/=
Kif. 8001 - *Animal Production…*Sh. 2,231, 413,000/=
Kif. 9001 - *Fisheries Development Division… … … … …* Sh.1,634,268,000/=
Kif. 9002 - *Aquaculture Development Division… … … … … …* Sh. 242,272,600/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

## TAARIFA

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumzi na kupitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya Mwaka wa Fedha

2012/2013, kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI**: Baada ya ushindi huo, sasa niombe kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Dkt. Matayo David na Naibu wake Mheshimiwa Nangoro; Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara. Tunaomba basi mageuzi hayo yaliyopendekezwa na Waheshimiwa Wabunge na mapendekezo na maoni na ushauri yafanyiwe kazi ili kuleta maendeleo katika Wizara hii.

Baada ya kusema hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 jioni Bunge liliahirishwa mpaka*
*Siku ya Ijumaa,Tarehe 10 Agosti, 2012*
*Saa Tatu Asubuhi)*